

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 6 Agosti, 2012

(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (*DART*) kwa mwaka ulioshia tarehe 30 Juni, 2011 (*The Annual Report and Audited Accounts of Dar es Salaam Rapid Transit for the year Ended 30th June, 2011.*

NAIBU WAZIRI, WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

NAIBU WAZIRI, WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Hotuba ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2011/2012 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 324

Kuwawezesha Wajasiriamali Nchini

MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. MOSES J. MACHALI) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wajasiriamali nchini hususani Mafundi Seremala wa Kasulu kwa kuwasaidia nyenzo za kisasa ili waweze kujikwamua kiuchumi na kukomesha hali ya Serikali na Taasisi mbalimbali kutumia fedha nyingi kununua fenicha za nje na badala yake wanunue fenicha zinazotengenezwa hapa nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali Machali Mbunge wa Kasulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*NEEC*) imeweka mikakati mbalimbali ya jinsi ya kuinua fani ya useremala kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa mafundi seremala; kuwawezesha kushiriki katika maonesho mbalimbali na kuunda shirikisho liitwalo *Tanzania Woodworking Federation (TAWOFE)* ambalo linajumuisha makampuni, watu binafsi, ushirika na vikundi vyta useremala. Wanachama waanzilishi wa shirikisho hilo wametoka Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Morogoro. Zoezi hili litaendelea kwa mikoa mingine na bila shaka Mikoa wa Kigoma hususani Wilaya ya Kasulu utafikiwa siku za karibuni.

Mheshimiwa Spika, katika mkuhanano wa Bajeti wa mwaka 2009/2010, Serikali ilizigiza Wizara, Idara na Taasisi zake kuacha kununua samani (*furniture*) zilizotengenezwa nje ya nchi na badala yake wanunue samani zinazotengenezwa nchini kwa malighafi za hapa nchini ili Seremala wetu wawe na soko la uhakika. Taasisi za Serikali zilizoko Kasulu zinapaswa pia kutekeleza agizo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo za Serikali, natoa wito kwa Mafundi Seremala wa Kasulu kuanzisha vikundi au Vyama vyatia Ushirika vyatia Useremala ili kuimarisha biashara zao. Lengo ni kuwezesha kupata mikopo ya kununulia nyenzo za kisasa za kufanya kazi pamoja na kuongeza mitaji yao kupitia mikopo kutoka kwenye taasisi za Fedha na vile vile kuongeza sauti zao.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini nina maswali mawili ya nyongeza; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba imekataza taasisi zake kununua bidhaa hizi, kwa nini isipige marufuku kabisa uingizaji wa bidhaa ambazo zinaweza zikatengenezwa na Watanzania ili tuweze kuboresha soko la ndani?

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema, bila shaka hawa watu Tanzania *Wooding Federation* watafika Kigoma, nataka kujua ni lini sasa watafika Kigoma, Baraza la uwezeshaji kichumi na Tanzania *Wooding Federation* hususani Kibondo na Kasulu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU,

UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mkosamali kwa maswali yake, kwa sababu yananipa fursa ya kuieleza Tanzania kwamba, nchi hii haitaki kuwa nchi ya kuagiza bidhaa nje, ingetaka kuimarisha uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi na wananchi wake kuthamini bidhaa zinazotengenezwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anauliza kwa nini Serikali haipigi marufuku uingizaji wa samani hizo kutoka nje ya nchi. Tanzania siyo kisiwa na ili Tanzania iwe imara katika biashara na katika kukuza ubora wa bidhaa zake inabidi ishindane na bidhaa kutoka nje, kwa sababu tukijifungia ndani wenyewe tutabweteka na vile vile tunapaswa kushiriki katika biashara ya dunia na kutumia fursa zetu za nchi zingine kupeleka bidhaa zetu. Kwa hivyo, itakuwa siyo vizuri kuwanyima wengine kuleta bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza ni lini Kigoma na Kasulu, Baraza la Uwezeshaji litafika kule kuhamasisha na kuwaunganisha Mafundi Seremala. Napenda kumwambia kwamba nikimwambia tarehe kamili na mwezi kamili pengine wao wanaweza wasiwe tayari au kukatokea jambo. Jambo ambalo nataka kumhakikishia ni kwamba, Serikali inataka wananchi wake na hasa vijana na mafundi seremala wajizatiti katika kujunga wenyewe ili uwezo wao uwe mkubwa na ili wawe na sauti kubwa ya kuliwezesha soko lenyewe likubali kwamba kuna seremala ambao wako tayari kutoa huduma ya kutengeneza samani kwa ajili ya Serikali na watumiaji wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ajaribu kufuatilia nami pamoja na Baraza la Uwezeshaji kuona ni lini tutafika Kigoma lakini bila kupoteza muda, naamini mikoa yote ya Tanzania tutawafikia na tutakapokuwa na nchi nzima ambayo ina umoja wa seremala tutakuwa nchi imara zaidi katika kuzalisha samani ambazo Serikali itazihitaji.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika nakushukuru, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Serikali inasema kwamba, Tanzania siyo kisiwa, lakini kitendo cha Serikali kuruhusu fenicha kutoka China kujaa kwenye *showroom* Dar es Salaam na Mikoa yote, inafanya bidhaa za Tanzania hasa wanaofanya shughuli za useremala bidhaa zao zinakosa soko. Je, Serikali inafanya nini kulinda viwanda vya ndani na kulinda ajira za vijana wa ndani angalau kuwe na kiwango maalum cha bidhaa zinazoingia ili bidhaa zinazotengenezwa Tanzania zipate soko?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa swali lake na nawashukuru Wabunge kwa kulikazania jambo hili la Serikali kununua samani zinazotengenezwa na Seremala wetu. Anauliza Serikali kuruhusu bidhaa za China ni kuwanyima soko Seremala wetu au bidhaa zingine za Tanzania kuwa soko.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuimarisha uzalishaji Tanzania na Watanzania wapende kununua bidhaa zao si kunyima bidhaa za nchi zingine, bali ni kuimarisha viwanda vyetu na kuimarisha vijana wetu. Hata hivyo,

kwa sababu sisi ni nchi changa ukiangalia kiviwanda, tuna mambo ambayo Serikali inayafanya kama kuongeza ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, kuna sera ambazo tumeziweka za kuweka upendeleo kwa viwanda vyetu na watu binafsi ambao wanazalisha bidhaa ndani ya nchi, lakini wakati huo ni lazima turuhusu ushindani ili kusudi na sisi Watanzania tuwe tayari kuwa kwenye soko la dunia.

Na. 325

Kuboresha Miundombinu Mji Mdogo wa Mbalizi

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Mji Mdogo wa Mbalizi –Mbeya Vijijini ni katika ya Miji midogo nchini inakuwa kwa kasi sana, lakini miundombinu kama Maji, Barabara na Upimaji wa Viwanja haiendelezwi:-

(a) Je, ni lini miundombinu ya Mji huo itaboreshwala ili kwenda sambamba na ukuaji wake?

(b) Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara na upimaji katika Mji huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Mbeya unakua wa kasi kiasi cha kuhitaji mipango madhubuti ili kuendana na kasi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri imefanya utafiti wa kupata vyanzo vipyta vya Nsalala, Sawala na Ilunga vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 5,016 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 836.54 kwa siku zilizopo kwa sasa.

Serikali imepanga kujenga upya mfumo wa usambazaji pamoja na kupanua mtandao wa maji katika Mji huo kazi ambayo inafanywa na mtaalam mshauri kampuni ya *SEURECA*. Hatua inayoendelea ni usanifu wa kina wa mradi baada ya kukamilika kwa usanifu wa awali ili kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha miundombinu ya barabara katika Mji wa Mbalizi, Serikali katika mwaka 2010/2011 ilitenga shilingi 91.7 ambazo zilitumika kujenga mifereji ya maji ya mvua mita 600 na matengenezo ya barabara kilomita tatu kwa kiwango cha changarawe. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 27.5 ambazo zilitumika kujenga mfereji wa maji ya mvua mita 65 kwa gharama ya shilingi milioni 15.2 na matengenezo ya kawaida ya barabara kwa gharama ya shilingi ya milioni 12.3.

(b) Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, zimetengwa shilingi milioni 150.8 kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi awamu ya kwanza kwa kiwango cha matofali ya zege. Mkandarasi tayari amepatikana ili kuanza ujenzi huo. Kuhusu upimaji wa viwanja, Halmashauri imeandaa michoro mitatu ambayo itawezesha upimaji wa viwanja 2,863 katika Mji huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya maeneo ya Mji huo yanahitaji kurasimishwa kutokana na kujengwa kiholela. Tayari ramani imepitishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji na Makazi ambapo jumla ya shilingi milioni 500 zitahitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na upimaji wa viwanja kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, Mji wa Mbalizi ulianza kupimwa miaka kumi iliyopita na kazi ile ya kupima Mji ule ikasimama sijui ni kwa nini haukuendelea tena? Naomba kupata jibu.

Pili, fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza barabara ni kiasi kidogo sana. Je, Serikali ipo tayari sasa kuongeza fedha ili kuboresha barabara za Mji ule wa Mbalizi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza analoniuliza Mchungaji Mwanjale ni swali zuri, wewe mwenyewe Mbalizi unaifahamu na kwa vile ameuliza katika eneo hili nataka nikifanye kikao chako hiki kiweze kuelewa mambo yafuatao:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 ndipo Serikali ilikubali kwamba Mbalizi iwe mamlaka ya Mji mdogo kwa rekodi zetu. Mwaka 2004 tulipokubaliana kwamba iwe mamlaka ya Mji Mdogo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ikasema kwa hali ilivyo ya bajeti na uchumi wasingeweza kuanza kuanzisha mamlaka ya Mji Mdogo. Januari 31, 2012 ndipo kikao cha Baraza la Madiwani kimekubali kwa mara ya kwanza na Mchungaji Mwanjale akiwemo mle ndani kwamba sasa wanakubali waanze ku-*operate* chini ya mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, anachosema Mchungaji Mwanjale ni kweli na wewe mwenyewe unapita pale unaangalia Mji ule unakua kwa haraka sana tusipouangalia utakuwa na *squatter* mengi na utaharibika. Kwa hiyo, naamini kwamba mpaka tukachelewa kiasi hicho, ni huu uamuzi wa kuchelewesha kuanzishwa kazi hii, ingeanza toka mwaka 2004, hii hali yote anayoizungumzia Mchungaji isingejitokeza pale. Kwa hiyo napenda kumpongeza sana kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mbunge ameuliza kuhusu fedha zinazopelekwa pale, hela ambazo zinapelekwa pale ni bilioni 1.3, takwimu zote ninazo hapa. Hizi ni kwa ajili ya barabara za lami kilomita mbili, kilomita tatu pamoja na barabara za udongo ambazo zipo pale na miundombinu mingine kwa ajili ya Mbalizi tu, sizungumzii mamlaka yoyote kwa maana ya Mbeya. Kwa hiyo, tutaendelea kusaidia Mji ule na nampongeza sana Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya pale, ni vizuri tukamsaidie tuondokane na *squatter* ambayo inaendelea katika Mji wa Mbalizi.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, miundombinu ya Mikoa mingine nchini ikiwemo Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Geita ni mibovu na hairidhishi pamoja na kwamba mikoa hii ndiyo inayozalisha dhahabu na almasi:-

Je, Serikali haioni kwamba ni busara kutumia mapato yote yanayotokana na madini kuboresha miundombinu katika maeneo haya kabla ya *ku-distribute* nchi nzima? (*Makofi*)

SPIKA: Swali la msingi lilikuwa linasemaje? Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 326

Tatizo la Upatikanaji wa Nishati ya Umeme Nchini

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. SYLVESTER MASELLE MABUMBA) aliuliza:-

Tatizo la upatikanaji wa Nishati ya Umeme inatokana na nguvu za maji imeendelea kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiombe msaada kwa nchi marafiki wa kujenga kinu cha Nyuklia ambacho kitazalisha umeme wa uhakika?

(b) Je, wananchi wangapi kwenye sekta ya viwanda na utalii wamepoteza ajira kutokana na mgao wa umeme kuanzia mwaka 2009-2011?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina madini ya urani ambayo yanaweza kutumika kuzalisha umeme na kuondokana na kutegemea nguvu za maji pekee kuzalisha umeme. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni uwezo wa kitalaam (*capacity*) na kukidhi vigezo vya Kimataifa vinavyoruhusu matumizi ya madini ya urani kuzalisha umeme kwa usalama. Matumizi ya madini ya urani yanaratibiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani yaani *International Atomic Energy Agency (IAEA)* hivyo kuanzisha vinu vya kufua umeme

kwa kutumia madini ya urani, ni lazima kupata ridhaa kutoka shirika hilo na taratibu zake zinachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tanzania ina vyanzo vya umeme vya kutosha ambavyo ni makaa ya mawe, gesi asili, upemo, juu na joto ardhi ambavyo vikitumika vizuri vinaweza kumaliza tatizo la umeme tulilonalo sasa na Serikali inajipanga kutumia vyanzo hivi. Hadi mwezi Juni, 2012 uwezo wa mitambo ya kufua umeme (*installed Capacity*) nchini ulikuwa *MW* 1,375.74 wakati matumizi yetu ya kawaida kwa siku ni katika *MW* 600 na *MW* 700.

(b) Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa kiuchumi na kijamii. Sehemu kubwa ya sekta ya biashara na huduma za kijamii zinategemea uwepo wa umeme wa uhakika ili ziweze kuendeshwa kwa ufanisi. Matatizo ya umeme kwa namna moja au nyingine yameathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii zikiwemo sekta za viwanda na uthalii, hivyo yawezekana kuwa fursa za ajira zimepotea ama kwa biashara kufungwa au sehemu za kazi kupunguza watumishi kutohaka na kushuka kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu kuweza kujua idadi ya watu walioathirika na tatizo la kutokuwepo kwa umeme wa uhakika kwa kupoteza ajira zao. Aidha, ili kuweza kufahamu idadi ya watu walioathirika inabidi ufanyike utafiti wa kina. Kwa kuwa suala la ajira ni mtambuka na linahusisha sekta ya umma na sekta binafsi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kuwalipa fidia watu walioathirika na tatizo la kukosekana kwa umeme wa uhakika wakiwemo waliopoteza ajira badala yake Serikali inaendelea kutekeleza mikakati iliyojiwekea ya kupata umeme wa uhakika na kutosheleza mahitaji ya hapa nchini na ziada kwa kutumia vyanzo vyenye gharama nafuu kama vile gesi, makaa ya mawe, juu, upopo, joto ardhi.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri amezungumzia la umeme wa gesi pamoja na makaa ya mawe. Lakini makaa ya mawe ya Ngaka ambayo yameshaanza kuvunwa bado Serikali haijaweka msisitizo wa kujenga *transmission* line kutoka Ngaka mpaka Songea, Njombe hadi kufika Mufindi. Je, nini majibu ya Serikali kuhusiana na mradi huo wa ujenzi wa *Transmission line?* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hawawezi kulipa fidia lakini kwa kuwa watu wengi ambao wamechukua mikopo katika mabenki wanashindwa kufanya marejesho kutokana na kutokuwa na uzalishaji wa kutosha kulingana na miradi yao ilivyokuwa. Kwa nini Serikali isitoe dhamana yaani wa *bailout* kwa kipindi fulani ili watu waweze kujenga uwezo wa kulipa madeni hayo kwa uhakika? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni

kweli kwamba maendeleo ya mipango ya uzalishaji wa umeme kupitia makaa ya mawe ya Mchuchuma, Ngaka na Kiwira yanaendelea vizuri. Tuna matarajio kwamba ifikapo mwaka 2015 tunaweza tukawa tumeshaanza kuzalisha takribani *MW* 200 kutoka Mgodi wa Kiwira na takribani *MW* 300 kwa Mchuchuma na Ngaka 120. Hayo ndio matarajio yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumhakikisha kwamba mipango ya ujenzi wa miundombinu itakayokwenda sambamba na uzalishaji huu mpya wa umeme iko mbioni na tuna mradi ambao unaendelea sasa na uko kwenye hatua nzuri ambao tunaanza kujenga *line* kubwa kutoka Makambako kwenda mpaka Songea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sambamba na hiyo mipango inaendelea ili kuhakikisha kwamba kabla ya uzalishaji huo haujafikiwa basi tumeshajenga *line* ya kutosha kuweza kusafirisha umeme huo ambao utazalishwa.

Lakini jibu la kipengele cha (b) kwamba mikopo iweze kutolewa, kuna watu wamekopa na wanahitaji kurejesha hapa nafikiri swali la msingi liliikuwa limejikita kwenye suala zima la watu waliopoteza ajira. Sasa kama kuna watu ambao wamekopa mikopo na wanahitaji kufanya marejesho kupitia tatizo hili la umeme kwamba wanapata shida, basi hili ni jambo ambalo nafikiri kimsingi ni lazima sisi kama Serikali tuliangalie. Lakini lina namna nyngi ya kuweza kuliangalia, si namna peke yake tu ya kuangalia katika

Wizara ya Nishati na Madini kwa maana ya kulipa fidia kupitia kwenye Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba, tatizo hili ni la Kitaifa na wote tunafahamu sababu zilizotupelekea kufikia kwenye hatua hii ni kuamini kwamba vyanzo vya maji vingeendalea kuwepo. Lakini sasa Serikali imejikita katika suala zima la kuhakikisha tunaanzisha vyanzo vingine vya kuzalisha umeme kwa njia nyingine kama jua, makaa ya mawe, gesi ambayo inatusaidia sana na hivi tunashukuru Mungu kwamba, tunaendalea kugundua gesi kwa kiasi kikubwa katika *exploration* zinazoendalea. (*Makof!*)

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa ni wazi kuwa nishati ya umeme ni uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yoyote ile na kwa kuwa hapa Tanzania kwa takribani miaka zaidi ya 70 toka Shirika la *TANESCO* limeanzishwa bado ni asilimia chini ya 20 tu ya watu wenyе umeme. Nataka kuuliza Serikali kwa nini sasa haioni umuhimu wa kuruhusu watu binafsi pamoja na wawekezaji waweze kufanya biashara hii ya umeme kama walivyofanya Shirika la Posta na sasa hivi watumiaji wa simu wameongezeka sana yaani kuondoa *monopoly* ya *TANESCO*, kwa nini hawafanyi hivyo? (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa ameuliza kwa nini haturuhusu sekta binafsi ikaingia katika masuala mazima ya umeme? Nafikiri jibu liko wazi tu kwamba, kwa kweli tunashirikiana sana na sekta binafsi katika masuala ya uzalishaji wa umeme

na katika masuala mbalimbali katika sekta hii ya nishati. Sasa ni kwa kiasi gani tunahitaji kuwashirikisha sekta binafsi maana kuna kipengele cha uzalishaji, lakini kuna kipengele cha usambazaji, viko vipengele vingi. Sasa hapa ni suala zima la kuamua kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunadhani mpaka sasa hivi changamoto inajionesha na iko haja ya kufikiri vizuri juu ya suala hili kwa sababu kweli siyo rahisi kudhani kwamba *TANESCO* peke yake wanaweza wakakidhi mahitaji yaliyosambaa nchi nzima ya watu wanaohitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini nini kifanyike kwa sasa, ni kukubaliana na hali iliyopo wakati tunaendelea na kushirikiana na sekta binafsi kwa kiasi kuanzia kwenye *generation* tunashirikiana nao. Lakini kwenye suala la usambazaji mjadala haukufanyika, nafikiri tukikubaliana siyo jambo baya, lakini kwa sasa ni kwamba, bado *TANESCO* ndio wanao-*monopolize* maeneo fulani fulani ya usambazaji na uuzaaji wa umeme.

Na. 327

Sheria ya Wazee Kuandaliwa

MHE. MARGARET A. MKANGA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaandaa Sheria ya Wazee kwa kuwa Sera ya Wazee ilishaandaliwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuchelewa kwa Sheria hiyo wazee wanaendelea kupata huduma tu kwa msingi wa huruma badala ya kuwa ni haki yao?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Wazee mwaka 2003, madhumuni ya kuwa na Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa Wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha ya kila siku kwa manufaa yao na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa inashughulikia kufanikisha kuwepo kwa Sheria ya Wazee ambapo hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa rasimu ambayo iliwasilishwa kwa wadau na kujadiliwa na sasa inafanyiwa maboresho ili iwasilishwe kwenye *Cabinet Secretariat* na kupata idhini ya kutungwa kwa Sheria ya Wazee. Kutokana na umuhimu wa sheria hii zoezi litafanyika kwa awamu na Serikali itawasilisha Muswada wa Sheria hii Bungeni mwezi Aprili, 2013.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchelewa kwa Sheria hiyo Serikali imeendelea kuchukua hatua zinazolenga kuboresha maisha ya wazee. Hatua hizi ni pamoja na:-

- Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea kutambua mahitaji na matatizo ya wazee na kuona namna ya kuyashughulikia. Aidha, baadhi ya Halmashauri za Wilaya/Manispaa zimeanza kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za wazee.
- Serikali imetua agizo kwa mamlaka husika ili wazee wasio na uwezo kulipa kodi za nyumba au jengo ambalo ni makazi ya wazee waweze kupata msamaha.
- Serikali imetua agizo kwa Waganga Wakuu wa Wilaya/Halmashauri na Mikoa ili waanzishe kliniki za wazee kwa maana ya kuboresha utoaji wa huduma kwa kundi hili.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, swali langu hasa (b) kwamba, kuchelewa kwa sheria hii wazee wanapata huduma kama huruma. Napenda kufahamu ni nini hasa kilichosababisha sera kuandika mwaka 2003 na sheria kutungwa mwaka 2013 miaka 10 hapo kweli kuna huruma ya wazee, niseme huruma ya wazee ndio inaendelea kwa sababu inaonekana si lazima watungiwe sheria, kuna sababu zippi naomba nielezwe zilizofanya miaka kumi suala hili halijakamilika?

Ni baadhi tu ya Halmashauri ndio zimeanza kutenga fedha kwa ajili ya huduma za wazee. Ni yale yale bila sheria watu wanafanya kazi kwa matakwa yao. Ni kwa sababu gani Halmashauri chache tu ndizo zimeanza kutenga fedha na isiwe ni lazima kwa zote kutenga fedha?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, Serikali inaanza sera kwanza na baadaye inafuata sheria. Tukisema ni sababu zippi zilizofanya sheria isitungwe mpaka sasa, tunachojaribu kusema ni kwamba, sera ikishaandaliwa taratibu zote zinafuata za kuandaan hiyo sheria.

Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba sasa matayarisho ya kutayarisha sheria hii yanawasilishwa katika *Cabinet* na baada ya kutoka pale utaletwa huu Muswada na kama nilivyoagiza kwamba utakuwa umeletwa hapa mwaka 2013 mwezi Aprili.

SPIKA: Swali lilikuwa, kwa nini miaka kumi imepita?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba baadhi ya mambo ambayo yanatakiwa kutekelezwa katika sera hiyo yalishatolewa maagizo na kwamba mambo yake ambayo yametolewa maagizo yamo katika kutekelezwa ikiwemo utoaji wa msaada wa majengo kama mapango, ikiwemo msamaha katika huduma hizi za afya. Lakini pia tunachoweza kusema ni kwamba, badala ya kuzungumzia nini kilitokea jana ni vema tuzungumzie leo, tunakwenda kesho kwa kutoa

ahadi ya kwamba mwaka 2013 mwezi Aprili, sheria hiyo inaletwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunatoa agizo kuhakikisha kwa Halmashauri ambazo bado hazijaanza kutekeleza agizo ambalo lilishatolewa na ni matumaini yangu kwamba Halmashauri zisitofautiane katika kutekeleza mambo ambayo tayari Serikali imeshaagiza. Kwa hiyo, naamini Wazee watapata haki stahili katika kutengewa fedha katika kuboresha huduma ambazo wanastahili kuzipata katika maeneo ya nchi yetu.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza lakini lenye umuhimu sana. Katika kuandaa Sera hii ya Wazee ilikuwa ni pamoja na kulitazama upya suala la *pension* kwa wazee ambacho ni kitu cha msingi sana katika kuwahudumia wazee na kuwaongezea maisha yenyeye afya na heri na amani baada ya kulitumikia Taifa hili kwa miaka yao mingi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kuniambia kwamba hiyo sheria ambayo sasa hivi inaandaliwa inahusisha pia suala la *pension* kwa ajili ya wazee hawa Watanzania ambao wanahangaika sana kimaisha kwa sasa? (*Makof*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi mazuri yanayofanywa na Wizara ya Afya kuhusiana na Sheria ya Wazee sisi Wizara ya Kazi na Ajira tumeshaanza kwa kweli kwa kasi sana kuandaa *pension* hii ya wazee na nafikiri ifikapo mwaka wa fedha ujao hii *pension* ya wazee

itaanza kutolewa na wakati huo nafikiri na sheria itakuwa tayari. (*Makof*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imeshatoa agizo wazee wapate misamaha kwa ajili ya matibabu katika zahanati, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Mikoa, lakini wazee ni kundi ambalo lina matatizo makubwa na wakati mwingine wanalazimika kupelekwa kwenye Hospitali za Rufaa. Je, Serikali sasa itatoa tamko ili hospitali zote za rufaa zipokee misamaha waliyopewa wazee na kupewa matibabu kwa gharama ya Serikali? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, msamaha unaotolewa katika huduma za tiba kwenye vituo vya afya unahusu pamoja na Hospitali za Rufaa. Agizo lilitolewa ni pamoja na Hospitali za Rufaa, za Mikoa na za Wilaya kuweka dirisha kwa ajili ya kutoa huduma kwa wazee. Naamini hili linatekelezwa na tumekuwa tukilifuatilia na nimetembelea baadhi ya Hospitali za Mikoa kuona hayo madirisha ya wazee.

Na. 328

Uundaji wa Baraza la Taifa la Vijana

MHE. SAID M. MTANDA (K.n.y. MHE. SARA M. ALLY)
aliuliza:-

Sera ya Vijana ya Taifa ya 2007 inaeleza kuundwa kwa Baraza la Vijana litakalounganisha vijana wote bila kujali itikadi zao:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa uundaji wa Baraza hilo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuanzisha vipindi maalum vya redio na Televisheni vitakavyotoa elimu kwa umma ili kuwawezesha vijana kuwa na uelewa wa pamoja juu ya uundwaji wa Baraza hilo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Sera ya Maendeleo ya Vijana ya 2007 inatamka wazi umuhimu wa kuwa na Baraza la Vijana la Taifa, kwa lengo la kuwaunganisha vijana wote bila kujali itikadi za kisiasa, kidini, kijinsia, ukabilla wala rangi. Wizara yangu imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri na kuuwasilisha kwenye ngazi husika ili kupata kibali cha kutunga sheria itakayoanzisha Baraza la Vijana.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ipo haja ya kutoa elimu kabla ya Baraza la Vijana halijaundwa. Elimu hii itatolewa kwa wadau wote wakiwemo vijana wenyewe ili kuwawezesha kuwa na uelewa wa

pamoja juu ya uundwaji wa Baraza hilo. Elimu hiyo itatolewa siyo tu kwa njia ya redio na televisheni bali pia mikutano itakayowahusisha vijana wenyewe na wadau mbalimbali. Zoezi hili litaanza mara baada ya sheria ya kuunda Baraza la Vijana itakapokuwa imetungwa.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka sita sasa, toka Sera hiyo ya Vijana ilipotungwa. Muswada haujaletwa hapa Bungeni, ili tupitishe Sheria hiyo. Sasa nataka kufahamu Serikali, ni lini italeta Muswada. Ili tutunge Sheria ya kuanzishwa kwa Baraza hili la Vijana?

Mheshimiwa Spika, swali lingine la pili, ni athari zipi hasa zinazopatikana mionganoni mwa vijana kutokana na kutokuwa na Sheria hii, itakayowawezesha wao kuwa na Baraza la Vijana, ambalo wanaweza kukaa na kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mchakato wa kuundwa kwa Baraza la Vijana, umekuwa ni wa muda mrefu na Sheria hii bado haijatungwa. Nataka kuwaahidi tu kwamba, mwaka huu wa fedha, Wizara yetu imejipanga kuwasilisha Bungeni, Muswada huu, ili kupata Sheria hiyo ya kuunda Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika, athari wanazozipata vijana ni pamoja na kwamba, zipo changamoto nyingi zinazowakabili vijana katika sehemu mbalimbali, ikiwepo Mijini, Vijijiini na Mashulen, ikiwemo pia ukosefu

wa ajira. Kwa hiyo, chombo hiki, kitakuwa ni chombo ambacho kitahusisha vijana mbalimbali kuanzia ngazi ya Vijiji mpaka Taifa, kuweza kujadili na kutatua matatizo yao.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, fursa nyingi wamekuwa wakizipata vijana wengi walioko mijini, je, Serikali, ina mkakati gani wa kuwafikia vijana walioko vijijini katika uundwaji wa Baraza hili?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, inawezekana kuwe na hofu kwamba, vijana wa Vijijini wasipate uelewa juu ya suala hili. Wizara yangu imejipanga kuwaelimisha vijana, kutakuwa na vipindi kuelekea katika kuunda Baraza la Vijana kuanzia katika *Television* na *Redio*, ili kupata uelewa. Pia Baraza hili, litakuwa na muundo kuanzia Vijijini hadi Taifa.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Lakini swali langu, nafikiri limeshaulizwa na Mheshimiwa Mtanda. Ahsante.

Na. 329

Upungufu Mkubwa wa Walimu Mikoa ya Pembezoni

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa Walimu kwenye Mikoa ya pembezoni na Mkoa wa Rukwa

ukiwa miongoni mwa hiyo Mikoa na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa Walimu katika Jimbo la Kalambo na maeneo mengine ambayo kwa kuzingatia jiografia ya maeneo hayo kwamba, yamepakana na Zambia, Congo DRC na Burundi, inazidi kufanya ugumu wa Walimu, kwenda kwenye maeneo hayo:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa makusudi wa kuziba pengo hilo la walimu hasa kwa kuwapeleka Walimu wenyewe utayari wa kufanya kazi kwenye Mikoa hiyo ya pembezoni, hasa Jimbo la Kalambo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini ikiwemo Jimbo la Kalambo. Pamoja na Changamoto hii Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Elimu, imekuwa ikifanya juhudzi za makusudi za kupunguza tatizo la uhaba wa walimu nchini. Juhudi hizi ni pamoja na kuongeza nafasi za mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu nchini. Aidha, Serikali, imekuwa ikiajiri walimu wote wa mafunzo ya ualimu, kipaumbele kikiwa ni katika Halmashauri za Wilaya zenyeye upungufu mkubwa wa walimu.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, ambapo Jimbo la Kalambo lipo, kwa takwimu za mwaka huu 2012, zinaonesha kuwa, walimu wa shule za msingi waliopo ni 1,984 na upungufu ni walimu 693 na walimu wa Sekondari waliopo ni Walimu 404 na upungufu ni walimu 172. Aidha, nafasi zilizotengwa kwa ajili, ya ajira ya walimu kwa mwaka huu, yaani ajira mpya katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, ni walimu 316 kwa shule za msingi na walimu 86 kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, baada ya ajira ya walimu hawa, upungufu wa walimu katika Halmashauri ya Sumbawanga, utakuwa ni walimu 377 kwa shule za msingi na kwa shule za Sekondari kutakuwa na upungufu wa walimu 86.

Kwa kuwa, idadi ya wahitimu wa mafunzo ya ualimu inaongezeka kila mwaka tena kwa kasi kubwa, ni matumaini ya Serikali kuwa, tatizo la upungufu wa walimu litapungua kwa kiasi kikubwa ifikapo mwaka 2014 na si Kalambo tu, bali Halmashauri nyingi nchini.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri huo upungufu mkubwa na kwa kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya upungufu wa walimu na ufaulu mdogo wa vijana na hasa kwa shule za Sekondari. Pia na kwa kuwa, Wazazi wengi sana wamekuwa wanakatishwa tamaa pale ambapo vijana

wanaokwenda Sekondari, wanaishia kupata *Division 0* na /V. Je, Wizara, inafanya mkakati gani wa makusudi ili isiendelee kuwakatisha tamaa wazazi, kuendelea kuwapeleka watoto kwa kuhakikisha kwamba ufaulu unakuwepo na hasa kwa kupeleka walimu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, katika upungufu huo mkubwa, upungufu zaidi uko kwa walimu wa masomo ya sayansi na kwa kuwa, unasababisha hata ukosefu wa vijana kwenda kijiunga na Vyuo vya Udaktari na hasa kwa sababu kwa Wilaya ya Kalambo tunakuwa na ukosefu mkubwa wa wauguzi. Je, Wizara, iko tayari kuhakikisha kwamba, katika idadi ya wanaopelekwa, walimu wa sayansi wanakuwa wengi zaidi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Halmashauri ya Kalambo au Jimbo la Kalambo, ukiangalia katika *data* tu nimesema kwamba, wanao upungufu wa walimu hao 693. Nikasema kwa mwaka huu tu ajira mpya, ambapo tumefanya upendeleo kwa baadhi ya Halmashauri nyingi zilizoko pembezoni kwamba, tutapeleka walimu 316 kwa shule za msingi na walimu 86 kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *data* hizi, unapata walimu 377 ndio watakuwa wamebakia kwa shule za msingi na walimu 86 tena kwa shule za sekondari. Hali hii nikiwa na maana kwamba, mwaka kesho ambapo ni mwaka wa fedha wa 2013/2014, suala hili la

upungufu wa walimu kwa Halmashauri ya Kalambo litakuwa limemalizika kabisa kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuwaagiza Waheshimiwa Wabunge au kuwaomba kwamba, nimekuwa nikiombwa sana, hata tukitoka hapo nje, tunapokuwa Kantini kule, Waheshimiwa Wabunge wengi, mna matatizo ya Walimu kwenye Halmashauri zenu na hasa ile Mikoa kama ya Shinyanga, Mtwara, Lindi na kule Sumbawanga, sehemu zenye mazingira magumu. Leteni, maombi kwa wale walimu wanaotaka kufanya kazi katika mazingira yale, tunapotoa ajira mpya, tuweze kuwaingiza kwenye listi, ili waweze kuripoti. Maana kumtoa mwalimu Ngara, kumpeleka lleje, unakuta anashindwa, hata nauli yenye we anakuwa hana. Lakini kule kule Ngara, kama akiomba afanyie kazi kwenye mazingira yale, Wizara tuko tayari kusikiliza na kuwaweka kwenye orodha ya walimu hao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, amesema kwamba, tunapopeleka walimu tuzingatie walimu wa masomo ya sayansi. Tumeshaanza mikakati ya kusomesha walimu wa sayansi. Tumeweka *bridging course* zinazofadhiliwa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia kwa fedha za *World Bank*. Tunachukua vijana wa Kidato cha VI, waliofaulu masomo ya Fizikia na Kemia, kuwaweka kwenye mafunzo hayo, ili angalau tuweze kupata walimu wengi wa sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Vyuo Vikuu, tunatoa asilimia mia moja kabisa kwa walimu wa sayansi. Kwa hiyo, tuna uhakika hata katika mwaka huu tunapoajiri,

walimu wa sayansi watakuwa wengi na hata Jimbo la kalambo, litapewa walimu wengi. Ahsante sana.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Naibu Waziri, unakumbuka kwamba, swali la kwanza uliloanza kujibu ulipoteuliwa kuwa Naibu Waziri, ni swali langu, kuhusu walimu na kuhusu wanafunzi wanaoomba kuijunga na ualimu. Kila siku nakufuata mpaka leo, bado naomba, je, kwa vile, taaluma imeshuka sana Longido kwa ajili ya walimu, unaweza sasa kutusaidia wale wanafunzi wote walioomba ualimu wapate nafasi ili waje kusaidia Wilaya ya Longido?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru kwa kuwa na kumbukumbu. Ni kweli, nilipoteuliwa tu na Mheshimiwa Rais, swali la kwanza kujibu hapa Bungeni na nilikuwa najifunza, ni swali la Mzee wangu pale, Lekule Laizer na lilihusu masuala haya haya ya walimu.

Mheshimiwa Spika, napenda tu nijibu kwa ujumla kwamba, kama nilivyosema, Wilaya ya longido na yenye ni Wilaya mojawapo mionganini mwa ambazo walimu wengi wanapopangwa kule, wengine wanaripoti wengine hawaripoti. Wito ni huo huo kwamba, Mheshimiwa Lekule Laizer, hata tukitoka hapa tuonane uniambie, kule kwako, walimu wanaopenda kufanya kazi katika mazingira yale ili Wizara, tunapopanga walimu mwezi Septemba na Oktoba, tuweze kuwaingiza wafanye kazi katika mazingira yale.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la vijana hawa wanaokwenda *TTC* kusomea ualimu, hata kama vijana wa Longido hawakuchaguliwa, si kwamba labda itasababisha upungufu wa walimu kule, la hasha. Vyo hivi ni vya Kitaifa na vijana ambao watatoka Wilaya ya Chunya, watatoka Wilaya ya Ngara, watatoka Wilaya ya Bagamoyo, watatoka sijui Wilaya ya Dodoma, watakwenda kufanya kazi kule na wanafunzi wanaotoka Longido nao wanaweza wakaenda kufanya kazi sehemu nyingine. Kwa hiyo, sio kwamba, utakosa walimu kwa sababu tu, vijana wa Longido hawajachaguliwa kwenda kusoma mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ualimu, ni suala la kitaaluma. Kwa hiyo, kama vijana wako wanakuwa hawajapata zile *points* za kwenda ualimu, tunachelea kusema kwamba, hatuwezi kuwachagua kuingia kusoma Vyo vya Ualimu kwa sababu, ufaulu wao unakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, na kama nilivyosema, Serikali iko katika mikakati ya kuboresha walimu sasa hivi, tunaposema elimu bora ni lazima tuwe na walimu bora. Kwamba, tumeshakataa *point* 28, sasa hivi tuko *point* 27 na mwaka kesho tutakataa *point* 27 tutakwenda kwenye *point* 26. mwaka 2014, tutakataa *point* 26 tunakwenda *point* 25. Nia yetu ni kufuta kabisa *Division IV* kuingia kwenye ualimu.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuiuliza Serikali kwamba,

kumekuwe na utamaduni wa walimu wengi kukawia katika maeneo ya pembezoni kama kule Misenyi na kukataa kwenda. Wakati huo huo walimu hao, wamesoma kwa fedha za Watanzania na wanalipiwa *school fees* na wakati mwingine hawawezi kurejesha pesa hizo. Kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, wale ambao wamepata nafasi wamesoma, waweze kwenda kwenye sehemu hizo na kuwepo mkataba wa namna gani wataweza kurejesha pesa hizo katika maeneo ambayo walimu wengi hawataki kwenda? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, nakosa majibu ya utofauti kwa sababu, suala hili linafanana. Nimesema, kama Halmashauri, ilikuwa na mpango wa kuwasomesha vijana na wamekwenda Vyuio vyta Ualimu na nia yao ilikuwa ni kuja kusaidia kwenye Halmashauri yao, tuwasiliane. Leteni majina hayo tuweze kuwapanga wakasaidie kwenye zile Halmashauri ambako waliwasomesha.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata. Waheshimiwa, tunatakiwa kuingia Wizara ya Ujenzi, lakini kwa sababu moja au nyingine, nafikiri Ofisi yangu imefanya makosa. Swali hili, mnaona mkisoma ni mambo ya afya, lakini kapewa ujenzi. Hivyo hivyo swali la Wizara nyingine utaona wamepewa Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, Maswali Namba 330 na 331 itabidi yaandaliwe tena upya.

Kwa Hiyo, ni kosa limefanyika pale Ofisini kwangu. Kwa hiyo, tunaingia Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini swali litaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis.

(Swali Namba 330 na 331, yaliondolewa na Spika katika Orodha ya Maswali)

Na. 332

Ahadi ya Gari la Kituo cha Polisi, Nungwi

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Waziri, alipokuwa akitoa majibu katika Hotuba yake ya Mambo ya Ndani, alilagusia swali langu. Kwa hivyo, nimeridhika na naomba kuliondoa.

(Swali Namba 332, liliondolewa na Muuliza Swali katika Orodha ya Maswali)

SPIKA: Haya na hilo nalo limeondolewa. Tunaingia Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Dkt. David Malole, atauliza swali hilo.

Na. 333

Uwekezaji Kwenye Viwanda Vidogo na Vikubwa Dodoma

MHE. DAVID M. MALOLE aliuliza:-

Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali, kutokana na ukweli huo, Serikali inaendelea kuboresha

miundombinu mbalimbali kama vile maji, umeme, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa - Msalato, mambo ambayo yanatoa fursa za uwekezaji katika Mji wa Dodoma:-

(a) Je, Serikali, inaweza kutoa ruzuku kidogo kwa wawekezaji wa ndani ili wawekeze kwenye sekta ya Viwanda vikubwa na vidogo Mjini Dodoma?

(b) Je, Serikali, ina mpango gani wa kufufua Viwanda vya *DOWICO*, Kiwanda cha Marumaru cha Zuzu, Kiwanda cha Pepsi na Magodoro Dodoma, ili viweze kutoa ajira na kuongeza pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kabla sijajibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, naomba nimpe pole Mheshimiwa Mbunge, kwa msiba wa Diwani wake maarufu wa Nkhome, John Lesangwa, pole sana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, imekuwa ikitoa fursa ya kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ili kuweza kuwekeza katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwemo Dodoma na si kutoa ruzuku. Serikali, inatoa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa. Aidha, kwa wawekezaji wanaoingia nchini na wale wa ndani,

hupata vivutio kupitia Kituo chetu cha Uwekezaji (*TIC*) na wale wanaowekeza kupitia Mamlaka ya *EPZ*, miundombinu ya barabara na umeme, huboreshwa, ili kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa viwanda nchini, hususan katika Mji wa Dodoma, Serikali, imetenga maeneo maalum kwa ajili, ya viwanda vidogo na vya kati, katika eneo lililoko Kizota (*Western Industrial Area*), eneo kwa ajili ya viwanda vikubwa lililoko Zuzu (*Zuzu Industrial Area*) na eneo kwa ajili, ya mradi wa *EPZ* lililopo karibu na eneo lililotengwa kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato. Vile vile Serikali, imetenga eneo kwa ajili ya viwanda vya kusindika ngozi na bidhaa za ngozi hapa Dodoma.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kufufua au kujenga viwanda vilivyokufa. Serikali ilishajindoa katika ushiriki wa moja kwa moja wa kuanzisha viwanda na kufanya biashara na jukumu hilo imepewa Sekta Binafsi, ambayo kwa sasa ndio injini ya kukuza uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, viwanda alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, vilikufa kutokana na ushindani ulojitokeza baada ya viwanda vipyta kufunguliwa kama vile *Tanganyika Vineyard Company (TAVICO)*, *Central Tanganyika Wine Company (CETAWICO)*, Kiwanda cha Magodoro cha Dodoma asili na vingine. Viwanda kama vile Kiwanda cha Pepsi na Magodoro Dodoma, vilihamishiwa Mikoani Mbeya na Dar-es-Salaam na vinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Wizara yangu, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kufanya utafiti ili kuweza kubaini sababu za Wafanyabiashara, kushindwa kuwekeza katika Mkoa wa Dodoma na kuamua kuhamia Mikoa mingine.

MHE. DAVID M. MALOLE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kunipa pole ya msiba wa Diwani wangu John Lesangu, aliyekuwa Diwani wa Nkhome, katika Jimbo la Bahi. Nashukuru sana kwa pole hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, napenda kusema kwamba, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri, ameahidi kushirikiana na mimi katika kutafuta sababu zinazofanya viwanda kuanza na baadaye tena kuhamia maeneo ya Dar-es-Salaam. Pia kwa vile Serikali, inajitahidi sasa hivi kuweka maeneo mbalimbali ya viwanda, basi nasema kwamba, kwa majibu hayo mazuri, wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini, wameshaelewa na sina swalii la nyongeza. Ahsante sana.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuiuliza Serikali, je, itakuwa tayari mahali ambapo kuna malighafi ambayo inazalishwa nchini, isiruhusu viwanda viendelee kuagiza malighafi hiyo, ili kulinda viwanda vya ndani? Mfano, ni Kiwanda hiki cha Mvinyo ambacho kiko hapa Dodoma, wanaagiza malighafi kutoka nje na kusababisha wakulima wa hapa kushindwa kuuza zabibu zao na kukosa ajira. Je,

Serikali, itakuwa tayari kusaidia malighafi inayozalishwa nchini na isiagizwe kutoka nje?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijajibu swalı la Mheshimiwa Mbunge, naomba nimshukuru sana Mbunge wa Dodoma Mjini na namwombwa atutumie fursa zilizopo ambazo Serikali inaweza kutoa katika maeneo mbalimbali ambayo yametajwa na kuweza kuongeza zaidi na hasa kilimo cha zabibu ambacho na ye ye anashiriki sana.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kujibu swalı la Mheshimiwa Mbunge la nyongeza nasema kwamba, Serikali ipo tayari kabisa kulinda viwanda vy a ndani kwa kutoruhusu bidhaa zingine kuja kuwekeza hapa nchini.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa wawekezaji wengi huenda kuwekeza kwenye mikoa kwa mfano kujenga viwanda kwa sababu ya kuwa na usafiri mwepesi, mfano viwanja vy a ndege. Je, Serikali ina mkakati gani wa Kitaifa kuhakikisha viwanja vy a ndege vy a mikoa ambavyo vilishaanza kukarabatiwa lakini vimeachiwa njiani kukamilika ili wawekezaji wawze kutumia usafiri wa ndege kwenda kuwekeza kwenye mikoa yetu.

SPIKA: Kama Kiwanja cha Dodoma, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu

langu la msingi kwamba, Serikali iko tayari kukarabati hivi Viwanja vya Ndege ambavyo vinakuwa katika mikoa mbalimbali. Kama nilivyosema kwamba, hapa Dodoma Kiwanja cha Dodoma ambacho kinataka kufanywa Kiwanja cha Kimataifa kwenye eneo la Msalato na viwanja vingine mbalimbali kama vile Mbeya, Serikali inaendelea kufanya juhudzi za kuimarisha viwanja hivi na kama vile vidogo vinapanuliwa na kule ambako hakuna vinajengwa kwa ajili ya kuruhusu wafanyabiashara waweze kuwa na usafiri wa uhakika.

MHE. JOELSON L. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kujenga viwanda siyo kufanya biashara na wala siyo kuendesha biashara kama Waziri wa Viwanda ambavyo amekuwa akisema mara kwa mara kwamba kujenga viwanda ni kuendesha biashara. Kwa kuwa nchi nyngi katika viwanda vya kimkakati kwa mfano, ujenzi wa Viwanda vya Kubangua Korosho, ujenzi wa Viwanda vya Nguo na Nyuzi na Viwanda vingine.

Mheshimiwa Spika, nchi zingine zimekuwa zikiamua kwa macho makusudi kujenga viwanda hivi na kisha wanakabidhi sekta binafsi kuendesha. Sasa Watanzania watasubiri mpaka lini hawa wawekezaji binafsi wanaosubiriwa kuja kuwekeza katika viwanda vya mkakati wakati Watanzania wakiteseka kwa kukosa soko la mazao yao kutokana na mazao yao kutokuongezwa thamani? Sasa Waziri atueleze ni lini sasa tutaendelea kusubiri badala ya Serikali kuingilia kati na kujenga viwanda hivyo vya kimkakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu kwa kifupi maana yake swali la nyongeza lilikuwa kama hotuba hivi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali kwa kiasi fulani imejitoa katika ujenzi wa viwanda, bali inahamasisha sekta binafsi ziweze kujenga viwanda. Serikali kwa ujumla imejitoa haifanyi biashara wala hajengi viwanda ila inahamasisha sekta binafsi kujenga viwanda ambavyo ni vya maendeleo ya nchi yetu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hatuwezi kuendelea tu tukawa na maswali ya nyongeza mpaka 20. Muda umekwisha na leo naona nina wageni wengi, ndiyo na nyie mnaona. Wageni walio katika ukumbi wetu leo nakwenda kuwatambua hapa.

Kwanza nina wageni wa Mheshimiwa Spika, hawa ni Makamishina wa Watumishi wa Bunge la Malawi, ambao ni Naibu Spika wa pili na kiongozi wa msafara, Mheshimiwa Juliana Mpande, can you raise up, thank you. Mheshimiwa Alfred Mwechumu, Mheshimiwa Akimu Mwanza, Mheshimiwa Watson Makala Ngozu, Mheshimiwa Profesa Eta Banda, Mheshimiwa Christina Chiwoko, Ndugu Renard Mapemba, Ndugu Leornad Mengezi, ndugu Harvey Chigumula na yuko ndugu Tamika Nyirenda yeye ndiye afisa, hawa wawili ndugu Harvey Chigumula and Tamika Nyirenda ni watumishi wa Bunge kule. Tunawakaribisheni sana, tumefurahi kuja kututembelea, nadhani Mheshimiwa Spika kule hajambo. Ndiyo aliyekuwa ameniambia, kwa hiyo

wageni hawa watakuwa pamoja na Naibu Spika kipindi chote. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Bernad Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambao ni mke wake mpenda Bi. Dorcas Membe na yuko Bi. Esther Membe yeye ni dada wa Mheshimiwa na bwana Stephen Membe, mdogo wa Mheshimiwa na familia yake. (*Makofi*)

Pia tuna wageni mahususi, yupo Mheshimiwa Dkt. Asha Rose Migiro, ambaye alikuwa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa. Ahsante sana, sasa hivi amerudi nyumbani na siku ya Jumamosi tulipata nafasi ya kuwa naye na atakuwepo hapa kushiriki katika Wizara hii. Kwa hiyo, ujuzi aliopewa tunaweza sisi kwa wakati mmoja au mwagine tukafaidika nao. Karibu sana. (*Makofi*)

Halafu tuna mgeni mwagine Meja Gen. Mathew Kisamba, huyu yuko kule Darfur ni Mkuu wa Kamandi ya Majeshi ya *UNAMID* Darfur, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao Mabalozi wanaowakilisha kanda zao (*Regional Deans*), hawa ni balozi Mheshimiwa Balozi Juma Halfan Mpango, yeye ni Balozi wa DRC, lakini ndiyo *Dean* katika Africa *Regional*, karibu sana, ahsante. Pia tuna Mheshimiwa Balozi Ibrahimu Mukundi, huyu wa Uganda, Mheshimiwa Balozi karibu sana tumefurahi sana kuwa na wewe hapa kwetu. (*Makofi*)

Sasa kuna Viongozi Wakuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni Mheshimiwa John

Haule Katibu Mkuu na Mheshimiwa Balozi Rajab Gamaha, Naibu Katibu Mkuu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao Wakurugenzi wapya ambao pia ni Mabalozi; yupo Balozi Dora Msechu, Idara ya Ulaya na Amerika, ahsante sana na hongera sana. Kuna balozi Bertha Samson, Idara ya *Diaspora*, ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunaye Balozi Simba, Idara ya Mashariki ya Kati, ahsante. Tunaye Balozi Irene Kasyanju, Kitengo cha Sheria, ahsante sana. Tunaye Balozi Mbelwa Kairuki, Idara ya Asia na Australia na yuko Balozi Celestine Mushi, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa. (*Makofi*)

Vile vile wako Mabalozi wengine ambao wanawakilisha nchi zao, hawa ni Mabalozi wa nchi za jirani, yuko Mheshimiwa Balozi Patrick Kisere Balozi wa Tanzania Malawi, yeye huyu atakuwa pia ameongozana na wale Makamishina wa kutoka Malawi. Yupo Mheshimiwa Balozi Joram Buswaro, Balozi wa Tanzania, Ethiopia; huyu Buswaro ni wa kwetu lakini yuko kule, karibu sana. (*Makofi*)

Balozi Buswaro yeye ni Balozi wa Tanzania Ethiopia na pia Umoja wa Afrika umeambana na wanafunzi wanne na walimu wawili wa Kiswahili kutoka Addis Ababa, Ethiopia nao hawa ni Elizabeth Magohiya Mwaikunda Mtenda walimu hawa maarufu wasimame ahsante sana. Wapo na wanafunzi Haleluya Abella, Suzanne Nyinawandoli, Caroline Okello na Marie-Goretti Harakeye. Kwa hiyo, wanafunzi wote akina

dada maana yake wanataka kuchukua Kiswahili hasa.
(Makofi)

Kuna wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara yupo; Mheshimiwa Balozi Mohamed Maundi, Mkurugenzi wa Chuo cha Diplomasia, Mheshimiwa Elishilia D. Kaaya, Mkurugenzi Mkuu AIC, ahsante sana. Yupo Bi. Rehema Twalib, Katibu Mtendaji wa APRM. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Wenje ndiye Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambaye huyu mgeni wake ni mke wake mpandwa kabisa, Bi. Flora Wenje, yuko wapi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Mama Fatuma Karume ambaye ni mdhamini wa *club* ya Yanga, naona bado yupo sijui inawezekanaje, yeye Mama Fatuma Karume ni mdhamini wa *club* ya Yanga ameambana na viongozi wa timu hiyo ambao ni Francis Kifukwe, Yusuf Manji, nasikia Yusuf Manji ndiye Mwenyekiti, Clement Sanga, Abdallah Bin Kleib, hawakuandika vyeo vyao. Pamoja kuna wachezaji wa timu hiyo, nataka kuwaambia wenzenu wapo hapa ndani, naomba wachezaji wote wa Yanga wasimame walipo. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa hawa ndiyo mabingwa, ndiyo timu bingwa ya *Young African* ni bingwa wa Kombe la Kagame mwaka 2012. *(Makofi/ Vigelegele)*

Sasa ndugu mmoja ananiuliza kwamba hawa Yanga wamevunja kanuni kuja hapa, ukisoma kanuni ya kutambulisha wageni na wageni maarufu walioleta kitu maarufu kwa nchi. (*Kicheko/Makofi*)

Basi Mheshimiwa Spika analetewa vitu vizuri anatangaza, sasa nikishatangaza hivyo wanasema mimi Yanga, kesho nikitangaza Simba watasema Simba na Simba leteni vitu vyenu nitatangaza tu hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika mstaafu yuko kimya kabisa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa.

MBUNGE FULANI: Tano bila.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 55 na walimu wao kutoka shule ya sekondari Azimio ya Dodoma, wanafunzi wa walimu wa Azimio naomba msimame mlipo, ahsante sana. Mnatakiwa kusoma kwa bidii. (*Makofi*)

Halafu nina Madiwani 40 kutoka Majimbo ya Mtama na Mchinga ambao wanaongozwa na Mwenyekiti Mathew Makwinya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo ya Lindi Vijijini, Mheshimiwa Abdu Makwita. Naomba Waheshimiwa Madiwani wasimame popote walipo, ahsante sana. Tunaomba mkashirikiane katika kufanya maendeleo katika eneo lenu. Maeneo yenu sasa hivi yana baraka kubwa

sana ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, muitumie vizuri Waheshimiwa Madiwani, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni 12 kutoka Shirika la Kitawa la Ndugu Wadogo Wakapuchini wenyewe makazi yao Miyuji Dodoma wakiongozwa na ndugu Leandry Kimaryo. Hawa watawa wako wapi, hawa watawa wa kiume karibuni sana. (*Makofi*)

Kuna wanachama 13 kutoka Muheza *Development Trust Fund* kutoka Tanga, wasimame walipo, ahsante sana. Tunaomba mfanye kazi vizuri zaidi. (*Makofi*)

Watumishi 13 kutoka Shirika la Hifadhi la Ngorongoro la Arusha, hao watumishi wa Ngorongoro wako wapi, ahsante sana. Tunaomba mwendelee kuilinda nchi yetu kwa ustadi zaidi. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Mkosamali ambao ni Padri Bonventure Kamuli na Patrobus Pascal, naomba msimame, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Luhanga Mpina ambao ni Wenyeviti wa Halmashauri mbalimbali kutoka Mikoa ya Kanda ya ziwa, hawa Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri wasimame popote walipo, kama wamekosa nafasi basi watacaa baadaye. (*Makofi*)

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Titus Kamani kutoka *Global Peace Network* ya Canada hawa ni Dkt.

Brian Budgell, mjumbe wa Bodi. *Then* tunaye Dkt. Joseph Lupande, Mwakilishi wa Tanzania na yuko ndugu Kahema Mawe, Mwakilishi wa *DMO*, Magu, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Saidi Mtanda ambao ni babu yake Mheshimiwa Said Mtanda anaitwa Mzee Said Abdallah Mtepo, ahsante sana. Yupo Katibu wa Mbunge na Msaidizi wa Katibu wa Mbunge hawa wawili wasimame walipo. Halafu yupo Diwani mstaafu Mohamed Kungwacha, ahsante sana. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Naibu Waziri Kivuli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mambo ya Nje ambao ni wadogo zake ni Hawa Mohammed, Misbah Mohammed, Suheil Mohammed, hawa ni wageni wake Mheshimiwa Raya. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo na hawa nimewapa ruhusa maalum, saa 5.00 asubuhi wakafanye kikao katika chumba namba 231.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa John P. Lwanji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa Msekwa B.

Mheshimiwa Zungu anasema niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha Jumuiya ya Madola (CPA), Tawi la Tanzania kwamba leo saa 7.15 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa Msekwa C.

Waheshimiwa Wabunge, tumetumia muda mwingi sana inabidi tuingie kwenye kazi. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnapotoka mnatakiwa kutoka kwa staha na kimya.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza kwa umahiri mkubwa Bunge hili la Bajeti la mwaka 2012/2013. Napenda pia kuwapongeza

Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wanaokusaidia kuongoza Bunge hili kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Chini ya uongozi wake Taifa letu limeendeleza utamaduni wetu wa kudumisha amani, utulivu na mshikamano. Nawaomba Watanzania wote tuendelee kudumisha hali hiyo ili kuimarisha umoja wetu ambao ni tunu isiyopatikana kwa bei yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine wote walionitangulia kuwapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wapya, Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Mei 2012. Nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge waliochaguliwa kipindi hiki kutokana na mabadiliko yaliyotokea kwenye nafasi mbalimbali humu Bungeni na ndani ya Serikali. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya kipekee kabisa, niruhusu niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge lako Tukufu kuiwakilisha Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Wizara yangu kwa kuwa ndiyo inayosimamia masuala yote ya

mambo ya nje, nawaahidi Waheshimiwa Wabunge ushirikiano wangu binafsi na ule wa Wizara nzima kwa kufanya kazi kwa karibu na kushirikiana na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa William A. Mgimwa, Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba zao za kina ambazo zimetoa ufanuzi na miongozo kwa masuala mbalimbali muhimu ya Taifa letu kwa mwaka wa fedha 2012/2013. (*Makof*)

Kwa ujumla wake, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha bajeti zao kwa kazi nzuri walizozifanya. Hotuba zao zote zimefafanua kwa kina masuala ya uchumi, siasa na jamii yanayohusu nchi yetu na hivyo kuigusa pia Wizara yangu kwa njia moja au nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati na za uongozi mzima wa Wizara kwa Kamati ya Bunge ya kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (*NUU*), chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati kwa ushauri wao mzuri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara kwa Wizara yangu. Kamati hii imetoa mchango mkubwa sana katika kuiwezesha Wizara kukabiliana na changamoto zinazoikibili katika kutekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naamini ziara walizozifanya kwenye nchi mbalimbali kutembelea Balozi zetu zimewapa fursa ya kujionea wenyewe na kusikia kutoka kwa maafisa wetu changamoto mbalimbali zinazotukabili kama Wizara. Aidha, kwa ujumla, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao wanayoitoa Bungeni katika kuishauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi maalum kwa Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vilevile, nawapongeza na kuwashukuru Bwana John M. Haule, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Balozi Rajabu H. Gamaha, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozi na wafanyakazi wote kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kuiongoza Wizara hii. Pamoja na kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao, nawashukuru kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kutetea maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ziwaendee wananchi na viongozi wa Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Lindi na hasa Wanamtama wote. Napenda pia nimshukuru mke wangu Mrs. Membe na watoto wangu kwa upendo na uvumilivu waliouonesha kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kueleza kwa kina kuhusu hotuba yangu, niruhusu niungane na

Viongozi wote, Wazanzibari na Watanzania kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote waliopoteza ndugu zao kwenye ajali ya meli ya *M.V. Skagit* iliyotokea Zanzibar. Kwa wale wote walioumia na wanaoendelea kuijuguza, namwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu waweze kupona haraka.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki nisipowapongeza mabalozi wa soka nchini wana Yanga ambao wametuletea heshima na kombe kubwa la hii ni heshima kubwa kwa taifa letu kwa kushinda kombe la Kagame. Nimefarijika kwamba wamekuja leo kwa shabiki mwenzao wakati ninapowasilisha taarifa yangu na ripoti yangu ya Bunge leo. Karibuni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa salamu za pole kwa wale Wabunge wote waliopatwa na misiba ya wapendwa wao. Kwa wote, namwomba Mwenyezi Mungu awape faraja na azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda naomba *Hansard* ichukue hotuba yote kama ilivyo na sasa itifaki yote imezingatiwa, nlende kwenye hali ya dunia.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya dunia kwa kipindi cha mwaka 2011/2012. Hali ya dunia. Ulaya na Marekani. Kwa ujumla, hali ya dunia kiuchumi, kisiasa na kijamii katika mwaka wa fedha 2011/2012 imekuwa ya mashaka makubwa na hivyo kuathiri utulivu katika nchi nyingi duniani. Hali hiyo imechochewa na

mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, eneo la Ulaya limeathirika sana kiuchumi kutokana na madeni pamoja na mdororo wa uchumi ulioikumba dunia katika kipindi cha mwaka 2008. Hali hii pia iliathiri kwa kiasi kikubwa sarafu ya Euro, uchumi wa nchi zilizo katika ukanda wa sarafu hiyo ujulikanao kama *Eurozone* pamoja na nchi ambazo zinafanya biashara na nchi za Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imechangia kwa kiwango kikubwa Viongozi katika baadhi ya nchi hizo kama vile; Ufaransa, Ugiriki, Italia, Hispania na Ireland kushindwa katika Chaguzi Kuu au kushinikizwa kujiuzulu. Kwa upande wa Marekani nayo ilikumbwa na misukosuko ya uchumi iliyosababishwa pia na mdororo wa uchumi wa mwaka 2008. Hata hivyo, uchumi wake umeanza kutengemaa baada ya mdororo huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mdororo huo, nchi hizo zimelazimika kuchukua hatua kadhaa kunusuru uchumi wao ikiwa ni pamoja na kubana matumizi, kukopa zaidi ili kuwekeza katika sekta zenye kutoa ajira na kupunguza kutoa misaada kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania kulingana na ahadi zao za awali. Kuna kila kiashiria kuwa uchumi wa Ulaya na Marekani hautapata utulivu kwa muda mrefu na hivyo uwezo wao wa kutoa misaada kupungua kadiri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Balozi zetu za nje zinaendelea kufuatilia kwa makini hali ya uchumi inavyoendelea duniani na kuishauri Serikali kutekeleza mikakati ya kukabiliana na changamoto zitokanazo na hali hiyo ili kuimarisha uchumi wa Taifa letu na kuondokana na utegemezi.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mashariki ya Kati bado liko katika hali ya tahadhari. Nchini Syria hali imeendelea kuwa tete kutokana na mapigano yanayoendelea nchini humo ambako waasi wanapigana dhidi ya Serikali ya Rais Bashar al-Assad tangu Januari mwaka 2011 na tayari wameshaingia kwenye Mji Mkuu wa Nchi hiyo. Umoja wa Mataifa na Jumuiya ya Nchi za Kiarabu (*Arab League*) zikiongozwa na Msuluhishi wa Mgogoro huo, Dkt. Kofi Annan wameshindwa hadi sasa kufanikisha kusitishwa kwa mapigano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limegawanyika ambapo wajumbe wa kudumu wenyewe kura ya turufu wametofautiana juu ya uamuzi wa kuchukua hatua za kijeshi dhidi ya Serikali ya Syria. Tanzania inaunga mkono jitihada za Msuluhishi Kofi Annan na kuwaomba wadau wote kutoingilia na kushinikiza matakwa yao nchini Syria na badala yake kumuunga mkono Msuluhishi ili kumaliza mgogoro huo kwa njia ya amani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuendelea kukua kwa uhasama baina ya Iran na nchi za Magharibi kunaleta changamoto ya ustawi wa amani katika ukanda huo. Uhasama huo unaletwa na hofu kuwa nchi ya Iran

inarutubisha madini ya urani yanayotumika kutengeneza silaha za nyuklia. Tayari, Iran imewekewa vikwazo vyta kiuchumi na Marekani ikishirikiana na nchi za Umoja wa Ulaya. Iran nayo imetishia kujibu mapigo kwa kufunga mlango wa Bahari ya Hormuz ambao hupitisha asilimia ishirini 20 ya mafuta yote ulimwenguni. Iwapo Iran itatekeleza uamuzi huo inaweza kuzusha vita ambayo italeta madhara makubwa kwa uchumi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya mtafaruku baina ya Iran na nchi za Magharibi inaathiri pia mustakabali wa ukanda mzima wa Mashariki ya Kati kwa kuwa Iran ina ushawishi mkubwa kwenye siasa za nchi nyingine zenye machafuko kama vile Syria. Kuendelea kwa migogoro na machafuko katika ukanda wa Mashariki ya Kati kunaathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa dunia kwa sababu asilimia kubwa ya mafuta yanayotumika duniani hutoka katika ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, habari njema ni kwamba tayari Irani, Marekani, Nchi za Ulaya pamoja na wadau wengine wameshakubaliana kurejea kwenye meza ya mazungumzo na tayari mzunguko wa kwanza wa mazungumzo haya umeshafanyika. Imani yetu kama nchi ni kwamba wahusika wote kwenye mazungumzo hayo wataonesha utashi wa kweli wa kumaliza tatizo hilo kwa njia ya mazungumzo na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashariki ya Mbali hali ni tulivu ukiachilia majanga ya asili yaliyozikumba nchi za Japan, Ufilipino na Thailand na

kusababisha athari za kijamii na kiuchumi kwa baadhi ya sekta, hususan viwanda na makazi ya watu. Hali ya kiusalama katika Peninsula ya Korea nayo imeonekana kutulia kidogo kufuatia mabadiliko ya uongozi nchini Korea Kaskazini baada ya kifo cha Rais Kim Jong-il aliyekuwa Rais wa Korea Kaskazini. Aidha, kwa upande wa Japan, hali ya kiuchumi imeanza kuimarika hasa baada ya kukumbwa na tukio la Tsunami la mwaka 2011 lilieloathiri kwa kiasi kikubwa kinu cha nyuklia cha Fukushima.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye maeneo mengine duniani, Bara la Afrika nalo limeathiriwa na hali ya mitikisiko ya aina mbalimbali duniani, ikiwemo ya kiuchumi, kisasa na kijamii. Maendeleo ya Bara hili yameendelea kukabiliwa na changamoto za kiusalama, kisasa, kiuchumi, kijamii, mabadiliko ya tabianchi, vitisho vya ugaidi, uharamia wa baharini, kupanda kwa gharama za bidhaa muhimu kama vile chakula, matatizo ya nishati ya umeme na kukosekana kwa ajira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala hayo ya jumla, yapo baadhi ya masuala ambayo yanaweza yakaipambanua hali ya Barani Afrika kwa sasa, hasa katika kipindi hiki cha miezi sita iliyopita. Aidha, kuna masuala yanayozigusa baadhi ya nchi kama inavyoelezwa hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Uongozi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Suala kubwa liliotawala hali ya kidiplomasia Barani Afrika ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012 ni uchaguzi wa Mwenyekiti wa

Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Kama itakavyokumbukwa, uchaguzi huo ulipangwa kufanyika mwezi Januari, 2012 wakati wa Mkutano wa 18 wa Umoja wa Afrika wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushindani mkali ulizuka kati ya wagombea wawili waliojitokeza kuwania nafasi hiyo ambao ni Bwana Jean Ping wa Gabon, Mwenyekiti wa Kamisheni aliyemaliza muda wake na Bibi Nkosazana Dlamini-Zuma, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Afrika Kusini. Mvutano huo ulisababisha Wakuu wa Nchi kushindwa kumchagua Mwenyekiti mpya wa Kamisheni hiyo baada ya wagombea wote wawili kushindwa kufikia theluthi mbili za kura zinazohitajika kisheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukosekana mshindi, Wakuu wa Nchi na Serikali waliamua kuahirisha uchaguzi huo hadi kwenye mkutano wao wa 19 uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Julai 2012. Katika uchaguzi huo, Bibi Nkosazana Dlamini-Zuma, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Afrika Kusini, alifanikiwa kuibuka mshindi.

Hivyo, Mama Zuma anakuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Kamisheni hiyo. Ushindi wa Bi. Nkosazana Zuma ni ushindi wetu pia kwa kuwa alikuwa ni mgombea wa *SADC* na Tanzania ilishiriki kikamilifu katika kampeni zake.

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Misri ilishuhu na matokeo ya machafuko yaliyopelekea kuangushwa kwa utawala wa aliyekuwa Rais wa nchi

hiyo, Mheshimiwa Hosni Mubarak. Baada ya utawala wa Mpito ulioongozwa na Jeshi la nchi hiyo, hatimaye Chama chenye mlengo wa kushoto cha Udugu wa Kiislam (*Muslim Brotherhood*) kimefanikiwa kushinda uchaguzi huru uliofanyika Juni, 2012 kupitia mgombea wake Mheshimiwa Dkt. Mohammed Mursi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashirikiana na Serikali mpya na kuendeleza mahusiano mazuri baina ya nchi zetu mbili ikizingatiwa kuwa Misri ni mdau muhimu katika kufanikisha matumizi ya rasilimali za Bonde la Mto Nile kwa maslahi ya pande zote husika.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kutambua kuwa ingawa uchaguzi umefanyika bado hali ya kisiasa ni tete. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa *Muslim Brotherhood* wameshinda kwa kuwa na Wabunge wengi Bungeni na kushika lkulu, bado Jeshi la Misri linaendelea kushika hatamu za uongozi. Jeshi limevunja Bunge na ndilo linalofanya maamuzi makubwa.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba hali hiyo tete ya kisiasa itatengemaa na hali kuwa nzuri. Tanzania itashirikiana na Serikali mpya ya Misri ili kuendeleza na kudumisha mahusiano yetu ya kirafiki na ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, baada ya aliyekuwa Kiongozi wa Libya Kanali Muammar Qaddafi kuuawa na Serikali yake kupinduliwa na wapinzani wa *NTC*, Libya ilikumbwa na matatizo ya usalama. Mauaji ya Walibya weusi yaliendelea. Hakukuwa na Serikali madhubuti,

hakukuwa na Bunge na wala hakukuwa na taasisi za Kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tulilaani mauaji ya Kiongozi huyo na tulisema kuwa tungaitambua Serikali ya NTC tu iwapo ingekuwa na viongozi wa kuchaguliwa, Bunge, Mahakama na uundwaji wa Serikali ya mpito ambayo itajumuisha wadau kutoka vyama vyote vyaa siasa.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa kwanza wa Kidemokrasia ulifanyika Libya mwezi Julai, 2012 kuchagua Wabunge 200. Waombaji 3,000 walijitokeza kugombea nafasi hizo. Pamoja na matatizo yote ya kiusalama, wananchi milioni moja na laki nane waliweza kuchagua Wabunge wao 200 na Bunge linategemewa kumchagua Rais na Waziri Mkuu katika kipindi cha siku 30 baada ya uchaguzi. Zoezi hilo limekamilika. Aidha, Bunge limechagua kutoka mionganini mwao Wabunge 60 wa kuunda Baraza la kuandika Katiba mpya, na Baraza hilo limepewa siku 120 kuwakilisha mapendekezo ya Katiba kwenye Bunge lao. Mchakato huo umeanza.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Serikali ya Libya umekutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete mjini Addis Ababa tarehe 15 Julai, 2012 na ukaeleza nia yake ya kutuma ujumbe Tanzania kuja kutoa taarifa ya hali ya usalama na kisiasa na kufufua rasmi mahusiano ya Kibalozi na Tanzania. Tunausubiri ujumbe huo na sisi sasa tumeridhika na mchakato wa kujenga demokrasia unaoendelea nchini Libya. Tunategemea kuletewa

hati za Balozi mpya hivi karibuni na tutazipokea ili tuweze kurejesha huduma za Kibalozi kama ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa na kiusalama nchini Somalia kwa sasa inatia matumaini ya kupatikana kwa amani kutokana na juhudini za Umoja wa Afrika pamoja na washirika wake katika kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa muda mrefu wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mpito ya Somalia inatarajiwa kumaliza muda wake mwezi huu Agosti, 2012 na tayari rasimu ya Katiba kwa ajili ya Serikali mpya imeandaliwa na inatarajiwa kupitiwa na Baraza la Katiba linalojumuisha Wazee kutoka Koo zote tarehe 20 Agosti 2012. Kupatikana kwa Serikali mpya ambayo uhalali wake utatokana na wananchi wenyewe inatazamiwa kutoa fursa kwa Wasomali kujenga mustakabali mpya wa Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika mji wa Mogadishu sasa ni ya kuridhisha kutokana na jitihada za majeshi ya *AMISOM* na yale ya Kenya kudhibiti maeneo na miji muhimu iliyokuwa ngome ya Al-Shabaab. Pamoja na kuwa wamedhibitiwa, Al-Shabaab wameendelea kufanya matukio machache nchini Kenya ikiwa ni njia ya kulipiza kisasi. Hali hiyo imeleta hofu kwa watalii na wageni kutoka nje wanaotembelea ukanda wa Afrika Mashariki. Serikali zetu zinashirikiana kwa karibu katika kuimarisha usalama dhidi ya vitendo vya uharamia vya Al-Shabaab.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, hali ya usalama katika pwani ya Bahari ya Hindi na Ghuba ya Aden nayo inazidi kuimarika na matukio ya uharamia kupungua kutokana na operesheni inayoendelea kati ya nchi za pwani ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya. Katika mwaka 2011/2012 peke yake, Jeshi la Wananchi liliweza kudhibiti matukio 27 ya uharamia.

Mheshimiwa Spika, tuungane kulipongeza jeshi letu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Tunachukua jitihada za makusudi kulisaidia jeshi letu kupata vifaa madhubuti kwa ajili ya ulinzi wa pwani yetu ambayo ina utajiri mkubwa wa gesi asilia dhidi ya maharamia hawa.

Mheshimiwa Spika, Ukanda wa Maziwa Makuu; hali ya usalama mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Ukanda wa Maziwa Makuu kwa ujumla nayo iko tete hata baada ya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ulimalizika na Rais Joseph Kabila kutangazwa mshindi dhidi ya mpinzani wake mkuu Bw. Etienne Tshisekedi. Mapigano yameripotiwa kutokea hivi karibuni tarehe 6 Julai, 2012 Kaskazini Mashariki mwa *DRC*.

Mheshimiwa Spika, kikundi cha waasi kijulikanacho kama *M23* kinachosemekana kinaongozwa na Jenerali Bosco Ntaganda anayesakwa na Jumuiya ya Kimataifa kwa tuhuma za uhalifu wa kivita kujibu tuhuma mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (*ICC*) kinadaiwa kuhusika na mapigano hayo.

Mheshimiwa Spika, kikundi hicho kinasadikiwa kuyateka na kuyadhibiti baadhi ya maeneo ya Mashariki ya *DRC* yakiwemo Rutshuru, Bunagana na Kivu. Majeshi ya Umoja wa Mataifa yameingilia kati kwa kutoa ulinzi katika mji wa Goma, na tarehe 25 Julai, 2012 yalilazimika kutumia silaha kuwasambaratisha *M23* kutoka kwenye maeneo wanayoyashikilia. *M23* ni Machi tarehe 23 siku ambayo Majeshi ya Lawrent Nkunda yalivyoanza kazi ya kuipinga Serikali ya Jamhuri ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, katika kikao chao tarehe 14 Julai, 2012 waliuomba Umoja wa Mataifa kuongeza wanajeshi wa kulinda amani kwa lengo la kudhibiti usalama wa mpaka kati ya *DRC* na Rwanda ili kurejesha hali ya kuaminiana baina ya nchi hizi mbili. Vilevile, walikubaliana kufufua mpango wa usuluuhishi uliokuwa chini ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais Mstaafu wa Tanzania na Mheshimiwa Olesegum Obasanjo, Rais Mstaafu wa Nigeria.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya kisasa na kiusalama nchini *DRC* kwa kuwa machafuko hayo yanatuathiri kiuchumi, kisasa, kijamii na kiusalama. Ni kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete atahudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu utakaofanyika Kampala nchini Uganda kesho tarehe 7 Agosti, 2012 kujadili suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetekeleza jukumu la uratibu

wa masuala ya ushirikiano wa kikanda kwa kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Ushirikiano ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (*IOR-ARC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Kwa kuwa eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki limeelezewa vizuri na Waziri husika kwenye hotuba ya bajeti yake, niruhusu nidurusu masuala machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Uenyekiti wa Tanzania katika Kamati ya Utatu ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC*. Mnamo mwezi Agosti, 2011 Tanzania iliteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC*. Kutokana na uteuzi huo, Tanzania imeingia katika Kamati hiyo ya Utatu (Troika) ambayo kwa sasa inaongozwa na nchi ya Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, ifikapo tarehe 17 Agosti, 2012 Tanzania itatwaa rasmi Uenyekiti wa Asasi hiyo muhimu ya *SADC* ambayo itaipa jukumu la kusimamia, kufuatilia na kushiriki kwa kina katika masuala yote ya siasa, ulinzi na usalama ya Nchi za *SADC*, hususan katika nchi za Madagascar na Zimbabwe ambazo ziko kwenye agenda ya *SADC* Troika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012-2015/2016. Wizara yangu imeendelea kupata mgao kidogo sana wa bajeti isiyokidhi mahitaji katika mwaka wa fedha 2011/2012. Katika kipindi tajwa, Wizara yangu ilipata asilimia 44 tu ya Bajeti iliyoombwa. Bajeti ndogo tunayopewa

imekuwa changamoto kubwa katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kiwango kinachostahiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na mapungufu hayo, Wizara yangu kwa nafasi yake kama kiungo muhimu cha nchi yetu na nchi za nje imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na sekta binafsi kuhakikisha kwamba nchi yetu inafaidika kwa kadri iwezekanavyo na fursa mbalimbali zenyen manufaa kwa nchi yetu katika sekta za uchumi na jamii.

Mheshimiwa Spika, juhudi zetu katika kutafuta fursa hizo zilizingatia vipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016. Niruhusu nitumie fursa hii kueleza kwa uchache mchango wa Wizara yangu kwenye sekta mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango huo wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya nishati, Wizara yangu kupitia Ubalozi wetu nchini China imeshirikiana bega kwa bega na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata mkopo wa Dola za Marekani bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Kama ilivyokwishaelezwa na Waziri wa Fedha hapa Bungeni, tayari mkataba wa kupata fedha hizo umekwisainiwa na Mheshimiwa Philip Marmo, Balozi wetu nchini China kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa ujenzi wa Bomba hilo ulifanyika tarehe 21 Julai, 2012 Mkoani Mtwara. Ujenzi wa bomba hilo utaleta mapinduzi makubwa sana katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi. Bomba la zamani lilikuwa dogo na lisilokidhi mahitaji ya kusafirisha kiasi kikubwa cha gesi kwenda Dar es Salaam. Pindi ujenzi wa bomba hilo utakapokamilika fursa nyingi za uchumi zitafunguka na kuimarika hasa zile zote zinazotumia gesi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia ilikuwa mstari wa mbele katika kuishawishi Tume ya Uhifadhi Duniani (*World Heritage Commission-WHC*) na Jumuiya ya Kimataifa kukubali kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Selous ili kuruhusu uchimbaji wa madini ya urani kufanyika kusini mwa hifadhi hiyo. Juhudi zetu zimezaa matunda ambapo mwezi Juni, 2012 *WHC* wameridhia hoja zetu, jambo ambalo huwa si rahisi kufanywa na Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushindi huu ni kielelezo cha nguvu ya ushawishi wetu na kuaminika kwetu duniani. Matarajio yetu ni kwamba Kampuni ya *Uranium One* kutoka Urusi itaanza kazi ya utafiti na hatimaye uchimbaji muda si mrefu mara baada ya kukamilisha taratibu zingine na Wizara husika za Maliasili na Utalii na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hofu za msingi juu ya usalama wa uchimbaji wa madini hayo, Wizara yangu imetoea pia msukumo katika upatikanaji wa wataalam na mafunzo na hivi karibuni Timu ya Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini

imekwenda Nchini Australia na Namibia kujifunza namna ya kuendesha miradi ya urani. Tanzania itatumia nafasi yake ya Ujumbe wa Bodi ya Shirika la Atomiki Duniani (*IAEA*) kupata kila aina ya utaalami na uzoefu kuhakikisha kuwa uchimbaji wa madini hayo unafuata taratibu na viwango vyta kiusalama vinavyotolewa na *IAEA*.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Wizara yangu kuufufua mradi wa umeme wa *Stiglers Gorge* nazo zinaanza kuzaa matumaini. Kufuatia jitihada za Wizara yangu, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu walifanya Ziara nchini Brazil ambapo agenda ya mradi wa *Stiegler's Gorge* ilipewa kipaumbele kikuu. Kutokana na ziara hizo, Kampuni ya Brazil ya *ODEBRECHT* na Shirika la *RUBADA* kwa upande wa Tanzania wameshasaini Makubaliano ya Awali (*MoU*) kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi wa uzalishaji wa umeme ambao unakadiriwa utazalisha zaidi ya megawati 2,100 za umeme wa uhakika na wa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kufuatilia ili kuhakikisha Wataalam wanaotakiwa kuja tena nchini kwa ajili kufanya mapitio ya taarifa ya *environmental impact assessment (EIA)* na upembuzi yakini fu wanafanya hivyo ili mradi huo uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Kilimo, Wizara yangu imeshirikiana kwa karibu na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika kufanikisha upatikanaji wa teknolojia ya umwagiliaji kutoka nchini India chini ya makubaliano ya Mpango wa Maendeleo wa India-Afrika. Makubaliano mahsusii haya ya

ushirikiano baina ya nchi zetu mbili yanayotokana na ziara ya Rais wa India hapa nchini mapema mwezi Februari 2012.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara yangu ilishiriki na kushuhudia utiaji saini wa Makubaliano ya Awali kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya *Jain Irrigation* ya India mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kutekeleza kwa pamoja miradi ya umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Wizara yangu pia imeendelea kuishawishi Serikali ya India kutupatia mkopo kwa ajili ya awamu ya pili ya mradi wa Matrekta. Matumaini yetu ni kwamba juhudii hiso zitazaa matunda katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshiriki katika kufanikisha ushiriki wa nchi yetu katika Mkutano wa nchi Tajiri na zenyeye Viwanda vikubwa duniani zinazojulikana kama *G8* uliyofanyika nchini Marekani. Mkutano huo ulikuwa na mafanikio makubwa kwa sekta ya kilimo nchini baada ya mataifa hayo kutoa ahadi ya Dola za Marekani milioni 890.

Mheshimiwa Spika, aidha, makampuni binafsi ya nchi hiso yaliahidi kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani bilioni 3 katika sekta ya kilimo. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu itaelekeza nguvu zake kuvutia wawekezaji kutoka nchi za Japan, Korea Kusini na China kuwekeza katika Ukanda wa Kusini wa *SAGCOT* na vilevile kuanzisha kanda nyinginezo za kilimo magharibi, kaskazini na mashariki mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Miundombinu, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi katika kutafuta misaada na mikopo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu kupitia Ubalozi wetu Japan, iliweza kuishawishi Serikali ya Japan kugharamia upanuzi wa barabara ya Gerezani na Mwenge-Morocco. Hivi sasa tunaendelea na juhudzi za kuwashawishi ndugu zetu wa Japan watusaidie kujenga barabara za juu (*Flyovers*) maeneo ya TAZARA. Wameonesha utayari wao kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kupata wawekezaji wa ujenzi wa barabara ya njia sita ya kutoka Ubungo hadi Chalinze chini ya mpango wa ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya umma (*PPP*). Matumaini yetu ni kwamba ujenzi wa barabara hizi utasaidia kupunguza tatizo sugu la msongamano wa magari jijini, Dar es Salaam na yale yanayokwenda mikoani na nje ya nchi na hatimaye kupunguza madhara ya kiuchumi yatokanayo na msongamano mkubwa wa magari.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Maji, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha tumeweza kuishawishi Serikali ya India kutupatia mkopo wa Dola za Marekani milioni 178.25 kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji katika miji ya Dar es Salaam na Pwani. Hivi sasa mchakato wa kupata fedha hizo umefikia hatua za mwisho na bila shaka inatarajiwa mapema mwezi ujao Mkataba utasainiwa na utekelezaji wa mradi huo kuanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ujenzi, Nishati na Maji za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikisha upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 50 kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Uchumi ya Korea kwa ajili ya mradi wa kilimo cha umwagiliaji Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Viwanda. Wizara imeendelea na juhudi za kuchangia katika sekta ya ukuaji wa viwanda. Kilicho dhahiri ni kuwa, kwa hali ya uchumi wetu kwa sasa, viwanda vinavyohitajika haraka ni vile vya msingi ambavyo vinatumia rasilimali za ndani, vinaongeza thamani na vinatoa ajira nyingi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka huu wa fedha tutapata wawekezaji wa viwanda vya kutengeneza nyuzi za nguo kutoka Japan na China.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu mkubwa sio tu utatengeneza ajira kwa wananchi wengi, bali pia utawahakikishia wakulima wetu wa pamba soko la uhakika kwani viwanda vyote hivi vikianza kufanya kazi, vitahitaji kiasi cha tani laki mbili za pamba. Hivi sasa nchi yetu inazalisha tani laki moja tu.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ipo fursa kwa nchi yetu kuzalisha pamba kwa wingi zaidi kutokana na kuwepo kwa soko la uhakika nchini. Aidha, uko uwezekano mkubwa kwa Serikali ya Marekani kuendelea na Mpango wake wa AGOA ambapo

bidhaa za nguo kutoka Afrika ikiwemo Tanzania, zitaendelea kupewa upendeleo maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Ajira. Katika kuwatafutia ajira Watanzania nje, Wizara ikishirikiana na mamlaka husika za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekamilisha mchakato wa makubaliano ya kusaini mkataba wa ajira na nchi ya Qatar.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Wizara yangu inatarajia kupokea ujumbe kutoka Qatar kuja hapa nchini kusaini mkataba huo ili Watanzania waweze kuchangamkia fursa hizo nyingi za ajira wakati Qatar ikijiandaa kuandaa Kombe la Dunia la mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, jitihada za Wizara yangu katika kuvutia misaada na uwekezaji katika sekta za miundominu, zimechangia kuchochaea uzalishaji wa ajira nyingi nchini. Tunatambua changamoto ya ajira bado ni kubwa lakini tunaendelea na jitihada hizi kwa kushirikiana na Sekta nyingine kadiri uwezo wetu wa kibajeti utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Elimu. Mbalii na kuendelea kutafuta fursa za mafunzo nje ya nchi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu ilisimama kidete kupigania urejeshwaji wa fedha za ziada kiasi cha pauni za Uingereza milioni 29.5, zilizojumuisha kiasi tulicholanguliwa na kile kilichotolewa mlungula wakati wa ununuzi wa rada kutoka kampuni ya Kiingereza inayojihuisha na uuzaji wa silaha (BAE).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi katika Bunge lako wakati wa kuwasilisha Kauli ya Serikali na baadae wakati nikiwasilisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012, fedha hizo zote zimerejeshwa Serikalini na sio kwenye Asasi za Kijamii kama Waingereza walivyotaka. Kwa pamoja, jitihada zetu zimewezesha kuipatia sekta ya elimu shilingi bilioni 90 kama ambavyo Bunge hili limejulishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki nisipomshukuru kwa dhati sana Mheshimiwa Rais kwa msimamo wake thabiti na Mheshimiwa Spika kwa kuiunga mkono Serikali na kuteua Kamati ya Wabunge iliyooongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, ambayo imefanya kazi ya kutukuka kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitambue mchango mahsusi wa Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, niwashukuru pia Mheshimiwa Balozi Peter Kalaghe, timu yake na watumishi wa Wizara waliosimama kidete pamoja nasi kwenye suala hili lenye maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimejifunza kuwa imo ndani yetu nguvu kubwa ya umoja pale tunapoweka kando maslahi yetu finyu ya vyama na itikadi na kusimamia maslahi mapana ya Taifa. Hii ndio Tanzania ninayolija na kujivunia, Tanzania yenyе umoja na Tanzania yenyе kuthubutu. Tumeonesha uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yetu na historia itatupa tuzo njema na kulikumbuka Bunge hili kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala mtambuka yaliyotekelizwa na Wizara. Mradi wa Kiswahili kwenye Umoja wa Afrika. Lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika tangu mwaka 2004 katika shughuli za Umoja wa Afrika na Serikali yetu imekuwa ikigharamia wakalimani wa Kiswahili hadi mwaka 2008 ambapo Kamisheni ya Umoja wa Afrika ilichukua jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaendelea kushawishi nchi wanachama walau thelathini na sita ambayo ni theluthi mbili kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Umoja wa Afrika (*Protocol on the Amendments to the Constitutive Act of the African Union*). Kuanza kutumika kwa Itifaki hiyo kutawezesha lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli za kila siku za Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudi hizo, mwezi Januari, 2012 Umoja wa Afrika umeanza kufundisha lugha ya Kiswahili katika Kituo cha kufundishia Lugha cha Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Tayari wamekwishajisajili wanafunzi 15 chini ya Wakufunzi wawili wa kujitolea kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitambue mchango wao wa dhati na kuwapongeza kwa uzalendo wao. Mimi binafsi nilipata fursa ya kuwatemebelea na kuwatia moyo mwezi Januari, 2012 wakati nikihudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayotukabili ni upatikanaji wa fedha za kuendesha

kituo hicho na walimu wa kutosha wa kufundisha. Mpango wa Serikali ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Utamaduni cha Kitanzania jijini Addis Ababa kwa lengo la kukuza utamaduni wetu na Lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamii ya Wanadiplomasia na Watumishi wa Umoja wa Afrika. Tukifanikiwa katika hili tutakuwa tumetengeneza fursa za ajira kwa Wakufunzi wa Kiswahili pamoja na kupanua wigo wa fursa kwa Watanzania kufanya kazi katika Taasisi za Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (*JN/CC*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (*JN/CC*) Jijini Dar es Salaam, umekamilika kwa Asilimia 95 na tunategemea kukabidhiwa mwezi Septemba 2012. Kituo hiki cha kisasa kinaweza kuhodhi mikutano minne kwa mara moja, yenye idadi ya watu 1,600. Kituo hiki kitakuwa na huduma nyingine muhimu kama vile huduma za benki, afya, ukalimani na migahawa. Kituo kimejengwa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri wa Watu wa China.

Mheshimiwa Spika, sanjari na Kituo hiki, pia Serikali hiyo imetoa msaada wa magari madogo na mabasi yapatayo 75 ambayo tayari yapo nchini kwa ajili ya kutoa huduma katika kituo hicho. Kuanza kufanya kazi kwa kituo hicho, kutachochea ajira nyingi zaidi za moja kwa moja na nyingine zinatarajiwu kutengenezwa katika sekta za huduma.

Mheshimiwa Spika, kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa; kwa kuzingatia wajibu huu,

Wizara imeshiriki kwenye majadiliano mbalimbali yaliyopelekea uwekaji saini Makubaliano ya Mikataba mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

(1) Mkataba wa mpaka wa Bahari kati ya Tanzania na Comoro, ambao uliosainiwa tarehe 05 Desemba, 2011 Jijini Maputo – Msumbiji. Mkataba huu utahakikisha kuimarika kwa usalama wa mpaka wa Bahari baina ya nchi hizi mbili;

(2) Mkataba wa mpaka wa Bahari kati ya Tanzania na Msumbiji ambao ulisainiwa tarehe 05 Desemba, 2011 Jijini Maputo – Msumbiji. Kama ilivyo kwa Mkataba baina ya Tanzania na Visiwa vya Comoro, Mkataba huu utahakikisha usalama wa mpaka wa bahari baina ya nchi hizi mbili unaimarika;

(3) Muhtasari wa Makubaliano ya Mkutano wa Pili juu ya Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari (*EEZ*) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Visiwa vya Comoro na Serikali ya Ushelisheli, uliosainiwa tarehe 7 Septemba, 2011 huko *Port Louis*, Mauritius. Utekelezaji wa makubaliano haya ni muhimu ili kuwezesha nchi zote husika kunufaika na ukanda wa kiuchumi wa Bahari ya Hindi;

(4) Makubaliano kati ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (*A/CC*) na Beijing *Construction Engineering Group Company Limited (BCEG)* kuhusu ujenzi wa Mount Kilimanjaro *International Convention Centre* ambayo yalisanwiwa mwezi Agosti, 2011 mjini Arusha. Mkataba huu unatoa fursa ya kujengwa kwa

Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Jijini Arusha ambao utaiingizia Serikali mapato na pia kuendelea kuitangaza Arusha na Tanzania kwa ujumla kupitia Diplomasia ya Mikutano; na mwisho

(5) Makubaliano ya Pamoja (*MoU*) kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) na China Petroleum Technology and Development Corporation (*CPTDC*) mwezi Machi, 2012 kufuatia ziara ya Naibu Waziri wa Biashara wa Jamhuri ya Watu wa China Mheshimiwa Li Jinzao hapa nchini ili kuendeleza eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuongeza Eneo la Bahari Nje ya Ukanda wa Kiuchumi (*Exclusive Economic Zone - EEZ*). Wizara yangu kupitia Ubalozi wa kudumu wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, New York, imekuwa ikiratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa kuongeza eneo la Tanzania la Bahari nje ya Ukanda wa Kiuchumi. Wizara ikishirikiana na Kamati iliooundwa kushughulikia suala hilo, imeendelea kufanya mawasiliano na Taasisi za Umoja wa Mataifa zenye jukumu la kupitia Maandiko ya Miradi kama hii ya nchi zote zilizofanikiwa kuongeza eneo la Bahari.

Mheshimiwa Spika, Andiko la Mradi la Tanzania liliwasilishwa Umoja wa Mataifa mwezi Januari, 2012 na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, mwezi Agosti, 2012 Timu ya wataalamu inatarajiwa kwenda kutetea Andiko hilo mbele ya *Commission on the Limits of the Continental Shelf (CLCS)*, inayoendelea na mkuu wake ulioanza tarehe 30 Julai, 2012 na unaotarajiwa kumalizika tarehe

10 Agosti, 2012 huko New York. Wizara imeendelea kushiriki katika maandalizi ili kufanikisha utetezi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (*JPCs*) ni nyenzo muhimu sana katika ufanikishaji wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Ni katika Tume hizi mikataba ya msingi husainiwa ambayo huweka mazingira kwa sekta binafsi kuweza kupata unafuu na fursa katika nchi ambazo tuna Mikataba nazo. Kwa mfano, soko la tumbaku nchini China ni kubwa zaidi kuliko lile la Marekani lakini wakulima wa Tanzania wanashindwa kupenya katika soko hilo kutokana na kukosekana kwa mikataba ya aina hii baina ya nchi zetu mbili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, tumeshindwa kutumia nyenzo hii vizuri kufungua na kufufua fursa za ushirikiano. Kwa kutambua umuhimu huo na kuzingatia ufinyu wa bajeti uliopo, tumedhamiria katika mwaka wa fedha 2012/2013 kufanya mikutano ya *JPC* walau na nchi tatu kwa kuzingatia vipaumbele vy'a Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, asili ya miradi mingi ya maendeleo inayotekelawa katika sekta nyingi nchini kwa kushirikiana na washirika wetu wa maendeleo inatokana na Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilifanikisha makubaliano kuhusu uanzishwaji wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini. Makubaliano hayo yalifikiwa mwezi Julai, 2011 Jijini Pretoria, Afrika Kusini. Lengo la Makubaliano haya ni kuzidi kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya nchi hizi mbili katika nyanja mbalimbali hasa za uchumi.

Mheshimiwa Spika, haya niliyoyataja ni maeneo machache tu ambayo Wizara yangu imeyafanya katika kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika sekta za uchumi. Yako mengine mengi ambayo tumeweza kufanyika katika kila sekta nchini lakini kwa ufinyu wa muda siwezi kuyasema yote kwa muda nilionao. Itoshe tu kuongelea haya machache kwa leo.

Mheshimiwa Spika, naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya kwanza. Zipo fursa nyingi za ushirikiano huko nje ya nchi ambazo nchi yetu inaweza kunufaika nazo. Tumejidhatiti kunufaika na fursa zitokanazo na China-Afrika *Forum (FOCAC)*, *TICAD V*, *EU-Africa*, *EBA*, *AGOA*, Turkey-Africa, *SADC*, *NEPAD*, Tume za Kudumu za Ushirikiano baina ya nchi yetu na Mataifa mengine. Tunachohitaji ni kuwezesha zaidi ili tufanye kazi hiyo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi ya Tanzania katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda. Bendera ya Tanzania imeendelea kupepea vyema katika medani za Kimataifa kutokana na uongozi mahiri wa Waasisi wa Taifa hili na uongozi uliopo kufuatia kazi kubwa na

nzuri iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na Watanzania katika Mashirika ya Kimataifa na Kikanda.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha Watanzania wengi wanajiunga na kufanya kazi kwenye Mashirika ya Kimataifa. Aidha, Tanzania imeendelea pia kugombania na kuchukuwa nafasi za uongozi kwenye mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola (*CHOGM*) uliofanyika Perth, Australia mwezi Oktoba 2011. Tanzania ilichaguliwa kuingia kwenye Kikosi Kazi cha Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Ministerial Action Group - CMAG*) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2013. *CMAG* ndiyo chombo chenye jukumu la kusimamia misingi, sheria, kanuni na taratibu za Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, kikundi Kazi hicho kinaundwa na jumla ya nchi tisa kati ya nchi 54 za Jumuiya hiyo. Kuchaguliwa kwa Tanzania kuingia kwenye Kikundi Kazi hicho kumezidi kudhihirisha imani ya Jumuiya ya Kimataifa kwa nchi yetu. Mbali na kuleta sifa kubwa kwa Taifa letu, nafasi hii inaipa nchi yetu nguvu kubwa ya ushawishi ndani ya Jumuiya ya Madola na pia nafasi ya kuingiza na kusimamia maslahi yake kwenye Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Dkt. Agness L. Kijazi ambaye ni Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (*TMA*) kwa kuchaguliwa

kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Shirika la Hali ya Hewa Duniani (*WMO*) kuanzia mwezi Juni, 2012 hadi mwaka 2015. Nafasi hii ni muhimu kwani kati ya nchi 189 ambazo ni wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, nchi 37 tu ndio wanaingia kwenye Baraza Kuu la Shirika hilo. Dkt. Kijazi anakuwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kuitia raia wake Prof. Chris Maina Peter, ilichaguliwa kwa kishindo kuwa Mjumbe kwa kipindi cha miaka mitano kwenye Kamisheni ya Sheria za Kimataifa ya Umoja wa Mataifa katika uchaguzi wa wajumbe wa Kamisheni hiyo uliofanyika mwezi Novemba, 2011 Mjini New York, Marekani. Profesa Maina ni Mtanzania wa pili kuiwakilisha Tanzania kwenye Kamisheni hiyo, baada ya Mheshimiwa Balozi James L. Kateka ambaye alikuwa Mjumbe kwenye Kamisheni hiyo kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano (1997 - 2006). Balozi Kateka sasa ni Jaji katika Mahakama ya Kimataifa ya Sheria za Bahari.

Mheshimiwa Spika, Majaji wawili Watanzania; Jaji William Hussein Sekule na Jaji Joseph E. Chiondo Masanche nao walichaguliwa kuwa Majaji wa Mahakama inayorithi shughuli za iliyokuwa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (*ICTR*) katika uchaguzi uliofanyika New York, Marekani mwezi Desemba 2011.

Mheshimiwa Spika, kuitia azimio namba 66/408 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la mwezi Novemba,

2011 lilimthibitisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania, Bwana Ludovic Utouh pamoja na Ofisi yake kuwa kwenye Bodi ya Wakaguzi ya Umoja wa Mataifa kuanzia Julai, 2012 kwa kipindi cha miaka sita. Mafanikio haya yanatokana na umakini wa Wizara yangu kwa kufanya kamjeni za uhakika hadi kufanikisha kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Septemba, 2011 Tanzania imekuwa mjumbe katika Bodi ya Magavana ya Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*) kwa kipindi cha 2011/2012. Kuwemo kwenye Bodi hiyo, kunaipa nchi fursa ya kushiriki kwenye masuala nyeti na muhimu kama vile kwenye majadiliano kuhusu mipango ya nyuklia ya baadhi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Bodi hiyo ina jukumu la kutathmini maombi ya nchi zinazoomba uanachama na kuthibitisha viwango vya usalama. Aidha, Bodi ndiyo inayomteua Mkurugenzi Mkuu wa *IAEA* ambaye huthibitishwa na Mkutano Mkuu wa *IAEA*. Hii ni fursa nzuri kwa nchi yetu hasa ikizingatiwa kwamba Tanzania inayo malighafi ya urani.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nilitaarifu rasmi Bunge lako Tukufu kwamba Mtanzania mwenzetu, Dkt. Asha-Rose Migiro, amemaliza kipindi chake kama Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kwa hakika Dkt. Migiro amefanya kazi nzuri na kubwa iliyotukuka katika Umoja wa Mataifa. Ameiletea sifa nchi yetu na Bara la Afrika kwa ujumla kutokana na kumsaidia Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Ban ki Moon. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Watanzania wote, namshukuru kwa kutuwakilisha vizuri na ninampongeza sana na kumkaribisha tena nyumbani ili aendelee kushirikiana na wananchi wenzake katika ujenzi wa Taifa letu. Aidha, napenda pia, kupitia Bunge lako Tukufu kumpongeza Dkt. Migiro kwa kuteuliwa tena kuwa Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa katika masuala ya Ugonjwa wa UKIMWI Barani Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, nchi yetu ilijipatia sifa kutokana na kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula akiwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa Jumuiya ya Nchi Wanachama wa Ukanda wa Maziwa Mkuu. Balozi Mulamula aliratibu, aliisimamia na kuongoza Jumuiya hiyo kwa mafanikio makubwa pamoja na changamoto nyingi zilizokuwepo katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Kutokana na kazi yake nzuri, ndio maana Mheshimiwa Rais amemteua sasa kuwa Msaidizi wake Mwandamizi wa Masuala ya Kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msimamo wa Tanzania katika masuala mbalimbali. Tumekuwa tukishuhudia mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii duniani kote ambayo wakati mwingine yanahitaji nchi kuonesha msimamo wake kwa baadhi ya masuala hayo. Moja ya sifa kubwa ambayo Mwasisi wa Taifa hili Hayati Mwalimu Nyerere aliyotuachia ni kuweka misimamo kwenye misingi tunayoiamini kama Taifa. Kutokana na hali hiyo, Tanzania kama nchi huru

imeweza kuwa na misimamo yake kuhusiana na masuala hayo kama yanavyoelezewa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mpaka kati ya Tanzania na Malawi kwenye Ziwa Nyasa. Lipo tatizo la muda mrefu kati yetu na nchi jirani ya Malawi linalohusiana na mpaka kwenye Ziwa Nyasa. Tatizo lenyewe ni kwamba Malawi wanadai kuwa Ziwa lote Kaskazini ya Msumbiji kuelekea Ruvuma na Mbeya ni mali yao kwa mujibu wa Mkataba wa Heligoland uliowekwa saini tarehe 1 Julai 1890.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa upande wetu tunasema kuwa mpaka wa kweli kati yetu na Malawi unapita katikati ya Ziwa hivyo kufanya eneo lote la kaskazini mashariki ya Ziwa kati ya *Latitude degree 9°* na *degree 11°* kuwa mali ya Tanzania kwa mujibu wa Mkataba huo huo wa Heligoland (*Anglo-German Agreement*) wa mwaka 1890 ambao ulikubali kuwa kwa vile kuna maeneo ya mpaka ambayo hayana mantiki, pande zinazohusika zikutane na kurekebisha kwa kuunda *Border Commissions*. Aidha, tunazo ramani ambazo Waingereza wenyewe (ambao wakati huo walikuwa wakitawala Nyasaland na Tanganyika) walikubaliana kurekebisha na hivyo kusogeza mpaka katikati kama ulivyo mpaka kati ya Malawi na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hili, mwaka 2005 Marehemu Rais Bingu wa Mutharika, alimwandikia Rais wa awamu ya tatu Mheshimiwa Mkapa akimtaka waunde Kamati ya kuliangalia tatizo hilo na kulipatia ufumbuzi. Awamu ya Nne ikaendeleza kwa kuunda

Kamati ya Mawaziri wa Mambo ya Nje kuliangalia tatizo na kulitolea mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, kama zilivyokutana mwaka 2010, mwaka 2012 zilikutana tena ili kuendeleza mazungumzo ya mwaka 2010 na pia kujadili matukio ya kuonekana kwa ndege ndogo ndogo za utafiti wa mafuta na gesi kwenye Ziwa Nyasa zikitafiti hadi pwani ya Ziwa hilo upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano makubwa kati yetu na Malawi, Serikali yetu iliwataka wenzetu wa Serikali ya Malawi pamoja na kampuni za utafiti au uchimbaji kusitisha mara moja shughuli zote za utafiti hadi majadiliano yatakapokamilika. Ni matumaini yetu kuwa wenzetu wa Malawi wametuelewa. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa mgogoro huu mbele ya safari kutatuliwa na Msuluhishi badala ya sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya mgogoro bado iko mezani kwa majadiliano. Kufuatia maelekezo ya Marais wa pande mbili, Mawaziri wa Mambo ya Nje na wataalamu wetu wa masuala ya mipaka, ulinzi na usalama tulikutana Dar es Salaam tarehe 27 Julai, 2012 kujadili kwa kina mgogoro na kuupatia suluhu ya kudumu. Majadiliano yanaendelea vizuri na tumekubaliana kuwa wakati tukiendelea na mazungumzo, nchi zote zijiipushe na shughuli zozote kwenye Ziwa Nyasa ambazo zinaweza kutafsiriwa kuathiri maslahi ya nchi mojawapo.

Mheshimiwa Spika, kwa makubaliano haya, naomba niwatoe hofu wananchi wa Mikoa ya Mbeya na Ruvuma kuhusu hali ya usalama mpakani mwa nchi yetu na Malawi. Chini ya uongozi wa Serikali ya CCM, wananchi wa Tanzania daima watakuwa salama dhidi ya tishio lolote la dhahiri au la kificho la kiusalama. Tumefanya hivyo tokea uhuru na hatutachelea kufanya vinginevyo wakati wote tukiwa madarakani. Hili limeelezewa katika Ibara ya Nane, aya ya 191 na 192 ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Morocco na Sahara Magharibi. Tanzania ina uhusiano mkubwa na wa kihistoria na Jamhuri ya Sahara Magharibi. Itakumbukwa kuwa nchi ya Sahara Magharibi inapakana na Morocco, Mauritania na Algeria ilikuwa ni koloni la Hispania. Wakoloni hao waliondoka Sahara Magharibi mwaka 1975 na wakati wananchi wanajiandaa kujitawala, ghafla nchi yao ikavamiwa na nchi jirani za Mauritania na Morocco. Mauritania iliondoka na Morocco ikaendelea kuikalia Sahara Magharibi tangu wakati huo yaani 1975 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Sahara Magharibi walianza kazi upya ya kudai uhuru wao kutoka kwa jirani yao na Mwanachama wa *OAU*, Morocco. Mwaka 1976 Umoja wa Afrika uliamua kuitambua Sahara Magharibi kama mwanachama wa *OAU*. Morocco ikajitoa kwenye Umoja huo. Kwa kuwa Tanzania ilikuwa ndiyo Makao Makuu ya vyama vyta Ukombozi Barani Afrika, kuanzia mwaka 1963, ukombozi

wa Sahara Magharibi ulikuwa ni moja ya agenda yetu kuanzia wakati huo hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Tanzania kuhusu Sahara ya Magharibi, haujabadilika na upo pale pale. Tunataka wananchi wa Sahara Magharibi waachwe waamue kuitia kura ya maoni (*referendum*) iwapo wanataka kujitawala (*independence*) wenyewe au wanataka kuwa chini ya Himaya ya utawala wa Morocco. Huo pia ndio msimamo wa AU na Umoja wa Mataifa tangu mwaka 1992. Serikali ya Morocco imekataa kura ya maoni (*referendum*) na badala yake wanataka Sahara Magharibi iwe sehemu ya Himaya ya Morocco. Wamekataa kwa sababu wanajua kuwa wakikubali kura ya maoni kufanyika, wananchi wa Sahara Magharibi watataka kujitawala.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inauomba Umoja wa Mataifa kuendelea na jitihada zake za usuluhishi na tunaitaka Serikali ya Morocco kubadilika. Tupo tayari kuwa na mahusiano na Morocco bila ya kuathiri msimamo wetu na Sahara Magharibi. Tunafanya hivyo kwa Israel na Palestina.

Mheshimiwa Spika, ziara za Viongozi. Wizara yangu imeendelea kuratibu ziara za Viongozi wa Kitaifa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nje ya nchi. Ziara hizo zimekuwa na mafanikio na faida kubwa kwa nchi yetu, hasa katika kulinda na kuendeleza maslahi ya Kitaifa ya kiuchumi na kijamii, kukuza mahusiano ya kidiplomasia na nchi mbalimbali, Mashirika ya

Kimataifa na Kikanda, Kampuni za Kimataifa na hata watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba ziara hizo zinaendelea kuwa na tija pamoja na kupunguza gharama katika mazingira ya kiuchumi tuliyonayo, kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais, Wizara yangu imeanza kuchukua hatua mbalimbali kupunguza utegemezi wa ziara hizo pekee katika kupata mafanikio mbalimbali, hususan ya kiuchumi. Mionganini mwa mikakati hiyo ni:-

(1) Kupunguza ukubwa wa ujumbe katika misafara ya Viongozi Wakuu;

(2) Kuwatumia Wawakilishi, hususan Mawaziri katika safari mbalimbali hatua ambayo inapunguza gharama kwani anaposafiri Waziri huongozana na wajumbe wachache sana;

(3) Kuelekeza nguvu katika kuziimarisha Balozi zetu ikiwa ni pamoja na kufungua Balozi Ndogo katika maeneo yenye maslahi ya kiuchumi kwa Taifa; na

(4) Kutoa kipaumbele katika kufungua Ofisi za Wawakilishi wa Heshima katika maeneo muhimu ambayo Tanzania haina Uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, katika kudumisha mahusiano na nchi nyingine, nchi yetu imeendelea kutembelewa na wageni mbalimbali katika ngazi ya Wakuu wa Nchi na Serikali, Mawaziri na Viongozi wengine wa Kimataifa. Katika diplomasia, kutembelewa na wageni

ni daraja muhimu la kukuza mahusiano na pia ni kielelezo cha sera za nchi yako kukubalika na Mataifa mengine yakiwemo Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012, tulitembelewa na Marais kutoka Ivory Coast, Somalia, Uganda, Liberia na Malawi. Vilevile, tulitembelewa na Makamu wa Rais kutoka Burundi, Kenya, Zambia, Iran na Afrika ya Kusini. Wageni wengine mashuhuri waliotembelea nchini ni pamoja na Prince Charles wa Uingereza na mkewe Duchess of Cornwall Camilla Parker, Mwana wa Mfalme wa Saudi Arabia na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dkt. Donald Kaberuka na wengineo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepokea idadi kubwa ya mawaziri kutoka nchi mbalimbali duniani kama vile China, Uingereza, Japan, Sweden, Finland, Afrika ya Kusini, Korea ya Kusini, Korea ya Kaskazini, Marekani na Umoja wa Falme za Kiarabu. Wizara inaendelea kutekeleza mwongozo unaowataka viongozi wanaofanya ziara nchini Tanzania pia kutembelea Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha wa 2011/2012, Viongozi wafuatao walitembelea Zanzibar: Mwana wa Malkia wa Uingereza, Prince Charles na Mkewe Camilla; Mfalme wa Ashanti wa Ghana; Waziri wa Uingereza wa Maendeleo ya Afrika; Waziri wa Finland wa Maendeleo ya Afrika; Waziri wa Afya wa Finland; Waziri wa Afya wa Marekani na Waziri wa Afya wa Norway.

Mheshimiwa Spika, changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara na hatua zilizochukuliwa; kama ilivyo kwa Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali, Wizara yangu imekumbwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake, hususan kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Changamoto hizo kwa kiasi kikubwa zinasababishwa na kuendelea kupungua kwa bajeti ya Wizara kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani ambayo hutumiwa na Balozi zetu nje nako kunasababisha bajeti kuendelea kutokukidhi mahitaji. Ufinyu wa bajeti umesababisha Wizara na Balozi zetu kushindwa kutekeleza kwa vitendo diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kupewa bajeti ndogo kumesababisha, pamoja na matatizo mengine, madeni makubwa, wafanyakazi kutolipwa stahili zao na uchakavu wa magari na majengo. Aidha, ufinyu wa bajeti umechangia kwa kiasi kikubwa kwa Wizara kushindwa kuwarejesha nyumbani watumishi waliomaliza muda wao Balozini na kuwapeleka wengine kutoka Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalam (*NUU*) imetembelea Balozi zetu mbalimbali na kujionea hali halisi. Naamini Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo watakuwa wasemaji wazuri wa matatizo yanayozikabili Balozi zetu kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha changamoto hizo zinapungua, Wizara yangu imepanga kuwa na majengo ya vitega uchumi katika baadhi ya Balozi zetu ili kusaidia kuongeza mapato na kuokoa fedha ambazo zingetumika kulipia pango katika maeneo hayo. Katika hatua nyingine, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhusu uwezekano wa kutumia utaratibu wa mikopo ya nyumba (*Mortgage Financing*) katika Balozi zetu badala ya utaratibu wa sasa ambao una gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara yangu katika mwaka huu wa fedha imepanga kuwasiliana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (*PPRA*) ili kuwaomba waruhusu Balozi zetu zitumie utaratibu wa *hire and purchase* kununua vifaa mbalimbali kama vile magari ya uwakilishi na hivyo, kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, ninayo kila sababu ya kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara yangu walioko Wizarani na Ubalozini kwa uvumilivu na kujitolea kwa moyo wao wote katika mazingira haya magumu. Wafanyakazi wameendelea kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu na uadilifu mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tumekuwa tukiihusisha kwa karibu kuhusu changamoto hizi na wameshuhudia hali hii kila walipopata fursa ya kutembelea Balozi zetu. Tunawashukuru kwa kuielewa hali yetu halisi na kushirikiana nasi katika kushauri

namna bora ya kuondokana na changamoto hizo. Nasi tunauchukulia ushauri wao na ule wa Kambi ya Upinzani kwa umakini mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteua Mabalozi, kuiwakilisha nchi yetu huko Kenya, Misri, Msumbiji, Uganda, Oman, Zambia, Italia, Ubelgiji na China. Vile vile, aliwateua Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa na Naibu wake pamoja na Wakurugenzi tisa katika Wizara yangu ambao wana hadhi ya Balozi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Wizara yangu ina jumla ya watumishi 430 ambapo kati yao 249 wapo Makao Makuu ya Wizara, 18 wapo ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar na 163 wapo kwenye Balozi zetu. Kwa kipindi cha Julai, 2011 hadi Juni, 2012 jumla ya watumishi 50 walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, 17 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 33 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hicho hicho, jumla ya watumishi 58 walipandishwa cheo baada ya kutekeleza majukumu yao vizuri pamoja na kutimiza masharti ya Miundo ya Utumishi inayosimamia kada zao. Vile vile, watumishi 51 walithibitishwa kazini baada ya kumaliza muda wa mwaka mmoja wa majaribio baada ya kuajiriwa na watumishi wanne walibadilishwa vyeo baada ya kujiendeleza na kupata sifa za kada husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweke mkakati wa kuongeza idadi ya watumishi kutoka Zanzibar katika kada ya Maafisa Mambo ya Nje kwa kuwapatia fursa Wanafunzi 18 kutoka Tanzania Visiwani kuingia kwenye Chuo chetu cha Diplomasia. Dhamira ya Wizara ni kuona kwamba, pindi watakapomaliza na kufaulu masomo hayo waweze kuajiriwa kwenye Wizara yangu kulingana na nafasi za ajira mpya tutakazokuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi zilizo chini ya Wizara. Wizara imeendelea kukisaidia Chuo ili kiweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyo kwenye nia na madhumuni ya uanzishwaji wake. Lengo ni kukiwezesha Chuo kuendelea kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa Kimataifa, stratejia, usuluhishi wa migogoro, ujenzi wa amani, kutoa ushauri na kuendesha mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, lengo tarajiwa ni kukifanya Chuo kuwa taasisi bingwa ya elimu ya juu na ushauri katika nyanja hizo pamoja na kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika masuala ya utekelezaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umiliki wa ardhi limemalizika baada ya Chuo kupatiwa Hati ya Umiliki wa eneo lake. Kwa kuwa Chuo kinaendelea kupanuka ni wazi kuwa eneo la sasa kwa Chuo haliwezi kukidhi mahitaji hayo. Hivyo, Serikali kupitia Wizara yangu

imeendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo. Hadi sasa eneo la ekari 1,000 limeshapatikana.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tathmini ya kulipa fidia ya ardhi imekwishafanyika ambapo Serikali inapaswa kulipa shilingi bilioni 2.5 kwa wananchi wa eneo la Buma liliopo Wilayani Bagamoyo na Wizara inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizo kutoka kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (A/CC) kimeweza kukaribisha wastani wa mikutano 64 kwa mwaka. Kati ya mikutano hii asilimia 30 ya mikutano ni ya Kimataifa na asilimia 70 ni ya Kitaifa. Idadi hiyo ya mikutano imeweza kuleta Arusha wageni wanaokadiriwa kufikia 44,578 kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2011 Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa 15 na ya Kitaifa 47 ilioingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 35,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimeendelea kupata hati safi ya hesabu zake zillzoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2011. Kituo kilipata faida ghafi ya shilingi milioni mia tano thelathini na moja, elfu mia sita na tano mia tatu na ishirini (531,605,320/=) na kinaendelea kufanya shughuli zake kwa ufanisi na bila kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya

shilingi bilioni tisa, millioni mia sita arobaini na tano, elfu mia tatu hamsini na tisa na mia saba (9,645,359,700/=) kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na baada ya kutoa gharama za uendeshaji, Kituo kinategemea kupata ziada ghafi ya shilingi milioni mia tano ishirini na tano, elfu mia moja hamsini na tisa, mia sita sitini na nne (525,159,664./=).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kufuatilia kuhusiana na kujengwa kwa Kituo kipyaa cha mikutano mjini Arusha kitakachoitwa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*. Mradi huu ni moja ya miradi itakayofadhiliwa na Serikali ya Watu wa China kupitia benki yao ya *Exim*. Napenda kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo, Menejimenti na wafanyakazi wote wa AICC na pia kuwatachia mafanikio mema katika kazi zilizo mbele yao.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora Barani Afrika (*APRM*). Kazi ya tathmini ya utawala bora hapa nchini imeendelea kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Kwa kuwa Taarifa ya tathmini iliyokuwa imetayarishwa mwaka 2009 haikufanyiwa uhakiki kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ilihuishwa ili kurekebisha takwimu mbalimbali zilizokuwa zimepitwa na wakati lakini pia kuakisi mabadiliko ya kisiasa yaliyokuwa yametokea baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. *APRM* Tanzania kwa kushauriana na Sekretarieti ya Afrika Kusini na Wizara, iliandaa pia Taarifa mahsusii ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ilitokana na maoni ya mara kwa mara ya wadau wa Zanzibar hasa Makatibu Wakuu na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa ingawa suala la *APRM* ni la Muungano, ingekuwa ni busara ikaandaliwa taarifa mahsusni ya Zanzibar kwa nia ya kurahisisha utekelezaji wa changamoto zitakazobainishwa. Taarifa hiyo nayo ilikamilishwa na kuwa sehemu ya Taarifa ya nchi iliyokuja kufanyiwa tathmini na uhakiki na Timu ya Wataalam wa kutoka nchi za Afrika tarehe 2 - 23 Machi 2012.

Mheshimiwa Spika, wataalam wa *Country Review Mission* wapataao 20 waliwasili nchini mwezi Machi 2012. Wakiwa nchini walikutana na Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Serikali ya Muungano, Makamu wa Kwanza wa Rais (SMZ), Makamu wa Pili wa Rais (SMZ), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wawakilishi wa Serikali, Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa, Wabunge, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Jumuiya ya Wafanya Biashara, Washirika wa Maendeleo pamoja na Asasi zisizo za Kiserikali ili kupata maoni yao. Aidha, Wataalam hao, waligawanyika katika makundi mawili tofauti walitembelea mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Mtwara, Mbeya, Dodoma, Arusha, Kagera, Ruvuma na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika mikutano mbalimbali iliyofanyika masuala yafuatayo yalijitokeza ambapo pamoja na kuwepo kwa amani na utulivu, maeneo

mengine yaliyoonekana kuwa ni tunu na yanayopaswa kuenziwa ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, utaratibu wa kurithishana madaraka kwa amani kila baada ya uchaguzi mkuu, Muafaka wa kisiasa Zanzibar na kazi nzuri inayofanywa kwa uhuru na uwazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatarajia kufanyiwa tahmini kwenye Kikao cha nchi wenza zinazoshiriki katika mchakato Januari, 2013 badala ya Julai, 2012 kutokana na Timu hiyo ya *APRM* kutokuweza kukamilisha taarifa yao katika muda ambao ungetoa nafasi kwa Serikali yetu kutoa majibu na kuyawasilisha kwenye Kikao cha *APRM* cha Tathmini cha Wakuu wa Nchi kilichofanyika Julai, 2012 Mjini Addis Ababa. Naipongeza Bodi ya Uendeshaji ya *APRM* kwa kazi nzuri walioifanyia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara yangu ilipangiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni mia moja ishirini na tano, mia moja na mbili milioni na mia nane sabini na tano elfu (125,102,875,000/=). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni themanini, mia sita na mbili milioni na mia nane sabini na tano elfu (80,602,875,000/=), ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni arobaini na nne na milioni mia tano (44,500,000,000/=), ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (*Recurrent Budget*), shilingi bilioni sabini na sita, mia tatu themanini na saba milioni na mia moja themanini na saba elfu

(76,387,187,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC) na bilioni nne, mia mbili kumi na tano milioni na mia sita themanini na nane elfu (4,215,688,000/=) ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Balozi zake ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi billioni kumi na nne, mia nane sabini na mbili milioni na mia nne tisini na mbili elfu (14,872,492,000=). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012, kiasi cha shilingi billioni kumi na tatu, mia nane hamsini na tatu milioni, mia nne arobaini na tisa elfu na mia tano hamsini na tisa (13,853,449,559=) ikiwa ni makusanyo ya maduhuli balozini na Makao Makuu. Kiasi hiki cha fedha ni sawa na asilimia 93 ya makusanyo ya fedha zote za maduhuli zilizokadiriwa kukusanya balozini na Makao Makuu kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi billioni mia moja na ishirini na tatu, milioni mia nane themanini na nne elfu mia saba sabini na nane na mia saba themanini na saba (123,884,778,787=) ikiwa ni pungufu ya asilimia 0.97 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Mishahara, pamoja na bajeti ya Maendeleo. Kiasi cha shilingi billioni tisini na saba, milioni mia mbili arobaini na moja elfu mia mbili thelathini na tisa, mia saba themanini na saba (97,241,239,787=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Mishahara ikionesha ongezeko la asilimia 20.64 ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili limechangiwa na kuibuka kwa majukumu mbalimbali ya kitaifa ambayo awali hayakupangiwa fedha kutokana na ufinyu wa bajeti kama vile; Ujio wa Timu ya Ukaguzi kuhusu Mpango wa Kujitathmini Wenyewe kuhusu Utawala Bora (*APRM*) kutoka Makao Makuu ya Taasisi hiyo, Mchakato wa maandalizi pamoja na uzinduzi wa Majadiliano ya Ubia Nadhifu (*Smart Partnership Dialogue*), Ujumbe na ushiriki wa Tanzania katika Kikosi Kazi cha Kamati ya Mawaziri ya Jumuiya ya Madola (*Common Wealth Ministerial Action Group - CMAG*), Mchakato wa ujumbe wa Tanzania katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za kusini mwa Afrika pamoja na Ujumbe wa Tanzania katika Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya Maendeleo, Wizara hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 imepokea kutoka Hazina shilingi bilioni ishirini na sita, mia sita arobaini na tatu milioni na mia tano thelathini na tisa elfu (26,643,539,000/=). Kiasi hiki ni sawa na asilimia 59.87 ya bajeti yote ya Maendeleo iliyotengwa kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Ikumbukwe kuwa Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ilipunguzwa kwa kiasi cha shilingi 16,898,098,757/= kutokana na hali ya mapato ilivyodhahirika.

Mheshimiwa Spika, *malengo ya Wizara* katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika hotuba hii. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza *malengo* yake iliyojiwekea kulingana na llani ya

Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015. Msisitizo utakuwa ushiriki wa Wizara katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016. Naomba kusitiza na kukumbusha Wizara nyingne kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara mtambuka na hivyo inahusika na ufanikishaji wa miradi mingi inayotekelzwa na Wizara, Idara na Taasisi nyingine mbalimbali za Serikali. Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu ina nafasi kubwa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya kuendeleza na kuhimiza njia mbadala za kukabiliana na changamoto zinazotokana na bajeti inayoendelea kupungua kila mwaka, pamoja na mambo mengine, Wizara inatarajia *kufaya mambo yafuatayo*:-

(i) Kufungua Balozi Ndogo katika miji ya Uturuki, Loss Angeles (LA), California, Lubumbashi na Guangzhou; ambazo sanjari na kuendeshwa kwa gharama nafuu zinaweza kukusanya maduhuli mengi kuititia utoaji wa viza na tozo, hivyo kuongeza idadi ya watalii na kukuza biashara nje ya zile nchi tulizozoea (*traditional allies*) zilizoko Ulaya ambazo uchumi wake unayumba kwa sasa;

(ii) Tume za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano (JPC) - Wizara inatarajia kuitisha mikutano ya Tume za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano angalau kwenye nchi tatu kwa lengo la kuzifufua Tume hizo na kupanua fursa za ushirikiano, hususan masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini;

(iii) Watanzania Waishio Ughaibuni (*Diaspora*) - nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kufuatia Mheshimiwa Rais kuteua Mkurugenzi wa Idara ya *Diaspora* mapema Mei, 2012 Wizara yangu sasa ipo katika mchakato wa kuandaa Sera na Mpango wa Kitaifa kuhusu masuala ya *Diaspora* ili kuweka mazingira mazuri zaidi ya kuwahuisha Watanzania hao katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Hatua hii muhimu itasaidia kuainisha wigo wa kisera, ushiriki wa wadau na majukumu ya Wizara, Idara na Taasisi nyingine katika kufanikisha ushirikishwaji wa Watanzania waishio ughaibuni kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Ni azma ya Wizara yangu kuona kuwa mchakato huu unakamilika mapema ili kutoa mwongozo kwa wadau na kurahisisha uelewa wa pamoja kuhusu mikakati bora ya kuwatambua na kuwashirikisha *diaspora* katika kuchangia maendeleo ya nchi yao;

(iv) Majukumu ya Kimataifa - Wizara imejipanga kutumia kikamilifu nafasi za Tanzania kimataifa katika kipindi hiki zikiwemo uenyekiti wa asasi ya *SADC organ Troika* na ujumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Afrika kukuza taswira ya nchi yetu nje na kukuza ushirikiano wa Tanzania na nchi zillizoendelea ambazo ndizo zinafanya vizuri kiuchumi kwa sasa;

(v) Utatuzi wa Migogoro na Uimarishaji wa Amani - Tanzania imeendelea kuwa nchi ya kutumainiwa katika ulinzi na ujenzi amani Barani Afrika. Kumejitokeza haja kubwa ya uzoefu wetu kutakiwa na nchi nyingine katika utatuzi wa migogoro na ujenzi wa amani katika nchi zinazotoka katika migogoro. Serikali imeamua

kujikita katika kutumia uzoefu wetu na sifa hii katika kupanua maslahi ya nchi yetu kwa kuitikia fursa hizo. Tunajipanga kutumia Wanadiplomasia wetu wastaaafu na waliopo katika kutafuta suluhu ya migogoro. Lengo ni baadaye kuanzisha taasisi ya usuluhishi wa migogoro katika Chuo chetu cha Diplomasia. Uwepo wa Taasisi hiyo nchini Tanzania itavuna mikutano mingi na hivyo kuingizia nchi fedha za kigeni, kupanua sekta ya utalii na kutoa fursa ya kujenga urafiki na kupanua maslahi yetu kwa nchi nyingi zaidi. Tutatumia fursa zetu za kuwa Mjumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Afrika na Uenyekiti wa Asasi ya *SADC* kufanikisha azma hiyo; na

(vi) Ulinzi wa Amani - sambamba na mkakati huo, eneo la ulinzi wa amani (*peacekeeping operations*) ni eneo jipya tunalotaka kulipa kipaumbele. Azma hiyo inakwenda sambamba na uanzishwaji wa Chuo cha Ulinzi wa Amani (*Peacekeeping School*) nchini kwa ushirikiano wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Canada. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari Hati ya Awali ya Makubaliano (*MoU*) imesainiwa mwaka huu. Kuanza kwa Chuo hicho kutatoa fursa kwa vijana wetu kujenga uwezo wa kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani, vijana wetu wa Jeshi kupata uzoefu na mbinu mpya za kivita nje ya nchi, kuwezesha Watanzania wa fani mbalimbali kupata ujuzi na utaalamu na kuweza kushiriki kwenye operesheni za *AU* na *UN* (*Civilian Peacekeeping Mission*) ambako kwa sasa ushiriki wetu ni mdogo kutokana na kukosa stadi za aina hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaomba fedha za Wizara, naomba nizungumzie agizo la Bunge lako na Muhtasari wa Kauli ya Serikali kuhusu Malawi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kutoa kauli ya Serikali kuhusu tatizo la mpaka wetu na Malawi kwenye Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la muda mrefu linalohusu mpaka wetu na Malawi kwenye Ziwa Nyasa au Ziwa Malawi kama linavyoitwa na wenzetu wa Malawi. Tatizo lenyewe ni kwamba ndugu zetu wa Malawi wanadai kwamba mpaka wetu na wao kwenye Ziwa Nyasa unapita pwani na kwa maana hiyo Ziwa lote la Nyasa kutoka kwenye mpaka kati ya Malawi na Msumbiji hadi Kyela ni mali ya Malawi. Msingi wa madai yao ni mkataba uliowekwa saini kati ya Waingereza na Wajerumani mwaka 1890 ulioweka mpaka kati ya Tanzania na Malawi kwenye ufukwe au pwani ya Ziwa Nyasa, Mkataba huo unajulikana kama *Anglo-German Treaty* au *Heligoland Treaty*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa upande wetu tunadai kwamba mpaka kati yetu na Malawi kwenye Ziwa Nyasa unapita katikati ya Ziwa hilo kutoka pale Malawi na Msumbiji wanapopakana usawa wa nyuzi 11 Kusini hadi mwisho wa Ziwa kule Kyela kwenye usawa wa digrii tisa (9) Kaskazini ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa madai yetu hayo ni kwamba kwa mujibu wa nyaraka na ramani zilizotengenezwa na wakoloni wetu Waingereza mwaka 1928 mwaka 1937 na mwaka 1939 zinaonyesha

kuwa mpaka wa Ziwa hilo uko katikati. Aidha, mkataba huo wa *Anglo-German* wa mwaka 1890 unaotumika kama msingi wa madai yao umebainisha katika Ibara 6 kwamba nchi zinazohusika yaani Tanganyika na Nyasaland wakati huo au Tanzania na Malawi sasa zikutane ili kurekebisha kasoro kadri ya mazingira yatakavyolazimu. Jambo hili si jipya, tumekwishafanya zoezi hilo kwa upande wa mpaka wa bahari kati yetu na nchi ya Comoro na Msumbiji tarehe 5 Desemba, 2011 na mwaka huu tarehe 17 Februari, 2012 Tanzania na Seychelles tumekaa, tumejadili na tumerekebisha mpaka wetu kule baharini kati ya Tanzania na Seychelles. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madai ya Tanzania yanakuwa na nguvu zaidi tunapolinganisha kesi kama hii na iliyotokea kati ya Cameroon na Nigeria kuhusu mpaka wao kwenye Ziwa Chad lilitopo katikati ya Nigeria na Cameroon. Katika kesi hiyo ambayo ilipelekwa kwenye Mahakama Kuu ya Dunia, Mahakama Kuu ya Dunia (*International Court of Justice*) iliamua kwamba mpaka huo upite katikati ya Ziwa Chad ukifuata mstari ulionyooka yaani *medium line* hadi kwenye mdomo wa Mto Ebeji. Uamuzi huo ultokana na sheria za desturi za Kimataifa ambazo zinaeleza pamoja na mambo mengine kuwa mstari upitao katikati ya Ziwa yaani *medium line* ndiyo mpaka unaokubalika kati ya nchi na nchi zinapopakana na Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana maelezo haya yote, ni dhahiri kwamba tuna tatizo linalohitaji kutatuliwa kati yetu na Malawi juu ya mpaka wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni la muda mrefu. Kutokana na mazingira ya miaka 1960 na 1990, suala hili lisingeweza kutatuliwa kwa sababu mbili kubwa. Moja, kiongozi wa Malawi wa kipindi hicho Dkt. Kamuzu Banda alikuwa rafiki wa Serikali ya Makaburu ya Afrika ya Kusini wakati ambapo sisi tulikuwa marafiki wa wapigania ukombozi ikiwemo ANC ya Afrika Kusini. Lakini kulikuwa na sababu ya pili, ni kuwa kutokana na Tanzania kuwa Makao Makuu ya Vyama vyia Ukombozi Duniani, Wapinzani wa Serikali ya Malawi wanakimbilia Tanzania na hivyo kumfanya kiongozi wa Malawi wakati huo kuamini kuwa Tanzania ilikuwa kichaka cha maadui dhidi ya Serikali ya Malawi. Haya hayakuwa mazingira mazuri ya kuanza mazungumzo ya kidiplomasia ya kutatua tatizo la mpaka wetu kati ya Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Spika, baada ya utawala wa Rais Kamuzu Banda kuondoka na utawala mpya wa Rais Muluzi, Rais Mutharika na Rais Joyce Banda kuja madarakani, uhusiano kati ya Tanzania na Malawi ukaanza kuwa mzuri zaidi na kukaribisha mazingira ya kujadili suala hili la mpaka kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2005, aliyekuwa Rais wa Malawi Mheshimiwa Mutharika alimwandikia Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa barua ya kumwomba iundwe Kamati ya Pamoja ya Wataalam yaani *Joint Committee of Experts* ili kuchambua, kushauri na kutatua tatizo la mpaka kati ya nchi zetu mbili. Kwa kuwa mwaka huo kilikuwa kipindi cha uchaguzi, Mheshimiwa Rais Mkapa alikuwa anaondoka na alimuachia kazi hiyo Rais ajaye

kushughulikia tatizo la mpaka. Mheshimiwa Rais Kikwete akaja na alikutana na tatizo hili. Wakati huu wa Rais Kikwete alikutana na Rais Hayati Rais Mutharika mara mbili kwenye Mikutano ya *AU*, Addis Ababa na kwa pamoja walikubaliana kwamba ziundwe timu za wataalam chini ya Mawaziri wa Mambo ya Nchi za Nje, timu mbili za wataalam ili zifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, timu mbili ziliundwa na zikaanza kukutana tangu mwaka 2010 kwa kutengeneza Hadidu za Rejea kuhusu ufumbuzi wa tatizo hilo la mpaka wa nchi mbili katikati ya Ziwa Nyasa. Wakati Kamati mbili hizi zikiendelea kukutana na kuweka mkakati wa kukusanya nyaraka mbalimbali, eneo hili la mpaka likaanza kuchukua sura nyingine mpya ambayo iliaširia kuhatarisha usalama wa nchi zetu mbili. Serikali yetu ilipata habari za kuaminika kupitia Shirika la *TPDC* kuwa eneo lote la Ziwa Nyasa, Kaskazini mwa Msumbiji limegawanywa kwenye vitalu na kwamba Serikali ya Malawi imevitoa vitalu hivyo kwa Kampuni ya Utafiti wa Mafuta na Gesi. Aidha, makampuni hayo yaliomba kibali cha kuruhusu ndege za utafiti Ziwani humo, ombi ambalo Jeshi la Wananchi wa Tanzania lilikataa. Pamoja na katazo hilo, Serikali yetu ilipata ushahidi kwamba ndege ndogo za utafiti zenyе uwezo wa kutua majini na ufukweni zinazokadiriwa kuwa tano zilionekana zikivinjari na kutua katika Ziwa Nyasa upande wa Tanzania na kwenye ufukwe wake. Matukio hayo yalitokea kati ya Januari 29 na Julai 2 mwaka huu. Serikali iliwasiliana na Serikali ya Malawi kwa maandishi tukiomba ufanyike mkutano kwa ngazi ya Mawaziri na watalaam wake kujadili mustakabali wa mpaka huu na hali hii.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mawaziri na watalaan ulifanyika tarehe 27-28 Julai, 2012 huko Dar es Salaam na kujadili tatizo hili. Baada ya majadiliano mrefu na ya uwazi mambo matatu yalijitokeza. Moja, pande zote mbili zilikubaliana kwamba lipo tatizo kwa kuwa kila upande ulishikilia msimamo wake. Pili, Serikali zetu mbili zilikubaliana kuendelea na mazungumzo na zikakubaliana kwamba tarehe 20 – 27 Agosti, mwaka huu mkutano wa watalaan na baadaye wa Mawaziri ukutane Mjini Muzuzu Malawi. Tatu, Serikali iliitaka Serikali ya Malawi kutokuruhusu mtu au kampuni yoyote ile kuendelea na shughuli za utafiti kwenye eneo lote linalobishaniwa.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo yanayohusu matatizo yetu na mpaka na Malawi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathamini sana uhusiano mzuri uliopo baina ya nchi mbili na ina dhamira ya kudumisha na kuimarisha uhusiano wa ujirani mwema kwa manufaa ya watu wetu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapenda kuchukua nafasi hii tena kuitaka Serikali ya Malawi kuheshimu makubaliano yetu ya tarehe 27 Julai, 2012 kwamba njia nzuri na bora ya kutatua tatizo hili, narudia, njia nzuri na bora ya kutatua tatizo hili liliopo mbele yetu ni ya mazungumzo ya amani na kwamba katika kipindi chote cha mazungumzo haya, Serikali ya Malawi isiruhusu mtu, kikundi au kampuni yoyote ile kufanya utafiti kwenye eneo la Ziwa Nyasa liliopo Kaskazini Mashariki mwa Ziwa Nyasa kati ya nyuzi 11 hadi tisa (9) kwani eneo hilo ni sehemu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia maisha ya Watanzania wapatao 600 wanaoishi kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa, kwao wao Ziwa Nyasa ni urithi wao yaani *natural heritage*. Kwa wao Ziwa Nyasa ni chanzo cha uzima wao na maendeleo yao. Kwa vyovyote vile Serikali inayo dhamana ya kuwalinda wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania inapenda kuchukua nafasi hii kuyaonya na kuyataka makampuni yote yanayofanya shughuli za utafiti kwenye eneo hilo kusitisha kuanzia sasa. Napenda kurudia sehemu hii, napenda kuyaonya makampuni yote yanayofanya utafiti kwenye eneo hilo linalobishaniwa kuanzia leo Jumatatu kuacha shughuli za utafiti katika maeneo hayo. Serikali haitaruhusu, narudia Serikali haitaruhusu utafiti huu kuendelea hadi makubaliano na majadiliano kuhusu mpaka yatakapofikiwa kati ya nchi zetu mbili yaani Tanzania na Malawi. *Let us give diplomacy a chance.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi wote wa Ziwa Nyasa kuendelea na shughuli zao Ziwani na nchi kavu kama kawaida na bila wasiwasi wowote kwa sababu Serikali yao ipo macho, ipo imara na ipo tayari kulinda mipaka yetu kwa gharama yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo, naomba nieleze kwa ufupi sana maombi ya fedha za Wizara.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013. Ili kuweza kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi bilioni tisini na nane, mia tatu thelathini na tisa milioni na mia saba na saba elfu (98,339,707,000/=) kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni themanini na moja, milioni mia sita themanini na sita, mia tano na tatu elfu (81,686,503,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni kumi na sita, mia sita hamsini na tatu milioni na mia mbili na nne elfu (16,653,204,000/) ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo. Aidha, jumla ya shilingi bilioni sabini na sita, mia tano arobaini milioni na mia tano ishirini na moja elfu (76,540,521,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na bilioni tano, mia moja arobaini na tano milioni na mia tisa themanini na mbili elfu (5,145,982,000/=) ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara; shilingi bilioni moja, mia tano arobaini na tisa milioni na mia tisa ishirini na tano elfu (1,549,925,000/=) ni kwa ajili ya mchakato wa APRM, shilingi bilioni moja, mia tano na nne milioni, mia tano sabini na nne elfu na mia nne sabini na nane (1,504,574,478/=) ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na shilingi bilioni mbili, mia tano ishirini na sita milioni, mia tisa sabini na tatu elfu na mia nne sitini na mbili (2,526,973,462/=) ni kwa ajili ya fedha za Mshahara na Matumizi ya Kawaida ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu, kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni

kumi na sita, milioni mia nane themanini na mbili elfu mia mbili thelathini na moja, mia tatu na thelathini (16,882,231,330/=) kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimehesabiwa kama sehemu ya Matumizi ya Kawaida ya Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyoshughulikia Wizara hii. Anakuja mwakilishi wake Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. EDWARD N. LOWASSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Spika, tunaungana na Watanzania wote kutoa pole kwa ajali iliyotokea karibu na Kisiwa cha Chumbe kutokana na ajali ya Meli ya Skagit ambapo Watanzania wengi walipoteza maisha. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara

ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuliarifu Bunge hili kuwa, baada ya Bunge kuchambua na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati imeendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Njia mbalimbali za Kibunge za kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Serikali zilitumika na kuiwezesha Kamati kubaini mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hali ya Balozi zetu na ushirikiano wa Kimataifa. Hali ya uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa Duniani. Kwa kuzingatia umuhimu wa Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa, Kamati iliendelea kuitaka Wizara hii itoe taarifa ya hali ya uhusiano na diplomasia duniani. Lengo la utaratibu huo lilikuwa kuiwezesha Kamati kufuatilia na kulishauri Bunge katika kuisimamia Serikali kuhusu hatua za kuchukua ili kuboresha maisha ya Watanzania kwa njia ya diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zillionesha kuwa hali ya diplomasia duniani imeendelea kuathiri diplomasia katika Bara la Afrika. Kwa ujumla, dunia imekabiliwa na changamoto

mbalimbali katika mambo ya uchumi, siasa na masuala ya kijamii. Aidha, Barani Afrika na Duniani kwa ujumla kuna maendeleo ya demokrasia na uwazi huku diplomasia ikitabiliwa na matatizo ya tishio la ugaidi, kulegalega kwa uchumi na matatizo ya umasikini katika bara la Afrika. Nchi za Magharibi kwa ujumla hususan zinazotumia sarafu ya Euro, zinakabiliwa na tatizo la m dororo wa Uchumi. Kutokana na hali hiyo, uwezo wa nchi hizo kutoa misaada kwa nchi zinazoendelea umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mambo mengi ya kujifunza kutokana na hali hiyo. Kwanza, ni kuchukua hatua muhimu ya kupunguza umaskini na utegemezi katika maendeleo ya kiuchumi. Jambo lingine ni kuwa na hadhari kubwa kwa changamoto za kiusalama, kisiasa na kijamii zinazoikabili dunia. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa Tanzania inafaidika na shughuli za kidiplomasia zinazolenga kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Kwa upande wa usalama, utulivu na ustawi, Serikali izingatie sababu za migogoro katika nchi mbalimbali duniani na kujihami kwa kuchukua hatua sahihi dhidi ya mambo yanayoweza kuifikisha nchi yetu katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la mpaka baina ya nchi yetu na Malawi linahitaji kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa na haraka iwezekanavyo ili kusimamia na kutetea maslahi ya Taifa letu. Dhana ya diplomasia inaweza kuwa na tija kwa wananchi wa maeneo ya mpaka huo iwapo juhudini zitazaa ufumbuzi katika tatizo la mpaka. Kamati imeendelea kufuatilia namna Tanzania inavyotumia diplomasia kulikabili tatizo la

mpaka huu na kubaini kuwa hali bado si nzuri. Ni kweli diplomasia ni njia nzuri ya kutatua tatizo baina ya nchi na nchi lakini ni kweli pia kuwa na diplomasia haina maana ya kuacha tatizo liendee na kutolitatu kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, hali halisi inaonyesha kuwa bado suala hili ni tete na linahitaji msukomo madhubuti kutoka pande mbili za Serikali. Kwa upande wa Tanzania, Kamati ina maoni kuwa Serikali iweke muda wa kukamilisha lengo lake la kutatua tatizo hilo kidiplomasia. Iwapo muda huo ukipita hatua nyingine muafaka zichukuliwe na wananchi walijue hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Waziri, mwezi Aprili, 2012 Kamati ilialikwa nchini Morocco ambapo ilijifunza kuhusu uwezo wa nchi hiyo katika teknolojia ya uchimbaji visima vya maji, kilimo na miundombinu. Katika ziara hiyo, Wajumbe walibaini kuwepo kwa uhusiano wa kidiplomasia baina ya baadhi ya nchi za Afrika kwa ujumla wakiwemo mionganoni mwao wanachama wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa uhusiano huu, nchi hizo zimeendelea kunufaika kwa masuala mbalimbali. Iwapo Tanzania ingeanzisha uhusiano huu na Morocco, tungefaidika katika misaada ya kielimu kwenye fani mbalimbali ikiwemo fani ya Umdatari na nyinginezo. Aidha, uhusiano huo ungesaidia kutatua matatizo ya miundombinu, kilimo na maji katika maeneo yenye ugumu huo nchini yangeweza kupatiwa ufumbuzi kupitia ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inakosa fursa nyingi wanazopata wenzetu wenyewe mahusiano ya kidiplomaia na Morocco. Sababu ambayo imekuwa ikielezwa kuifanya Tanzania isiwe na uhusiano wa Kidiplomasia na nchi hiyo ni msimamo wa Umoja wa Afrika kuhusu mgogoro wa Morocco na nchi ya Sahara Magharibi. Kamati inasitisiza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa Tanzania kujenga uhusiano wa kidiplomasia baina yetu na nchi ya Morocco kama tunavyodumisha uhusiano na Israel licha ya tatizo baina yake na Palestina.

Mheshimiwa Spika, hali ya Balozi zetu nje ya nchi. Suala la diplomasia ya uchumi, uhusiano na ushirikiano wa kimataifa linategemea sana namna nchi inavyojipanga na kutumia Balozi zake katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, lengo la kuzitafutia masoko bidhaa zetu zenyе ubora unaotakiwa katika nchi za nje linategemea namna Balozi zetu zinavyojipanga na kuweza kutekeleza jukumu hilo. Ili kujiridhisha kuhusu namna Wizara hii inavyotekeleza jukumu la Ushirikiano wa Kimataifa na diplomasia ya uchumi kupitia Balozi zetu, Kamati hii ilipata kibali cha Mheshimiwa Spika ili kutembelea Balozi mbalimbali za Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakupongeza sana kwa maelekezo na uamuzi wako ulioiwezesha Kamati kutekeleza jukumu lake la kuisimamia Wizara hii kwa kufuatilia utekelezaji wa majukumu katika Balozi mbalimbali nje ya nchi. Ni uamuzi unaozingatia nafasi ya Bunge Kikatiba na umuhimu wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuwa chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia shughuli zinazotekelezwa na Balozi zetu nje ya nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini ya Uongozi wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard K. Membe, ilishirikiana na Ofisi ya Bunge kuratibu ziara hizi. Tunawashukuru Maafisa wa Wizara hii chini usimamizi wa Ndugu John M. Haule, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kutoa ushirikiano wa kutosha na kuziarifu Balozi zetu kuhusu ziara ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na Wajumbe jijini London na kueleza jinsi alivyofurahishwa na namna Kamati inavyofuatilia Diplomasia ya Uchumi. Mheshimiwa Rais aliiomba Kamati ifanye ziara ya kwenda nchini Brazil haraka iwezekanavyo ili kuona jinsi nchi hiyo ilivyopiga hatua kubwa za kiuchumi na kutoa ushauri wa jinsi ya kushawishi mbinu hizo za kiuchumi zinavyoweza kusaidia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya ziara hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kamati la kusimamia shughuli za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mujibu wa Kifungu cha 8,(4)(a), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Msingi wa shughuli hizo ni Hati ya Serikali inayoonesha mgawanyo wa majukumu ya Wizara (*Government Instrument*) toleo la 2010. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ziara hizi zimeiwezesha Kamati kubaini mambo mengi katika Balozi zetu ambayo si rahisi kuyapata kwa kuangalia kwenye maandishi na mawasilisho katika vikao. Kwa

mfano, moja kati ya changamoto kubwa iliyooonekana waziwazi katika ziara hizi, ni Serikali kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuchelewa kufanya maamuzi ili Balozi zetu ziweze kufanya kazi zake za msingi. Jambo hili limeanza kuigharimu Serikali katika uendeshaji wa kazi za Kibalozi. Ni maoni ya Kamati kuwa mfumo wa uwakilishi wa kiuchumi katika dunia ya sasa inayotegemea kwa kiwango kikubwa mchango wa sekta binafsi (*private sector*) unahitaji maamuzi ya haraka wakati changamoto zinapotokea.

Mheshimiwa Spika, mbali ya mfano huo, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu hali za Balozi zetu kama inavyoelezwa kwenye kiambatisho pamoja na taarifa hii. Kwa muhtasari, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

- (i) Kanuni za Utumishi wa Nje ya Nchi (*Foreign Services Regulations*) zimepitwa na wakati na kusababisha maisha magumu na ya udhalili kwa watumishi wa umma katika Balozi hizo;
- (ii) Kuchelewa au kutopata kabisa fedha za uendeshaji wa shughuli za Balozi zetu jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi (*core functions*) ya Balozi hizo. Aidha, Balozi zetu kuwa na madeni yanayoathiri heshima na hadhi ya Tanzania katika nchi hizo. Kati ya madeni hayo mengine ni kwa ajili ya gharama za makazi ya watumishi wa umma na baadhi ni madeni kwa ajili ya ada kwa watoto wa watumishi hao. Katika sehemu nyingine watumishi hulazimika kutekeleza majukumu yao kwa gharama

zao binafsi na wakati mwingine hata kutumia fedha zao binafsi kusaidia gharama za uendeshaji wa Ofisi kwa mategemeo kuwa watarejeshewa;

(iii) Tatizo la Balozi wa Heshima jijini Milano nchini Italy kutoa viza kwa kugonga mihuri ni changamoto katika ukusanyaji wa maduhuli. Aidha, kuna tatizo kubwa la Balozi wa Heshima (*Honorary Consul*) anayeishi mji wa Nice nchini Ufaransa kutoa viza kwa njia ya kugonga mihuri badala ya mashine za '*Visa sticker*' na kusababisha mapato ya Serikali kupotea;

(iv) Tatizo lingine ni kuhusu Balozi wa Heshima nchini Uhlanzi ambaye utataratibu wake wa kutoa viza una mashaka katika makusanyo ya mapato ya Serikali. Kwa kuwa hali hii inasababisha kutokuwa na takwimu za kutosha kuhusu makusanyo ya maduhuli, Kamati ilihoji msingi wa utaratibu huu usiokuwa na uhakika wa makusanyo. Kamati inashauri kuwa ni vema Wizara isimamie utaratibu huo na kuhakikisha kuwa maduhuli yanayopatikana ni kiasi sahihi. Serikali isitishe idhini hiyo na kumtaka Balozi huyo atumie *Visa Sticker Mashine* ili kujihakikishia kiasi cha maduhuli;

(v) Uchakavu wa majengo kwa ajili ya makazi na ofisi Balozini unaaibisha na kudhalilisha uwakilishi wa Tanzania pamoja na kuathiri ufanisi katika huduma za kikonseli;

(vi) Kutozingatiwa kwa umuhimu wa *exchange rate* wakati wa kutuma fedha jambo linaloathiri ufikiaji wa malengo ya bajeti yaliyowekwa. Aidha, ingawa hali ya ugumu wa maisha haitofautiani katika nchi za

ukanda wa Euro, ilibainika kuwa viwango vya *Foreign Services Allowances* vinatofautiana;

(vii) Balozi nyingi kutochuwa na Wakalimani kwa ajili ya kupata taarifa muhimu zinazowezesha utekelezaji wa majukumu yao ya msingi;

(viii) Kuwepo kwa watumishi wachache ikilinganishwa na idadi ya watumishi inayoweza kufanikisha tija ya Balozi zetu nyingi hususan katika Diplomasia ya Uchumi. Hali hii katika Balozi nyingine inasababisha kutochuwa na taarifa muhimu kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu katika kukuza uchumi;

(ix) Tabia ya baadhi ya Maafisa wa Serikali wanaokwenda kwenye Majadiliano ya Kiuchumi na Maendeleo (*Government Negotiation Team*) kutoshirikisha Balozi zetu jambo linalowafanya Mabalozi kushiriki majadiliano hayo pasipo kuwa na taarifa za kutosha;

(x) Kucheleweshewa kodi za pango za nyumba za watumishi na Ofisi na kusababisha migongano ya mara kwa mara na wenyewe nyumba pamoja na kukatwa fedha zao katika akaunti zao;

(xi) Kukosekana kwa fedha kwenye vifungu vya matumizi muhimu na ya lazima kama malipo ya ankara za mawasiliano, ada za shule, mafuta ya gari, umeme na gesi;

(xii) Kuchelewa kutolewa kwa posho (*Foreign Service Allowances*) na malipo ya matibabu katika baadhi ya Balozi na mishahara kwa baadhi ya balozi zetu;

(xiii) Pamoja na Kanuni za Utumiishi kutaka watumishi kutokaa zaidi ya miaka minne kwenye kituo kimoja cha Ubalozi, Kamati ilibaini kuwa wapo watumishi waliokaa muda mrefu zaidi ya miaka minne (4) kinyume cha Kanuni;

(xiv) Kukosekana kwa kifungu maalum kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zinazohusu Diplomasia ya Uchumi;

(xv) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutotumia vema utaratibu wa *Diplomatic Bag* kwa mawasiliano na Balozi zetu na hata kuhtarisha usalama;

(xvi) Kuna tatizo la lugha katika Balozi zetu mbalimbali kutokana na kukosekana kwa wajuzi wa lugha katika eneo la uwakilishi wa Balozi hizo. Hali hii inasababisha Ubalozi kukosa taarifa muhimu kwa majukumu;

(xvii) Kuwepo kwa malalamiko ya Balozi zetu kuhusu tabia ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutojibu hoja na barua kutoka Ubalozini. Aidha, kuchelewa kufanya uamuzi kuhusu mambo muhimu na ya msingi kwa maendeleo na mustakbal wa nchi; na

(xviii) Maoni na ushauri wa Balozi zetu kwa Serikali yetu kutofanyiwa kazi ipasavyo na kuathiri mantiki ya kuwa na Balozi hizo.

Mheshiwa Spika, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2012, tarehe 04 Juni, 2012, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kupitia na kujadili taarifa ya Wizara hiyo kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika mapitio hayo, Kamati ilielezwa kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti sanjari na taarifa kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina kwa kipindi husika. Aidha, taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Wizara hii ilipanga kutekeleza malengo kumi (10). Miongoni mwa malengo hayo ni kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli. Maeleo ya Wizara yalionesha kuwa Wizara imeendelea kutatua matatizo na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini. Hali halisi iliyopo kwenye Balozi zetu inaonyesha kuwa Serikali hajijatimiza wajibu wake ipasavyo katika jukumu hilo. Watumishi waliopo katika Balozi hizo wanaonekana kukata tamaa jambo ambalo si jema.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wizara ilitekeleza baadhi ya malengo na kutofanikiwa katika malengo mengine kati ya yale yaliyopangwa. Kamati ilitaka kujua sababu za hali hiyo na kupata maelezo ya changamoto zilizoathiri utekelezaji huo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti uliosababisha upungufu wa fedha kwa asilimia 44 ikilinganishwa na mahitaji halisi. Aidha, mtiririko wa fedha kutoka Hazina ulielezwa kuwa mionganini mwa changamoto hizo. Changamoto nyingine kati ya changamoto kumi na mbili zilizotajwa ni kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu ya Dola ya Kimarekani, Paundi ya Kiingereza na *Euro*, sarafu ambazo hutumika kufanya malipo ya Wizara kwa karibu asilimia 80 ya malipo yote.

Mheshimiwa Spika, ingawa taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilionyesha kuwa Wizara ina jumla ya majengo 92 Balozini, lakini tatizo mojawapo ni kushindwa kujenga majengo zaidi na kutokarabati baadhi ya majengo kinyume na ilivyokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kamati ina maoni kuwa changamoto nyingi zilizoelezwa zinaweza kupatiwa ufumbuzi kwa Serikali kuongeza juhudhi na msukumo wa kutosha. Kwa mfano, iwapo Hazina italipa kwa wakati fidia kwa hasara inayopatikana kutokana na kubadilisha fedha kipindi husika, Balozi zetu zitawezeka kuboresha uendeshaji kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha tarehe 4 Juni, 2012, Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyotekelzaji majukumu yake na namna ilivyojielekeza kwenye dhima, dira na malengo yake ya bajeti kwa mwaka wa

fedha 2011/2012. Aidha, taarifa ilionyesha kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa malengo hayo. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuwa mipango hiyo ilitengewa jumla ya Sh.125,102,875,000/- kwa kutumia uwiano wa shilingi 1,499.25 kwa Dola moja ya Kimarekani. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, Wizara inapolipa malipo hutumia fedha za kigeni. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa kiasi hicho cha bajeti kilikuwa sawa na asilimia 0.92 ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2012 ambapo maelezo ya Waziri yalionyesha kuwa jumla ya shilingi 93,705,202,878.00 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikiwemo malipo ya mishahara. Hata hivyo, kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara hii ilipangiwa shilingi 80,602,875,000.00. Takwimu hizi zinaonesha ongezeko la asilimia 16.3. Sababu kubwa ya ongezeko hili ilitajwa kuwa ni kuibuka kwa majukumu ya kitaifa ambayo awali hayakupangiwa fedha kutokana na ufinyu wa bajeti. Mchakato wa Maandalizi pamoja na Uzinduzi wa Majadiliano Nadhifu (*Smart Partnership Dialogue*), ni moja ya majukumu mapya yaliyochangia ongezeko la matumizi ya Bajeti ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya Maendeleo, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2012, Wizara ilipokea asilimia 59.42 ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya Mmaendeleo. Kutokana na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, upungufu huo

umetokana na hali ya mapato ya Serikali ilivyokuwa. Kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ina maoni kuwa Makadirio ya Mapato na Matumizi yanapaswa kuzingatia vipaumbele na majukumu ya msingi ili kuepuka kutotenga pesa kwa ajili ya jukumu muhimu lakini kutumia fedha kwa jukumu hilo wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano wa kimataifa na diplomaisa kwa ujumla. Ushauri huo ulihusu mambo manane ikiwemo tatizo la umiliki wa ardhi katika Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini na ukarabati na ununuzi wa wa majengo Balozini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa sehemu ya ushauri imezingatiwa na nyingine kuna maelezo tofauti. Kwa mfano, Kamati iliishauri Serikali kutatua tatizo la umiliki wa ardhi kwa Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini. Maelezo ya Serikali yanaonesha kuwa ushauri umezingatiwa na Chuo kimepatiwa Hati ya Umiliki wa eneo lake. Kuhusu upanuzi wa Chuo, Kamati ilijulishwa kuwa limepatikana eneo la ekari elfu moja (1000) kwa ajili ya upanuzi wa chuo kama ilivyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi na ukarabati wa majengo ya Balozi zetu, Kamati iliishauri Serikali iongeze juhudzi za kuboresha makazi ya watumishi wa

Serikali Balozini sambamba na kuboresha maslahi yao. Taarifa ya Waziri ilionyesha kuwa Wizara inaendelea na kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika Balozi zetu. Hata hivyo, kwa hali halisi katika Balozi nyingi, makazi na majengo kwa ajili ya Ofisi za Balozi vipo katika hali mbaya. Watumishi Balozini wanaendelea kucheleweshewa stahili zao.

Mheshimiwa Spika, malengo na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Kabla ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa majukumu kumi (10) yanayopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Majukumu hayo ni pamoja na kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi za Balozi. Jukumu lingine ni kuzitafutia masoko bidhaa zetu zenye ubora unaotakiwa katika nchi za nje. Majukumu hayo kwa ujumla ni mazuri lakini utekelezaji wake unahitaji usimamizi wa hali ya juu. Kubainisha majukumu ni jambo moja na kuyatekeleza ipasavyo ni jambo lingine. Kwa mfano, jukumu la kuboresha makazi ya watumishi Balozini na ofisi za Balozi ni tatizo la muda mrefu na linahitaji mkakati mahususi badala ya mazoea ya kuwekwa katika bajeti na kasma za Wizara hii bila kuainisha mpango maalumu kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Kamati, Mto hoja alieleza Kamati kuwa Wizara hii imepangiwa jumla ya Shilingi 98, 339,707,000/. Kati ya fedha hizo, Shilingi 81,686,503,000/- ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 16,653,204,000/- ni kwa Matumizi ya Maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu

yanayopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, Kamati inaunga mkono hoja pamoja na kuliomba Bunge lako Tukufu likubali maoni na ushauri wa Kamati na ushauri mwingine unaofaa kama utakavyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua makadirio haya na kubaini kuwa kiasi cha fedha inayoombwa ni asilimia 0.65 ya bajeti yote ya Serikali. Kamati ilitaka kulinganisha makadirio haya na mwaka wa fedha 2011/2012 na kubaini kuwa ingawa kwa ujumla bajeti ya Serikali imeongezeka kwa karibu asilimia 11.78, bajeti ya Wizara hii imepungua kwa asilimia 21.39. Aidha, wakati uwiano wa bajeti ya Wizara hii kwa ile ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 ulikuwa ni aslimia 0.92, makadirio ya mwaka huu yanaonesha kuwa ni asilimia 0.65. Uchambuzi huu unaonesha dhahiri namna utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii utakavyoathirika ikilinganishwa na mwaka jana. Kamati ina maoni kuwa kwa mwenendo huu wa bajeti ni vigumu kushughulikia baadhi ya matatizo ya Balozi hizo na kuyatatua. Kwa mfano, suala la ukarabati wa majengo ya Serikali Ubalozini linahitaji mpango maalum.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Kamati ilijadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na kupitia kifungu kwa kifungu. Katika majadiliano hayo, Kamati ilizingatia majukumu ya Wizara hii kama yalivyoainishwa katika Hati ya Serikali kuhusu mgawanyo wa majukumu ya Wizara (*Government*

Instrument). Aidha, Kamati ilizingatia ahadi za Serikali, hali ya ushirikiano Duniani, mambo yanayojadiliwa na wananchi nchini na llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 na kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

- (i) Kwa kuwa utaratibu wa mikutano ya Mabalozi utasaidia sana kufanya tathimini na kuboresha mambo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya Balozi zetu, Kamati inasitiza kufanyika kwa mikuatano hii na utekelezaji wa maamuzi yake;
- (ii) Ili Balozi zetu ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara hii ikamilishe Hati za Utambulisho na za Wito zinazokosekana na kusahihisha kasoro ya hati zilizotumwa katika Balozi zetu mbalimbali duniani. Si jambo la kawaida kuwa na Balozi asiyewasilisha Hati za Utambulisho na kutegemea Ubalozi huo uwe na tija inayotarajiwa;
- (iii) Serikali ianzishe chombo maalumu kitakachoshughulikia uamuzi wa kukarabati na kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, kwa kuwa mtindo wa Serikali kuwa na fedha kwa ajili ya kununua majengo umepitwa na wakati, uwekwe utaratibu wa Balozi hizo kununua majengo nje ya nchi kwa utaratibu wa kupata fedha kwa njia ya kuweka mali rehani (*Mortgage financing*) na Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii. Pamoja na ushauri huo, Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati hii na kununua majengo ya

Washington na New York. Uamuzi huo ni uamuzi wenye tija na ufanisi katika uwakilishi wa Balozi zetu;

(iv) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iombe kibali cha kuondoa samani, majalada na kumbukumbu nyingine zilizopo Ubalozini ambazo ni za muda mrefu sana na hazitumiki ili kutoa nafasi ya kutosha kwa Balozi hizo;

(v) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa isimamie na kuhakikisha kuwa Balozi zetu zote zinashirikisha diaspora katika masuala muhimu ya kitaifa kama vile Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba, sensa na uwekezaji wao nchini;

(vi) Ifanyike tathmini na uhakiki wa watumishi Ubalozini ili kuona mahitaji halisi ya watumishi kwa kazi na majukumu yaliyopo pamoja na kuweka vigezo madhubuti vyta mtumishi wa Serikali kuhudumia Ofisi za Balozi;

(vii) Kwa kuwa kuna utaratibu wa kupata msaada wa masomo (*scholarship*) kuitia Balozi zetu, ni vema kuboresha na kuweka wazi namna ya Watanzania kufikiwa na habari hizo. Aidha, fursa za ajira nje ya nchi zibainishwe vema na kuwarahishia vijana utaratibu wa kupata habari kuhusu fursa hizo. Aidha, kwa kuwa Tanzania inaendelea kupokea misaada ya bure kutoka China katika upande wa *scholarships and training*, Kamati inashauri Bodi ya Mikopo itumie fursa hii kusomesha Watanzania nchini China, kwani kwa maelewano yaliyopo ni kwamba Serikali yetu ikifadhili wanafunzi 100 na China itatoa nafasi nyingine 100 za

ufadhili (*scholarship*) kuwasomesha wanafunzi wa Kitanzania;

(viii) Serikali iongeze juhudzi za kuimarisha Balozi zetu nje ya nchi na kutekeleza kwa dhati azma hiyo kwa vitendo;

(ix) Wizara izingatie utoaji wa mafunzo kwa watumishi waliopo nje ya nchi ili kuongeza uwezo wao wa utendaji kazi;

(x) Suala la kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi ni muhimu kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu. Ni maoni ya Kamati kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuongeza ushirikiano na Wizara za Viwanda na Biashara, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi na mashirika yanayohusika na utalii kuandaa mpango utakaosaidia kuboresha namna ya kutangaza fursa za uwekezaji na vivutio vyta utalii Tanzania;

(xi) Ipo haja ya kulinganisha *Foreign Service Allowances (FSA)* katika nchi zinazotumia sarafu ya *Euro*, kuwa sawa kwa kuwa hali ya maisha katika nchi za ukanda huo inalingana;

(xii) Kuna umuhimu wa kurejesha Ubalizi wetu nchini Uholanzi ambapo kuna jengo la Serikali. Eneo hilo la kibalozi lina fursa za kuiwezesha Tanzania katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini pamoja na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Taarifa kutoka Uhamiaji zinaonyesha kuwa kwa wastani zinatolewa

viza za Tanzania 50,000 nchini Uholanzi. Iwapo kila viza itatolewa kwa USD 50, Tanzania inapata USD 2,500,000 kwa mwaka karibu sawa na Shilingi za Tanzania Bilioni nne (4). Kamati inahoji kama kweli Balozi huyo anatuma kiasi hicho. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa hakuna mantiki ya kutokuwa na Ubalozi katika eneo hili muhimu kiuchumi na maendeleo. Mbaya zaidi, ni maelezo yaliyopatikana kuwa Balozi wa Heshima nchini Uholanzi anashauri Serikali iliuze jengo lake lillilo Uholanzi. Ushauri huu haupaswi kupokelewa;

(xiii) Utaratibu wa Hazina kutuma fedha Ubalozini kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa unachelewesha upatikanaji wa fedha za uendeshaji kwa wakati. Ili kupunguza tatizo hilo pamoja na kuzingatia misingi bora ya uwajibikaji wa matumizi ya fedha na upatikanaji wake, ni vema Hazina ipeleke fedha hizo moja kwa moja bila kupitishia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama inavyofanyika kwa Halmashauri za Wilaya na Miji bila kupitishia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa; na

(xiv) Kufuatia kuwepo kwa tuhuma za wizi wa fedha kwa ajili ya safari za viongozi hivi karibuni, Kamati inashauri kuwa Wizara iongeze umakini katika usimamizi wa fedha za umma ili kudhibiti matukio ya wizi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuunda Tume ya kuchunguza tuhuma hizo kwa lengo la kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kabla ya kuhitimisha, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa

kazi nzuri ya kuitangaza Tanzania na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa katika diplomasia. Ni vema watendaji wengine Serikalini wafuate juhudii za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kutoa taarifa hii pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Namshukuru pia Mheshimiwa Bernard K. Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuratibu ziara iliyofanywa na Kamati kutembelea Balozi zetu. Vilevile nawashukuru watumishi wote wa Wizara hii chini ya uongozi wa Ndugu John M. Haule, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, naomba kuwapongeza watumishi wa umma wanaofanya kazi katika Balozi zetu nje ya nchi kwa uvumilivu na kujituma kwao kufanya kazi muhimu ya uwakilishi wa Tanzania na hasa katika eneo la diplomasia ya uchumi licha ya changamoto kubwa ya kuchelewa kupata fedha na wakati mwingine kutopata kabisa. Nawashukuru sana watumishi hao kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wajumbe wa Kamati walipotembelea baadhi ya Balozi zetu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa umakini mkubwa na ushirikiano wa kutosha waliokuwanao na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa kuthamini mchango wao naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti na Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Vita R.M. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Sadifa J. Khamis Mheshimiwa Mohamed S. Khatib, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Augostino M. Masele, Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Mohamed I. Sanya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Annastazia J. Wambura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ramadhani Issa, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza wajibu wake wa msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii pamoja na maoni ya Kamati na hatimaye liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kamataifa kama alivyowasilisha mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuendelea kunisimamia katika shughuli zangu za kutumikia wananchi wa Jimbo la Nyamagana huku nikiamini kwamba hakuna silaha itakayopandikizwa dhidi yangu itakayoniangamiza maana hiyo ni ahadi ya Mungu kwangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru familia yangu, mke wangu Flora pamoja na watoto wetu, mama yangu mzazi na wapigakura wangu wa Jimbo la Nyamagana, kwa maombi yao na kwa kunitia moyo siku zote huku wakinikumbusha kuwa imara na jasiri kama Mungu alivyomuagiza Joshua.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe (Mb), kwa imani yake kwangu pamoja na Naibu wangu Mheshimiwa Raya Ibrahim (Mb), kuwa wasemaji wakuu katika Wizara hii ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Sambamba na hilo, ni kwa chama changu - CHADEMA kwa kunipa moyo na kwa maelekezo ya mara kwa mara katika kuhakikisha kuwa CHADEMA kinaendelea kuwa Chama Tawala Wilaya ya Nyamagana na tunaamini wakati utafika

Watanzania wote watasimama na kupaza sauti zao kwa kusema Nguvu ya Umma (*People's Power*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la mwaka 2007, napenda kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, diplomasia yetu na sura yetu Kimataifa. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kimataifa, Tanzania kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi duniani, ililazimika kufuata upemo kwa kukubaliana na kitu kinachoitwa Diplomasia ya Kiuchumi, ambayo kwa hakika, moja ya malengo yake hasa ni kuhakikisha masuala na maslahi ya msingi ya taifa huru yanazingatiwa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaoisha, 2011/2012, tumeshuhudia nchi yetu ikiendelea kuzungumza kwa maneno na maandishi kuwa nchi yetu inatekeleza Diplomasia ya Kiuchumi wakati katika matendo ya Serikali yetu hasa wakiongozwa na viongozi wakuu wa nchi, tunaonekana tukitekeleza Sera ya Diplomasia ya Ombaomba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa sababu ya Serikali hii hasa kuitia kwa viongozi wake wakuu, kutekeleza kwa vitendo Sera ya Kuombaomba Kimataifa, kwa Nchi za Magharibi na Asia, ni mojawapo ya sababu kubwa ya Tanzania kupoteza heshima katika siasa za dunia na kwa hakika sasa mahusiano yetu na nchi nyingi za nje

yamejengeka kiutegemezi zaidi, kupungua kwa urari wa kibashara na kuachia mianya ya uporwaji wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, historia iko wazi kuwa sauti ya leo ya Tanzania katika mahusiano na nchi za nje, si ile iliyokuwa ikitufanya tutembee na kujitapa kifua mbele kimataifa kwa Utanzania wetu wakati wa uongozi wa Awamu ya Kwanza wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika tutatoa mifano miwili hapa iliyotokea katika mikutano ya kimataifa ambayo inadhihirisha kuwa Tanzania imepoteza sauti yake katika medani mbalimbali za kimataifa na hata viongozi wetu kupoteza heshima mbele ya macho ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa Davos, hasa wakati ambapo aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, Gordon Brown alipokuwa akiongoza mdahalo juu ya Afrika, kuliibuka mjadala katika Mtandao wa Gazeti la *The Guardian* (itakumbukwa kuwa hili ndilo gazeti ambalo liliandika sana juu ya ufisadi wa rada uliofanywa na *BAE Systems* na baadhi ya viongozi wa Serikali hii).

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge lako na Watanzania, tutanukuu baadhi ya maoni ya gazeti hilo. Baadhi ya maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

"Rais Kikwete wa Tanzania ni mmoja wa viongozi wa Afrika ambao dhaifu/pathetic katika nyakati hizi, ni

kiongozi wa nchi ambayo ni moja ya nchi zenyе utajiri mkubwa wa rasilimali duniani, lakini bado anaongoza duniani kwa kuomba. Kampuni nyingi za kigeni zinaijua Tanzania kama moja ya nchi yenye mianya myepesi ambayo unaweza ukaingia na ukachukua unachotaka bila kuulizwa chochote.

Nashindwa kabisa kuelewa juu ya akili za viongozi wa nchi hiyo ambao wanaabudu Wazungu...nimefanya kazi katika nchi hiyo kwa miaka 8, nikiwa mtumishi wa UNDP. Niligundua jinsi uongozi wa nchi hiyo usivyokuwa na ufanisi na ulivyoathiriwa na rushwa. Mawaziri wake waliokula rushwa katika kashfa ya rada kutoka Kampuni ya BAE hawajawahidi kushtakiwa mahali popote pale, pamoja na kuwepo kwa ushahidi ulio wazi dhidi yao.

Walipa kodi wa Uingereza lazima waache kuendelea kusapoti ziara za nje za viongozi hawa wala rushwa. Rais Kikwete hana sababu yoyote ya kwenda Davos kuomba misaada kwa mataifa ya nje. Nchi yake tayari ni ya tatu kwa kuongoza kupokea misaada. Anapaswa kuona aibu kusema mbele ya dunia nzima kuwa watu wake ni maskini. Watu wake kuendelea kuishi malsha ya umaskini...ni uzembe wa viongozi. Huo ni mzigo wake mwenyewe.

Watanzania wana matatizo yao, Waingereza nao wanayo ya kwao, lazima tutambue hilo. Hatuwezi kugharamia ziara zake za nje ya nchi. Anapaswa kutumia vyema rasilimali za nchi yake. Badala ya kuachia maofisa wake wala rushwa na wageni kuendelea kupora nchi yake, anapaswa kufikiria

vyema asiendelee kuwa mtu wa ajabu duniani. Niliwahi kusoma katika moja ya magazeti ya Kenya yakidhihaki ziara zake nje ya nchi. Uchumi wa nchi Lebanon, Haiti, Palestina hata Rwanda ni mzuri kuliko Tanzania.

Kunapaswa kuwepo na sheria kuwazuia viongozi wote wala rushwa na watoto wao kuingia Ulaya. Simlaumu Kikwete, nawalaumu Watanzania kwa kuachia haya yatokee. Wanapaswa kuwajibika asilimia 100 kwa umaskini na matatizo yanayowakabili. Tusingependa waendelee kuombaomba. Wapo Waingereza hawana kazi, tungetumia fedha hizo (za misaada) kuwalipa malipo yao ya kutokuwa na ajira."

Linda Croucher

([www.guardian.co.uk/business/2012/jan/26/davos-2012-day 2](http://www.guardian.co.uk/business/2012/jan/26/davos-2012-day-2)).

Mheshimiwa Spika, Tanzania iliyokuwa na sauti katika mazungumzo baina ya Nchi za Kusini (Nchi zinazoendelea) na Nchi za Kaskazini (Nchi zilizoendelea), Tanzania iliyokuwa na sauti mstari wa mbele Kusini mwa Afrika, sasa imekuwa nchi ya kunyamaza kwenye masuala ya msingi kabisa kama haya. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, i-wapi sauti ya Watanzania katika anga la kimataifa? Serikali ya CCM imeipeleka wapi sauti hiyo ya Watanzania iliyokuwa ikiheshimika miaka ile wakati wa Mwalimu?

Mheshimiwa Spika, hali ya Tanzania kupoteza sauti katika medani ya kimataifa pia ilidhahirika katika mkutano kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*COP 17*) uliofanyika nchini Afrika Kusini; wakati nchi yetu ikiwa ni

miongoni mwa waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabianchi kutoka hewa chafu inayozalishwa na mataifa makubwa (ambayo ndiyo tunayakimbilia kuomba misaada), Tanzania haikuweza kusema lolote. Tunaweza kukubaliana na watu wengine wanaotoa maoni kuwa ujumbe wetu katika masuala muhimu ya kimataifa kama hili la namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi unahusisha watu wasiokuwa na ushawishi na diplomasia hitajika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa iwapo hatua za makusudi hazitachukuliwa kurejesha heshima na sauti ya Tanzania kimataifa maamuzi mengi yatafanyika yenye athari kwa wananchi wengi bila ushiriki wao thabiti kama yanayoendelea hivi sasa kuhusu Mikataba ya Kiuchumi na Nchi za Jumuia ya Ulaya (*EPA*) yenye madhara kwa wakulima na wenge viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu nje ya nchi. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ni kuwa kwa kipindi cha miaka 50 ya uhuru tumefanya ufunguzi wa Balozi mbalimbali katika nchi za nje na zipo Balozi 32; Balozi Ndogo tatu; Vituo viwili vya Biashara na Konseli za Heshima 17. Aidha, Serikali, kwa kupitia Wizara, inamiliki majengo yake yapatayo 90 nje ya nchi. Kati ya hayo 22 ni ofisi za Balozi, 20 ni makazi ya Balozi na 48 ni makazi ya maofisa. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kujua majengo haya yako nchi gani na je, yana hatimiliki au yako hali gani mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Sera ya Tanzania katika Mahusiano ya Kimataifa sasa inaongozwa na

Diplomasia ya Uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa kiwango gani Serikali hii kupitia kwa Mabalozi wetu, hususan katika nchi ambazo ni maeneo maalum katika mikakati yetu ya kunufaika kiuchumi, imefanikiwa kutekeleza dira na dhima ya sera yetu hiyo mpya tangu mwaka 2004?

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu, pamoja na Serikali kusitiza sana sera yetu katika mahusiano ya nje kuwa ni Diplomasia ya Kiuchumi, mpaka sasa tunazo taarifa za Balozi hizi kutokuwa katika hali yoyote ya kuweza kufanikisha lolote katika utekelezaji wa vitendo wa sera hiyo, kwa sababu ofisi zao hazitengewi fedha, hazina watumishi wa kutosha na hazina vitendea kazi. Kutokana na ukweli huo, imefikia hatua Waambata katika baadhi ya Balozi zetu hawawezi kufanya kazi, hata inapolazimika kusafiri, wanashindwa kwa sababu hawana mafungu. Hali hii inadhihirisha kuwa hii dhana ya Diplomasia ya Uchumi inayozungumziwa sana na Serikali hii, haiko katika uhalisia wake kimatendo bali iko zaidi katika maneno na maandishi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni kwa nini Serikali haionti kuwa ni wakati mwafaka sasa wananchi wakapata tathmini ya kina namna gani kila Balozi yetu nje ya nchi imeweza kutekeleza kwa vitendo dhana hii, wakijielekeza katika kuhakikisha nchi inanufaika kiuchumi katika kila uhusiano inaofanya nje ya nchi katika mataifa na taasisi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika randama ya Serikali, mbali ya kutengewa fedha za posho, hakuna mahali popote ambapo Serikali imethubutu kufanya uamuzi wa busara wa kutenga fungu kwa ajili ya utekelezaji kwa vitendo wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa namna ambavyo Balozi zetu nje ya nchi, zikiwemo kwenye Balozi muhimu kabisa, zimeshindwa kutekeleza sera yetu hiyo kwa vitendo kwa sababu hakuna fedha zilizotengwa. Maana yake ni kwamba watu wanaoitwa Waambata wa Masuala ya Uchumi hawana fedha hata za kuwawezesha kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara ya Mambo ya Nje inaomba jumla ya fedha Tshs.81,686,503,000 katika Fungu 34 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na mishahara, hakuna mahali popote ambapo Serikali imeona kuna umuhimu wa kuziwezesha Balozi zetu kufanya kazi zake kwa ufanisi katika kuhakikisha tunanufaika kiuchumi katika mahusiano yote ambayo nchi hii inafanya.

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara hii katika kasma 6391 inaomba jumla ya Tshs.16,653,204,000, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambayo pia inahusisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya Balozi zetu mbalimbali nje ya nchi, hakuna mahali popote katika randama ambapo Serikali imeomba fedha kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa majengo kwenye Balozi Muhimu kama Ujerumani, Urusi, Canada, Ubelgiji, London, Kuala Lumpur na nyingine ambazo majengo mengine yanavuja, yamebomoka na hata kunuka.

Kambi Rasmi ya Upinzani tunajiuliza ni mtu gani mwelewa katika nchi za Asia, Ulaya na kwingineko ambaye anaweza kwenda kufanya mazungumzo ya maana kiuchumi katika jengo linalonuka au ambalo limewahi kumkosakosa kumwangukia Balozi wake (Mfano Ubalozi wa Urusi, ambako silingibodi ilikosa kumwangukia Balozi wetu)!

Mheshimiwa Spika, utendaji mbovu wa Wizara kuhusiana na Balozi zetu. Balozi zetu na Mabalozi wetu wana hali mbaya sana huko waliko na hii inatokana na ukweli kuwa Serikali haipeleki fedha kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na mikataba mbalimbali ya kimataifa kama ule wa *Vienna Convention* ambao unataja haki na stahiki zao. Nitatoa mifano michache hapa.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1975, Msumbiji chini ya FRELIMO walitoa jengo na kutupatia ili liwe Ubalozi wetu nchini humo na mpaka leo ndilo tunalitumia. Jambo la aibu ni kuwa tangu tupewe jengo hilo bure tumeshindwa hata kulikarabati na hali hii imapelekwa hata wapangaji waliokuwa wamepanga kwenye jengo hilo hususani Ubalozi wa Uganda sasa wameondoka kutokana na ubovu wa jengo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kujua ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kwa ajili ya kulikarabati jengo hilo na ni kwa nini mpaka leo fedha hazijapelekwa? Aidha, fedha za kodi tulizokuwa tunalipwa na wapangaji wetu zimetumika kufanya nini, zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, Balozi wetu wa Japan ambaye anahudumia pia nchi ya New Zeland, Balozi wetu wa India ambaye pia anahudumia nchi ya Bangladesh, Nepal na Sri Lanka wote wameshindwa kwenda kujitambulisha kwenye nchi hizo kutokana na Hati za Utambulisho kukosewa kwenye uchapaji na tayari Wizara ilishaletewa taarifa hizo ili warekebishe lakini mpaka leo hakuna hatua zilizochukuliwa kurekebisha makosa hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani, tunataka kujua ni lini Hati hizo zitaweza kurekebishiwa ili Mabalozi wetu waweze kwenda kujitambulisha kwenye nchi hizo na hatimaye huduma za kibalozi ziweze kupatikana?

Mheshimiwa Spika, tulipewa kiwanja nchini Dubai kwa ajili ya kujenga jengo la Kitega Uchumi lakini mpaka leo hatujaweza kujenga jengo hilo ambalo pia lingekuwa sehemu ya kuhifadhi Ubalozi wetu. Kambi Rasmi ya Upinzani tunaishauri Serikali kama inaona haiwezi kujenga jengo hilo peke yake na kutokana na umuhimu wa mji huo kibiashara kwa sasa basi Serikali iingie ubia na wawekezaji binafsi (*PPP*) ili kukiendeleza kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Uingereza ilitupatia kiwanja namba 19 barabara ya Denewood Jijini London kwa ajili ya sisi kujenga jengo la Ubalozi wetu ili tuweze kupunguza gharama kubwa za kupangisha ila mpaka leo tumeshindwa kujenga na nchi ya Uingereza imetuandikia barua ya kikitaka kiwanja hicho kwani kimekuwa maficho ya wahalifu kutokana na sisi kushindwa kukiendeleza. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kujua ni kwa nini Serikali imeshindwa kujenga kwenye kiwanja hicho na badala yake tunaendelea

na utaratibu wa kupanga ambapo inatugharimu fedha nyingi kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, mpaka leo tumeshindwa kupata hati miliki ya jengo la Ubalozi wetu nchini Kenya. Aidha, makazi ya Balozi wetu nchini Canada yana hali mbaya sana na mpaka leo hatujaweza kuyakarabati. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupata majibu ya kina kuhusiana na hatua ambazo Serikali imefikia katika kuitafuta hati miliki za majengo yetu ya Balozi mbalimbali ulimwenguni pamoja na mpango wa kukarabati na kuweka ofisi na makazi ya mabalozi wetu kwenye hali nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria zetu, moja ya stahiki za Mabalozi wetu ni pamoja na watoto wao kusomeshwa na Serikali, ila ukweli ni kuwa wako watoto wa Mabalozi wetu ambao wanarudishwa nyumbani kutoka kwenye shule kutokana na Serikali kushindwa kupeleka fedha kwa ajili ya ada na mifano ni mingi. Kambi Rasmi ya Upinzani, haiwezi kuendelea kuona hali hii ikiendelea kuvumiliwa tena kwani ni vitendo vya kuwadhalilisha Mabalozi wetu katika nchi wanakotuwakilisha.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa baadhi ya Balozi zetu zinatuhumiwa kwa kutoa hati za kusafiria kwa wananchi wa mataifa mengine na hasa ya Afrika ya Magharibi na baadhi ya Balozi hizo ni zile zilizoko China, Uingereza na *Hong Kong*. Kutokana na uzito wa tuhuma hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka ufanyike uchunguzi mara moja ili kuweza kubaini ukweli wa tuhuma hizi na kuliondolea Taifa aibu hii.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya ajabu ambayo inahitaji majibu ya kina kwelikweli kuweza kueleweka ni juu ya Ubalozi wetu nchini China, mbali ya majengo ya Ubalozi huo kuwa na nyufa na kuvuja wakati wa mvua, Ubalozi wetu nchini China hauna hata samani za kawaida za ofisi na nyenzo muhimu kama mashine ya nukushi (*fax*) au mashine za kurudufu. Tunajiuliza, hivi Ubalozi wa namna hii unaweza kufanya kazi gani katika kutekeleza Diplomasia ya Kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, aidha, tunaitaka Serikali hii itoe kauli Bungeni, inapata wapi uhalali wa kuzuia magari ambayo muda wake wa kutumika umepita, wakati nchini China magari yetu matatu pekee yaliyopo katika Ubalozi wetu yanavunja sheria mpaka muda huu tunapozungumza kwa sababu yametumika tangu mwaka 2001 na sheria ya nchi hiyo zinasema magari hubadilishwa kila yanapotumika kwa miaka 10?

Mheshimiwa Spika, katika randama ya Serikali hakuna mahali popote ambapo Ubalozi huu umetengewa fungu kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jengo hilo lenye nyufa na linalovuja, wala hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kununua magari, badala yake Serikali inaomba Tshs 32, 400,000 kwa ajili ya kununulia mafuta na vilainishi vya magari na Tshs 10,000,000 kwa ajili ya kulipia bima ya magari!

Mheshimiwa Spika, tunauliza hivi hatuoni aibu kuendelea kuvunja sheria huko? Tutakuwa wapi na jeuri ya kuwakemea Wachina pale watakapokuwa wanavunja sheria zetu hapa nchini kama Balozi wetu anaongoza kuvunja za kwao?

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, Ubalozi huu pamoja na umuhimu wa China katika mahusiano yetu hasa kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, haina mtaalam yeyote wa masuala ya uchumi, achilia mbali kwamba hata wafanyakazi waliopo bado hawawezi kumudu majukumu yao kusafiri kwenda maeneo mbalimbali, kutokana na ukubwa wa nchi hiyo! Hali hii inakwamisha kwa kiasi kikubwa sana utendaji kazi wa Ubalozi huu.

Mheshimiwa Spika, kashfa ya Rada na Mabilioni ya Gesi. Kwa mara nyingine tena, bila kuchoka, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalazimika kuzungumzia moja ya kashfa kubwa kuwahi kutokea katika nchi yetu, kashfa inayotokana na rushwa ya rada tuliyouziwa na Kampuni ya *BAE Systems* ya Uingereza. Tunaendelea kuhoji kwa nini mpaka sasa watuhumiwa wa kashfa hiyo wanaendelea kutembea kifua mbele dhidi ya Serikali bila hatua zozote kuchukuliwa? *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa haieleweki ni kwa sababu gani nchi hii pamoja na kudai kuwa ina uhuru wa kujiamulia mambo yake yenyewe, illamua kuliachia suala hili kufanyiwa kazi na Serikali ya Uingereza, kuanzia uchunguzi hadi mashtaka ya kurudishiwa fedha zilizotokana na rushwa ya rada, ambazo kwa sasa zimebatizwa jina tamu la 'chenji ya rada'.

Mheshimiwa Spika, katika hali inayoonesha kuwa baniani mbaya kiatu chake dawa, pamoja na Serikali hii kushindwa kufanya uchunguzi na hatimaye

kuwashtaki watuhumiwa wa rada, bado ilipobainika Mahakamani kuwa tunatakiwa kurudishiwa chenji iliyotokana na rushwa, Serikali ilikuwa mstari wa mbele kwelikweli katika kufuatilia chenji ya rushwa na katika kuipangia matumizi.

Mheshimiwa Spika, tunashindwa kuelewa umakini wa Serikali hii uko wapi kwamba inaweza kuweka msisitizo pekee katika kuhakikisha fedha za rushwa ya rada zinarejeshwa nchini, lakini haiwezi kuthubutu kabisa kushughulikia wale waliosababisha upotevu huo wa fedha za nchi kwa njia ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, tunahoji usikivu wa Serikali hii ambayo pamoja na kelele zote za wananchi walioiweka madarakani kutaka watuhumiwa ujisadi kupimwa kwa kipimo kilekile katika mizani ya sheria na utoaji haki, kama wanavyofanyiwa Watanzania wengine wanyonge, bado Serikali imetia masikio pamba na kufumba macho yake kwa mikono, kwamba haiwaoni mafisadi hao wala haisikii kelele za wenye nchi.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali zinazotokana na utafiti na uchambuzi wa kina, zimeweka wazi wahusika wa kashfa ya ununuzi wa rada, zikieleza mchakato mzima namna wizi huo ulivyofanyika, ukiwahuhsisha Watanzania, wengine wakiwa ni viongozi waandamizi wa Serikali ya CCM na sasa Watanzania wanashangaa kuona watuhumiwa haohao waliopaswa kuwa mikononi mwa sheria, sasa wanachaguliwa kuongoza mhimili muhimu wa Bunge!

Kambi Rasmi ya Upinzani tunahoji, je, hii ni dalili ya kuwa dola imetekwa na mafisadi? (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa zilizoandikwa na vyombo mbalimbali vya habari kuwa kuna zaidi ya shilingi bilioni 315 kwenye Mabenki ya nchini Uswisi na wanaotuhumiwa na fedha hizi ni pamoja na wanasiasa na wafanyabiashara wa Tanzania. Aidha, taarifa hizo zinabainisha kuwa sehemu ya fedha hizo imetokana na uwekezaji unaofanywa kwenye sekta ya gesi na mafuta nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua nini msimamo wa Serikali kuhusiana na tuhuma hizi na Wizara ilichukua hatua gani katika kufuatilia tuhuma hizi nzito.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za Rushwa ya Rada. Taarifa za Serikali zinaeleza kuwa fedha za Rada zilizokuwa zimeporwa na Kampuni ya *BAE Systems* ya Uingereza inayotengeneza na kuuza vifaa vya kijeshi ilirejesha shilingi bilioni 72.3 ili zitumike katika sekta ya elimu. Katika Kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alisema, nanukuuu:-

“...Serikali ya Uingereza na Serikali yetu zilljadiliana na kukubaliana kuwa ni vema fedha hizi za wananchi wa Tanzania zikarejeshwa kupitia Serikali ya Tanzania. Serikali hizi mbili zilikubaliana kuwa fedha hizo zitumike kwenye Sekta ya Elimu. Mpango huo ulikuwa moja ya ushahidi muhimu uliotolewa Mahakamani kumshawishi Jaji kutoa uamuzi wa kuridhia makubaliano kati ya SFO na BAE Kununua vitabu milioni 4.4 kwa ajili ya wanafunzi, vitabu 192,000 Kwa ajili ya Walimu

kufundishia, madawati 200,000, kujenga nyumba 1,196 za Walimu wa shule za msingi vijijiini, kujenga vyoo 200,000 kwenye shule za msingi".

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika sana kwamba, Serikali yetu imekiuka makubaliano ya namna ya kuzitumia fedha hizo, kama yalivyofikiwa Mahakamani, hali ambayo ni sawa na kusema kuwa lengo lilikuwa kumdanganya Jaji ili fedha hizo zirejeshwe Serikalini na hasa ikizingatiwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani, wananchi na wadau mbalimbali walipinga fedha hizo kurejeshwa kupitia Serikalini kwani tulijua kwa uhakika kuwa hazitatumika kwa malengo tarajiwa kama ambavyo sasa imedhihirika.

Mheshimiwa Spika, lakini habari mbaya zaidi katika matumizi ya chenji hii iliyotokana na kashfa ya viongozi wa Serikali hii kuhongwa, taarifa za Serikali ambazo mpaka sasa hazijabadilishwa ni kwamba zabuni ya kuchapa vitabu ilitolewa kwa Kampuni ya Kiingereza ya *Oxford University Press*, kwa maana hiyo fedha zote hizi kwa kiwango cha thamani ya vitabu zitarudi Uingereza.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kwamba msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani ni kutaka kuona zabuni ya hiyo itolewe kwa wachapaji wa vitabu wa ndani na sio Waingereza, ili fedha hizo zibakie kwenye uchumi wa ndani kwa kiasi kikubwa, bado tunahoji ni kwa nini mpaka sasa Serikali haijabatilisha maamuzi yake ya kuipatia kampuni hiyo ya kiingereza kazi ya kuchapisha vitabu hivyo baada ya kukumbwa na kashfa

inayofanana na namna *BAE* walivyofanya wakati wa 'deal' ya kuuza rada. Kwa sasa tayari Kampuni hiyo imefungiwa (*blacklisted*) na Benki ya Dunia pamoja na mamlaka ya manunuzi nchini (*PPRA*).

Mheshimiwa Spika, kufungiwa kwa kampuni hii ambayo ilikuwa imepewa zabuni ya fedha hizo za rushwa ya rada, ni dalili moja tu ya wazi inayothibitisha wasiwasi waliokuwa nao Watanzania wengi namna ambavyo chenji hizo zilizotokana na vitendo vya kifisadi zitakavyoweza kusimamiwa bila kuhujumiwa kifisadi, jambo ambalo ni tabia sugu ya Serikali hii ya CCM. Tayari tumeanza kwa mguu mbaya, tunakokwenda mbele katika matumizi ya fedha hizi inaweza kuwa giza tupu, ikizingatiwa kuwa mmoja wa watuhumiwa wa kashfa hiyo kubwa ndiye kwa namna moja ama nyingine anapaswa kuzisimamia namna zinavyotumika, hii ni zaidi ya ajabu!

Mheshimiwa Spika, kashfa ya fedha za Posho za Safari ya Rais. Hivi karibuni kuliandikwa habari juu ya ujisadi uliotokea ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika gazeti mahiri kwa habari za uchunguzi la Mwanahalisi kuwa fedha zillizotengwa kwa ajili ya kugharamia safari za Rais Dkt. Jakaya Kikwete nje ya nchi zimeibwa. Baada ya taarifa hizo za utafiti wa kina kutolewa, haraka Waziri wa Mambo ya Nje, alijitokeza na kusema kuwa utafanyika uchunguzi kubaini kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya siku chache Waziri Membe akajitokeza na ambapo safari hii alinukuliwa akisema kuwa baada ya uchunguzi wa mwanzo

imebainika kuwa fedha hizo shilingi bilioni 3.5 zilizotengwa kwa ajili ya safari za Rais ndani na nje ya nchi, zipo salama hazijaibwa, bali kilichojojitokeza ni kasoro na taratibu za fedha zilizokiuwa na hakuna dalili zozote za wizi.

Mheshimiwa Spika, Gazeti la Mwananchi lilimnukuu Waziri Membe akisema kwamba baada ya Kamati aliyounda kumaliza uchunguzi wa mwanzo, ameiagiza kumaliza kazi hiyo mapema iwezekanavyo ili kubainisha kasoro zilizojitokeza. "Kasoro hizo tutakapozibaini, tutatoa barua za karipio kali kwa wahusika, hivyo wafanyakazi wa Wizara yangu kuweni na amani kwani hakuna aliyehusika."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kusikia Kauli ya Serikali juu ya tuhuma hizi za ujisadi ambao sasa unaonekana kukithiri hadi fedha za Rais za safiri nazo zinajisadiwa, kwa sababu kwa nukuu hizi inaonekana dhahiri Waziri Membe anajichanganya. Hatujui hali hii ya Waziri kuwa na tabia ya kutoa kauli zenye utata, zina lengo gani. Aidha, tunamtaka Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na fedha hizi kwani ni aibu kwa taifa na taarifa yake itolewe hadharani.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu hivi karibuni pia Waziri huyuhuyu alinukuliwa akisema anawataka watuhumiwa wa kashfa ya ujisadi wa rada wajitokeze wao wenyewe la sivyo atawataja!

Mheshimiwa Spika, tunapenda kumtaarifu Waziri husika kuwa watuhumiwa kashfa hiyo mbali ya kutajwa

katika kitabu hicho alichokinukuu, wametajwa na kuzungumzwa kwa kina katika Orodha ya Mafisadi iliyotangazwa pia na CHADEMA, mwaka 2007, Viwanja vya Mwembeyanga. Hivyo, badala ya Waziri huyu kutumia kipindi cha propaganda za CCM na Serikali yake kutishia kutaja majina, tunamwambia majina yapo siku nyingi, Serikali itoe kauli hapa inachukua hatua gani dhidi ya watuhumiwa hao?

Mheshimiwa Spika, ushirikiano baina ya *SADC* na *BRICS*. *BRICS* ni ushirikiano wa nchi ambazo kutokana na kukua kwa maendeleo ya viwanda, sayansi na kukua kwa kasi kwa uchumi wa mataifa hayo kwa sasa, kuzikimbilia nchi za dunia ya kwanza ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zikiitwa nchi zilizoendelea. *BRICS* inaundwa na nchi za Brazil, Russia, India, China na *South Africa*. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mpaka sasa Serikali imeweka mikakati gani ili Watanzania wanufaika kwa kiasi kinachotakiwa kutoka katika soko linalotokana na umoja wa nchi hizo tano, ambazo hakika zinapaswa kuwa mfano wa kupigiwa upatu kwa namna ambavyo Serikali zake zimepambana kutoka katika hali ya chini katika maendeleo ya uchumi mpaka sasa zinatishia mstakabali kwa mataifa makubwa. Aidha, pamoja na kuitaka Serikali kutupatia mikakati ya namna ambavyo taifa limejipanga kunufaika katika soko la *BRICS* ambalo wataalam wa utafiti wanasema sasa lina watu takribani bilioni tatu (3), ambao kwa vyovyote vile ni soko kubwa na muhimu, bado tunaendelea kuitahadharisha Serikali hii kuwa makini katika ushirikiano na jumuiya yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana katika mahusiano yetu na nchi au jumuiya yoyote, iwe *BRICS*, iwe *EU*, au katika mahusiano yoyote ya kibashara kama *AGOA* na *EPA*, jambo la kujiuliza ni kama uwekezaji kutoka nje ya nchi ni kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu kukua kiuchumi au ni njia tu nyingine ya kuendeleza ukoloni mamboleo kwa kuchuma rasilimali zetu kupeleka kwao, Ulaya au Asia?

Mheshimiwa Spika, tunayasema haya kwa sababu ni ukweli unaodhihirishwa katika mijadala, uchambuzi na tafiti mbalimbali kuwa wenzetu wa nje, kuanzia wale wa zamani kutoka Ulaya hadi hawa wa sasa kutoka Asia, Latini America na Amerika Kusini, pamoja na nia nzuri kama sehemu ya mahusiano yao na sisi, lakini pia wamekuwa na mikakati ya siri ya wao kunufaika na rasilimali za Afrika kuliko Afrika yenye.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kujitathimini na Utawala Bora Afrika (*APRM*). Mpango wa *APRM* ungeweza kuisaidia nchi yetu kufikia malengo ya Dira ya Taifa, malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Milenia, iwapo Serikali hii ingekuwa makini katika masuala ya maendeleo na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo mpango huu unaendeshwa nchini itakuwa ni vigumu sana kuweza kufikia malengo tarajiwa; mathalani katika mwaka wa fedha unaoisha, *APRM* Tanzania waliomba jumla ya fedha shilingi bilioni 3.835 kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali iliyokuwa

imepangwa ili kutekeleza wajibu wake wa kutusaidia kujitathmini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wajibu mkubwa walionao, mpaka mwaka wa fedha ukielekea mwisho, mpango huu ulikuwa umepelekewa asilimia 53 ya bajeti ambayo ni shilingi bilioni 2.04. Kwa vyovytote vile haimhitaji mtu kuwa mchumi wa kiwango cha juu kujua kuwa *APRM-Tanzania*, haikuweza kutimiza majukumu yake inavyotakiwa kwa sababu kiwango hiki kilikuwa hakitoshi.

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali itoe kauli juu ya tatizo la fedha ambalo limekuwa ni jambo la kawaida sasa tangu mpango huu uanze kufanya kazi hapa nchini, lakini pia Serikali inawajibika kusema hapa Bungeni ni namna gani majukumu ya *APRM-Tanzania* ambayo yameathiriwa na kushindwa kufanyika kinyume kabisa na Mkataba wa *APRM-AU* unavyohitaji na je majukumu hayo sasa yatafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, mbali ya suala hilo la kutopata fedha kadri inavyotakiwa kuendelea kukwaza shughuli za *APRM-Tanzania*, lipo suala lingine ambalo bila shaka linatutia aibu mbele ya watu wengine wa mataifa ya nje na linatia doa nia (kama kweli ipo) ya kujifanyia tathmini katika masuala ya utawala bora na hatimaye maendeleo ya watu wetu, nalo ni deni la miaka minane tunalodaiwa na Makao Makuu ya *APRM* (Sekretarieti) kama michango ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka maelezo ya Serikali ni kwa nini mathalani

mpaka sasa, pamoja na mwaka huu tunadaiwa Dola za Marekani 800,000. Ni hali ya kusikitisha kwamba Tanzania ambayo kwa muda mrefu imejjengea heshima katika kutekeleza makubaliano ya Kimataifa, katika eneo hili la udhati wa kuchangia uendeshaji wa mpango huu muhimu kwa nchi na Bara zima la Afrika, tumezidiwa na nchi kama Msumbiji, Burkina Faso, Mali, Kenya, Uganda, Lesotho, Ghana, Benin na nyingine katika kulipia michango yao ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikatoa kauli kwa nini tumefika mahali Tanzania inashindana katika nafasi za mwishomwisho katika masuala muhimu kama haya na nchi kama, Sao Tome & Principe, Sierra Leone, Mauritius, Kongo na Djibout? Serikali imechukua hatua gani kuondokana na aibu hii ambayo ilianikwa hadharani mbele ya Wakuu wa Nchi, kwenye Ripoti ya *APRM* mwaka 2010? Kambi Rasmi ya Upinzani hatukubaliani na udhalilishaji huu ambao unatendeka dhidi ya nchi yetu mbele ya nchi nyingine kwani huku kuendelea kudaiwa na ripoti kuendelea kutusema inatufanya tukose sauti kwenye masuala muhimu Barani Afrika na haikubaliki tena kamwe.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka huu, Serikali imeendelea kupuuza umuhimu wa *APRM*. Ujisoma katika randama ya bajeti, hakuna mahali popote ambapo mpango huu umepangiwa fungu. Kwa hiyo, ukiongeza na masuala mengine hapo juu ya kupangiwa fedha pungufu na Serikali kutokuwa tayari kulipa ada kama inavyotakiwa, kwa pamoja inadhahirika kuwa Tanzania, kupitia Serikali ya CCM, haina nia ya kujitathmini juu ya masuala ya utawala

bora, hivyo inaweza kuwa nchi ya kwanza kufunga ofisi za *APRM* hapa nchini!

Mheshimiwa Spika, ni vyema Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa akaliambia Bunge hili ahadi mbili alizozitoa Bungeni hapa zimefikia wapi; kwanza aliahidi kuwa ataileta ripoti ya *APRM* hapa Bungeni. Mpaka sasa hatujaona utekelezaji wa suala hilo; tunazo taarifa kuwa Tanzania tayari imeshabitisha kuwasilisha ripoti yake Januari mwaka ujao, je, lini italetwa hapa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, ahadi ya pili ni kuwa watafanya utafiti ili sasa *APRM* iwe na hadhi ya kisheria, lakini mpaka sasa hili nalo halijafanyika, tofauti na nchi zingine kama Kenya au Uganda, hali ambayo inafanya Tanzania kutoweza kutekeleza mapendekezo au maagizo ya *APRM*. Hali hii nayo inavunja mkataba wa *APRM-AU* na miongozo ya kiutendaji ambayo tumeridhia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani hatukubaliani na mwenendo huu kwani ni kuendelea kumdhaliisha Rais wetu anapokuwa kwenye vikao vya *APRM*. Kila siku ripoti zikitoka zinaonyesha kuwa tunadaiwa deni kwa kipindi cha miaka nane (8) sasa na huku nchi ndogo zikiwa zinatusema tena nyingine zimetoka kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe, uzembe huu kamwe hatukubaliani nao na hatuko sehemu yake na ndio sababu nchi yetu inakosa ushawishi na sauti yake mbele ya Mataifa ya Ulimwengu huu.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la *APRM* mwaka 2006, wajumbe wa Baraza hili ambao jumla yake ni 20 na ambao kimsingi ndio wenye jukumu la kusimamia utendaji kazi wa Sekretarieti ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi, wameteuliwa kwa muda usiokuwa na ukomo isipokuwa kwa upande wa wawakilishi wa Bunge ambao wana ukomo wa muda.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wajumbe hawa kutokuwa na ukomo wa muda wa kukaa kwenye nafasi zao, kumelifanya Baraza hili kuwa na mawazo yaleyale na utendaji wake ni uleule kutokana na kuwa na wajumbe walewale na ambao barua zao za uteuzi ziliwateua kwa kipindi kisichokuwa na ukomo. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza sasa ni wakati muafaka kwa wajumbe wa Baraza hili kuanza kupimwa utendaji wao wa kazi na wawe wanateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kama inavyofanyika kwa wawakilishi wa Bunge na baada ya hapo wanaweza kuteuliwa ama kuachwa kulingana na utendaji wao wa kazi. Hii italisaidia Baraza kuwa na mawazo mapya na hivyo kuboresha utendaji wake kuwa wa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ipo Ripoti ya Ndani (*Country Self Assessment Report*) ambayo iliandaliwa na Baraza na kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya *APRM* ya Umoja wa Afrika tarehe 14 mwezi Julai 2009. Ripoti hiyo ilibaini mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali katika miaka mitano. Aidha, ripoti ilibaini upungufu wa utawala bora nchini ambao unatakiwa kufanyiwa kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iiwasilishe ripoti hiyo hapa

Bungeni na kuweza kujadiliwa ili tuweze kujitathimini na kupanga mpango wa kuondoa upungufu iliobainika kwenye tathimini hiyo kwa ajili ya kukuza demokrasia hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waishio nje ya nchi na Vitambulisho vya Uraia. Zoezi la Vitambulisho vya Uraia limeanza hapa nchini mwetu kwa Watanzania kuanza kujiandikisha kwenye Jiji la Dar Es Salaam na kisha zoezi litaendela kwa nchi nzima ili kila mwenye umri wa miaka 18 aweze kujiandikisha na kupata Kitambulisho cha Uraia.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa taarifa zilizopo ni kuwa zoezi hili la vitambulisho litahusika moja kwa moja na haki ya kupiga kura na mpaka sasa haujatangazwa utaratibu wowote ule wa wazi ni jinsi gani Watanzania waishio nje ya nchi watakavyoweza kushiriki katika zoezi hili. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu Wizara imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa Watanzania waishio nje ya nchi wanapata fursa ya kujiandikisha na kupata Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya Kimataifa. Kumekuwapo na changamoto nyingi kutokana na migogoro mbalimbali ya kimataifa ambayo imeendelea kuutikisa Ulimwengu kwa kipindi cha hivi karibuni na migogoro hii imekuwa ikichochewa na Mataifa makubwa ya Magharibi. Kutokana na migogoro hii ya Kimataifa, Tanzania kwa sasa haijulikani iko upande gani kati ya wanaoonewa na wale wanaoonea kwani kwa miaka ya hivi karibuni tumekuwa na utamaduni wa kukaa kimya na

kuachana na utamaduni wetu wa kusema na kuonyesha tuko upande gani. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua nini msimamo wa Tanzania kuhusiana na migogoro kama ule wa Syria, Iran, Korea Kusini na Korea ya Kaskazini. Tuko upande upi hasa?

Mheshimiwa Spika, upo mgogoro baina yetu na nchi ya Malawi kuhusiana na umiliki wa Ziwa Nyasa na rasilimali zake na huu ni mgogoro wa muda mrefu ambao unatishia amani na usalama wa nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani, inaamini kuwa Serikali itatoa taarifa ya kina kuhusiana na mgogoro huu na hatua ambazo kama Taifa tutachukua ili kuweza kuumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida, safari hii wanaotaka kuchangia Wizara hii wamejitokeza wengi sana lakini Wizara hii ni ya siku moja. Kwa hiyo nitaanza na Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Cynthia Ngoye, nafikiri watatosha kwa asubuhi hii.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niwe *genuine* kwa sababu nitakachokiongea nimekiona kwa macho yangu na pengine kwa sababu tulikuwa tumetawanyika...

SPIKA: Wewe sema tu ni Mjumbe wa Kamati hiyo basi.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi ni Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa katika Balozi zetu ambazo zipo nje. Matatizo mengi yamezungumzwa kwenye taarifa yetu ya Kamati, pamoja na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amezungumza baadhi, lakini napenda kuzungumzia hasa matatizo ambayo nimeona ni kero na ni matatizo ambayo yanawafanya Mabalozi wetu wakose imani na Serikali yao ambayo imewapeleka kule.

Mheshimiwa Spika, tuna majengo ambayo yalinunuliwa na Mabalozi ambao wamepita miaka ya nyuma, lakini cha kushangaza bajeti tunaipitisha hapa lakini majengo haya hayatengewi fedha kwa ajili ya *maintenance*. Balozi tulizokuwa tumekwenda, kuna hali ya hewa tofauti, kila baada ya *summer* kwa mfano, kunatakiwa kufanyiwe *service* kama *cooling* au kama ni *heating*, lakini *service* hizo hazifanyiki matokeo yake majengo yanaharibika na wanapata shida sana misimu hiyo inapokuwa imeingia.

Mheshimiwa Spika, kuna nyumba ya Balozi wa Canada, nyumba hii ina matatizo makubwa sana lakini Wizara imetuma pesa kama sikosei ni dola laki tatu na kitu hivi, mpaka leo hawajaanza matengenezo wanadai kwamba wametuma barua wapatiwe kibali cha kumwondoa Balozi pale ili wamtafutie sehemu nyingine waanze kuitengeneza kabla ya kipindi cha *winter hakijaanza* mpaka leo hii, hizo hela zipo zimekaa na Wizara haijawajibu na wanashindwa kuifanyia matengenezo nyumba hiyo. Sijui Wizara ina mpango gani na matengenezo ya hizo nyumba kwa sababu tunazo *assets* nzuri lakini tunashindwa kuzi-*maintain*.

Mheshimiwa Spika, Ubalozi wa Washington, pale tuna Ubalozi wa zamani. Ubalozi huo tungeufanyia *maintenance* ungeweza kuiingizia nchi dola laki nne kwa mwaka lakini mpaka leo hii tumefika pale, nyumba ina majani, nyumba imebomoka lakini inakaa pale na Serikali ya Marekani wameshasema hii nyumba wanatakiwa waitengeneze lakini mpaka sasa hivi hakuna hatua iliyochukuliwa, matokeo yake tunakosa hicho kipato na kubaki kuadhalilisha Mabalozi ambao wanakaa huko.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie suala la magari, kwa kweli Mabalozi wetu wanadhalilika sana. Kuna Balozi mmoja katika nchi hizo za Ulaya wenyewe wana mtindo wa kupokeana, kwa mfano Balozi akiteuliwa kwa mfano wa Afrika, Mabalozi wengine wa Afrika wanaenda kumpokea. Katika kwenda kumpokea mgeni ni lazima atangulie kwenye msafara, ametoka nje vizuri *airport Benz* nyingi, nzuri zimepangana pale nje, kulikuwepo na kibenzi kimoja

kibaya kibaya hivi, sasa akawa anasema mwenyewe hichi kibenzi hiki sijui cha wapi mbona kibaya hivi! Huwezi kuamini hicho kibenzi ndyo kilikuja kumchukua yeye Balozi wetu wa Tanzania ndyo kikaongoza msafara. Kwa kweli alifedheheka sana, alisikitika sana ni kwa nini Serikali yetu ya Tanzania inawasahau hata kwa vitendea kazi. Wanaendaje kuwakilisha nchi zetu wakati hawana usafiri? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, inafikia kipindi hata Mabalozi wanakosa fedha za mafuta inabidi apande usafiri wa *public*, kitu ambacho kinadhalilisha sana nchi yetu na kinadhalilisha Mabalozi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Visa ambalo limejitokeza na tumelizungumza kwenye taarifa yetu. Kuna mji mmoja unaitwa Nice, kuna Mzungu mmoja yeye anagonga Visa kwa mhuri, ninataka kuiuliza Serikali, huyu mtu mniamfahamu? Anagonga Visa ngapi na hizo hela zinaingia kama zilivyo na nani anayedhibiti kwamba leo au mwezi huu amegonga Visa kadhaa. Hii ni mianya inayosababisha kukosa mapato mengi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo Mzungu huyu kuna mashine ambayo ni ya kutolea *Visa Sticker*, iko Paris wala siyo mbali, anadai kwamba hawezi kwenda kuichukua kwa sababu ofisi yake ni ndogo, najiuliza kwamba yeye ni tembo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napata wasiwasi kwa sababu naweza kusema inawezekana ni mchezo unaofanyika sisi hatuuju labda tunacheza ngoma tusiyoijua.

Matatizo haya yameonekana tena Milan, Visa zinagongwa kwa mhuri, unahakiki vipi hizi *Visa* kama unagonga kwa mhuri? Una uhakika gani kama mapato unayoyapata kweli yanatokana na hizo *Visa*?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limeonekana tena Australia, kuna tatizo hili pia na mashine iko Japan wanadai kwamba hawana pesa ya kuipeleka, lakini bahati nzuri juzi tulikuwa na Waziri wa Mambo ya Nje, akasema hilo ni tatizo la Wizara ya Fedha. Hizo mashine zinawekwa na Wizara ya Fedha. Nataka kujua kwa nini Wizara ya Fedha inafanya nchi ikose mapato kwa kutokwenda kuweka hizo mashine sehemu husika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa hao Mabalozi wa Heshima watumie hizo mashine, *Visa Sticker* siyo kugonga mihuri ili tuweze kujua ni kiasi gani cha maduhuli yanayopotea na kiasi gani cha maduhuli Serikali inapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nzungumzie suala la Diplomasia ya Uchumi pamoja na utalii. Wizara pamoja na Kamati tumelalamika kuhusu suala hili. Pamoja na kutengewa pesa ndogo kwenye hii Diplomasia ya Uchumi, bado kwenye Balozi zetu hatuna watendaji wala hawa Waambata wa Uchumi, tunategemea kitu gani? Hakuna watu wanaoshughulikia utalii, hakuna Waambata wa Uchumi bado tunalia habari ya Diplomasia ya Uchumi, hatuko *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tufanye kazi kwa vitendo, tunalalamika tu pesa hazitoshi, kama fedha

hazitosh, unazipeleka wapi wakati hauna Waambata wa Uchumi kwenye Balozi zako? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie suala la rada. Mimi nilikuwa nataka Serikali kwa sababu nilishawahi kumsikia Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje akisema anawafahamu kwa majina, tumepata chenji, ndio tuwajue, kama anawafahamu kwa majina leo hii naomba awaambie Watanzania ni akina nani ambao walihusika na kuiibia Serikali katika tukio hilo la rada? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ubalozi wa *Paris*. Ni jambo la aibu, tumepanga katika Ubalozi wa Uganda, Idd Amin alinunua jengo zuri sana pale. Cha kushangaza zaidi Ubalozi ule wa Uganda kwanza pale tuna deni tunadaiwa matokeo yake yule Balozi wetu amekuwa akijificha, akimwona Balozi mwenzie anajificha, anaogopa. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa sababu dakika 10 ni kidogo sana, nianze kwa kukushukuru wewe.

Mheshimiwa Spika, naenda moja kwa moja kwenye ziara yetu ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje. Nashukuru wewe na Katibu kwa ushirikiano mliotupa na kutuwezesha kuzunguka kutathimini kazi kwenye Balozi kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana pia Waziri pamoja na Naibu wake. Jamani mimi nasikitishwa sana nikiona kwenye vyombo vya habari mnavyoandika, Waziri Bernard Membe anashirikiana na Kamati vizuri. Kila jambo tunafanya naye jamani, mimi nashangaa mnavyogeuza maandishi na kusema mambo mengine, huwa ana taarifa na anatupa maelekezo na kutueleza twende wapi, wapi tusiende, inasikitisha sana tunapoona mambo yanakuwa tofauti. Sisi jamani Wabunge tuko hapa kushirikiana na Mawaziri kuhakikisha kwamba nchi yetu inafikia mahali katika medani ya kimataifa na wananchi wananza. Sasa haya mambo naomba yafike mwisho.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, pamoja na Wakurugenzi wote ambao wengi wote ni Mabalozi. Kwa kweli wanashirikiana vizuri na sisi tatizo ni mfumo mzima na bajeti ndogo. Nawapongeza sana Mabalozi na Maafisa wote katika nchi zote ambazo Kamati yetu imepita, tumepewa ushirikiano wa ajabu, hii ilifanikiwa kutokana na barua zilizotoka Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwenye hizo Balozi kuwaarifu ujio wetu, madhumuni na kila kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba niseme napongeza wote, naomba nipongeze pia uteuzi wa Mabalozi wanawake umefanyika kwa sana. Naenda kifupi kifupi kwa sababu ya muda. Naomba nichukue fursa hii pia kupongeza sana APRM, Katibu Mtendaji Rehema na Watendaji wake ambao wakati wa ujio wa ile timu ya tathimini kwa kweli walifanya kazi kubwa na ya kusifika kwa Tanzania. Walituhusisha Kamati pamoja

na Baraza lenyewe ambalo liko chini ya Profesa Hassa Mlawa. Niombe tu kusema kwa kweli nashukuru baada ya ile tathimini kama *APRM* ingehamia chini ya Mipango ingeleta maana kwa sababu wale wanajua masuala yote, kwa sababu mengi wanayotathimini ni kuhusu mambo ambayo yanaendana na mipango na nchi kadhaa iko katika Idara ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe pia pamoja na kazi nzuri wanayofanya lakini wajumbe wa Baraza wawe na ukomo wa muda kama ambavyo Wabunge wanakuwa na ukomo kwa sababu wale wamekuweko muda mrefu na ni vema pia tukawa na mawazo mapya kila mara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana walioandaa ziara ya Morocco, ziara ya Morocco ndugu zangu hatuna tu muda wa kusema lakini wale watu wana fursa nyingi sana za kimaendeleo kwa ajili yetu. Wako tayari, wametoa *scholarship*, tumeshindwa kuzitumia, zimerudi. Wamejitahidi kwenye maeneo mengi. Sisi kama Wabunge haya masuala mengine ambayo tunaheshimu ya nchi yetu, Serikali yetu, *AU*, *UN* tunayaheshimu, sisi kama Wabunge tunashirikiana kuweza kufanya kazi kwa pamoja kuishauri Serikali yetu katika mambo ya maendeleo. Tunaheshimu mkakati unaoendelea lakini kama Wabunge, tunaendelea kushirikiana na hivi punde tu mtaona Wabunge wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje wa Morocco watafika hapa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto, jamani mimi naomba niseme, mimi huwa ni msema

ukweli, tumekwenda Marekani, Canada jamani sifa ambazo Mheshimiwa Jakaya Kikwete ametuwekea Tanzania ni za kutukuka, jamani naomba tumpongeze. Tunasifiwa sana hata Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ameweka jina zuri kule jamani Tanzania tunasikika. Mimi mtu aki-*generalize* na kusema kwamba Tanzania sijui tumefanya nini, mimi nitabishana kwa sababu nimeona, tumeingia *State Department* kama mambo ya nchi za nje ya Marekani, tumekwenda kuonana na asasi mbalimbali za biashara maofisi mbalimbali na Canada, wote walikuwa wanasema jamani Tanzania *you are special*. Kinachoharibu tu ni kimoja, Rais ana nia nzuri, amefanya kazi nzuri sana lakini sasa utekelezaji wake, sisi huku chini ambao tunatekeleza inabidi tuangaliane. Wenzangu wamesema watumishi, kwa kweli kuna haja kwenye Balozi ambazo tunazitegemea sana kwa mambo ya uchumi, kwa kweli naomba tuweke watu madhubuti. Sisemi walioko siyo madhubuti lakini nahisi kama wana pengo kubwa. Niwaombe sana Idara ya Utumishi, tushirikiane na Idara ya Ajira pamoja na *Foreign* mchague watu ambao wakienda kule unasema hii ni Tanzania, wanasema wenyewe Tanzania mko *passive*, mna- *miss out*. Yuko mtu mmoja tu bwana Mafongo, ana shirika na *Bretton Woods*, huyu alikuwa hawezি kushiriki na masuala yote hayo mengine ya uwekezaji, utalii na biashara. Kwa hiyo, mimi naomba sana tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, maisha bora yanawezekana, nimeamini alichokuwa anasema ni sisi wenyewe tunakwamisha.

Mheshimiwa Spika, niwaeleze kwa nini kuna nafasi kule, kumbe katika Umoja wa Mataifa kuna Kamati

ambayo inashughulika na uzalishaji wa pamba, maslahi yote ya pamba, uuzaji, soko na kila kitu. Jamani ndugu zangu Watanzania niombe niseme pamoja na kwamba tunasikia kuna mwakilishi wa Bodi ya Pamba anatoka hapa kila mwaka kwenye hiyo mikutano hamwezi kuamini mwaka huu Januari mpaka Desemba, Mwenyekiti wa hiyo Kamati ni Tanzania. Sisi tunapiga kelele hapa tuna shida ya masoko, tuna shida ya nini, kumbe Mwenyekiti kule ni Tanzania, hata faida moja? Wenzetu wakiwa kwenye madaraka wanahakikisha nchi yao inanufaika. *Nothing has been done* ndio maana nasema maisha bora inawezekana tunakwamisha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu kutokana na *initiative* ya Mheshimiwa Dkt. Koffi Annan alianzisha kikao fulani cha wawekezaji, wanakuja wawekezaji kwenye sekta ya kilimo na sisi hapa tunasema sekta ya kilimo ndio uti wa mgongo, hiyo ilikuwa ifanyike Ghana mwaka 2010 kwa heshima ya yale yaliyo mema ambayo Tanzania inayafanya ambayo Rais wetu ameanza kueleza na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na wengine wote inakuja Tanzania tarehe 26 mpaka tarehe 28 Septemba. Tulisikitika kuambiwa kwamba Sekretarieti wanaondaa iko Kenya inaitwa AGRA. Halafu licha ya hivyo ni kwamba wao wameshaandaa, kuna *manual* inaandaliwa kama *directory* ya majina, Kenya zilikuwa kampuni si chini ya 100 zimeshajiorodhesha, Rwanda, Uganda, Tanzania zilikuwa sijui mbili au tatu, tukachukua jukumu, tukasema tupeni muda tunakwenda Tanzania zitaandikishwa. Mimi niombe kupitia jukwaa hili, wale wote wadau wenyewe makampuni, kiingilio ni dola 300

Iakini naomba Serikali mfanye utaratibu angalau hii iweze kusogezwa, haiwezekani kitu kama hiki kinaletwa Tanzania halafu sisi tumelala, masuala ya kilimo ndio kipaumbele. Mimi Kilindi tumeshajipanga tunakwenda huko, tutakuwepo kwa sababu na sisi tunalima sana mazao mengi, naomba wadau wote mfike Arusha. Halafu niombe Serikali, hii ndio fursa ya kujitangaza, maandalizi yalishafanyika, Sekretarieti ya Kenya iliandaa mpaka ulinzi, Marais 14 wanakuja, iliandaa magari, aliyekuwa anatoa usafiri wote ni Mkenya, mambo yote yalikuwa yamefanyika Iakini kwa jitihada za Kamati hii na safari hii sasa hivi Tanzania wako *full fledged*, wameingia ndani na wanahakikisha kwamba tunafika pale. Tarehe 26 Septemba mpaka tarehe 28, msikose hiyo fursa ndugu zangu Watanzania. Mambo ni mengi mazuri Iakini kwa kweli inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, ila niseme tu kingine ambacho naomba tuombe sasa hivi jamani ukisafiri sana unapata mawazo mapya. Wengi wanasemajje, mimi naomba niwe mkweli, wanasema Watanzania ni hodari sana kwa kujenga uchumi Iakini kwa maneno. Sisi tunaendelea kulumbana, kunyosheana vidole na nini, wenzetu wanakwenda mbele. Mimi naomba pamoja na kwamba tunasema lazima tuseme ili mambo yarekebike, Iakini tuwe mstari mbele kila mtu mwenye nafasi, tuendelee na uchumi, mapato, mapato iwe ni agenda yetu. Sasa hivi tumeagiza chai dola mbili unalipa dola mbili na nusu, unaauliza hii nusu ya nini unaambiwa kodi na hela hizohizo wanafanya maendeleo yao na wanatuletea sisi Afrika. Sasa mimi naomba jamani twende pamoja kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, *mortgage financing* ni muhimu sana jamani, biashara hii zamani ilikuwa inaonekana kwamba Serikali inafanya biashara, lakini naomba sasa hivi tuichukulie kama kitu ambacho ni lazima kifanyike na wakati ni huu.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano kama walivyosema wenzangu na taarifa yetu, jamani mawasiliano naomba waruhusiwe Mabalozi vitu vingine waamue wao kule watoe taarifa. Kwa sababu mpaka vitu vidogo, kitu cha dola 10,000 mpaka apate kibali Tanzania. Kujibu hawajibiwa. Sasa mimi niombe basi kama ni kusimamia kwamba matumizi bora na uadilifu, tuwaruhusu, baadhi ya vitu vingine vitafanyika baadaye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niongelee pia kuhusu fedha ambazo zinakwenda kule kwa mfano kama London safari hii wamepewa 2,300,000,000 na kitu. Lakini hii hela mpaka ifike kule itakuwa imekatwa *by half* kutokana na *exchange rate*. Tufungue *foreign account* basi *Foreign Affairs* ili wale watumishi wapewe *ATM card* halafu hela zao zinaingizwa moja kwa moja, hii itaondoa tatizo hilo. Kwa hiyo, napendekeza hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba pia tuwe na kikao cha kufanya tathimini ya Balozi zetu. Hawa Mabalozi nadhani mwaka wa nne kama siyo wa tano hawajaweza kukutana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na nitatafuta fursa pia ya kutoa hoja ili tuongelee, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Wakati wa Mkutano wa *IPU* uliofanyika Uganda mwaka jana, Serikali ya Uganda ilikodi magari ya Sumri ya Tanzania kama kumi na kitu, tulipanda, yalikuwa ni magari ya Sumri ya Tanzania na kulikuwa na wageni kama 7000 hivi. Kwa hiyo, tumo tu.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niseme naunga mkono bajeti ya Wizara hii. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, lakini pia Katibu Mkuu wa Wizara hii. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Balozi Mushi pamoja na mwenzake Kairuki kwa uteuzi huu wa hivi karibuni. Naamini wataongeza chachu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na uchungu mkubwa sana kuzungumzia juu ya suala la mpaka katika eneo la Ziwa Nyasa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wa kina alioueleza, naamini wananchi wengi hasa wa Mkoa wa Ruvuma waishio kandokando ya Ziwa Nyasa watakuwa wamepata nafasi ya kusikiliza na kujua nini ambacho Serikali yao inakifanya. Hii inanifundisha kwamba kwa sababu katika majibu yote yanazungumzwa kwamba mipaka hii imewekwa katika nyakati tofautitofauti na hata walioweka mipaka ni watu tofauti na sio sisi wenye Tanzania. Kwa hiyo, kimsingi nchi nyingi za Afrika zinapata shida na matatizo kutokana na *influence* ya nchi nyingine lakini

zinapopata haya matatizo zinakaa pbeni na kushawishi upande mwingine kuwa upande mwingine ndio chanzo cha mfarakano. Kwa hiyo, mimi naamini busara zitatumika na hasa ikizingatiwa kwamba wadau wanaokaa katika Ziwa Nyasa, maji ya Ziwa Nyasa ni maisha yao kwa sababu ndimo wanamopata maji ya kunywa, ndimo wanamopata samaki, ndimo wanamoendeshea shughuli zao katika maisha ya kawaida. Kwa hiyo, nategemea kwa sababu kuna baadhi ya watu wanaokaa upande wa Ziwa Nyasa asili yao ni Malawi na kuna watu wanaokaa Malawi asili yao ni upande wa Tanzania, kwa hiyo, hao wote ni ndugu watafikia mahali katika kusuluuhisha jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hiyo haitoshi, ni vema tukaendelea na maandalizi mojawapo ikiwa ni kutengeneza mazingira bora ya usafiri katika maeneo ya Ziwa Nyasa. Barabara zile ni mbaya, zinahitaji kuwekewa kipaumbele kwa sababu ziko mpakani mwa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudi katika suala la Balozi zetu, nashukuru sana, nakushukuru wewe mwenyewe kwa safari ambayo tulikuwa tumekwenda hivi karibuni kwenye mkutano wa SADC Msumbiji. Kwa bahati nzuri nikiwa nimeongoza na Mama Anna Abdallah tukiwa kule tuliona kwamba si vema tukaishia kwenye ule mkutano bila kutembelea Balozi zetu. Nadhani iwe ni utamaduni kwa Waheshimiwa Wabunge wote wanapokwenda nje ya nchi, ni vema pia kuchukua nafasi hiyo ya kutembelea Balozi zetu ili kuwasikiliza wenzenetu kama wana matatizo tuweze kuyaleta badala

ya kusubiri mpaka Kamati husika itakapofanya ziara. Yawezekana kwa sababu nchi ni nyingi hawataweza kumaliza ziara hizo kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji, sisi kule ni matajiri, ni matajiri kwa sababu tunazo nyumba takribani tatu lakini tunalo ghorofa kubwa la *flat 8* pamoja na kiwanja. Kama nyumba hizo zingekuwa katika hali nzuri wasingekuwa na sababu ya kuhitaji fedha kutoka huku nyumbani lakini ukweli ni kwamba hata Ubalozi wetu wenyewe sasa hivi uko katika ofisi ya kupanga. Nyumba ya Mheshimiwa Balozi haikaliki, *fence* imeharibika yaani hata mtoto anaweza akavunja kiasi kwamba hakuna usalama. Balozi imebidi aende akapange.

Mheshimiwa Spika, mimi nilimtania nikasema naona umekimbia nchi kwa sababu hakai tena pale kwake. Tuone na tulipe umuhimu suala hili kwa sababu kwanza Ubalozi wa Msumbiji naamini ni katika nchi rafiki zetu na tunaheshimiana na ninaamini ni Ubalozi endelevu. Kwa bahati nzuri nyumba zile tulivyozitembelea kwa kweli zimejengwa kwa kiwango na ziko katika maeneo ambayo ni *very potential*. Kwa hiyo, zikishughulikiwa zitasaidia sana, hasa lile ghorofa ambalo tayari alishapewa mkandarasi. Kimsingi linahitaji ukarabati wa takribani dola 600,000 mkandarasi tayari yuko *site*, ameshavunjavunja, ameshaanza ukarabati, lakini fedha hazijatumwa. Ana *bond* ya kuchukua fedha za mkopo kutoka kwenye benki zake lakini wanataka wapate *commitment* kutoka nchini kwetu, bado hizo fedha hazijatumwa. Tuliongea na yule mkandarasi, tulimliwaza lakini

nimeona tufikishe ujumbe huu nikiamini kwamba pamoja na kwamba Balozi nyingi zinahitaji matengenezo lakini tuanze na zile ambazo tunaamini baada ya kuzisaidia zitaweza kujitegemea zenyewe. Kwa sababu nyingine tukizisaidia kweli zitaisha lakini hazitaongeza fedha zaidi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kama hujatembelea basi utembelee Msumbiji ukajionee mwenyewe hali halisi iliyopo. Yule mama pale amekwenda, tunashukuru sana alivyotupokea, Balozi Nyaduga lakini kwa kweli anahitaji kusaidiwa ili aweze kufanya vizuri zaidi, kwa sababu namwamini Waziri najua hayo yataweza kutekelezwa vizuri. Kwa sababu ule mkataba bado ni mchanga tu, kadri unavyokaa ina maana unaendelea ku-charge. Kwa hiyo, ni vema tuchukue hatua mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudi katika suala ambalo nimelisikia hivi karibuni kuhusu Watanzania 26 walioshikwa kule Zambia kwa kuishi kinyume na sheria. Afadhali wenzetu wanachukua hatua, kwenye maeneo ya mipakani kama sisi kule Rukwa, maeneo ya Kigoma kuna watu wengi sana wanaoishi kutoka nje ya Tanzania na wanaingia kinyemela kutokana na mipaka yetu kuwa wazi. Eneo la Mkoa wangu wa Rukwa na Mkoa wa Ruvuma kunahitajika sasa kuwekewa uimara wa kuweka Ofisi za Uhamiaji katika maeneo yale ambayo wenzetu wageni itatakiwa wapitie humo. Lakini mipaka iko wazi, ukiangalia mipaka kwanza haina huo udhibiti wa kutosha, lakini pia hata vitengo vyetu vyta kijeshi vyta kutosha haviko katika maeneo hayo. Kwa hiyo, niombe sana, sawa siwezi kuzungumza zaidi sana, lakini kama wenzetu ambao wameonyesha

kwa vitendo kukamata Watanzania ambao wako kule na sisi ifikie mahali tuwaambie waende kwao. Nasema hivyo kwa sababu pia haiishii tu kwamba wamekuja lakini pia *sometimes* wanajiingiza hasa katika masuala ya kisiasa. Kwa hiyo, huwezi ukasema huyu ni nani, huyu nani lakini iko haja sasa na sisi kama Tanzania kujipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba wanaishi katika nchi yao kwa amani lakini kama ni wageni waishi kwa kutambuliwa na kujua kwamba wapo kwa ajili ya shughuli zippi. Hiyo pia inaleta hatari kwa sababu ya Sheria yetu ya Ardhi inayowapa Wenyeviti wa Vijiji kugawa ardhi kwa hiyo watu wakishaingia hapa wanakaa siku mbili, tatu wanakuambia nilitokea Kigoma au nilitokea Tabora, unafikiria ni Mtanzania mwenzio kumbe ni mgeni na anachukua ardhi. Kwa hiyo, ni vema sana pia kuiangalia hiyo Sheria yetu ya Ardhi vizuri ili kuweza kuona ni jinsi gani ugawaji wa ardhi hautaathiri maendeleo ya Watanzania hasa vijana ambao hawana ardhi, wanaishi kwa kutegemea ardhi za wazazi wao na wenyewe wanaona kama wakiwafanyia kazi wazazi wao wanakuwa kama pengine hawalipwi wanaamua kwenda mijini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kusema maneno machache kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wenzangu wamesema mengi, lakini mimi ningependa nzungumze katika maeneo machache sana.

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza hapa ni tazito kubwa liliopo la kutokuwa na maamuzi ya msingi baina ya Serikali na mali zake zilizoko nje. Haiwezekani hata kidogo viongozi waliotutangulia, wamenunua mali, wamenunua nyumba, nyumba katika nchi za nje ni mali kubwa, halafu hazitengenezwi, maana yake ni nini? Mtu yejote anashindwa kuelewa! Ni kama tunadharau rasilimali ambazo tunazo. Katika umasikini huu, nani anatuelewa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati umefika Wizara ya Fedha ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje, watengeneze hizi nyumba zote zilizoko nje. Ni aibu kubwa, unakwenda katika Kituo kikubwa kabisa katika Ofisi zetu zote za Kibalozi, *United Nations*, unakwenda kwenye nyumba unashindwa kuingia ndani na viongozi wanakwenda, wanarudi, inabakia vilevile? Mpaka lini itakuwa hali kama hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi hata siku moja kunyamaza vitu kama hivyo, ni lazima tuseme na tusiwe tunasema kwa kuimba, tuseme ili nyie mpare fursa ya kurekebisha hali. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mie nimeshtuka kidogo hapa katika suala zima la Malawi. Ni kama kwamba tunaanza kutunishiana misuli. Kimsingi, hatugombani na Malawi katika hili, unaposema ndege zinaruka kufanya utafiti, hatugombani na Malawi; ni Mataifa makubwa, ndio yanafanya utafiti. Sasa kama wao wanafanya utafiti wa mafuta na gesi kwao na sisi tuwaite watu wafanye utafiti wa gesi na mafuta kwetu, huo ugomvi

utamalizika kuliko kuwaambia usirushe ndege, nitaitungua, usifanye hivi nitakupiga, vita si suluhisho leo. Katika suala zima la ugomvi huu, mimi nashauri kuwa, hili jambo lazima twende Umoja wa Mataifa. Historia inaonesha migogoro mikubwa kama hii, haimaliziki kwa mazungumzo ya nyumbani. Mtaitana Dar-es-Salaam, *Move-n-Pick*, keshokutwa Arusha, jamaa wakirudi wanafanya vilevile lakini pakiwa pana *guarantor* wa Kimataifa, hili jambo litafikia mwisho. Hao Nigeria na wenzao huko *West Africa*, wasingefikia mwisho hata siku moja na mwisho wangepigana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba hili Serikali isilichukulie kuwa mnaweza kulimaliza kwa mazungumzo ya juu ya meza Dar-es-Salaam, hammalizi, lazima mwende *The Hague*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji. Inaonekana tuna tatizo kidogo. Utamaduni wa kizamani wa kuelekea Ulaya na Nchi za Magharibi, mimi nafikiri sasa tuuangalie upya. Tunapiga foleni kule kuomba misaada na wale jamaa wenyewe tunaowaomba msaada, wao wanakwenda nchi nyingine, wanakwenda China kuchukua mikopo, wanakwenda Mshariki ya Kati, wanakwenda nchi za Asia ya Mbali, sasa na sisi tuuangalie huko, lakini kuwa kila leo tunakwenda kuomba kule msaada, utaambiwa utachangiwa kwenye *Basket Fund*, mwisho wa siku pesa hazifiki. Sasa mimi nashauri, tunapotafuta paka, tusimtafute kwa rangi, tumtafute kwa uwezo wake wa kukamata panya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hapa ambalo kidogo linasikitisha sana. Watumishi wa Ubalozi walioko nje, wana tatizo la maisha. Wale ni wenzetu tuliowapeleka watuwakilishe ugenini, katika hali ya kawaida tu mtu mgeni anahitaji *extra care*. Mgeni hata kutoka nje tu amekuja kwako, unahitaji kumpa *extra care*, je, yule wako ambaye unampeleka ugenini sasa?

Mheshimiwa Spika, sasa inasikitisha sana unapokwenda kwenye Ofisi ya Ubalozi, unasikia mishahara haiendi, posho haziendi, ilhali wenyewe mnaelewa watu wa Wizara, mnaelewa kule kuna vitu mbalimbali wanatakiwa kutumia pesa, watazipata wapi kama hamkuwapa ninyi? Kama hamkuwapelekea *OC* zao, kama hamkuwapelekea mishahara yao kwa wakati, mnategemea wafanye nini? Mwisho wa siku mtakuja kusema wanashiriki kwenye mambo ambayo si ya kawaida na kumbe sababu ni nyie wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini mbaya zaidi, kuna tatizo katika Wizara ya Fedha. Kama Benki Kuu, wanaweza ku-*predict flactuation* ya shilingi ya Tanzania ama itaanguka au itakwenda mbele, kwa nini basi hiyo huitumii ukaweza kutafsiri *exchange rate* ya pesa ambayo unampelekea mtu aliyeko nje? Kila wakati unapeleka pesa, ukiangalia kuna tofauti, pesa ulizopaswa kuzipeleka, lakini kulingana na hali halisi ya *change*, wanapata matatizo. Tabirini kwa kiwango cha juu kabisa cha mabadiliko ambayo mnaweza mkayafikiria yanaweza yakatokea, mpeleke basi hizo pesa katika kiwango hicho, malalamiko yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia zaidi niseme hapa kwenye Wizara. Wizara, inapokuja hapa au inapokuja kwenye Kamati kuomba pesa za bajeti, zile Balozi mbalimbali wanazichukulia kuwa ni *vote*, lakini pesa wakishapewa, wanazichukulia, mimi niseme labda ni *very minor subvote*, wanapeleka pesa wanavyotaka wao. Sasa kila *vote*, iwe *vote* basi pesa zao ziende na ziende katika *rate* inayokubalika, msipeleke pesa leo ambapo mkijua baada ya mwezi mmoja shilingi itakuwa imeanguka pesa zile, watu wale mnawatesa sana. Lazima makisio haya yafanywe kiutaalamu na utaalamu huo mnao. Kwa nini utaalamu mnao halafu mnaumiza watu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamesema jambo hapa na mimi naomba nilikazie. Mheshimiwa Waziri, ninyi ndio mnaotuletea wawekezaji hapa, lakini nyie pia ndio mnapaswa kuangalia maslahi ya Watanzania nje. Sasa kama Wizara kubwa kama hii, Waziri wa Mambo ya Nje, Mwanadiplomasia wa pili katika Nchi, wa kwanza anakuwa Rais, wa pili unakuwa wewe na wewe mwenywewe umekuwa kwenye Ofisi za Kibalozi, hivi kweli hujui watu wanaotuibia pesa zetu ukatuambia? Kweli hujui? Hivi kweli hujui wawekezaji matapeli ukatwambia, unaruhusu wanakuja tu hapa? Mwisho wa siku vinasombwa vitu kama hivi, ambapo kwa maoni yangu na watu wanafanya utafiti, hii ni aibu; ni aibu kubwa sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi hata siku moja tukavumilia nchi inadhalilishwa na watu na nyie mnawajua, mnawanyamazia. Ukija uki-*wind up*, ulichukua ahadi kwa Watanzania, utawatajia wale wote waliohusika na kashfa ya rada. Hata kama nimo mie, nitaje hapa kwenye *podium*, lakini na kama umo wewe mwenyewe useme ulihusika kwa kiasi fulani. Hamwezi kuwaficha waovu kwa sababu tu mnawaonea haya, unamwonea haya nani? Mtu ambaye ikifikia mahali unamficha mtu muovu, humsemi na unamjua, maana yake na wewe mwenyewe unahusika, ndio tafsiri ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sitaki tuzungumze vitu kila wakati tunarudia, ukija uki-*wind up* hapa, waambie Watanzania, kwa sababu, uliwaahidi kuwa unawajua; ni nani na nani waliohusika katika balaa ile? Usifurahie kwenda kuchukua chenji tu, ule ni udhalilishaji mkubwa, ule ni wizi mbaya sana uliofanywa. *Day light robbery* ya namna ile, haiwezekani ikaja ikanyamaziwa, tukawa tunawachekeachekea watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafas ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Pili, naomba niipongeze Wizara pamoja na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba nzuri, ya kina ambayo

imetupa picha kamili ya nini kinachoendelea huko Serikalini.

Mheshimiwa Spika, hakuna Mbunge ambaye atasimama hapa, ambaye amewahi kutembelea nchi za nje, akafika katika Balozi zetu, akaja hapa asisikitishwe na hali halisi ya majengo ya Balozi zetu, hakuna! Hali ile ni *pathetic*, ni mbaya na ni mbaya kweli kweli, wala haitoi picha nzuri kwa Taifa zuri ambalo lina heshima kubwa kimataifa kama Tanzania, kuwakilishwa na nchi yetu ambayo majengo yetu huko nje hayafanani na nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kushauri, ninamwomba Waziri wetu wa Fedha, labda mwenyewe au mtu anayemuamini, amteuwe aende akazitembelee hizi Balozi, ni nyingi lakini afanye kwa awamu; aende akazitembelee, atarudi hapa kwa hakika, mimi ninaamini atatoa maamuzi tofauti na haya mambo yanayofanyika hivi sasa. Ninaomba sana, Serikali, ijaribu kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni nchi gani ambayo unakwenda kutembelea, unasema tuonane na wafanyakazi, wanatafuta mahali pengine ili muweze kuzungumza mambo yenu kwa sababu kule kwenye Ubalozi wao, eti jengo halina nafasi ya kuweza kukaa na kuzungumza. Kwa hiyo, naona hapa pana tatizo. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mtuokoe katika suala hili, wenzeni tunaona aibu. Wale Mabalozi, baadhi yao wako *frustrated*, hawajui hata la kufanya, wanasesma labda kuletwa Ubalozini ni adhabu. Enzi zile mtu ukipelekwa

Ubalozini kwenda kufanya kazi, watu tulikuwa tunawaonea wivu, sio hali ya sasa. Kwa hiyo, naomba marekebisho hayo tuyafanye haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nichangie machache kuhusu mpaka wa nchi yetu na Malawi kupitia Ziwa Nyasa. Hii ni mara ya nne nazungumza hapa Bungeni. Ninasema hivi, hili suala tumelichelewesha sana sisi wenyewe. Wakati wa Utawala wa Awamu ya Kwanza wa Malawi, yule Bwana alishaleta chokochoko; Rais wa Tanzania wakati huo, Marehemu Julius Nyerere, alikemea kwa sauti moja tu, akanyamaza na tangu wakati huo, kukawa kimya.

Mheshimiwa Spika, alipoingia Rais wa Awamu ya Pili, pale ndipo palipotakiwa kuanza mara moja, kuanza mazungumzo ya karibu sana na jambo hili lingekuwa limejirekebisha. Tumelichelewesha sana hili suala mpaka limefikia hatua hiyo tunayoiona hivi sasa. Ni hatua ambayo si nzuri, si nzuri hata kidogo. Kama tulivyosema, kuna wananchi ambao wanaishi kandokando ya Ziwa Nyasa kwa upande wa Tanzania na Waziri amesema wanatumia ziwa lile kwa uchumi wao na wamekuwa wakifanya hivyo tangu mababu zao, leo unawaambia waishi kwa hofu, waishi kwa kutokuwa na matumaini; kwa kweli, jambo hili halipendezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wetu kutoka Wilaya ya Kyela kule kandokando ya ziwa Wilaya ya Ludewa, kandokando ya ziwa Wilaya ya Nyasa na Mbinga, kweli mpaka sasa wanaishi kwa

wasiwasi. Wanaenda kuvua kwa wasiwasi, wanasafiri kwa meli kwa wasiwasi, naomba jambo hili liishe.

Mheshimiwa Spika, huo Mkutano wa tarehe 27 uliofanyika Julai, naomba maamuzi yake yafuatiliwe kwa karibu. Maana ni rahisi kuzungumza tukayaacha, lakini yakifuatiliwa kwa karibu, mimi naona litatusaidia sana. Watu ambao watatusaidia wengine ni wananchi wanaokaa kule, wanaona haya mambo yote. Sisi hizi taarifa zilipotujia, nyangi zilitoka kwa wananchi, lakini ukienda huko mawasiliano yenyewe ni matatizo, hakuna barabara kati ya vijiji ambavyo ni vya Wilaya ya Kyela na Vijiji vya Wilaya ya Mbinga, kati ya Manda na Vijiji vya Kyela, Matema huko, hapo katikati hamna barabara, hamna mawasiliano ya simu, unapelekaje taarifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba sana Wizara hii, iwasiliane na Wizara ya Sayansi na Teknolojia, iwasiliane na TAMISEMI, jamani tuwasaidie wale wananchi wa kule, hawana njia ya kuwasiliana na Serikali. Endapo itatokea, hii kazi tunayowatuma kufanya kwamba wafanye mawasiliano na Serikali, wafanye mawasiliano na huku kwenye vyombo vinavyohusika, watafanyaje hayo mawasiliano? Hawawezi wakafanya kwa sababu miundombinu hiyo ninayoisema hakuna kabisa. Ukienda sehemu zile, ukienda kutembelea sehemu zile, utakaa kule wiki nzima. Ukikaa kule kwa wiki moja, hutafanya mawasiliano na maeneo mengine kwa sababu hakuna simu, hakuna barabara, isipokuwa meli zinazotembea kwenye ziwa hilohilo lenye mgogoro. Sasa hapo kweli kuna usalama? Hamna usalama.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali, ilichukulie suala hili kwa uzito kama walivyoanza kulifanya. Sasa uzi uwe uleule wa ufuatiliaji wa karibu kabisa ili kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, nilipenda niyagusie hayo mawili kwa sababu yana uzito kwangu na kwa Taifa hili ili Tanzania yetu iweze kulinda heshima yake. Tanzania yetu ina jina kubwa iweze kuendelea na heshima hiyo daima milele na milele. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia. *(Makofi)*

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja yetu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ambayo Wizara yake imefanya na tumelona katika kitabu. Tumesikia hotuba yake, ameiandaa vizuri sana, kwa kweli na tumefurahi sana na hasa kwa kuwezesha kupatikana ule mkopo wa kujenga bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, mimi nianze kuzungumzia kwanza jambo moja la hii Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Hii Sera ya Diplomasia ya

Uchumi ni sawasawa na moyo, kwa mtazamo wangu, ni sawasawa na moyo wa Wizara na pengine moyo wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna tatizo moja. Utakapokwenda nchi za nje hasa kwenye Balozi zetu, inasikitisha sana. Hii Sera ya Diplomasia ya Uchumi, haijitokezi wazi katika bajeti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti inayotolewa kwa Wizara yake ni *almost 40 and something percent*. Lakini vilevile ukiangalia kwenye Balozi zetu, utakuta kwamba hii Diplomasia ya Uchumi haijitokezi katika kazi katika Balozi zetu hizi. Vilevile ukija kuangalia tena kwa upande wa watumishi, Diplomasia ya Uchumi, haijitokezi katika suala la watumishi.

Mheshimiwa Spika, nirudi katika kazi. Katika Balozi zetu, wanahitajika wafanye mambo mengi tu, lakini mojawapo ni mikutano, kuhudhuria mikutano mbalimbali lakini hata hivyo, kuitisha mikutano. Sasa utakuta kutokana na ufinyu wa bajeti ambao kila mara tunalia katika Wizara zote na katika Wizara hii kwamba bajeti ni finyu, hawahudhuri mikutano mingi wanayoalikwa kutokana na kwamba hakuna pesa za nauji, hakuna pesa za kujikimu huko wanakokwenda lakini mikutano ni muhimu sana. Kwa sababu, ni katika mikutano ndipo mtu utaweza kujua ni masuala yapi ambayo yana maslahi ya kiuchumi katikia Taifa letu na ni masuala yapi ambayo ni hatarishi katika uchumi wa Taifa letu. Haya yote, hayajitokezi wazi katika Diplomasia ya Uchumi kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile utakuta kwamba katika kazi hizihizi masuala ya maonesho, Balozi zetu hazihudhurii maonesho,haziendi kufanya maonesho yoyote. Kwa mfano, yanatangazwa maonesho ya Utalii, Balozi zetuhaziendi. Masuala ya maonesho ya vitu kama maua, Balozi zetu hazihudhurii kule, sasa ni wapi tunapoweza tukapata masoko ya utalii au masoko ya bidhaa zetu?

Mheshimiwa Spika, katika suala la watumishi, pia utakuta kwamba, ni hilihili la ufinyu wa bajeti. Utakuta watumishi ni wachache kuliko kazi tunazohitaji kuzifanya; kwanza wana hali ngumu kama wenzangu walivyokwishatangulia kusema, lakini pia, idadi ni chache na aina yenewe ya watumishi pia utakuta haikidhi. Kwa mfano, kuna maeneo mengi hatuna Maafisa Utalii, hatuna Maafisa wa Uchumi, kama Waheshimiwa Wabunge, walivyokwishakuchangia, hatujui ni lini hii bajeti itajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hili, nianze tu labda kupendekeza kwamba, ili tuendane na hiki kibajeti kidogo ambacho tunacho, pengine niishauri Wizara kwamba sasa labda iainishe tu katika zile kazi ambazo zinatakiwa kufanyika kwenye Diplomasia ya Uchumi, iainishe maeneo mawili; eneo moja ni zile kazi ambazo zinaweza zikafanyika katika mwenendo wa kawaida wa shughuli za kila siku, iziweke pemberi ambapo bajeti yake itakuwa ni ileile ya kazi za kawaida lakini pia iainishe yale masuala yote ambayo yanaweza yakafanyika kwa kutumia bajeti maalum ili kusudi iweze kutengewa bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningeomba Wizara iainishe ni kuainisha zile fursa zote za pekee katika kila nchi ambazo zina Balozi zetu. Kwa mfano, utakuta kwa maeneo kama ya China, kuna wawekezaji wengi kule na nchi nyingine za aina hiyo, basi Wizara iainishe hizo nchi na pale sasa tuangalie kwamba ni lazima maeneo kama hayo wawepo Watafiti ambao wanaweza wakafanya utafiti mbalimbali na vilevile wawepo watalaaamu katika Ubalozi ule, ambao watahusika na masuala ya wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo nchi zinakuwa ni masoko makubwa, kwa mfano masoko ya biashara. Tunaona tuna matatizo makubwa sana katika bei za korosho, bei za pamba, na hata sasa hivi tunasikia bei ya samaki inashuka. Maeneo ya nchi kama hizi inabidi pia Wizara iangalie, wawepo wataalam wa biashara, wawepo wataalam wa masoko ili waweze kutusaidia kujua ni kwanini kila mara bei za mazao yetu zinashuka. Lakini wanaweza wakatusaidia pia kuhakikisha ni mbinu gani tuzitumie ili tuweze kupandisha bei za mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Wizara ingeainisha ni nchi zile ambazo zinatoa watalii wengi wa Taifa letu, kwa mfano Marekani. Nchi kama hizi lazima ziwe na Maafisa Utalii. Nasema hivi kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini vinginevyo ingebidi angalau kila nchi ambayo tuna Ubalozi kule, basi kuwepo na Maafisa wote wa aina hii. Sasa pale lazima pia awepo Mtafiti ili kusudi kuweza kujua ni watalii wangapi tunaowapata wanaogongesha Visa kule na

wanaogongesha *Visa* huku nchini na pia kujua ni jinsi gani tunaweza tukaboresha hizi huduma za utalii.

Eneo la nne ni nchi ambazo ni kitovu cha Mashirika ya Umoja wa Mataifa, kwa mfano ukienda nchi kama Geniva utamkuta Balozi peke yake, labda na mtu mmoja tu ndiyo wanaopaswa wahudhurie mikutano yote ya Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kule utakuta ni mashirika zaidi ya 30 kama siyo 30. Sasa wanashindwa kuhudhiria mikutano mingine kwa sababu hawatoshelezi kabisa. Kwa hiyo, eneo kama hili ni vyema Wizara ikaangalia, wawepo watumishi wa kutosha ambao wanaweza wakajigawa, kwa siku wakahudhuria mikutano yote. Kama nilivyosema kwenye mikutano, ndipo mnapoweza kujua maeneo gani yana maslahi ya kiuchumi katika nchi yetu na unaweza ukatetea masuala yale ambayo unaona ni hatarishi.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho, labda ni zile nchi ambazo zinatoa misaada kwa nchi yetu, pia ziwe na wataalam pengine wa ushawishi ili kusudi tuweze kuhakikisha kwamba pale ambapo misaada inakwama kwama, basi waisukumesukume ili iweze kutolewa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hili la hati ya utambulisho. Maeneo mengi yaliyozungumziwa ni ufinyu wa bajeti. Lakini sasa tutaona kwamba, Mabalozi wameshateuliwa na Mheshimiwa Rais. Sasa ukifika kule, unakuta Balozi amekaa bila kazi kwa sababu hana hati ya utambulisho wa kumtambulisha kama yeye ni Balozi. Sasa niiulize Wizara: Je, hili ni tatizo

la bajeti au Wizara imesahau? Au kuna tatizo gani? Ningombu kupata ufanuzi wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akifanya majumuisho.

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho, nitoe msisitizo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Fakharia Shomar.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa hotuba nzuri walijotuletea hapa leo hata tukaweza kuichangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sina makubwa mengi ya kuelezea isipokuwa nataka nielezee masuala ya Zanzibar tu kidogo. Kwa kweli jengo lilikuwepo Zanzibar ambalo tayari ndiyo Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje, kuanzia mapinduzi yalipoingia mwaka 1964, naona lile jengo lilikuwa siyo la Ofisi, lilikuwa ni jengo la nyumba ya kuishi mtu, ambalo lilikuwa anaishi mtu kwa makazi. Lakini jengo hilo lilitanywa kuwa Ofisi na kwa kipindi chote hicho lilikuwa Ofisi, lilikuwa halina ukarabati. Ukititembelea jengo lile, halitoi pitcha nzuri ya Ofisi, na

kwa kipindi hiki Ofisi nyingi za Muungano zimekuwa zinajenga Ofisi zao Zanzibar.

Nimelitembelea jengo lile nimelikuta liko katika ukarabati na zimepelekwa Shilingi milioni 50 kufanyiwa ukarabati wa kuta, paa pamoja na kupakwa rangi. Sasa mimi nikaona kwanini fedha hizo wasingelizitenga kwa kutafuta kiwanja na kuweza kujenga Ofisi nyingine badala ya kutumia jengo lile ambalo ni nyumba ya makazi na haitoi sura nzuri kwa kuwa Ofisi, na tunasema ile ni Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje. Sasa ndiyo hili. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri aliangalie ili kulisaidia jengo lile liweze kupata sehemu nyingine kwa kujengwa Ofisi na kuachana na jengo liliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuelezea habari ya utendaji kazi katika jengo lile. Katika kitabu chake Mheshimiwa Waziri amesema lina wafanyakazi 18 na ni kweli na kuna Idara tatu, kuna Idara ya Protokali, kuna Idara ya Siasa na Uchumi na kuna Idara ya Utawala. Idara hizo kwa kweli hazifanyi kazi ipasavyo, kwa sababu kutokana na ufinyu wa fedha zilizokuwepo, kutokana na ufinyu wa kazi zilizokuwepo pale, utazikuta zile Ofisi zimekaa hazina kazi. Wanapotoka wageni wa Kimataifa wakienda nje, ndiyo hupokewa wakaenda kuonana na wageni wa juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Uongozi mwingine uliokuwepo pale.

Baada ya shughuli hizo kufanyika, utakuta hawana ratiba nyingine za kazi. Sasa ningependa kujua kwamba, uongozi wa Wizara kutoka Makao Makuu unatembelea mara ngapi pale? Nikaambiwa

kipindi kimoja tu alikwenda Mheshimiwa Waziri na akatoa ahadi pale ya kutengeneza, lakini Katibu Mkuu kama Mtendaji wa Wizara hajafika, *DAP* kama Mtendaji wa Wizara hajafika, na Maofisa wengine ambao wanatakiwa wawe wanakwenda kule kwa ajili ya kuona matatizo, hali halisi ya Ofisi na masuala mengine kwa ujumla ya utendaji, lakini hakuna aliyefika. (*Makofi*)

Katika miaka ya tisini, Balozi Mtango yeye alikuwa ni Kiongozi mzuri tu. Wakati alipokuwa Katibu Mkuu, alikuwa akitembelea Zanzibar na kusikiliza matatizo ya Zanzibar na kuona vipi huko Zanzibar wanavyofanya kazi. (*Makofi*)

Sasa ukiangalia kwa uelewa, mwaka 1964 baada ya mapinduzi kulikuwa Naibu Waziri anakuwepo Unguja, Waziri anakuwepo Bara, sasa kulifanya mwamshe wa ari ya kazi kwa kipindi kile na panapokuwa na kiongozi mkubwa anashughulikia masuala hayo, kila mmoja hufanya kazi yake.

Vilevile Mkurugenzi wa Idara ya ofisi ya Zanzibar pia amestaifu, sasa pia pamekuwa na unyeti wa hizi idara angalau Idara ya *Protocol* ina uwezo wake lakini idara ya uchumi haina. Ukiangalia madereva hawana, usafiri hakuna. Ina maana ugeni unapokuja Zanzibar, inabidi waazime gari ya SMZ au wakodi gari na hapo katika kukodi gari ndiyo mwanzo wa kutafuta watu kupata *ten percent* na kutafuta kupata rushwa. Sasa ningeliomba angalau kama ilivyokuwa Bara, wanayo mabasi kwa ajili ya Uongozi wa Kitaifa unaoingia na wangechukua angalau basi moja wakaliweka Zanzibar

au gari moja wakaliweka Zanzibar kwa kutegemea kwamba uongozi utakaokuja wa Kimataifa uwe na usafiri wao wa kuupeleka na kuwarejesha. (*Makofi*)

Kwa kweli Unguja kuna gari mbili za Ofisi ingawa kuna Idara tatu. Gari moja ya Mkurugenzi na gari moja ambayo ndiyo watumie Idara zote tatu na gari yenye we sijui kama ni nzima, haiko katika hali nzuri. Nafasi za madereva zipo, sijui kwanini madereva waazimwe wasiajiriwe. Kuna Masjala lakini hajaajiriwa mfanyakazi wa Masjala, inabidi Masekretari wale wakamatane ndiyo wapokee barua. Kutokana na kwamba nafasi hizi zipo, naomba Wizara ilifanyie kazi kuzijaza. (*Makofi*)

Mtu akifanya kizuri huna budi umpongeze. Nampongeza kwa hawa vijana 18 ambao walipelekwa kuchukua *post graduate* na vijana hawa ni mahiri, na katika kuwachagua mmeshirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wanaendelea kusoma. Lakini pia nilikuwa naomba kujua uteuzi wao wa kuwapanga katika hizo nafasi zitakuwa vipi? Watapangwa wapi na watakwenda wapi? Kwa sababu inawezekana mtu ukamsomesha fani ya aina nyingine na ukaenda kumpa shughuli nyingine. Sasa toka mwanzo, umekuwa na mwanzo mzuri, basi ningeomba pia na mwisho mzuri uendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli za *protocol* nzuri zinakwenda Unguja na Watendaji wake ni wazuri wanakwenda vizuri Unguja, basi pia ningeomba Watendaji hawa wapatiwe promotion angalau na wao waende kama Ubalozi au kama Wasaidizi wa Ofisi

za Ubalozi ili na wao wakapanue mawazo kwa shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua uajiri wa shughuli za Muungano kwa wafanyakazi wa Zanzibar upo sawa na Tanzania Bara. Lakini wakati unapokuwa unatoka uajiri ule sijui wanatumia vigezo gani au mbinu gani hata kuwapata Wazanzibar kuingia kwenye nafasi zile. Kwa sababu Zanzibar vijana wamesoma, wana elimu, wakitaka wenye *degree* wapo, wakitaka wenye *Masters* wapo, *postgraduate* wapo. (*Makofi*)

Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri atuelezee tunavyotaka kuajiri vijana kuingia Ofisi za Ubalozi, tunatumia mbinu gani? Tunafanya shughuli gani na tunatumia mikakati gani ili vijana hao nao waweze kuajiriwa?

Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza tena Mheshimiwa kwa shughuli zake anazozifanya katika Balozi zetu za nje. Wenzangu wamelizungumza na wamezieleza, lakini tunazungumza haya kwa kumpongeza, lakini bado tuna matatizo ya Ofisi. Ofisi zetu siyo nzima, matatizo yapo, na mtu anapopata uhamisho hapa kwenda Ubalozi, anafurahi. Lakini anapofika kule anayaona matatizo ya kule. Lakini hata hapo Mheshimiwa Waziri anapopeleka jicho la rehema, alitupie na Zanzibar, kwamba na Wazanzibar nao wana haki na wana hamu, na watafurahia nafasi hizi. Wakati Bara wanapelekwa, na Zanzibar mtuchukue japo wawili. Wapo vijana wetu ambao wamesoma! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haya mafupi, naunga mkono hoja ili kutoa nafasi ya kuahirisha. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Wala hujaniachia muda, umeumaliza mwenyewe. Nawashukuru sana kwa michango yenu.

Jamani kama nilivyosema, hii ni Wizara ya siku moja. Tutakaporudi, nitamwita Mheshimiwa Martha Moses Mlata na Mheshimiwa Shibuda. Kwa hiyo, sina matangazo, naomba nisitishe shughuli mpaka saa 10.00 jioni.

(*Saa 7.12 Mchana Bunge lillahirishwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilrudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii.

Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara yake kwa namna ambavyo wamekuwa wakitekeleza majukumu yao tangu bajeti iliyopita na hatimaye kuwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka huu. Lakini pia niwapongeze

Mabalozi wote ambao wamekuwa wakituwakilisha katika nchi mbalimbali kwa kazi ambayo wamekuwa wakiifanya na kutuwakilisha vizuri huko walipo na Watendaji ambao wapo kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana mama na dada yetu Dkt. Asha-Rose Migiro kwa nafasi kubwa ambayo alikuwa ameipata ya kuwa Naibu Katibu Mkuu katika Umoja wa Mataifa akiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Afrika na Tanzania. Kwa kweli tunampongeza kwa utumishi wake, kwani ameweza kutumikia vizuri na sifa yake ilikuwa ni mama mchapakazi, alituwakilisha vizuri na sote tulisikia na tuliosafiri tulifika kule tukapata sifa zake. Lakini pia tunampongeza kwa kumaliza salama, kwani ukipewa kijiti ukikifikisha salama, basi unamshukuru Mwenyezi Mungu. Hivyo, tunamshukuru Mungu kwa ajili yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nitoe masikitiko yangu kwamba kila mwaka bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje imekuwa ni ndogo sana ukilinganisha na majukumu ambayo wanayo. Sasa sielewi bajeti hii itakuja kupanda lini? Naiomba Serikali iangalie vizuri, kwa sababu kazi zake ni nyingi sana. Kwanza hata ile dhana tu ya kwenda kutuwakilisha katika mikutano mbalimbali, ile mikutano ambayo ina tija na Taifa letu, naamini wakati mwingine hata ile *delegation* ya kwenda kule inashindwa kukamilika kutokana na bajeti ndogo. Lakini pia bado kuna mambo mengi katika Balozi zetu, hasa kwenye maofisi ya Balozi zetu, yaani majengo katika Balozi zetu. Inakuwa ni aibu sana unapofika katika Ofisi ya Ubalozi

wa nchi yako ukiwa katika nchi ya ugenini unakuta Ubalozi ule, yaani kwa kweli naona hata kutamka ni fedheha. Kwa hiyo, ni Wizara ambayo inahitaji fedha nyingi sana za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna Balozi tatu ambazo wanategemea kuanzisha, lakini bado hata hizo Balozi tatu ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja sina hakika kama bajeti yake iko hapa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, atuambie hizo fedha za hizo Balozi tatu zinazokwenda kuanzishwa kama zipo.

Mheshimiwa Spika, lakini uhusiano wa nchi mbalimbali kwa Tanzania ndiyo salama yetu, kwa sababu hata ukienda Mitaani, unakuta watu wanaanzisha jumuiya mbalimbali kwa ajili ya kushirikiana katika mambo mbalimbali na unakuta shughuli zao zinakwenda kwa pamoja, hata unapopata tatizo basi umoja huo unakuwa na nguvu. Kwa hiyo, nafikiri kuanzisha Balozi na kuongeza Balozi zetu kwa uhusiano wa nchi nyingine mbalimbali nafikiri ni jambo la muhimu sana, naomba tulitilie maanani.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumemwomba pia Mheshimiwa Waziri hivi karibuni kwamba ni kwa nini tulivunja uhusiano, yaani Balozi zetu katika nchi ya Israel? Tunaomba aliingize kwenye mipango yake ili na kule tuweze kupata Ubalozi, kwa sababu ni watu wengi ambao wanatarajia kwenda Israel, lakini na Waisrael pia tumeona namna ambavyo tunashirikiana hata katika masuala ya kilimo na hata katika mambo ya

imani ya dini. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri alizingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka kuzungumzia suala la uraia wa nchi mbili. Kuna Watanzania kweli ambao wamekana uraia wa Tanzania kutokana tu na kukosa haki yao ya msingi ya kuwa raia wa Tanzania. Kwa hiyo, naishauri Serikali au Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, atueleze hili suala la uraia wa nchi mbili limefikia wapi? Kwa sababu miaka mitano iliyopita lilikuwa kwenye mchakato, sasa hivi tumefika miaka miwili ni mchakato tu. Sasa kuna Watanzani wengi wanataka kurudi nyumbani ili kuja kuwekeza, kujenga nchi yao, kuongeza ajira na kudumisha mambo mengine, lakini wanashindwa kutokana na kwamba uraia wa nchi moja unawabana kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba dirisha la *Diaspora*. Kuna Watanzania wengi ambao wamekuwa wakikutana na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais amekuwa anakwenda na anatoa wito wa kurudi nyumbani na kuja kuwekeza, wapo wanaoitikia wito huo, lakini kuna ukiritimba mkubwa sana ambao wanakutana nao. Najua katika nchi zillizoendelea hakuna longolongo, kwani unakaa kwenye mstari, zamu yako ikifika unahudumiwa. Lakini Tanzania hata huo utaratibu hawaelewi. Wakifika wanashindwa wamwone nani, waanzie wapi na wakienda bandarini matatizo matupu na hata kwenye *TIC* ni matatizo matupu, wakija kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje napo pia ni matatizo matupu. Kwa hiyo, naomba ikiwezekana kuwekwe dirisha la kuweza kuwahudumia

Wana-diaspora wanapokuja na mikakati yao kwa ajili ya kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naangalia ni mabalozi wangapi wanawake tulionao? Tunamshukuru Mheshimiwa Rais amekuwa ni kiongozi wa mfano katika kuteua nafasi za viongozi wanawake. Lakini kwenye Mabalozi wako watano tu. Naomba Mabalozi wanawake waongezwe. Wapo wanawake wengi sana na wanaweza. Naomba nafasi hizi ziongezwe na Mheshimiwa Rais katika Balozi mpya ambazo tunakwenda kuziongezea, basi itakuwa ni vizuri sana kama watakuwa ni wanawake, hata wakifika 50% kwa 50% mimi naamini wanawake tunaweza, basi tupewe hizo nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, naomba Wizara iendelee kuzungumza na kusuluhiha kwenye migogoro mbalimbali na kutatua migogoro mbalimbali ya nchi jirani na marafiki ili hata sisi tuendelee kuwa na amani, kwa sababu tukiwa na uhusiano na nchi zenye amani, basi na sisi pia tutakuwa na amani. Lakini hatuwezi kulala kwa kuona jirani yetu moshi unafuka, wewe ukalala. Naomba Mheshimiwa Waziri aendeleze gurudumu hilo akiongozwa na Mheshimiwa Rais katika kusuluhiha migororo ya nchi mbalimbali ili kwa kweli Afrika yetu tuwe na amani na tuishi kwa amani na tuweze kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka kuzungumzia kuhusu misaada ambayo tunaipata kutoka nchi wahisani. Ni kweli tunashukuru, lakini tunaomba wawe

wanatuletea basi kwa wakati. Pale wanapokuwa wametuahidi, basi tunaomba Wizara hii isimamie na kuzungumza nao kwa sababu, Tanzania ni nchi inayokua na uchumi wetu unaendelea kukua na tunawategemea sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ushirikiano wa nchi za nje ndiyo daraja kubwa tunalolitegemea Watanzania katika kutambulisha juhudini mbalimbali za siasa ya Taifa na vilevile kuwatambulisha wageni wanaokuja kuhusu msimamo na mtazamo wa nchi yetu katika masuala ya ushirikiano wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katambulisha katika hotuba yake masuala ya msingi mkuu wa kumuenzi Baba wa Taifa. Maana yake ni kuenzi Siasa za TANU ambazo zimerithiwa na CCM. Ukweli ni kwamba, "bila Agano la Kale hakuna Agano Jipya." (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumuunga mkono na kumpongeza kwa msimamo alioutoa dhidi ya nchi ya Malawi ambayo inaleta chokochoko. Lakini ningependa vilevile nyimbo zilizomwondoa Nduli Idd Amin sasa zianze kuhamasisha upya ili Tanzania tuwe

tayari kwa lolote litakalotokea ili tuweze kuhakikisha kwamba mipaka ya nchi yetu pamoja na raia wetu ambao wapo mpakani hawadhusuriki.

Mheshimiwa Spika, TANU ilidai uhuru na CCM inaendeleza ari ya *Afro Shiraz* pamoja na TANU. Tanzania tulikataa kuwa malighafi.

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba wewe vilevile ni mwasisi wa Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi kinakataa Tanzania tusiwe malighafi na tuhakikishe ya kwamba nchi yetu inasonga mbele. Lakini naomba kusema jambo moja la msingi kwamba, "Mdai chake kwa Mdaiwa Huambiwa Mmbaya." Naomba kusema kwamba, wahisani na wawekezaji wanaokuja Tanzania kwa kweli hawawezi kuwa ni mtaji wa kuondoa umaskini wa Watanzania. Napenda kusema hilo kwa kishindo kabisa na ninaomba kukumbusha ya kwamba wakati wa TANU tuliwaita walowezi, masetla na hata wanyonyaji, leo tunawaita washiriki wazuri na marafiki wa maendeleo. Lakini sidhani kama duniani kuna mfanyakibashara ye yote ambaye ni mtaji wa kuondoa umaskini wa mtu ye yote. Hakuna hata kidogo! (*Makof*)

Kwa hiyo, naomba Tanzania na siasa yetu ya Chama cha Mapinduzi, nasema Siasa ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu gani? Ndiyo Chama kilichoshika dola na siasa ya TANU, ndiyo inayoongoza maslahi ya nchi hii. Kwa hiyo, siasa ya TANU ambayo ndiyo imezaa CCM, naomba ilindwe ili kuhakikisha kwamba Watanzania wasikate tamaa na msimamo wa Watanzania wa kuelewa kwamba walielimishwa

kuwa Tanzania hawezi kuwa malighafi na kwamba hatuwezi hata siku moja kuwa na maisha bora kwa nchi za Ulaya. Lakini hivi sasa wawekezaji mnaowatafuta nje ya nchi, mishahara yao siyo kidogo. Unyonyaji ni mkubwa, ajira wanazopata, wavuja jasho hawa sijui kama nao mnawanadi kule. Hivyo wawekezaji wakija hapa wawape mishahara ambayo ni posho tu za kutolewa pishi.

Mheshimiwa Spika, diplomasia ya uchumi Tanzania, naomba basi ihakikishe ya kwamba Watanzania hatuitwi tundapori la kuliwa hovyo hovyo na mtu yeote. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anguko la imani ya Watanzania kuhusu ushirikiano wa Kimataifa upo hivi sasa katika masuala ya makundi ya wakulima na wafugaji. Wakulima wa zao la Pamba leo ukiwaulizia diplomasia ya uchumi imewasaidia nini, hawaelewi! Wanalamika. Wanasema diplomasia ya uchumi imekuwa ni gulio au vituo vyta kunadi raslimali za Watanzania, siyo kwenda kunadi Pamba kwamba bei ya pamba isiwe na mtikisiko kama ilivyoupata, na hivyo hivyo Korosho na Kahawa: Je, mazao haya yanafaldika nini na diplomasia ya uchumi? Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha utuambie diplomasia ya uchumi inasaidia nini? Watanzania wataienzi na kuiheshimu CCM, lakini kwa nini wanaienzi? Ni kwa sababu utamu wa kuku unategemea chakula anachokula. Je, utamu wa CCM hivi ni kitu gani ili wananchi wasipate anguko la kutokuwa na imani nayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hotuba ya Waziri haina viarifu na haina vihusisho vya juhudini ya diplomasia ya uchumi kwa wakulima na wafugaji. Wafugaji kila siku tunawazungumzia kwamba mifugo ipungue katika diplomasia ya uchumi. Je, ni Balozi gani kahangaika kutafuta viwanda ili wafugaji wapate viwanda vya nyama? Je, hao Mabalozi waliopo nchi za nje hawajui hata kuna matatizo ya bei ya Pamba? Sijui bei ya Korosho, mimi nimewauliza nilipokwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Waziri, ni lini utakaa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Wavuvi mjadili na kuweka msimamo mmoja, baadaye muelimishe ili Mabalozi wetu na Ofisi zetu wajue kwamba wako kule kuwakilisha wakulima, wafugaji na Watanzania wengine? Hawapo kule kwenda kutafuta wawekezaji na minyororo ya unyonyaji, hawapo kule kwa ajili ya kusema tunatafuta wawekezaji. Hii diplomasia ya uchumi maana yake nini? Mimi nasikitika sana. Je, Balozi zetu hazijui kwamba kuna kauli mbiu ya Kilimo Kwanza? (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri, hotuba yako haijanogesha, haina vivutio, haina viambatano, haina mang'amuzi ya kusema kwamba kuna kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Sasa hao Mabalozi wetu mmejiandaa nini? Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje mna viarifu gani ambavyo vina mang'amuzi ya kwamba kuna wakulima wanaoteseka, wanalima sana mazao yao na yako hoihoi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasikitika sana kwamba Wizara hii inakuwa ni daraja la kujenga diplomasia ya uchumi na kujenga motisha kwa wawekezaji kuja Tanzania. Lakini wakulima wa hapa hawana motisha yoyote na diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Waziri, uzalendo wako na ninakuelewa, lakini naomba usinipe majibu kifuniko, maana wewe ni mwanadiplomasia. Naomba usinipe majibu kifuniko, bali naomba majibu yawe na mchanganuo na mpambanuo kwamba Tanzania na CCM mnafanya nini ili kuendeleza hisia za Watanzania za kuendelea kuiamini Siasa iliyoachwa na Baba wa Taifa? La sivyo, kwa kweli nasema kwamba, huwezi kuficha kaa la moto katika mfuko wa suruali. Kwa hiyo, mko hatarini mnajivika mabomu, mtajilipua wenyewe na hususan wewe Mheshimiwa Membe ndiyo utakuwa Kamanda wa kufadhili mabomu ya kujilipua kwa Chama cha Mapinduzi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda ku-declare *interest* kwamba Mheshimiwa Membe, kweli Baba yake alikuwa ni rafiki yangu pamoja na Dorcas Mkewe, Baba yake alikuwa Mzee rafiki yangu. Lakini nawajibika vilevile kusema kwamba msema kweli mpenzi wa Mungu. Nisipomsema na kumwambia ukweli katika dhamana yake, nitakuwa simtendei wema na nitakuwa natendea fadhila ubinafsi ambao siyo mzuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, siasa ya Mambo ya Nchi za Nje isipoleweka vyema kwa wawekezaji na ikaeleweka vyema kwa Watanzania, maana yake itakuwa ni siasa

ya Mambo ya Nchi za Nje siyo siasa ya Chama cha Mapinduzi. Imebatilishwa kuwa ni siasa inayotekelizwa kwa maslahi ya wawekezaji, kwa sababu kila siku tuna Mabalozi ambao wako hapa kulinda maslahi yao. Kuna *big power diplomacy* ambayo wewe unaielewa vizuri sana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna mafuta na gesi na ukiangalia chokochoko za nchi za Syria na *Middle East* hii ni kwa sababu nchi zile zinatakiwa kuwa malighafi. Je, mikataba mibovu? Je, sisi tumejiandaa viyi na Ushirikiano wa Kimataifa? Wewe umekaa viyi na *Attorney General*? Umekaa viyi na Waziri wa Viwanda na Biashara, Kilimo na wafugaji ili kuelewa kwamba diplomasia ya uchumi haitaweza kuwa ni kitengo cha kuingizwa na tukawa ni Sera ya Panya ya kuumwa na kupuliziwa, Sera ya Mataifa ya nchi za nje. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taswira ya watumishi katika Balozi zetu ni ya uzalendo na uaminifu mkubwa sana. Mheshimiwa Waziri hakikisha Balozi zetu zisiwe na viongozi ambao wanategemea umangimeza na wa kuandaa makundi ya Balozi na kuwepo makundi ya huruma ya Serikali.

Nayasema hayo kwa sababu nimesafiri na nimeona. Wakale husema, ukaidi haubadili ukweli. Nakuomba sana uelewe ya kwamba mwendo korofu uliopo katika baadhi ya Balozi ni kwa sababu ya Mabalozi ambao hawapendi kushauriwa na wasaidizi wao. Hao hao Mabalozi hutisha kwamba kama hunisikilizi nitakurudisha Tanzania. Naomba udhibiti

unyanyasaji na unyanyapaa uliopo katika Balozi zako.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tena kusitiza Viwanda vya Nyama. Ujanja mwingi wa kusema, sasa Ujamaa na Kujitegemea sioni ukitekelezwa katika diplomasia ya uchumi. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, ni Ubalozi gani ambao unaweza kusema umetekeleza diplomasia ya uchumi ya kulinda maslahi ya wakulima? Pamba tunalia hatuna bei na mpaka hata hivi sasa naomba Mheshimiwa Rais ajue kwamba wakulima wa Pamba bado wanabiriki diplomasia ya uchumi inawasaidia nini? Je, diplomasia ya uchumi huo mwaka 2015 itakuwa ni sehemu mojawapo ya 60% ya kura za wakulima. Je, CCM imejiandaa vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli jambo hili, nikushauri Mheshimiwa Waziri kwamba simu yako haipatikani hewani kwa 95%, nakuomba uongeze fursa ya kuwasiliana na wenzako, haya yote ninayoyasema hapa ningekuwa mimi ambaye ni rafiki wa karibu na wewe nakupata, ningekuwa nimekunong'oneza. Je, raia wa kawaida watakupataje? Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, utamu wa chai ni sukari na si majani ya chai. Naomba uwe sukari, uwe mtamu angalau uwe unapatikana, unashauriwa na wenzako.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize swalii la mwisho Mheshimiwa Waziri, kwamba: Je, Tanzania leo ataihakikishia vipi kwamba hatutakuwa mateka wa *big power diplomacy* ambao hivi sasa wanatunyemelea? Hivi sasa tunapewa mikopo chungu nzima: Je hii

mikopo tunayopewa Tanzania dhamana yake ni nini? Kwani kukopa ni harusi, kulipa ni matanga. Je, huo ushirikiano wa Kimataifa unaleta nini kwa Watanzania? Chonde chonde Mheshimiwa Waziri ambaye siku zote nakupongeza, kwani una sifa ya kuwa Katibu Mwenezi wa CCM kwa uwezo wako mkubwa wa kuongea.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tena alishanilaumu kwelikweli, na mimi namwambia usinitishie kama nafasi ipo, basi lakini usinitishe, ingawaje hujasema waweja. (*Kicheko*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara hii kwa kuwa mstari wa mbele kuishawishi Tume ya Hifadhi Duniani (*World Heritage Commission-WHC*) kukubali kurekebisha mpaka wa hifadhi ya *Selous*.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupongeza Wizara na Kamati kwa kusimamia urejeshaji wa fedha za ziada za *change* ya Rada. Hali kadhalika, katika suala zima la ajira, pamoja na pongezi hizo, bado kuna changamoto nyingi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Mgogoro huu

umechukua muda mrefu. Ni vyema sasa kujua mgogoro huu utatatuliwa lini?

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iangalie upatikanaji wa *visa*, mfano, kama kupata *visa* hapa Tanzania ya kwenda Marekani ni Dola 100, basi hali kadhalika nao Ubalozi wa Tanzania uwatoze kiasi hicho hicho na ifanyike hivyo kwa nchi zote.

Mheshimiwa Spika, nashauri wakati Waziri anahitimisha hotuba yake, ni vyema atueleze: Je, Tanzania inazo nyumba ngapi katika nchi zote? Je, tuna hati miliki za majengo hayo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza, lini Wizara itashughulikia tatizo la kukosa Balozi nchini Israel ukizingatia kuwa Watanzania wengi huenda huko kwa masuala ya imani, na siyo hilo tu, na suala la kibashara? Kuna watanzania wengi wanashirikiana na Waisrael kwa masuala ya kilimo na mengine mengi. Je, Serikali haioni kama ni wakati muafaka wa kuwa na Ubalozi kamili huko Israeli kama ilivyo Jiddah ambapo watu huingla au huenda kwa masuala ya kiimani? Huko kuna Balozi na siyo mwakilishi.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi na misukosuko ya kisiasa pamoja na kiuchumi ambayo inaikabili dunia kwa sasa, sina budi kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Membe na

Naibu wake pamoja na Balozi zetu zote za nje na Watendaji kwa ujumla kwa kuhimili miliki hiyo na nchi yetu kubaki salama pamoja na uwakilishi wetu huko nje.

Mheshimiwa Spika, majengo ya mabalozi nje ya nchi yanaonekana kulalamikiwa sana kutokana na aidha ubovu au uchakavu wa majengo hayo. Kutokana na hadhi tuliyonayo Watanzania katika uso wa dunia, ni vyema Wizara sasa kufanya kila njia ili kuyafanyia ukarabati majengo yetu ambayo yanatumiwa na Balozi zetu. Vile vile kuna baadhi ya nchi za nje Tanzania imepata na inamiliki viwanja, ni vyema basi mchakato wa kujenga nyumba kwa ajili ya Mabalozi wetu uanze haraka ili kuondokana na adha ya kuendelea kukodishwa majengo, na hii itapunguza matumizi mengine ya hazina.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara juu ya msimamo alioutoa wa Tanzania kuhusu mpaka ambao umeanza kuleta mzozo baina yetu na jirani zetu wa Malawi katika Mto Nyasa. Naiomba Serikali ihakikishe inaweka ulinzi wa kutosha katika maeneo hayo na zaidi, katika yale maeneo ya majini ambayo wenzetu tayari wameyapata Makampuni kwa ajili ya utafiti ama uchimbaji wa mafuta. Lakini pia ni vyema kuzidisha ulinzi kwa raia wetu waliopo Ziwa Nyasa ambao ni haki yao kupatiwa ulinzi na usalama wao na mali zao, kwani hali inayoonyeshwa na jirani zetu inaanza kutia shaka.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atapokuja kujumuisha hotuba yake ni vyema atueleze

suala zima la Tanzania kujinga na OIC, kwani naona muda umekwenda sana bila ya kuelewa nini kinaendelea. Vile vile naomba maelezo juu ya vikosi vyetu ambavyo vinapelekea kulinda amani katika nchi ambazo zinakua na matatizo ama ya vita vyatwenyewe kwa wenyewe, au kuhatarishwa kwa usalama wa nchi husika. Tunataka kujua ni faida kiasi gani ama Tanzania inalipwa kiasi gani kwa kupeleka Askari wetu nje na je, wale Askari wetu amba wanapoteza maisha yao huko, Wizara inawathaminije?

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zina matatizo mengi ya kiutendaji ofisi hizi hazina fedha na vitendea kazi kwa ajili ya kazi zao. Tukumbuke kuwa hizi Balozi ni Wawakilishi wa nchi yetu katika nchi hizo. Ni aibu kubwa kuona kuwa ofisi hizo hazina hata *stationary*, hazina usafiri. Hivi kule nje wataomba kwa nani?

Mheshimiwa Spika, ofisi hizi nyingi zina matatizo ya wafanyakazi. Tumesahau umuhimu wa Ofisi hizi na inapotokea Ofisi hizi kuwa na wafanyakazi kidogo, kazi nyingi zinashindwa kufanywa. Ni aibu kuwa na ukosefu wa wataalam. Hivi Balozi hizo zinaendeshwaje?

Mheshimiwa Spika, Ubalozi wa China, lile eneo letu ni kubwa na linaweza kututosha kwa ajili ya wafanyakazi na Ofisi. La kusikitisha, lile eneo tunashindwa kuliendeleza. Hivyo wafanyakazi wanapata matatizo ya makazi na Ofisi. Ofisi za Balozi

zilizo jirani na Balozi yetu (Uchina) kwa kweli wanalionea choyo sana hilo eneo. Hivi Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza hilo eneo?

Mheshimiwa Spika, linguine ni malalamiko makubwa kwa wanafunzi wetu wanaosoma nje. Wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mengi ya kifedha. Kwa hiyo, maisha yao yanakuwa magumu sana, kwani wanafikia kuishiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kwa Watanzania hao, kwani wanaweza kujingiza katika mambo mabaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kupitia Balozi zetu kuandaa mpango na mikakati mizuri ili kuhakikisha Watanzania walioko nje wanasoma kwa amani.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuchangia. Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa izingatie yafuatayo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, mwaka 2011 nilihoji Wizara kupitia mgawo mdogo wa bajeti pamoja na umuhimu wa Wizara katika utekelezaji wa Sera ya diplomasia ya uchumi na mpango wa Taifa wa

Maendeleo. Hali hii imejirudia tena ambapo katika aya ya 34 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 19 Wizara ilipata asilimia 44 tu ya bajeti ni muhimu katika majumuisho. Waziri Mkuu kama Kiongozi wa shughuli za kila siku za Serikali na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, kwa mujibu wa Katiba, aeleze ni kwanini Serikali haitoi kipaumbele kwa Wizara hii katika mgawo wa fedha?

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu Sekta ya Nishati na Madini aya ya 35 ukurasa wa 20 na 21 juu ya mkataba wa ujenzi wa bomba la gesi toka Mtwara mpaka Dar es Salaam uliosainiwa na Balozi kwa niaba ya Serikali, Wizara itoe maelezo: Ni kwanini mkataba huo umesainiwa bila Kamati husika za Bunge kuhusishwa katika maandalizi, kinyume na azimio la Bunge la mwaka 2008 katika mwaka 2012/2013? Ni muhimu mkataba huo mkubwa uletwe Bungeni. Hatua hii ni muhimu wakati huu ambapo kuna tuhuma za viongozi wa Tanzania kuingiziwa fedha takribani Shilingi bilioni 400 katika Benki Uswisi na Makapuni ya Utafutaji wa Mafuta, Madini na Gesi Asili.

Aidha, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika aya ya 36 kuhusu kuruhusiwa kwa uchimbaji wa madini ya urani na kazi zinazokusudiwa kufanywa na Kampuni ya *Uranium one* kutoka Urusi, naomba Wizara ieleze pia ushirikiano iliota kwa Wizara ya Fedha kuhusu katika mwaka wa fedha 2011/2012 kufuatia hotuba yangu ya tarehe 15 Julai, 2011 madai ya kukwepa kodi (*Capital gain tax*) kufuatia mauziano baina ya Kampuni ya Australia na ya Urusi katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ifuatilie mauziano

yaliyofanyika kwa upande wa Makampuni ya utafutaji wa mafuta na gesi asili.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu Sekta ya Maji aya ya 42 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 25 na 26 Wizara inaeleza ushirikiano na Wizara ya Fedha kuhusu mkopo kutoka Serikali ya India kwa ajili ya mkopo wa mradi mkubwa wa Mji katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani. Hata hivyo, nasikitika kuwa maelezo ni kuwa mchakato umefikia hatua ya mwisho kwa kuwa ni kaui hiyo hiyo ilitolewa kwa nyakati mbalimbali na Mawaziri kadhaa nilipohoji mwaka 2011.

Aidha, Wizara ifuatilie kuhakikisha matumizi hayahamishwi kwenye miradi mingine kinyume na mkataba, kufuatilia mkopo huo, fedha za miradi ya ujenzi wa Bwawa la Dunda upanuzi wa chanzo cha Ruvu juu, ujenzi wa Bomba toka Mlandizi mpaka Dar es Salaam ziongozwe kwa mujibu wa viwango vyaa mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango ufuatao wa nyongeza kuhusu utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa miaka mitano 2011/2012 – 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu Sekta ya Miundombinu aya ya 41 ukurasa wa 24 na 25. Wizara imeeleza kuwa inaendelea kushawishi Serikali ya Japan kuhusu kujenga barabara za juu (*fly over*) maeneo ya Tazara. Wizara ikumbuke kuwa maombi ya awali hayakuhusu eneo la Tazara pekee, bali ni pamoja na eneo la Ubungo. Wizara itoe maelezo, ni kwanini eneo

Ia Ubungo limeondolewa kwenye ushawishi wa sasa wakati kwa mujibu hata wa vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Miradi yote miwili ilipangwa kutekelezwa kwa pamoja?

Aidha, Wizara itambue kuwa barabara ya juu za Ubungo ni muhimu kutokana na mchango wa barabara ya Morogoro katika uchumi wa nchi kama barabara ya usafirishaji pia wa mizigo kimataifa (*transit road*). Hatima ya kutafuta mwekezaji wa ujenzi wa barabara ya njia sita kutoka Ubungo mpaka Chalinze kwa ubia kati ya Sekta binafsi na ya umma (PPP) italeta tija ikiwa itatanguliwa na ujenzi wa njia za juu katika eneo la Ubungo. Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje ieleze ni mwaka gani mwekezaji huyo atapatikana na lini ujenzi unatarajiwa kuanza?

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu Sekta ya Viwanda aya ya 43 ukurasa wa 26, Wizara imeeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 watapatikana wawekezaji kwenye viwanda vya kutengeneza nyuzi na nguo kutoka Japan na China. Pamoja na hatua hiyo, Wizara ieleze katika mwaka wa fedha 2011/2012 imechukua hatua gani kutokana na mchango nilitoa wa kutaka Wizara kwamba ifuatilie kwa Serikali ya China ambayo ilikuwa inamiliki asilimia 51 ya hisa ya kiwanda cha nguo cha Urafiki na Serikali ya Tanzania ikimiliki asilimia 49? Kiwanda hicho kiko katika hali mbaya, uzalishaji uko chini na ujisadi umekithiri kati ya China na Tanzania. Yaliyoasisiwa na Mwalimu Nyerere kuhusu kiwanda hicho natambua kwamba kwenye mwaka 2011/2012 Serikali ya China imeuza hisa zake kwa mojawapo ya Majimbo ya nchi yetu. Hata hivyo, hatua

hiyo haijaweza kurekebisha upungufu uliopo, hivyo Wizara ya Mambo ya Nje itumie mawasilliano ya kidiplomasia kuwezesha ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, sita, katika aya ya 45 ukurasa wa 28 kuhusu kurejesha kwa fedha za ujisadi wa rada kutoka Kampuni ya Uuzaji wa silaha ya Uingereza (*BAE*) Waziri ametaja kuwa kiasi kilichotajwa ni pamoja na kilichotolewa mlungula. Hii ni tofauti na kauli ya Rais iliyonukuliwa na baadhi ya Vyombo vya Habari kuwa hakukuwa na rushwa. Serikali ieleze Bungeni, ni kwanini mpaka sasa watuhumiwa wa rada hawajachukuliwa hatua kamili na vyombo vya uchunguzi vya ndani na kufikishwa Mahakamani? Kufungwa kwa uchunguzi wa *SFO* na uamuzi wa Mahakama za Uingereza kuitoza Kampuni hiyo badala ya kuchukua hatua dhidi ya tuhuma za kijinai usitumike kama kisingizio cha kuacha kuchukua hatua za ndani.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Mambo ya Nje kwa kazi nzuri inayoifanya kuendeleza diplomasia ya Tanzania na nchi za nje. Naipongeza hasa ukizingatia kuwa wanafanya kazi hii katika mazingira magumu sana hasa ya kibajeti. Nichukue nafasi hili kuihimiza Wizara kuongeza bidii na jitihada hasa kukuza utalii wa Tanzania. Ni lazima tuongeze jitihada kutangaza utalii wetu nje ili kuongeza utalii na kuongeza watalii wanaokuja Tanzania na hivyo kuongeza mapato ya nchi kutokana na utalii. Ukiwa nje ya Tanzania na ukisema unatoka Tanzania, watu wengi hawajui Tanzania iko wapi, na hawaijui kama ni nchi, hawajui kama ina vivutio vingi sana vya utalii. Tufanye jitihada

za juu sana kuongeza kujulikana kwa nchi yetu na Utalii wake ili tuongeze mapato yetu.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa hii ya kuchangia hoja katika Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu suala la marejesho ya pesa za rada. Hali ya suala hili jinsi ilivyoshughulikiwa linatia shaka kubwa sana. Serikali hali ikijua kuwa kuna ujisadi uliofanyika katika manunuzi ya chombo hiki muhimu, leo hii wahisani au wenzetu wameamua kuturudishia pesa hiyo, lakini la ajabu pesa hiyo jinsi ilivyokuwa imegawanywa kwa matumizi yake imekuwa tofauti. Pesa ilipangiwa inunue vitabu hapa nchini kiasi kwamba Kampuni za kuchapisha zipo nyingi, lakini pesa hiyo hiyo inarudi kwao huko huko Uingereza; kuwa Kampuni ya Uingereza ndiyo ichape vitabu hivyo! Je, hapa usimamizi wa pesa zetu zinaeleweka au imekuwa ni suala la kubahatisha tu? Naiomba Serikali sasa irudishe pesa hiyo hapa nchini na Serikali iwataje hadharani hawa walioshiriki katika vitendo hivi vya ujisadi. Tumechoshwa na kauli, na tutawataja ikibidi watajwe leo hii hadharani.

Mheshimiwa Spika, Serikali makini ni ile ambayo inatoa fursa au nafasi kwa ajili ya kujitathmini yenewe. Leo hii nafasi hii imekuwa ya kinadharia tu, utendaji na utekelezaji wa majukumu haya umekuwa kinyume kabisa! Kama Serikali haiwezekani kujitathmini

yenye, basi kuwepo na kauli rasmi ya kujibu kwenye azimio hilo la APRM, na kama basi tunaendelea kuwa washiriki wa azimio hilo, basi suala hilo limo chini ya Idara ya Mipango na uwepo utaratibu wa kujitathmini kuanzia ngazi mbalimbali katika Taasisi na Idara zetu mbalimbali ili kuwepo na utandawazi katika ngazi yote.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya nchi yetu sasa inatia wasiwasi. Ukweli wa mambo ni kuwa mipaka ya nchi yetu hairidhishi na aidha, inazidi kuingiliwa kila kukicha. Leo hii tunasikia habari ya mgogoro uliopo Ziwa Nyasa baina ya nchi yetu na Malawi, lakini bado kuna sehemu nyingine hususan kwenye Ziwa Victoria na hii ilikuwa inaleta hali ya wasiwasi kwa wananchi wetu na hususan wale wanaojishughulisha na uvuvi. Lakini kubwa ni pale hata wale wahamiaji haramu hawawezi kudhibitiwa, na watu hawa wakiwa ndani ya nchi yetu ndio wa kwanza huwa hodari wa kuteka ardhi, kugombea vyeo na madaraka au nyadhifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikalli iwe makini sana, kwanza iangalie upya na kwa umuhimu mkubwa wa uraia wa nchi mbili. Pili, mipaka yetu iangaliwe kwa umakini sana, kwani hapa suala la mipaka linaangaliwa kwa maslahi na rasilimali zilizopo, kwani kama mpaka upo sehemu ambayo haina chochote cha maana haiji akilini kuanza kugombania. Lakini kama kuna chochote au jambo la maana, hapo tayari kila upande utaonesha kulihitaji eneo hilo. Hiyo Serikali ihakikishe suala la mipaka yetu imelindwa na kanuni, tusiruhusu wenzetu watuingilie ndani ya nchi yetu.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii nami niweze kutoa mchango na maoni katika Wizara hii. Pamoja na shukrani hizo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia Watendaji wote wa Wizara hii wakiwemo Mabalozi wote wanaotuwakilisha katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni mionganini mwa nchi nyingi duniani ambazo zina mahusiano na nchi nyingi duniani na mahusiano hayo yanaonekana wazi kuwa ni kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii pamoja na Mabalozi wetu huko nje. Hivyo, nawapongeza. Ukweli ni kwamba bado nchi yetu inatakiwa kuwa na mahusiano mazuri na zaidi ili tuweze kupata fursa ya kukuza uchumi wetu kibiashara na pia kisiasa. Mfano hata Mikutano tu ya Kimataifa ni muhimu ihudhuriwe ili yote yatakayojiri na nchi yetu isiwe nyuma.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho mpaka sasa bado najiuliza, *are we serious?* Kwa sababu bajeti ya Wizara hii inakuwa ndogo kila mwaka! Hivi hata hiyo mikutano yenye tija, watu hawa waendeje? Jamani mimi kwa uelewa wangu mdogo tu, naona ni aibu. Kwani natambua hata kama mtu binafsi unataka uaminike kwa jambo lolote, kwanza ni *the way* utakavyo-*appear* mbele ya unayemlenga. Sembuse Taifa! Jamani nimeshuhudia Mikutano mbalimbali niliyowahi kuiona, wenzetu (mataifa mengine) wanavyohudhuria kwa wingi na hawakosi (*delegation*), inakuwa ya kuvuna walichoendea. Lakini Tanzania fedha za kusafirisha wataalam husika huwa ni

mgogoro. sasa tutavunaje vya kutosha kama bajeti
yenye hii?

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni Balozi zetu jamani na hata watumishi wa kwenye Balozi zetu. Yaani huruma! Majengo yamechakaa!

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango cha fedha kilichotengwa ni kidogo sana kwa sababu fedha hii inatakiwa ibadilishwe kwa Dola, kweli shughuli nyingi zitakwama za Wizara. Hii Serikali iangalie mipango mkakati iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Balozi, ifike mahali sasa Serikali itenye fedha maalum ili ziweze kukarabati majengo ya Balozi ambayo yamechakaa na yenye muda mrefu, mfano Ubalozi wa Kinshansa. Pia Serikali ione umuhimu wa kununua majengo katika Balozi nyingine ambazo zinapanga na kulipa kodi kubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara bado ina upungufu wa wafanyakazi, hivyo kwa bajeti ndogo hivi watawezaje kuajiri? Naomba Wizara iongezewe fedha iweze kuajiri wafanyakazi ili kuboresha ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna Watanzania wengi ambao wamekosa haki yao ya msingi ya kuwa raia wa Tanzania kwa kuwa wana uraia wa nchi moja na hivyo kupoteza ushiriki au mchango wake katika ujenzi wa Taifa lao. Wako Watanzania wengi ambao wako nje wameukana uraia wa Tanzania kwa sababu kwa sasa suala la uraia wa Tanzania bado halijapatiwa ufumbuzi na kuitishwa na Serikali. Naishauri Serikali ishughulikie

hili jambo mapema. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze suala hili la uraia wa nchi mbili atalishughulikia lini na kukamilika?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Serikali kutambua usawa wa jinsia hasa katika nafasi za uteuzi. Lakini kwenye suala la Mabalozi wa kutuwakilisha nje, bado usawa haujazingatiwa. Pamoja na hilo, bado kuna wanawake wengi wenye uwezo mkubwa sana.

Naomba Wizara na Serikali iongeze uteuzi wa idadi ya Mabalozi wanawake kuwa wengi zaidi. Hivi sasa Mabalozi wanawake ni watano tu. Idadi hii ni ndogo sana. Tunaomba nusu kwa nusu, yaani 50 kwa 50.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Wizara ikahakikisha wamefanikiwa Watanzania wengi zaidi kushika nyazifa za uongozi mbalimbali za juu na kawaida, ngazi ya Umoja wa Mataifa na Mashirika yake pamoja na Taasisi nyingine. Hii itasaida pia kuongeza ajira na pia kuitangaza nchi yetu Kimataifa na kuhakikisha maslahi ya nchi yetu nje na sehemu zote, yanalindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya Sera ya Wizara ya Mambo ya Nje ni pamoja na kudumisha amani, usalama na utulivu katika nchi yetu na nchi jirani. Ni vyema basi ili kutekeleza azma yetu hii Serikali ijishughulishe kikamilifu kutafuta suluhu ya migogoo ya kisiasa katika nchi za jirani na Afrika kwa ujumla. Tuendelee kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kushiriki kikamilifu katika kudhibiti na kutatua migogoro katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara wajitahidi kuwaalika viongozi mbalimbali mashuhuri na kimataifa kuja kutembea Tanzania kwani ziara hizi zitasaidia kuimarisha ubia wetu na nchi nyingine mbalimbali. Mafanikio ya ziara zitokanazo na viongozi wa Kimataifa zinasaidia hata kupata mikataba mbalimbali ya maendeleo na kudumisha uchumi. Wizara pia iendelee kushawishi nchi wahisani kuongeza misaada yao kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE.CHARLES J.P.MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutokana na mgogoro wa mipaka na nchi ya Malawi tuangalie kwa ujumla wake mipaka yote ya nchi yetu. Zaidi ya mipaka lipo tatizo la wananchi wa nchi jirani kujipenyeza nchini kwetu. Kwa utaratibu maalum, wanunua maeneo ya mpakani kwa wingi na ukubwa. Kimipaka eneo linakuwa letu Tanzania, lakini kijamii kiutamaduni na kiuchumi eneo linakuwa siyo letu. Hii ndiyo hali halisi ya mipaka. Mkoa wa Kagera moja kwa moja au kuitia madalali na watu wenye uchu wa fedha, wageni wamehodhi maeneo makubwa kwa kundi la wafugaji moja ya dalili zao ni kuita ndugu au wafanyakazi toka nchi hizo za jirani.

Mheshimiwa Spika, upande wa mahusiano hasa mipaka ya Maziwa Makuu, mwingiliano wa watu unaingiza wahalifu wa kivita. Inasikitisha, watu wenye sifa na visasi vya kivita wanakimbilia Mikoa ya jirani ikiwemo Kagera, kujificha au kujejandaa kwa shughuli za mapambano nchini kwao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipange utaratibu wa kuwapa malengo Mabalozi wetu katika nia nzima ya kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi wanakotuwakilisha. Nashauri wataalam wa kiuchumi na masoko wapangiwe kazi kwenye Balozi zetu na wavezeshwe kufanya kazi. Ni imani yangu kuwa endapo kada hii itatumika moja kwa moja na kuwa kiungo na Mashirika, Idara za Serikali, Bodi za Mazao na hata Sekta binafsi, utaongeza tija katika kuteka fursa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, muda haukutosha. Naomba haya nayo mzingatie. Tumepata sifa za Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro akiwa Marekani, hakika ameweka siyo sifa ya Tanzania tu, bali Afrika na wanawake kwa ujumla / *wanted to add my voice from 1st hand information in USA.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo yetu, naomba *TBA Stock Verifier* na Wizara waunde chombo ambacho kitasimamia majengo yote ya Serikali nje ya nchi. Tunapoteza fedha nyingi za kungoja majengo

yaharibike kabisa ndiyo yafanyiwe ukarabati. Majengo mengine Bima wamekataa na majirani kulalamika kuwa tunahatarisha usalama wao. Tunatumia fedha nyingi kupangisha watumishi kumbe tungeweza kukarabati majengo kwa wakati kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipompongeza Mheshimiwa Maajar - Balozi Washington. Hakika anaheshimika na kusifiwa na watumishi, *diaspora* na Serikali na Taasisi za Marekani. Anajituma, anabuni mambo mbalimbali na amegawa *Business Cards* kwa *Diaspora* Marekani. Hivyo wako karibu naye, wanakutana kubadilishana mawazo na kadhalika. Naomba wapelekewe Katiba ya zamani na wapewe fursa ya kutoa maoni. Aidha, karibu nchi zote zimeomba wasisahauliwe kwenye sense ijayo. Vile vile *dual citizenship* imefikia wapi? Wanaomba tukamilishe.

Mheshimiwa Spika, watumishi waliokaa muda mrefu Ubalozini warudi ili tupate mawazo mapya. Je, kwa nini wataalam ambao *originally* siyo wa *foreign hupewa orientation* katika *centre for foreign relation for at least two to three weeks* kabla ya kuondoka ili wakidhi matakwa ya *foreign affairs* (kama Maafisa Utalii, Biashara, Uwekezaji)? *Local staff* miaka 30 kwenye Ubalozi London inakuwa sawa kweli? Wenzetu Kenya wana wataalam wote kwenye *consulate*. Tujitahidi kama ulivyosema, Los Angeles California iwe mapema.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimwa Waziri wa Mambo ya nchi za

Nje kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunayofahamu, Wizara hii ni roho ya ustawi wa nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa, hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika uetekelezaji. Ni heri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa upungufu unaojitokeza kila siku. Maana sidhani kama ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka makubaliano na nchi ya Trinidad na Tobago kwa ajili ya kupata msaada wa kitaalam kuhusu masuala ya gesi na uendeshaji wake. Lakini kuna ajabu kuwa, hatutoi ushirikiano wa kutosha kwa wenzetu hawa. Kwa kipindi cha miaka minne sasa, Balozi wao ameomba kuthibitishwa hapa nchini, lakini hajafanikiwa. Pia Waziri wa Sayansi na Teknolojia wa nchi hii ameomba kuja, lakini hapewi majibu. Je, ni kweli tunahitaji mahusiano?

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii licha ya Serikali kukiri kuwa kuna Watanzania wengi ambao wanaishi nje ya nchi na kuwa na uwezo wa kutosha kuweza kusaidia nchi, bado hatujafanya tathmini ya uhakika kujua ni Watanzania wangapi wako nje, ujuzi wao na nini ambacho wako tayari kusaidia Taifa lao? Naishauri Serikali iharakishe zoezi hili muhimu ili tuweze kutumia vyema fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wageni ambao wanatamani

kutembelea nchini kuhusu upatikanaji wa *visa*. Kwanini tusianzishe *Electronic Visas* ili kuleta wepesi japo kwa nchi ambazo tunaamini wananchi wake huwa wana sababu za kweli kutembelea nchini hasa watalii na wafanyabiashara, kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kuweka Balozi kila mahali.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaoishi nje washawishiwe kuwekeza hapa nchini kutokana na mapato yao huko waliko ikiwa ni pamoja na kulipa kodi hapa nchini. Hii inawezekana kwa kuweka mazingira mazuri kwao na kuweka vivutio kama tunavyofanya kwa wawekezaji wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana katika ajira kwa Watanzania kutokana na kuwa na wageni ambao haijulikani ujuzi wao, kupewa nafasi na fursa kubwa sana katika Soko la Ajira nchini hali ya kuwa Watanzania wanaweza kufanya kazi hizo. Serikali iliangalie hili kwa mapana na kuchukua tahadhari stahiki.

Mheshimiwa Spika, uvumbuzi mkubwa wa gesi nchini ni jambo jema, lakini changamoto kubwa ni kuthibiti wimbi la Makampuni ya kigeni, watu kutoka nje kuvamia fursa ya ajira. Naiomba Serikali ishirikishe Balozi zetu nje ili kujiridhisha kwa kufanya uhakiki (*due diligence*) kwa Makampuni haya na watumishi wao kabla ya kuja hapa nchini ili kuthibiti mianya ya matapeli.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri asirudi nyuma katika jitihada zake za kuhakikisha

suala la uraia wa nchi mbili linafikia ukomo na kutekelezwa. Tahadhari tu ni kuwa hii iwe ni fursa kwa Watanzania waliozaliwa hapa nchini ama wana asili ya hapa ili kudhibiti wanaotaka kujinufaisha na Utaifa wetu tu.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, ninayo mambo mawili hii leo katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, mosi, hali ni mbaya sana katika Balozi zetu nje na wazalendo hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kwa kucheleweshewa mishahara na posho, hawapelekewi katika muda muafaka. *OC* wanayopata haitoshelezi, inachelewa na haikidhi katika kuendesha Ofisi zetu za Ubalozi kwa ufanisi. Udhaifu huu ni dhahiri unachafua taswira ya nchi yetu katika nchi ambazo zipo Balozi zetu. Aidha, kwa Mabalozi wanaowakilisha zaidi ya nchi moja, wanashindwa kutekeleza majukumu yao katika hizo nchi kwa tatizo la ukosefu wa fedha za kutosheleza kutimiza wajibu wao ipasavyo, pamoja na mpango wa *retention* ya *visa fee*, siyo chanzo cha kuaminika kuondoa matatizo ya Balozi zetu. Kwani utalii, usafiri wa kutembea (*visiting*) au biashara ni vya msimu (*seasoual*). Hivyo kuna kipindi hakuna makusanyo. Je, Wizara ina mkakati gani wa kubadili tabia hii mbaya?

Mheshimiwa Spika, majengo na samani katika Balozi zetu nyingi hazipo katika hali nzuri, na kwa kuwa nchi hii tulishasahau utamaduni wa matengenezo (*culture of maintenance*), hakuna fedha zinazotengwa

kwa matengenezo. Makazi ya Balozi wetu Ottawa Canada yanahitaji matengenezo ya dharura na haraka ili kunusuru jengo ambalo kihistoria limenunuliwa toka Awamu ya Kwanza ya Uongozi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa, tumekuwa tunapoteza fedha nyingi kwa ajili ya ada ya pango ya Ofisi na Makazi ya Balozi zetu. Wizara ina mpango mkakati wa muda mfupi na mrefu wa kuondokana na tatizo hili hatua kwa hatua na kama upo mpango huo, unaanza lini?

Mheshimiwa Spika, pili, *APRM* nimepata kuwa Mjumbe wa *GC* ya *APRM* mara ilipozinduliwa, na kazi kubwa ilifanyika, na pia rasilimali fedha, na kufikia kuandaa taarifa na mpango kazi (*POA*) kwa wakati. Lakini urasimu wa Wizara hii ilichukuwa muda mrefu sana hata kuwezesha timu ya wataalam kuweza kuja kuhakiki taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa nia yake njema, kwa kuwa anafahamu umuhimu wa kujitathmini. Pamoja na nia njema aliyonayo, Wizara ama kwa ujumla au watu wachache wa Wizara kwa sababu wanazozijua wao, wanatumia mamlaka na madaraka yao kukwamisha mpango huu kwa kutupa uzito unaostahili na hususan rasilimali fedha. Hata kulipa ada tu nayo ni tatizo kubwa. Ni aibu kwa Rais wetu na Taifa kwa ujumla mbele ya Baraza la *APRM Africa*; jambo hili lina maslahi makubwa kwa Taifa letu. Wizara kama wanazo sababu za kutosheleza, basi ni vyema wakamshauri Rais

tukajiondoa kuliko fedheha hii. Tena ni kwa sababu Wizara tu kwa makusudi na hailipendi jambo hili. Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kukubali mahusiano na Morocco. Nchi yetu itapata manufaa makubwa. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Membe kwa maamuzi mazito.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba iliyosheheni hali halisi ya siasa yetu ya nje kama ilivyoelekezwa na ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, mwanadilpomasia nambari moja kwa namna ambavyo anaipa heshima nchi yetu. Kote tunakopitapita huko anatajwa tajwa vizuri tu jambo linalonifanya niamini kuwa kweli nabii hakubaliki kwao. Baadhi yetu Waheshimiwa Wabunge tumepata fursa ya kushiriki ziara za Mheshimiwa Rais huko nje. Tumeshuhudia kwa macho yetu kazi anazofanya, msururu wa watu mashuhuri na wawekezaji anaokutana nao na matunda yenyewe ya uwekezaji nchini mwetu. Majuzijuzi alikuwa Marekani kwenye Mkutano wa nchi tajiri Nane duniani (G8).

Nasikia tutapata fedha nyingi tu za kilimo. Vyombo vya habari vinapotosha kuhusu manufaa ya ziara ya Mheshimiwa Rais. Sisi Wabunge kimya! Sijui tumelogwa! Maana najiuliza, Marais wepi hawasafiri nje ya nchi? Hata Mgombea Urais tu wa CHADEMA na CUF wanasafiri nje ya nchi na wanatutangazia hapa na wakirudi wanapokelewa kwa maandamano, sembuse Mkuu wa nchi? Wengine humu humu nchini wanatembelea helikopta. Hali hii hawajapata madaraka bado!

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi kubwa ya Mkuu wa nchi ni kuiwakilisha nchi yake nje na kujenga mahusiano na nchi nyingine. Hivyo ndiyo mojawapo ya kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais na ndiyo maana ni mwanadiplomasia namba moja katika nchi yoyote. Marais wa Ulaya wanasafiri China, akisafiri wetu kweli iwe nongwa? Marais hawana haiba na uwezo mkubwa na hivyo kutokubalika kimataifa au wakiondoka. Sababu zote hizo tatu Mheshimiwa Rais wetu hana. Kinachomzuia kusafiri ni nini? Mimi nasema Mheshimiwa Rais aendelee kusafiri, na nitafurahi zaidi nikimwona anakwenda China, India, Japan, Korea Kusini na Uturuki angalau mara moja kwa mwaka. Maana wenzake wa Marekani, Ulaya na Afrika hawakauki kwenye nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Membe anachosisitiza katika safari za Rais na zake ni kuhusiana na Sekta binafsi ili waweze kukutanishwa na wenzao huko nje. Utaona hapa wakija Viongozi Marais na Mawaziri huambatana na wafanyabiashara na

wawekezaji. Nasi tufanye hivyo, maana sekta binafsi yenye we wakati mwingine inakuwa vigumu kukutana na mamlaka za juu za nchi nyingine kama hawaambatani na misafara ya Rais. Mimi naamini mkijipanga kisayansi, mkashirikisha Taasisi na hasa Sekta binafsi, safari hizi zitakuwa na tija zaidi na pengine vijimaneno maneno vitapungua. Mie nitapenda kuona Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba akiambatana na Mheshimiwa Rais ili akifika kule anamkutanisha na Mkuu wa Taasisi zinazonunua Pamba au Korosho wafanye biashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni kwa kiasi gani Wizara hii inashirikiana na Wizara ya Utalii na Bodi ya Utalili na *TANAPA* katika kutangaza utalii wetu? Nashindwa kuelewa ni kwa kiasi gani Cuba ambayo iko katika vikwazo vikali vyta kiuchumi kwa miaka 50 sasa, inapokea watalii milioni 2.5 kwa mwaka wakati sisi na Mlima wetu Kilimanjaro Mbuga za Wanyama adimu za Serengeti na Ngorongoro, fukwe mwanana za Zanzibar, tupate watalii milioni moja kwa mwaka. Sijasema kwa makusudi takwimu za Egypt ambayo inapokea watalii milioni 9. Egypt zaidi ya milioni 10 na Kenya zaidi ya milioni moja kwa mwaka. Nataka kufahamu, ikiwa zoezi hili la kuvutia watalii na kutangaza utalii wetu mnalifanya kwa pamoja: Je, Maofisa Utalii au Ofisi za Utalii ziko katika Balozi zetu? Tuna mpango gani mathalan kuvutia watalii wengi kutoka China, Uturuki na Arabuni ambazo wananchi wake wengi husafiri kwa shughuli za Utalii nje?

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, endeleeni kusafiri mtufungulie fursa na kutuletea manufaa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi name nichangie hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wa kuwasilisha hotuba. Kweli imesheheni hali halisi ya siasa yetu kama ilivyoelekezwa na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mabalozi na Maafisa wa *Foreign* popote walipo na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri unavyotupa moyo kwa utendaji wako mzuri na jinsi unavyoiweka nchi yetu katika nafasi ya juu Kimataifa, yaani tumepata kiwango cha juu, *international personality* ya Tanzania ikiangalia kipindi hadi kipindi.

Mheshimiwa Spika, kote tulikotembelea tumepokewa na kukarimiwa vizuri na Mabalozi pamoja na Maafisa wao, yaani tumepata *Consular Assistance first class* kabisa. Naomba Serikali iongeze malipo ya fedha za tahadhari katika Balozi zetu nchi za nje. Aidha, Mabalozi na Maafisa hawa walipwe motisha kubwa ili wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, sifa zote za Wizara hii inatiwa doa na hali ya Balozi zetu. Moja, ni uchakavu wa

majengo na magari ambayo hayaendani na unadhifu wetu kama nchi. Tunashindwa hata na vinchi vidogo vidogo na nchi nyingine tumezikomboa wenyewe kwa damu yetu, leo zinamiliki majengo makubwa na zina Balozi hata kule ambako sisi hatuna Balozi. Naiomba Serikali ikubali na kuhakikisha kuwa Balozi zinakuwa na usafiri wa kutosha na wa kuaminika. Heshima ya Taifa ni ghali sana. Kwa hiyo, Serikali isiwe na kigugumizi, ila kukubali kuipa Wizara ya Mambo ya Nje bajeti ya kutosha ili itekeleze majukumu kwa ufanisi zaidi. Kama Serikali inaona mzigo kuhudumia idadi hii ya Balozi, ni heri kuzifunga baadhi ya Balozi ili tuwe na Balozi chache tunazoweza kuzimudu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nadhani hii iwe ndiyo bajeti ya mwisho ya ufinyu wa kiwango hicho. Mwaka hadi mwaka kumekuwa na kilio cha aina hii huku mwelekeo wa bajeti ukiwa ni wa kushuka ikizingatiwa kuwa thamani ya dola ya Kimarekani inapanda. Ikiwa mwakani Mheshimiwa mtaleta bajeti ndogo isiyotosha tena, sitaunga mkono kabisa bajeti ya Wizara hii. Ni bora mje mtamke kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na masuala ya diplomasia siyo kipaumbele chetu, hivyo mtuletee mpango wa kufunga baadhi ya Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, mwanadiplomasia nambari moja kwa jinsi anayoipa heshima nchi yetu. Duniani kote anaheshimika sana na anatajwa vizuri, tunakopita ama kweli Nabii huwa hakubaliki kwake. Baadhi yetu Wabunge tumeshiriki ziara za Mheshimiwa, tumeshuhudia kazi anazofanya, msururu wa watu

mashuhuri na wawekezaji anaokutana nao na matunda yenyewe ya uwekezaji nchini mwetu.

Majuzi alialikwa Marekani kwenye Mkutano wa nchi tajiri nane Duniani (G8) ambapo tumepata fedha nyingi kwenye Kilimo. baadhi ya watu wanalipotosha jambo hili kwa makusudi kwa kusema Rais anasafiri sana. Ni Rais yupi hasafiri? Angalieni Viongozi wa Upinzania wana safari mara kwa mara nje ya nchi wengine humu humu wanasafiria na helkopita, Rais kusafiri tunaona gharama licha ya faida tunazoziona! sijui tumelogwa?

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize tu kuwa zinapotokea safari za Rais ni vyema tukashirikisha sekta binafsi ili waweze kukutanishwa na wenzao huko nje. Utaona hapa wakija Marais wa nje huambatana na wafanyabiashara na wawekezaji. Nasi tufanye hivyo ili kuwapa fursa sekta binafsi kukutana na mamlaka za juu za nchi nyingine bila ya kutumia misafara. Natamani kuona viongozi wa Bodi za mazao wakiambatana na msafara wa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu, ni kwa kiasi gani Wizara ya Mambo ya Nje inashirikiana na Wizara ya Utalii na Bodi ya Utalii na *TANAPA* katika kutangaza Utalii? Nashindwa kuelewa ni kwa kiasi gani Cuba ambayo iko katika vikwazo vikali vya kiuchumi kwa miaka 50 inapokea watalii milioni 2.5 Misri zaidi ya milioni 10 Kenya zaidi ya milioni moja, sisi wenye Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Serengeti na Ngorongoro, fukwe za Zanzibar, tunapata watalii kidogo. Je, kuna

Maafisa Utalii katika Balozi zetu? Tuna mpango gani wa kutumia Balozi za nje kutumika kukuza utalii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Diplomasia, nawapongeza Dkt, Maulidi Dkt. Kitojo na Dkt. Achiula kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia changamoto zilizopo katika Chuo hicho. Kwanza, Chuo hakina hosteli wakati wanafunzi wanatoka maeneo mbalimbali ya nchi. Usafiri kwa Watendaji Wakuu – Dkt. Achiula na Dkt. Kitogo ni fedheha kwa Watendaji hawa kuja Chuo kwa daladala. Wizara imekuwa haitoi nafasi kwa wanachuo kufanya *field* katika Wizara na vitengo, mamlaka zilizo chini ya Wizara kama A/CC. Hivi ni upi ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji? maana uhusiano uliopo katika kuendesha Chuo ni ule wa kupandisha na kushusha bendera ya Msumbiji pale Chuo.

Mheshimiwa Spika, wako Watanzania walioomba *Visa* ya Saudia kwa ajili ya Umra, lakini wamekosa wakati walilipa tiketi, hoteli, hivyo kuwasababishia hasara kubwa. *Visa* hadi itoke Saudia, na Balozi hana uwezo wa kutoa *visa* hiyo. Tunaomba Wizara kuwanusuru Watanzania hao waliokwama na safari yao ni wiki hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Honorary Consulate*, wapo watu wenye mapenzi ya kufungua ofisi kule Czech Republic lakini ofisi zetu za Ujerumani kwa

takribani mwaka mmoja imeshindwa hata kutoa majibu kwa mhusika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya kulinda diplomasia na kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha. Naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri Naibu Waziri na Wataalam wa Wizara kwa hotuba yao iliyowasilishwa vizuri. Nawapongeza pia kwa kujitahidi kufanya kazi katika mazingira magumu ya bajeti isiyotosheleza mahitaji. Naipongeza pia Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni ambayo Serikali inapaswa kuyazingatia katika majumuisho na pia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, lengo la Wizara ya Mambo ya Nje ni kuhakikisha Taifa linakuwa na mahusiano mazuri ya kisiasa, kiuchumi kibashara kiutamaduni na kadhalika na nchi nyingine. Lengo lingine ni kuhakikisha Taifa linajijengea hadhi ya kiwango cha juu katika nyanja mbalimbali za siasa, uchumi, utamaduni, michezo na kadhalika. Katika awamu ya kwanza, Tanzania ilijijengea hadhi na sifa ya kiwango cha juu sana katika anga za Kimataifa, hasa kwa sababu tulikuwa watetezi wakuu wa haki za binadamu. Tanzania ilisifika nyakati hizo, siyo kwa sababu tu ilikuwa na msimamo thabiti usiotetereka katika masula ya uhuru wa nchi za Afrika, bali pia kwa sababu haikuhofu kutofautiana na Mataifa makubwa

kuhusiana na suala lolote lililohusu haki kuhusu uhuru wa nchi za Afrika. Tanzania ilitofautiana na nchi zote za Magharibi pamoja na Marekani. Ni kweli kuwa, kwa kiasi fulani msimamo huu bado upo, ingawa siyo kwa uthabiti wa mwanzo na ni kweli kuwa kwenye anga za Kimataifa Tanzania kwa kiasi kikubwa inakula pensheni ya hadhi iliyokuwa nayo awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna hisia kuwa sifa ya Tanzania imeshuka Kimataifa, hii inachangiwa na ukweli kwamba katika mambo mengi Tanzania inafuata maamuzi yaliyofikiwa kwa shinikizo la Mataifa makubwa. Kwa mfano, msimamo wa Tanzania kuhusu suala la Iran ni upi? Iran inachotaka ni kuijendeleza katika utafiti wa nyukilia, Marekani na nchi za Magharibi hazitaki kwa kisingizio kwamba eti Iran inataka kutengeneza zana za nyukilia, dai ambalo mpaka leo halijathibitishwa na Tume ya Kimataifa ya Nyukilia. Nchi nyingine za Kiafrika pamoja na Tanzania zimefuata msimamo wa Marekani na nchi za Ulaya bila kueleza sababu za msingi kwa nini zinafanya hivyo. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa wakati wa awamu ya kwanza ambapo kila uamuzi ulielezwa waziwazi na ukaeleweka na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mahsusि kutoka kwenye awamu ya kwanza. Msimamo thabiti kwenye anga za Kimataifa awamu ya kwanza ulisaidia pia kwenye migogoro ya mpakani. Tunakumbuka jinsi Rais Banda wa Malawi alileta chokochoko kwa kudai kuwa Ziwa Nyasa ni mali ya Malawi na kisha akabadilisha jina lake na kuliita Ziwa Malawi. Rais wetu, Mwalimu Julius Nyerere alilishughulikia suala hili kwa uthabiti na hadi

hivi majuzi hakuna yeote aliyerudia dai hilo. Serikali yenye msimamo thabiti huwa haichezwi chezewi na nchi jirani. Hata suala la wahamiaji haramu maeneo ya Mkoa wa Kagera na mengineyo ambao wameweza hata kuchukua mali za wenyeji bila kuchukuliwa hatua, ni kiashiria cha ulegevu wa msimamo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa nitaongelea kidogo jambo ambalo limeongelewa na Wabunge wengine kuhusu majengo mabovu ya Balozi zetu nchi za nje. Napenda kusitiza tu kwamba sura na hali ya majengo ya Balozi hutoa taswira hasi kuhusu Taifa letu kwa watu wowote. Wanaotaka huduma kwenye Balozi zetu, majengo ya namna hiyo yanalipunguzia Taifa hadhi kimataifa. Taifa linaonekana ni la watu wasiojali, wasio makini, wazembe na labda hata wachafu! Serikali ijipangie mpango mkakati wa namna ya kuyafanyia matengenezo majengo hayo ili katika kipindi kisichozidi miaka mitano, majengo yote ya Balozi yawe yamekarabatiwa. Fedheha ya kuwa na majengo mabovu ya Ubalozi imalizwe kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Serikali inaweza kufanya ili kuzidi kujijengea sifa katika anga za Kimataifa ni kuanzisha Vituo vya Utamaduni katika Balozi zetu. Wizara ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na BAKITA, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), BASATA na Taasisi nyingine za kitamaduni za Kkimataifa, inaweza kufanya shughuli hii. Zipo nchi nyingi ambazo zimejjijengea sifa kwa kuanzisha Vituo vya Utamaduni katika nchi nyingine. Kwa mfano, Uingereza (*British Council*), Ufaransa (*Alliance Française*) Urusi, Iran na kadhalika. Vituo vya

Utamaduni vinavyopendekezwa kuanzishwa katika Balozi zetu viwe na lengo la kuwa vitovu vyatua kuenezea Kiswahili na utamaduni wa Tanzania. Katika kutafakari namna ya kutekeleza jambo hili, wakati wote tuzingatia ukweli kwamba lugha na utamaduni ni biashara na vinaweza kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ili tujenge Taifa lenye hadhi chanya kimataifa, lazima Serikali ikubali kuwekeza fedha ya kutosha. Ni kama biashara nyingine yoyote. Jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa uwekezaji huu unaleta tija baada ya muda na tuwe na vigezo vyatua kupima tija hiyo.

MHE. JAMES FRANCIS MBATIA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutumikia Taifa letu. Napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yetu ijitahdi kurudisha uhusiano wetu kwa kiwango chenye tija inayoridhisha na Serikali ya Uholanzi ukizingatia kwamba mahusiano yetu na Serikali ya Uholanzi pamoja na mambo mengi yamesaidi sana kuanzishwa kwa Kituo cha Demokrasia Tanzania (*TCD Tanzania Centre for Democracy*) chini ya juhudhi za ufadhilli wa *the Netherlands Institute for Multiparty Democracy (NIMD)* ambapo tangu kuanzishwa kwa *TCD* Julai, 2005 tumefanikiwa kuratibu meza ya mazungumzo ya Vyama vyatua Siasa Tanzania hasa vile vyenye uwakilishi Bungeni.

Kwa pamoja tumefanya: *Capacity building programs*; midahalo mbalimbali kuhusu uandikwaji wa Katiba Mpya; mikutano ya nchi mbalimbali za Afrika, kwa mfano mkutano wa kuvijengea Vyama vya Siasa uwezo wa kifedha uliokutanisha nchi 11 za Bara la Afrika na kufanyika jijini Dar es Salaam tarehe 10 - 13 Julai, 2012; *NIMD/TCD* kututafutia marafiki wapya wa kukuza na kuimarisha demokrasia kama vile Danish *Institute for Parties and Democracy (DIPD)* *International Institute for Democracy and Electoral Assistance (International IDEA)*; tathimini ya ukuaji wa Demokrasia katika Serikali za Mitaa; kuratibu Kamati ya Fedha za pamoja na *UNDP* kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Kuizamisha Demokrasia ndani ya Vyama na katika jamii ya Watanzania na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushauri kwamba Ofisi zetu za Kibalozi nje zifanyiwe ukarabati unaoendana na hadhi ya nchi husika pamoja na samani za ofisi; maslahi ya wafanyakazi wetu kwenye Balozi yaendane na hadhi ya viwango vya nchi husika; Serikali yetu ijjitahidi kufungua Ubalozi na Australia unaojitegemea kutokana na ukubwa wa nchi hii (Bara la Australia) na uwezo wake kiuchumi duniani; Balozi zetu zijitahidi kutafuta na kuhamasisha wanafunzi wa kusoma Kiswahili waweze kuja kusoma katika Vyuo vyetu vya Tanzania. Pia uwezekano wa *exchange programs* mbalimbali kati ya Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu (Vyuo Vikuu) na vya nchi marafiki.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ijayo Wizara itupatie takwimu za hatua ambazo tumefikia

ukilinganisha na Mataifa mengine kuhusu Lengo la Nane la Milenia *Global Partnership*

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Balozi zetu nje ni machakavu na hayana vitendea kazi. Mabalozi wetu wamekuwa wakipata shida kutokana na uchakavu wa majengo hayo. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje kwa upande wa Zanzibar hawana gari, hawana watumishi wa kutosha, yaani Ofisi hazieleweki. Ni vigezo gani vinavyotumika kuajiri watumishi kwa upande wa Zanzibar? Kuna malalamiko kutoka kwa Wazanzibar kuwa, nafasi ambazo zinatolewa kwa Mabalozi kwa upande wa Zanzibar, ni chache na ambao wanapata nafasi hizi wamekuwa wakipelekwa katika nchi za kiarabu.

Mheshimiwa Spika, ni kwanini Wazanzibar hawateuliwi kuwa Mabalozi katika nchi za bara la Ulaya na Amerika? Ni Wazanzibar wangapi ambao wameteuliwa katika Ofisi za Ubalozi na wamepelekwa katika nchi za Bara la Ulaya na Amerika?

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, zaidi Balozi zetu zimekuwa hazifanyi kazi ipasavyo hasa katika kutangaza utalii na biashara zilizopo nchini, na kuufanya uchumi wa Tanzania kudorora tofauti na nchi nyingine kama Kenya ambapo wao wanatuzidi kwa kiasi kikubwa sana katika kutangaza utalii na biashara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ni kwanini Serikali na Wizara isiboreshe Balozi zetu ili wapate kutangaza utalii nchini kwetu ili tuweze kuongeza kipato (pato) la Taifa na Balozi kuweza kujitegemea zenyewe?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na desturi kwa viongozi wa Serikali ambao sio waadilifu, wamekuwa wakiiibia Serikali au kupokea rushwa kutokana na mikataba mibovu, fedha hiso wanaziweka katika akaunti za nchi za nje na hata inapobainika Serikali inakuwa na kigugumizi jinsi ya kuflisi pesa hiso na kuzirudisha nchini. Kutokana na Serikali kushindwa kuchukua hatua hiso za kurudisha pesa nchini, kunafanya wafanyakazi hao wa Serikali waibe pesa na kuendelea kupeleka pesa katika akaunti zao za nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali isichukue hatua za kurudisha pesa zilizopo katika akaunti za nje za Viongozi wenyе kutuhumiwa kujihusisha na masuala la rushwa au wizi ili uwe mfano kwa viongozi wengine?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wanaoishi nje wanakosa haki zao kama vile kupiga kura wakati wa Uchanguzi Mkuu. Kwa mfano, Kenya sasa hivi wana mtandao wa wananchi wao kupiga kura popote walipo duniani. Ni kwanini Watanzania wanaoishi nje wasipewe fursa ya kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu?

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, naomba nishauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nilifanya ziara Canada na nikiwa na wenzangu, tukatembelea Ofisi ya Ubalozi wetu Canada. Wafanyakazi wa Ubalozi walituomba tukifika Tanzania tueleze matatizo makubwa tuliyoyaona Ubalozini. Tatizo kubwa ni ukosefu wa fedha. Fedha zinazotumwa huko ni kidogo, haziwawezeshi kuishi, kuhudumia Ubalozi na hata kufanya ukarabati. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, aeleze jinsi atakavyotatua tatizo hili ili na wenyewe wajue tulifikisha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ni lugha inayokua na kuenea kwa kasi sana. Wizara ya Mambo ya Nje inaweza kukuza lugha hii ikaenea duniani kote na walimu watakaokuwa wanaeneza Kiswahili duniani wakawa wanalipwa mishahara na kuliletea Taifa letu mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Malawi wanataka kutunyang'anya Ziwa Nyasa kwa sababu ya tetesi kwamba Ziwa Nyasa lina gesi na mafuta. Ningeshauri Serikali ya Tanzania itafute wawekezaji haraka sana ili kama kuna gesi au mafuta tuanze kuyachimba kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni fedha za rada. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje aliwahi kusema anawafahamu watu waliochukua fedha za rushwa, tunaomba awataje kwa majina ili wafkishwe Mahakamani. Asipowataja watu,

watadhani Serikali inawajua lakini inawalinda kwa manufaa binafsi.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti hii, hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo ningependa myatambue ni kama haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kufikia mkakati wa mia kwa mia wa usawa katika nafasi mbalimbali za maamuzi na uongozi, ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja, alieleze Bunge lako Tukufu takwimu zinazoeleza tuna nafasi ngapi za Ubalozi wa Wanawake? Mabalozi tulionao katika Balozi zetu ni wangapi na mgawanyo uko vipi kimabara?

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kufahamu endapo tuna takwimu za Watanzania ambao wamefungwa nchi za nje (wanawake na wanaume) na pia kuna utaratibu wowote ambao nchi yetu inatoa msaada wa kisheria kwa Watanzania wanaoshtakiwa nje ya nchi? Kuna utaratibu wa kubadilishana wafungwa? Hapa kwetu kuna wageni wengi wamefungiwa hapa: Je hakuna uwezekano wa kubadilishana ili tuje tuwasaidie?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais amekuwa akipita katika nchi mbalimbali na

kuwahamasisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuona umuhimu wa kuja kuwekeza katika nchi yao: Je, ni vivutio gani mmewekeza ambavyo vitawafanya kuja kuwekeza au wataalam kufanya kazi hapa nchini kwetu kama Madaktari na wengine? Yamekuwepo malalamiko makubwa kwamba Watanzania wanapokuja hapa nchini mizigo yao hutozwa kodi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la akina mama ambao wameolewa na wanaume wa kigeni, waume zao kutopata angalau kibali cha kuishi hapa. Ni unyanyasaji wa kijinsia na ni sheria iliyopitwa na wakati kama tunaongelea haki za binadamu. Wanaume wanapooa raia wa kigeni anaruhusiwa kupata kibali cha kuishi hapa na hata kufanya kazi. Ni lini utaratibu huu utabadilishwa? Maana kama ni suala la kazi, hata hao wanawake wa kigeni huwa wana elimu ya kupata kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja, atoe ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania nje ya nchi. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Diplomasia ya Uchumi ni kubwa na lenye umuhimu wa kipekee katika kukuza uchumi wa nchi yetu, lakini utekelezaji una upungufu unaohitaji ufanyiwe kazi. Wataalam Ubalozini katika

Ofisi zetu za Ubalozi, nyingi hazina wataalam wa kushughuliki suala hili. Ushirikiano na Taasisi zingine, utekelezaji wa Serikali hii, hauwezi kufanywa na Ofisi za Ubalozi peke yake. Ni lazima ushirikiano uwepo na Wizara za kisekta na mashirika kama *TTB*, *TANAPA* na kadhalika. Hivi sasa ushirikiano ni mdogo na wa kibajeti ndiyo haupo kabisa.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba upungufu huu ufanyiwe kazi ili kutoa uzito na msukumo wa utekelezaji wa sera hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Makansela wa Heshima za Mibro (Italia), *nice (France)* na Uhlanzi zinatoa *visa* kwa wageni wanaoingia nchini bila ya kutoa *visa stickers*, matokeo yake mapato makubwa yavuja na hivyo Balozi zinakosa mapato. Ushauri ni kwamba, Wizara ishirikiane na Hazina na *immigration* ili wale wote wanaotaka *visa* huko Ughaibuni wasimamiwe watoe *visa* kwa kutumia *visa stickers* na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, linguine ni *foreign service regulations*. Kanuni hizi zimepitwa na wakati na hivyo zina upungufu mwingi, baadhi watumishi wa Ubalozi wanalipwa posho ya kufanya kazi nje (*foreign service allowance*) kwa kupishana nchi kwa nchi katika kanda ambazo hali ya mwisho ni sawa. Kwa mfano, ukanda wa *Europe* (Ulaya) ni kwanini viwango vipishane? Tazameni upya suala hili.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la watoto kusomeshwa Shule ya Msingi tu, lakni Sekondari hairuhusiwi; hili nalo litazamwe upya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Pili, hongera kwa kusoma vizuri, hongera sana. Tatu, bajeti hiyo haitoshi. Sh. 98,339,707,000/= ni ndogo sana, kwani Mabalozi wa Ufaransa na Ujerumani wapo hoi, fedha haziwatoshi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni marejesho ya vitu viliwyopo nje ya nchi (masuala mtambuka). Mikoa ya Kusini ina kiu ya muda mrefu ya kutaka *Dinosaur* (mjusi) aliyechukuliwa tarehe 10 Januari, 1910 kwenda *Museum* ya Ujerumani, Berlin (*Namkunde Museum*). Hivi sasa anazalisha karibu ya zaidi ya bilioni tatu kutohana na watalii wanaokuja pale, karibuni watalii 500,000 kwa mwaka. Kwani kimekuwa kivutio kikubwa duniani kumwona mjusi mwenye kilo 80 uzito na urefu mita 22.70 na upana mita 11.90. Ni mdudu aliyeishi miaka milioni 150 iliyopita duniani. Ndugu zetu wa Umoja wa Afrika na nchi za Afrika na Bunge la Afrika (*Pan Africa Parliament*) waliopitisha azimio mwaka 2004 la kusema kuwa nchi zinazotaka kurudishiwa mali zao zilizotoka wakati wa Ukoloni watarudishiwa na *UNESCO*, wapo tayari kusaidia marejesho hayo na utunzaji.

Je, Serikali ya Tanzania inatoa kauli gani kuhusu kumrudisha mjuzi *Dinosaur* huyo. Wajumbe wa Lindi wapo hapa leo wanataka wasikie kauli yako kuhusu *Dinasaur*, Mjusi wa Tendeguru, Mipingo, Lindi, angalau tupate maelezo tu, kwani suala hili sasa limeingia kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara husika haitoshi, kwani bado kuna limbikizo ya madeni ya pango za Ofisi nchi za nje, pango za nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaosoma nchi za nje, ada hazitoshi. Hivyo bajeti iongezwe ili wanafunzi nje wasome bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, chokochoko zinazotoka Malawi zisidharauliwe. Tanzania tuwe macho ili wakianza uvamizi wa dhahiri tuchukue hatua kama vile Uganda mwaka 1978.

Mheshimiwa Spika, Mabalozi wa kike waongezwe. Tumeona wanawake ni waaminifu na wachapakazi kama Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, ameonyesha mfano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara ambayo mara nyingi inaitangaza nchi katika kuipatia maendeleo kwa kutangaza sekta muhimu katika nchi kama vile kuwekeza katika Sekta ya Kilimo, Uvuvi, Viwanda na Ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pia ni Wizara ambayo inaomba misaada mingine kutoka nje yenye maslahi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar alipokuwa akichangia katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar alisema kwamba, namnukuu: yeye na Waziri wa fedha wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee walipata msaada wa Shilingi billioni 200, wakatakiwa ili wakabidhiwe fedha hizo wapate saini ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, lakini Mheshimiwa Waziri Bernard Kamili Membe alikataa kuweka saini. Sasa: Je, katika hili tunawatakia heri kweli Wazanzibar?

Mheshimiwa Spika, suala la mipaka ya Bahari ya Hindi ibaki kama ilivyo. Suala la kusema kwamba kuna ujumbe ulioondoka kwenda Umoja wa Mataifa kuangalia upya au kuongeza ardhi ya Zanzibar kuingiza katika Muungano, ni jambo haliwezekani.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia Wizara hii kwa maandishi. Tanzania na Msumbiji ni nchi ndugu, rafiki na zinategemeana kwa mambo mengi sana. Tanzania tumesaidia sana upatikanaji wa uhuru wa Msumbiji na kupelekea Mikoa ya Kusini hasa Mtwara na Lindi kuchelewa sana kupata maendeleo, kwani ulikuwa ni ukanda wa vita.

Watanzania tulikuwa rahimu sana katika kuwapokea wakimbizi wa Msumbiji na kuwatunza hadi

hivi sasa tukitarajia kuwa Msumbuji wakiwa huru tutazidi kushirikiana kiuchumi na kiundugu. Pia kwa kukamilisha hilo, Serikali ya awamu ya tatu ilisaini Mkataba wa Ujenzi wa Daraja la Umoja na Serikali ya awamu ya nne. Kukamilika kwa daraja hilo kulileta matumaini makubwa kwamba sasa uchumi utafunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa wananchi wetu wananyanyasika sana wanapokwenda Msumbiji. Hata kama taratibu zote wamekamilisha, lakini wananyanyasika, wanapekuliwa wakiwa uchi, wanapigwa, wananyang'anywa mali zao, jambo ambalo wananchi wetu hawaoni maana ya ushirikiano wala huruma yote tuliyowafanyia katika kipindi chao chote cha kupigania uhuru.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wananchi wa Msumbiji wanakuja upande wa Tanzania bila tatizo, wanakuja kupata matibabu bila tatizo, wanakuja kibiashara bila tatizo. Kwa nini Watanzania wakivuka wanawanyanyaswa? Kwanini wananyang'anywa mali zao? Hali ambayo hivi sasa Watanzania wanapita njia za panya kukwepa adha ambayo wanaipata mpakani.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kikao na Balozi wa Msumbiji pamoja na Viongozi Wakuu wa Msumbiji kufanya mazungumzo ili kuweka hali nzuri na Watanzania wanufaike na ushirikiano wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Masasi akutane na

wananchi ili waweze kumpa matatizo ambayo wanayapata huko Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi, Mabalozi na Wafanyakazi wote kwa kuandaa bajeti nzuri na ya kisayansi.

Mheshimiwa Spika, Ubalozi wa *UK* upo Tanzania tangu uhuru. Miaka yote, *visa* zilikuwa zinatolewa Dar es Salaam. Katika miaka ya karibuni *visa* za *UK* zimekuwa zinatolewa Nairobi na huchukua wiki mbili. Jambo hili linasikitisha, kwani Ubalozi wa Uingereza hapa Dar es Salaam ni Ubalozi kamili na siyo *Consulate*. Kwa nini Ubalozi huu hautoi *visa* kama zamani?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri afafanue hili.

MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA: Mheshimiwa Spika, ofisi za Zanzibar kwa kweli iko nzuri nje, lakini ndani haina haiba ya jina la ofisi. Ushauri wangu ifanyiwe *extension* na nafasi iongezwe ndani. Jambo hili pia linasisitizwa na vitendea kazi vya ndani pamoja na usafiri wenyewe staha za kiitifikasi ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, nashauri diplomasia ya kiuchumi igawike katika sehemu mbili; ile inayoshughulika na *Macro Economical Issues* na pili

Micro Economical Issues lengo uhusiano uongezeke na ufikishe na kushughulika wafanyabiashara wa kawaida. *Diaspora* itumike vizuri na wana-diaspora kuleta na kuwekeza pesa zao nyumbani na benki zetu zifunguliwe nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, *SADC* mahusiano ya kiuchumi na kiulinzi/maafa yaendelee. Yapo katika kiwango kizuri cha kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *EPA*; tuwe waangalifu sana na mashauriano haya. Ni wazi vipo vipengele vizito vinavyotoa uangalifu, lakini lazima tutafakari kwani ndio hawa hawa wanaotusaidia katika shughuli zetu za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, *AMISOM* nashauri kamwe Tanzania isijiunge na jeshi hili kwa faida ya kutumia *Geographical* na *Political shield*, kama tungejunga basi tungekuwa na hali mbaya sasa.

Mheshimiwa Spika, pili, *negotiation* za *mutual defence pag*, tuwe waangalifu pia kwa kuwa tayari tumeshakuwa na *bilateral* yetu na *SADC*. Nashauri Tanzania katika *negotiation* tumalize kama Japan na *NATO*. Tuishie na kitengo cha huduma, tuishie kitengo cha mafunzo baada ya mapigano, ustawi wa jamii, sio kwenda *front line*, kazi hii tumeshafanya katika ukombozi wa Afrika.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa

Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hii kwa maandalizi ya hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kwenda India kikazi na nilishangaa kuambiwa kuwa Naibu Waziri wa Tanzania hayupo kwenye orodha ya VIP kama ilivyo kwa Mawaziri, namshauri Waziri katika kuweka mahusiano na nchi ya India alifanyie kazi hili .

Mheshimiwa Spika, suala la mpaka wa Tanzania na Malawi limechukua miaka mingi bila kufikia muafaka, sasa imekuwa kila Rais wa Malawi anakuwa na msimamo unaobadilika badilika. Tufike mahali tupate muafaka, ramani nyingi zilizopo na ambazo zingine tunatengeneza wenyewe hatuoneshi waziwazi kama mpaka wa Malawi na Tanzania umepita katikati ya Ziwa Nyasa kama ilivyo kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:
Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwenye suala la uraia wa nchi mbili kwa raia wa Tanzania ambao wanaoishi nje ya nchi. Kuna Watanzania wengi wapo nje si kwa sababu ya kutoipenda Tanzania ila ni kutafuta maisha. Kwa mustakabali huo, naomba Serikali iandae Muswada wa Sheria ya kutoa nafasi kwa Watanzania kuweza kuwa na uraia wa nchi mbili.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana

Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi ya leo. Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Membe kwa ufanuzi mzuri na wa hali ya juu ambao ameutoa kuhusu mpaka halali kati ya Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa. Jambo hili limeelezwa vizuri na sasa kuna haja ya kuimarisha ulinzi katika eneo husika ili kuzuia vitendo vyovyote vya uchokozi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mahadhi Juma Maalim kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tuimarishe ulinzi na maeneo ya mipaka yote ya nchi yetu, Wilaya ya Siha ni moja ya Wilaya ambazo imeshuhudia matukio ya hapa na pale kuhusu wizi wa mifugo ambao umekuwa unawasumbua wananchi waliopo katika maeneo ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wizi wa kupitisha mazao mpakani bila kulisipia ushuru, kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Siha tunapendekeza tuwe na soko la sura kama lile la Himo ili tuweze kuzuia upotevu wa fedha kupitia kutolipwa ushuru kupitia katika eneo la West Kilimanjaro katika eneo la Mji mdogo wa Ngarenairobi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, suala la mgogoro wa mpaka Tanzania/Malawi ni kwamba ikiwa Malawi watatii maelekezo yetu ya (*maintenance of status Quo*). Tuwe na mizunguko mitatu ya mazungumzo ya kidiplomasia (Dar es Salaam *three meetings*, Lilongwe *three meetings*). Mazungumzo yasipozaa matunda bora kwetu tutumie njia nyingine haraka.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Malawi watakaidi na kuendelea na uvamizi katika eneo la Tanzania kwa shughuli yoyote ikiwemo tafiti za mafuta na kadhalika. Baada ya mukutano wa Lilongwe wa kwanza tuwe na mmoja tena Dar es Salaam na kumalizia Lilongwe. Tukitoka Lilongwe katika mukutano wa nne ama wa pili kwa Lilongwe tuchukue hatua mbadala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti hasa Ofisi zetu za Ubalozi nje ya nchi, fedha zinazotengwa ziwe *ring fenced* ili kuepusha aibu kwa kuwa Ofisi zetu za Ubalozi pamoja na wafanyakazi wake ni kioo cha Taifa nje ya nchi, tusikubali kujiaibisha, bora tujibane nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kujipanga vema zaidi Kibalozi (kutuwakilisha nje ya nchi) Balozi zetu ziwe *ranked* kufuatana na umuhimu kiuchumi, kiulinzi na usalama, kisiasa na kadhalika. *Ranking* hiyo ipitiwe mara kwa mara ili kuboreshwa na kuwa *updated, ranking* hiyo ndiyo iwe mionganoni mwa vigezo vikubwa vyataga mgawanyo wa rasilimali zikiwemo rasilimali fedha, rasilimali watu, rasilimali vifaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji na matunzo ya majengo na vifaa vingine vya Balozi zetu nje ya nchi; ili kuondokana ama kumudu vema zaidi jukumu hili ni vema Serikali ikafanya mojawapo ya yafuatayo aidha:-

- (a) Kiundwe chombo kitakachokuwa na majukumu yatakayofanana na *TBA (Tanzania Buildings Agency)* ili kishughulikie/kisimamie/kiratibu shughuli zote za *real estate* na mengineyo yanayofanana; ama
- (b) Majukumu hayo yapewe *TBA* kwa kufanya maboresho ya sheria ilioanzisha *TBA* au pengine kuanzisha vitengo maalum kwa shughuli hizo.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu kwa kazi nzuri wanayofanya. Nashauri michango tunayopaswa kutoa katika Taasisi za Kimataifa tulijojiunga nayo tujitahidi kulipa mapema kuepuka kudaiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mpaka wetu na Malawi lishughulikiwe mapema sana kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya Bajeti yenyе mwelekeo wa matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kuhusu uteuzi wa Mabalозi wetu katika nchi mbalimbali

pamoja na nchi yetu kuendelea kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa, kazi kubwa tuliyonayo ni kuondoa umaskini mionganoni mwa Watanzania. Hivyo basi, uteuzi wa Mabalozi hawa uzingatie pamoja na mambo mengine elimu (weledi) ya uchumi ya wanaoteuliwa ili waweze kuwavutia wawekezaji hapa nchini na kubuni biashara mbalimbali ambazo zinaweza kufanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, nchi yetu ni lazima iwe na Balozi katika nchi mbalimbali na hususan baadhi ya nchi muhimu kwa Tanzania kidiplomasia na kiuchumi. Hata hivyo, si lazima Tanzania iwe na Balozi katika kila nchi! Pamoja na kwamba Serikali imekwishalionna hilo na kuanza kutekeleza kwa kiasi fulani, kwa kuzingatia mawasiliano ya kisasa, ni vema Balozi zetu zikawa za Kikanda kuliko kuwa na balozi katika kila nchi.

Mheshimiwa Spika, ukifungua Kanda za Balozi, utawafanya Mabalozi wetu na wafanyakazi wao kuwa na kazi za kutosha kuliko hali ilivyo sasa.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Benard Membe kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais kuiongoza tena Wizara hii muhimu, aidha nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri pia. Napongeza Wizara kwa kuiwakilisha nchi vizuri nje za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro wa mpaka baina ya Malawi na Tanzania, naunga mkono hatua ya Serikali ya kuchukua hatua za kidiplomasia na

Mahakama za Kimataifa, lakini kuna umuhimu wa kuimarisha ulinzi mpakani kwa kupeleka Jeshi letu kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupata majibu baada ya mwaka mmoja kupita, ni kwa nini Wizara hii haina majibu juu ya Kampuni ya *General Business and Equipment Supplies* ya Itigi iliyodhulumiwa magari yake na Serikali ya Rwanda.

Mheshimiwa Spika, sina maslahi na Kampuni hii, sijapewa kishawishi chochote kuwatetea, ila ni Kampuni iliyoko Jimboni na inatoa ajira kwa vijana wetu. Tumefungua milango kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini ili kukuza uchumi na kutengeneza ajira, lakini inaonekana wawekezaji wa ndani hawatiliwi maanani pale wanapopata matatizo nje wanaposafirisha bidhaa au malighafi mfano, ni Kampuni hii iliyosafirisha *gypsum* kwenda Rwanda ambako magari yao yakawa *impounded*.

Mheshimiwa Spika, hivi Balozi wetu huko Rwanda anafanya nini? Anatekeleza Diplomasia ya uchumi kweli? Naomba kupata majibu ili kuniepusha na usumbufu wa kudai kuzuia mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na juhudii

zao katika kusimamia na kuzidi kuimarisha mahusiano ya nchi yetu na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa kuimarisha na kuboresha (Balozi) Ofisi zilizoko katika hali mbaya ya majengo na hata kuhakikisha viwanja vyote ambavyo vimenunuliwa kwa ajili ya makazi au ofisi kwani gharama za ujenzi zinaongezeka na hata kupelekea gharama ya pango kuongezeka. Jambo la msingi ni vipi Serikali itakuwa imejipanga kwenye suala hili. Nafurahi kama nitapata majibu ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa hotuba nzuri, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Balozi zetu, wakati huu ambapo tunaendeleza *Economic Diplomacy*, tuimarishe staff na kuweka staff wenyewe uwezo hasa kwenye masuala ya uchumi. Tuweke staff hao kwenye Balozi *strategic* kama *far east-Malaysia ili kuhudumia Asian Countries*. Brazil kwa ajili ya nchi za Latin America; China kwa ajili ya China, Vietnam, Laos na Cambodia.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina *Joint Permanent Commissions* na nchi nyingi na mara nyingi huwa ni *bilateral*, lakini hizi huwa hazikutani kwa mwaka 2012/2013 kupanga *Joint Commissions* tatu tu ndogo. Inaonekana tunakwenda zaidi kwenye *multilateral* na

kusahau *Bilateral*, kwenye *Bilaterals* ndipo ambapo matatizo na mashirikiano ya nchi kwa nchi yanatekelezwa. Kwa mfano, suala la Malawi lingeibuka kama *JPC* ingekuwa inakutana. Najua kuna mradi mkubwa kati yake na Malawi unafadhiliwa Norway wa kuangalia matumizi ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwahimiza *Diaspora* kuwekeza nyumbani, nawapongeza Wizara kwa kuanzisha Idara ya *Diaspora*, Watanzania waliopo Ughaibuni wana biashara na kazi nzuri na wengine wana *influence* kubwa. Hivyo tuwatumie katika kuleta uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, natoa hongera sana kwa ujenzi wa Julius Nyerere *International Center*, ni jengo zuri na limeongeza mandhari ya Dar es Salaam, ushauri ni kwamba, barabara zinazoelekea *JNICC* ziboreshwili kuondokana na msongamano kuelekea *JNICC*. Nashauri kwamba kutafutwe *Management Company* wa kuendesha ukumbi huu. *Management Company* ipewe jukumu la kuza mikutano (*marketing conference and meeting*).

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kuwapongeza sana kwa jitihada zenu, nawapongeza sana wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka kati yetu na Malawi ni suala la haraka na muhimu sana kutafutiwa ufumbuzi wake. Ni kweli suala na utafutaji wa mafuta na gesi kunakofanywa na makampuni ya nje (siyo toka Malawi). Malawi kudai kuwa Ziwa Nyasa ni mali yao kwa mtazamo wangu huo ni msukumo toka Mataifa ya Magharibi. Naishauri Serikali ya Tanzania itafute makampuni ya kutafuta mafuta na gesi toka Urusi na China watafute mafuta kwa upande wa Tanzania, hii itakuwa *solution* kwa wababe hao.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu za nje, Serikali iwe na mkakati wa makusudi kuhakikisha kuwa Balozi zetu zinahudumiwa ipasavyo, vinginevyo kama nchi haiwezi kuzihudumia Balozi zetu sawasawa, basi ni heri kuwa na Balozi chache zenye tija kuliko uitiri wa Balozi *all over the world*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Economic Intelligence*; kuna vitu ambavyo Taifa linapaswa kuliwekea nguvu ni intelijensia ya kiuchumi ili kuachana na umaskini pamoja na rasilimali nyingi tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zote ziwe na wataalam waliobobea katika uchumi na kuweza kugundua fursa za uchumi duniani na Tanzania kunufaika nayo.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Benard Membe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miaka kadhaa iliyopita tumesikia kwamba Balozi zetu za nje hivi sasa zinaendeshwa kwa diplomasia ya uchumi, pamoja na dunia kukabiliwa na mdororo wa uchumi yakiwemo Mataifa makubwa ya Wilaya na Amerika. Je, kuna mafanikio gani yatokanayo na mfumo huo mpya wa diplomasia ya uchumi?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi (Wakristo) wanaofanya safari kwenda Israel kwa masuala ya dini yao, yaani kufanya ziara ya kimaombi wanapata adha kubwa katika ufuatilia *visa* zao Nairobi za kuingia Israel, ni juhudhi gani zimefanyika ili kuwa na Ubalozi wa Israel hapa nchini na hivyo kuwapunguzia usumbufu wale wote wanaofanya safari kwenda Israeli?

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wengi wanaosoma nje ya Tanzania na hasa wale wanaosoma Marekani wanapata shida sana pale wanapohitaji huduma ya Ubalozi wetu ambao uko Washington *DC*, kwa mfano, mwanafunzi akihitaji kwenda Washington na mara nyingine hapatiwi huduma hiyo kwa urahisi. Napendekeza Balozi zetu zitengewe fedha za kutosha na uwekwe utaratibu mzuri wa afisa wa pasi katika Balozi zetu kwa mfano Marekani, awe na ratiba ya kutembelea Majimbo tofauti kwa ratiba atakayoiweka ili aweze kukutana na Watanzania/wanafunzi na kutatua matatizo yao kwa pamoja. Hiyo itaondoa usumbufu unaojitekeza na badala yake hawatakuwa

Watanzania wanaoishi nje ya nchi bila kuwa na pasipoti iliyo hai.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (*A/CC*) kipo katika eneo zuri sana kijiografia kutokana na kwamba Mkoa wa Arusha una vivutio vingi vya utalii zikiwemo mbuga za wanyamapori na hoteli mbalimbali. Kituo hiki kinaweza kutengeneza mapato mengi zaidi ya hayo yaliyopatikana katika mwaka huu uliopita wa fedha. Aidha, Mikutano ya Kimataifa 15 na ya Kitaifa 47 iliyofanyika, bado ni michache sana, kituo kiboreshe matangazo yake, hivyo kuwavutia watu wengi zaidi/vikundi na mikutano mingi zaidi katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi wanazozifanya za ujenzi wa Taifa hili Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yetu ni nchi inayosifika Kimataifa kwa kuwa na amani, utulivu na kuwa na Rais wanaopendana na kuwapenda wageni. Pamoja na sifa lukuki tunazopipata kutoka nchi mbalimbali, bado kuna changamoto zinazotutia aibu kama nchi, changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

Kucheleweshwa kwa fedha za kuendeshea ofisi katika Balozi zetu na kufanya Balozi hizo kuwa ombaomba na kuishi maisha ya shida na yenye kutia aibu.

Mheshimiwa Spika, ni aibu Balozi anayewakilisha Taifa linalosifika duniani kushindwa kulipa ankara za maji, umeme, simu, matibabu, ulinzi na kadhalika. Balozi kushindwa kushiriki mikutano na vikao mbalimbali vyenye tija kwa Taifa letu. Balozi kushindwa kutangaza fursa mbalimbali zilizopo nchini za kibashara na kiuchumi majengo katika baadhi za Balozi zimechakaa na zinavuja na kutia aibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi yaliyoonekana kuwa na upungufu katika Balozi zetu, hii ni aibu kubwa kwa nchi. Serikali ione aibu kwa changamoto zilizopo kwenye Ofisi, Balozi zetu na kuchukua hatua za haraka za marekebisho. Hakuna haja ya kuendelea kujenga majengo ya Wizara mbalimbali ndani ya nchi wakati Balozi zetu nje ya nchi zinatia aibu. Mabalozi hawakuteuliwa kwenda kuteseka nje ya nchi kwa nyadhifa kubwa na mateso kibao.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua kwa nini mpaka sasa nchi yetu haina ubalozi wa Israel kwani nchi hiyo ina historia kubwa na Watanzania wengi wanaokwenda huko kwa ajili ya hija hukosa mambo muhimu pia usumbufu wa kupata *Visa* kwa ajili ya Safari ya hija. Israel huenda wenye dini na wasio na dini kwenda kushuhudia na kujiona makumbusho ya

mambo mbalimbali pia ni Taifa teule la Mungu kwa nini hatuna Ubalozi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:
Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2005, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri aliridhia na kukubali uhamisho wa watumishi wanne ambao ni Ndugu Sumira Ahmed Diria, Ndugu David Mwakanjuki, Ndugu Asha Mkuja Suleiman na Ndugu Abbas Ngwali Juma.

Kuhamishwa kutoka SMZ na kufanya kazi SMT katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Nje (Balozi Ali Shauri Haji) alimwandikia Katibu Mkuu BLM (*Chief Secretary*) juu ya maamuzi hayo na kutaka achukue hatua muafaka. Katibu Mkuu BLM alimwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kumb. Na. UM/40/C1/30 ya tarehe 30/6/2005. Pia Katibu Mkuu BLM aliandika barua Kumb. Na. BLM/40/UM/C1/42 ya tarehe 13/7/2005 kwa Ofisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii ili kupeleka *salary particulars* zao.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu (*DAP*) alimwandikia Dokezo Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje na kupendekeza namna ya

kupangwa kazi. David na Asha walipangiwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Waandamizi. Lakini tarehe 5 Agosti, 2005 wakapokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Kumb. Na. C/DC/299/350/01/27 kwamba wamepokelewa mambo ya nje kwa mpango wa kuazimwa kwa muda wa miaka miwili na miaka miwili ikimalizika watapewa tena miaka miwili, nayo ikimalizika waamue kurejea Zanzibar au kubakia hapo Wizara ya Mambo ya Nje, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa ni miaka saba ndugu hawa wamekosa haki zao zote na fursa zote za utumishi wa umma, hawawezi kupelekwa kufanya kazi Ofisi za Kibalozi hadi hivi leo hakuna aliyechaguliwa wanabaguliwa hata kualikwa kwenye mikutano ya Maafisa Mambo ya Nje, maslahi yao duni sana. Miaka yote waliyofanya kazi SMZ, utumishi wao hautambuliki katika *Foreign Affair*, hawajawahi kupandishwa vyeo wala kupata nyongeza ya mshahara.

Mheshimiwa Spika, baadhi yao wamehusika au kuazimwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, *Customs Union Protocol, Common Market Protocol, Foreign Policy Coordination Protocol, Financial Rules And Regulation 2006*.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mmoja wao ndugu David aliomba nafasi ya Indian Ocean Rim, kimsingi Waziri alikubali lakini Mkurugenzi Kitengo cha Sheria akapandikiza jina lake katika Mkutano wa Mawaziri, lakini jina halikupelekwa.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi katika usafiri wa ndege Tanzania hasa *SA Airline insecticide (Servopak)* Reg. No. L1907, *ACT* 36 ya 1947. *Active ingredient permethrine 209/kg (Avoide excessive inhalation)*. Kwa nini hadi leo ndege ya *SA* inapoondoka Dar es Salaam asubuhi lazima ipulizwe *insecticide* lakini pia ikiondoka Mozambique, lakini *SA* hiyo hiyo ikiondoka Namibia au Botswana haipulizwi dawa, tunaomba sababu kwa nini iwe hivyo ndani ya *SADC*?

Mheshimiwa Spika, Maafisa wa Kibalozi katika Balozi zetu wanafunga biashara kutokana na kutopata mafao yao kwa wakati. Kwa nini Balozi wa Heshima (*Honorary Consul*) anayeishi Mji wa Nice anatoa *Visa* kwa kugonga mihuri badala ya mashine za *Visa Sticker*? Hii inasababisha kutokuwa na takwimu za kutosha na fedha kupotea. Tatizo hilo pia liko Milano kwa Balozi wa heshima na eti sababu zake yeye Ofisi ni ndogo? Kwa nini? Tunaomba majibu.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, baada ya kumalizika vita baridi vya Mataifa makubwa, licha kuwa siasa yetu ya nchi za nje ilikuwa ni kutofungamana na upande wowote lakini bado athari za Mataifa makubwa yaliyotukumba na kwa hivyo Balozi zetu zilikuwa zinafanya kazi kwa misingi ya kambi hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, mabadilko ya vita baridi, inabidi sasa iwepo sera ya diplomasia ya uchumi ambayo ndiyo dira ya Balozi zetu na Wizara kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Waziri ameeleza kwa undani kiasi gani Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inavyotekeleza Diplomasia ya uchumi, uthibitisho wa hilo unapatikana kwanza ukurasa wa 19 mpaka ukurasa wa 29 wa hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuelezwaji, Balozi zetu wenyewe wanaitekeleza vizuri hii sera ya Diplomasia ya uchumi, ni vyema mkapewa mifano hai ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Wizara ukurasa wa 29 amezungumzia umuhimu na juhudi zinazofanywa katika kukikuza Kiswahili, licha ya juhudi ya kufunzwa Kiswahili huko Ethiopia Wizara inashauri vipi katika kutafuta ajira nje ya nchi kwa walimu wa kufundisha somo la Kiswahili, kama hatutakuwa na mkakati maalum wa kuzitafuta ajira hizo, basi nchi jirani watazichukua nafasi hizo wakati Kiswahili hasa asili yake ni Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametoa kauli kuhusiana na mgogoro wa mpaka baina ya Tanzania na Malawi, licha ya maelezo yote yaliyomo kwenye kauli ya Serikali bado suala hilo ninavyoona kuwa Serikali hajakuwa makini kuutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huo unazihusu Wizara mbili, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ndiyo watekelezaji pale ambapo makubaliano yanapokuwa yameafikiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika mpango wao wa kazi za maendeleo kwa mwaka 2012/2013 hawakujipangia kutatua mgogoro huo. Kwa hivyo, hakuna fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo. Hivyo na pia ndio ninaposema kuwa Serikali haikuwa makini katika kutatua mgogoro huo, labda nchi yetu itakuja kusimama kutetea/kutatua mgogoro pale ambapo itapotokezea Malawi kugundua mafuta na ikawa yako upande wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna aina nyingi za utalii, mfano utalii kwenye mbuga, fukwe, malikale na utalii unaotokana na mikutano. Eneo maarufu kwa mikutano hiyo ni Arusha, lakini ziko kambi ambazo zinakidhi mikutano hiyo? Je, A/CC inatosheleza lengo hilo la kuleta mikutano hiyo mikubwa na baada ya mikutano hiyo wahusika wanaweza kufanya utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pamoja na wahusika wengine ipo haja kushawishi Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili upatikane uwekezaji mkubwa kwa ujenzi wa kumbi za mikutano.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu, kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, sina budi kutamka *Alhamdulillah!*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Mambo ya Nje ina umuhimu wa pekee katika nchi, ambao ni kuunganisha ushirikiano mwema baina ya nchi yetu, majirani zetu na hata nchi za ng'ambo ili kuleta ustawi wa nchi wenye neema, maelewano lakini pia udugu ni lazima Wizara hii iwe makini, mahiri na yenye weledi na upeo mkubwa. Nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Bernard Membe, Naibu Waziri Mheshimiwa Mahadhi kwa kuwa na sifa hizo!

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Waziri kueleza katika hotuba yake juu ya upatikanaji wa mikopo kwa sekta ya kilimo, naishauri Serikali kutumia vizuri fedha hizo ili kuinua kilimo nchini na kuboresha hali za maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, soko la *AGOA* kule Marekani limekuwa likzungumzwa sana bila ya kuonekana tija yake hasa kwa Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati akifanya majumuisho alieleze Bunge hili kwa ufasaha fursa hizi ni namna gani Watanzania wataweza kufaidika na soko hilo la *AGOA*, ni njia gani Mtanzania apite ili aweze kusafirisha nguo mpaka Marekani. Ni nguo za aina gani kutoka Tanzania zenye soko huko Marekani na bei ya soko ikoje?

Mheshimiwa Spika, Qatar ni nchi yenye uchumi mzuri na kwa vile inaonesha nia njema ya kutaka ushirikiano na Tanzania mpaka kuhitaji vijana wa kufanya kazi huko. Kwa mantiki hiyo, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kufungua Ubalozi Mjini Doha nchini Qatar? Jambo hilo litaimarisha zaidi

uhusiano wetu na kuwa chachu ya kuongeza kupata fursa za kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu Serikali ya Zanzibar kupitia kwa Waziri wake wa kazi na ajira Mheshimiwa Haroun Suleiman alipiga marufuku upelekaji vijana nchini Qatar. Je, Serikali ya Muungano ina kauli gani juu ya kauli hii/ nikiwa Mbunge kwa wajibu na majukumu yangu ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge nahitaji Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi wa utata wa kauli hizi mbili. Kauli ya SMZ na hii ya SMT aliyoitao Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, ni ipi mantiki ya kutokuwa na uhusiano na nchi ya Morocco kwa nchi hiyo kuwa na mivutano ya kimaslahi na nchi ya Sahara Magharibi? Sisi kama nchi huru tuangalie maslahi yetu ya ushirikiano na nchi za nje bila kuangalia mambo yao ya ndani. Zanzibar iliachiwa ikafanya *referendum* ilipotaka kuunda Serikali ya umoja wa Kitaifa. Naishauri Serikali kuanzisha uhusiano na Morocco kwani Morocco ni nchi yenye fursa nyingi, uchumi imara na ustaarabu mkubwa. Kwa nini tuna uhusiano na Israel hali ya kuwa nchi ya Israel inainyanyasa na kudhulumu Palestina?

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Tanzania na Malawi kadri vizazi vinavyokuja, hali ya kuvumiliana inapungua kwa kasi ya ajabu mionganoni mwao! Nashindwa kuelewa sababu ya jambo hili! Baada ya kutafiti kwa muda mrefu kidogo sababu za tatizo hili nimegundua kuwa linasababishwa na elimu ya

computer na utandawazi. Hali hii inapelekea kila mmoja kujiona ni mkubwa kama au kuliko mwenzake! Kwa mantiki hiyo basi, naishauri Serikali ilitatue tatizo la mpaka wa Tanzania na Malawi wakati bado tunao viongozi wengi wastaaafu. Hekima na busara zao zitumike haraka kumaliza tatizo la mpaka wetu na Malawi kuepuka maafa muda mfupi ujao!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu wake na watendaji wengine wote wa Wizara kwa jitihada zao katika kutekeleza sera ya CCM ya Mambo ya Nje. Nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tufungue Ubalozi Cuba, pamoja na kufahamu kwamba tuna tatizo la rasilimali, zipo nchi rafiki kama Cuba ambazo manufaa ya Ubalozi yatakuwa makubwa, sisi katika CCM tuna mahusiano mazuri na Chama cha Kikomunisti cha Cuba na tungependa Serikali ikawa na Ubalozi pale ukizingatia pia umbali wa uwakilishi wetu pale kutokea Canada.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu ndio taswira ya nchi yetu huko nje, taarifa za ukosefu wa fedha, uchakavu wa magari, vifaa na majengo zinasikitisha. Ni dhahiri kwamba Mabalozi na watumishi wanadhalilika na hivyo nchi yetu pia inadhalilika. Si sahihi kuwa na Balozi nyingi, lakini zote zikawa na ufanisi mdogo kutokana na ukosefu wa rasilimali, kama tunashindwa kuendesha

hizi Balozi tuzifunge tubakie na chache tunazoweza kuziendesha kwa ufanisi. Hali ya sasa ambapo kila mtu analalamika, Balozi analalamika, Maafisa wanalamika, Wizara inailalamikia Hazina, Wabunge nao wanalamika, haipaswi kuendelea. Maamuzi magumu yafanywe kama hali hii haiwezi kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipeleke Afisa wa masuala ya uchumi kwenye Ubalozi wetu wa Beijing CCM na Chama cha Kikomunist cha China tumeamua kwamba nchi zetu zitumie urafiki wa kihistoria wa nchi zetu na vyama yetu kuimarisha mahusiano ya kiuchumi. Haieleweki kabisa, kutokana na umuhimu wa nchi kama ya China na kutokana na maelewano yetu kwamba leo hakuna Afisa wa Uchumi, Ubalozi wa Beijing.

Mheshimiwa Spika, masuala ya hati za utambulisho kukosewa mara kwa mara au baadhi kukosekana, ni *embarrassment*. Ili kuilinda heshima ya Rais wetu, nchi yetu na Serikali yetu, kuwepo na umakini mkubwa kwenye suala hili kwani pia tumeona suala hili limechelewesha uwasilishaji wa hati hizi katika nchi kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina uongozi na watendaji mahiri na wenyе *commitment* kubwa kwa maendeleo na ustawi wa Diplomasia iliyobobea. Hata hivyo, jitihada za Wizara bado hazifahamiki sana kwa Watanzania wa kawaida, vile vile ule utaratibu wa mihadhara ya wazi kuhusu *issues* zinazoendelea duniani na kwenye kanda, urudishwe na Wizara iratibu

mihadhara hiyo ili kuleta chachu ya fikra kwenye namna ya kuendeleza diplomasia yetu.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za Rada, Serikali ichukue hatua dhidi ya watu wote waliohusika kwenye ununuzi wa rada, kwani kurudishwa kwa fedha ni jambo moja na kuchukua hatua dhidi ya watuhumiwa ni jambo la pili. Naomba kupewa majibu waliosababisha ununuzi na akina nani na wamechukuliwa hatua gani.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu kuhusu ujisadi wa fedha nje ya nchi, kwa nini Serikali haiwataji watu wanaotajwa kwa kuficha billioni 315 nchini Uswizi, kama Serikali haifahamu watu hawa Idara ya Usalama wa Taifa inafanya kazi gani? Je, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Mambo ya Nje na kadhalika zinafanya kazi gani na kwa nini fedha za nje ziliibiwa na kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuifahamisha Serikali kuhusu uhusiano wa Kibondo, Kigoma, Burundi, Rwanda na Kongo kwamba mpaka sasa bado kuna ujambazi unaofanyika na watu wanaosadikika kutoka nchi za Burundi, Rwanda na Kongo. Pia kumekuwa na mifugo mingi kutoka Rwanda Wilayani Kibondo na maeneo ya Kagera. Je, Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali juu ya kuendelea kutumia lugha ya Kiswahili

kwenye mikutano ya Afrika na Kimataifa, pia iweke wazi fursa ambazo Watanzania wanaweza kuzipata kupitia lugha ya Kiswahili, mfano ajira za kufundisha Kiswahili na kadhalika ili kila Mtanzania afahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Pamoja na kuunga mkono bajeti hii naishauri Serikali na Wizara kuhakikisha kwamba fedha zote zinazopangwa katika bajeti ya Serikali ziwe zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba, Wizara inapangiwa fedha kidogo wakati Wizara inayo majukumu makubwa katika kuliwakilisha Taifa letu huko nje ya nchi. Inashangaza kuona kwamba watumishi walioko nje ya nchi ambao wanaishi ugenini wanacheleweshewa maslahi yao hasa stahiki ya msingi ya mishahara kwa watumishi wa umma kutakiwa kupata mishahara yao kutokana na maduhuli yanayokusanywa Ubalozini. Jambo hili halikubaliki, hivyo ni vema mishahara pamoja na *foreign service allowance* ni vema zikapelekwa na Serikali yenewe badala ya ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, *foreign services allowances* zinazolipwa kwa sasa zimepitwa na wakati, hivyo ni vema *foreign services allowance regulations* ni vema zikapitiwa upya ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, watumishi katika Balozi zetu wanapata wakati mgumu kulipia huduma mbalimbali kutokana na kucheleweshewa fedha zao na vile vile kiasi cha fedha zao kinachotolewa hakiendani na wakati tulionao.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika sehemu mbalimbali duniani, ni vema Serikali ikajipanga na kutenga fedha mahsus kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa majengo katika Balozi zetu. Hali hii italijengea heshima Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni vema mgogoro baina ya nchi yetu upewe kipaumbele ili kumaliza sintofahamu iliyopo kwa sasa ambapo nchi ya Malawi inadai kulimiliki Ziwa Nyasa kwa asilimia mia moja. Naipongeza Serikali kwa kutoa msimamo kwamba mpaka wa Tanzania katika Ziwa Nyasa unapitia katikati ya Ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Diplomasia ya uchumi, pamoja na kuitangaza nchi yetu ulimwenguni ni jukumu linalohitaji uwepo wa rasilimali fedha. Hata hivyo, upo upungufu mkubwa kutokana na fedha kidogo sana kwa sekta hii. Hivyo, naishauri Serikali kuibadili hali hiyo na kuwekeza katika Diplomasia ya uchumi ikiwemo kuitangaza nchi yetu kuwa ni kivutio cha utalii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ishughulikie uwepo wa Balozi Heshima Hamburg Ujeruman baada ya aliyekuwepo kufariki. Ushiriki wa Serikali uwekwe wazi katika matengenezo ya meli ya *M.V. Liemba* kwa vile

nchi ya Ujerumani kupitia Jimbo la *Lower Saxony* wako tayari kuchangia matengenezo ya nchi hiyo hasa katika kipindi hiki ambapo mwaka kesho nchi hiyo itafikisha umri wa miaka mia. Tutumie mwanya huu kuifanyia matengenezo meli hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikaweka kipaumbele katika kuwekeza katika majengo na kununua magari kwa ajili ya watumishi wake katika Balozi nje ya nchi. Hati za utambulisho kwa Balozi mbalimbali nchini kuna upungufu wa kiutendaji, ni vema Serikali ikaufanya kazi upungufu huu, kwa mfano, hati za Balozi wetu aliyepo Sweden kumtambulisha nchini Finland na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuishauri Serikali iongeze fedha hasa kwa ajili ya maendeleo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunatumia fedha nydingi sana kama Taifa kuwezesha kuendesha Ofisi za Balozi kwenye nchi mbalimbali nje na duniani. Naiomba Serikali itueleze Tanzania inanufaikaje na uwepo wa Balozi zetu nje katika suala la utafutaji wa masoko kwa mazao ya biashara tunayozalisha kwa wingi, lakini hatuna soko la uhakika mfano, la tumbaku, pamba, *cocoa* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye Balozi zetu kuna wataalam wa fani mbalimbali, Serikali inatumiaje wataalam hao walioko nje kufanya uchaguzi wa Kampuni mbalimbali zinazokuja kuwekeza miradi mbalimbali kabla hazijapewa mikataba ya uwekezaji ili kuepuka makampuni ya kitapeli mfano *IPTL* kuja kuwekeza na matokeo yake kuingizia Taifa hasara kubwa?

Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani hasa vinafuatwa katika kuteua hawa Mabalozi ambao ni wawakilishi wa nchi nje ya Taifa? Wakati wa kuteuliwa tunaangalia fani zao walizo nazo na uwezo wao walionao kama chachu ya kusaidia majadiliano na kujenga hofu ya kuibua hoja zinazolenga kuondoa au kupambana na matatizo au umaskini wa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, wapo Mabalozi wameteuliwa na kupewa nafasi kama za wazi, tumeona huko nje hawana uwezo wa kufikiri umeshapungua kabisa. Je, kwa nini Serikali inatumia fedha za walipa kodi kulipa Mabalozi/kugharamia Balozi zilizoweza kunufaisha Taifa hili kwa namna yoyote?

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuwakilishwa na watu makini wenye uwezo mkubwa, taaluma nzuri na uzoefu wa kutosha wa *International Relation* ili waweze kutumia taaluma zao na uzoefu walionao kusaidia Taifa letu, sio kwenda kutembea na kusubiri viongozi watembee huko wawapokee.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuchelewesha posho na mishahara ya Mabalozi na

watendaji kwenye Balozi mbalimbali ni aibu kubwa sana kwa Taifa na pia inawadhalilisha Watanzania hao wanaofanya kazi kwenye Balozi zetu. Tulikwenda South Africa Juni, 2012, Balozi alikuwa hajapata mshahara kwa muda wa miezi miwili! Wanaishije huko?

Mheshimiwa Spika, sio lazima kuwa na Balozi nyingi ambazo hazina faida kwetu na hatuwezi kuzihudumia kikamilifu. Serikali ikae chini itafakari na kuthamini Balozi zetu tulizo nazo, tupange kuwa na Balozi chache ambazo tunanufaika nazo, pia tuna uwezo wa kuhudumia vizuri kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zimefanywa na vyombo mbalimbali na kugundua wizi mkubwa wa fedha za Watanzania unaofanywa na wafanyabiashara wakubwa na watendaji/viongozi wa Serikali. Fedha nyingine zimewekwa kwenye akaunti za nje ya nchi katika maeneo mbalimbali (Serikali haijakanusha).

Mheshimiwa Spika, Serikali ni kwa nini kupitia Wizara hii haijatoa tamko/kauli yoyote kuhusu wizi huu? Watanzania tueleweje kuhusu ukimya wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Serikali itueleze suala la kupatia Uraia Watanzania walioko nje ya nchi wana uraia wa nchi za nje? Majadiliano yanaendelea na yamefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwe makini sana sana kwenye suala hili muhimu sana, tunajua wapo Watanzania wameishi nje muda mrefu,

wameoa, wameolewa wengine wanataka uraia Tanzania kwa nia njema waweze kuchangia maendeleo ya asili yao, lakini wapo wanaotaka/wanatafuta uraia kwa sababu zao, ili waje kwa uhuru wavune mali hizo (shamba la bibi) waende zao.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, nomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa utendaji kazi mzuri na kuisaidia Tanzania kuondokana na migogoro duniani. Naunga mkono hoja na kuchangia baadhi ya sehemu ili kuboresha Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jengo la Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje, Zanzibar kwa kweli jengo ni kongwe na halina hadhi ya kuwa jengo la Afisa, jengo lilikuwa nyumba ya makazi tokea wakati wa ukoloni na tayari limechakaa, ingawa sasa limo katika ukarabati wa kuta na paa na kupaka rangi kwa kutumia Sh. 50,000,000/= lakini siyo kwamba tatizo litaondoka. Tutaweza kuondoa tatizo baada ya kuchukua hatua ya kujenga jengo la ofisi ya Mambo ya Nje, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi za Muungano Zanzibar sasa ni jambo la kawaida, kwani Ofisi ya Makamu wa Rais imejenga Ofisi, Tunguu, Ofisi ya Mambo ya Ndani imejengwa Kilimani Zanzibar, Ofisi ya Wizara ya Ulinzi imejengwa Mazizini na Ofisi ya Bunge, Tunguu na kadhalika. Naomba ofisi yako nayo itafute mifano ya Ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi kwa Zanzibar unahitaji msukumo wa Wizara yako, kwani hali ya Ofisi, vitendea kazi na wafanyakazi bado mtihani, kwani kuna idara tatu ambazo ni *Protocol*, Siasa na Uchumi na Utawala. Vitengo vyote hivyo havijitoshelezi kikazi, wafanyakazi finyu, hawana gari, hivi sasa kuna gari mbili tu ya Mkurugenzi na sasa amestaafu na ile ya Ofisi kwa ujumla ambayo ni moja.

Mheshimiwa Spika, vile vile uongozi wa Ofisi wa juu wote upo Tanzania Bara na wala hawana hamu ya kutembelea Zanzibar kwa kupata matatizo ya Zanzibar. Katika miaka ya 1990, Balozi Mtango ambaye alikuwa Katibu Mkuu hapo yeye ndiye alikuwa akitembelea Zanzibar na kujua matatizo ya wafanyakazi wa Zanzibar, ningeliomba Wizara angalau kupanga ratiba ya kutembelea Zanzibar viongozi wa Ofisi, Katibu Mkuu, *DAP* na baadhi ya Maafisa ili kujua kero za kazi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Zanzibar haina gari ya viongozi wa Kimataifa, Mabalozi wa nchi za nje wanapoingia Zanzibar kuonana na viongozi wa Kitaifa waliopo Zanzibar, lakini Wizarani Tanzania Bara gari za aina hiyo zipo kama mabasi na kadhalika. Hivyo, naomba Ofisi ya Zanzibar wapatiwe angalau basi moja na gari ili zikae *pool* ya magari.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iliangalie hilo, ili kuondosha tatizo la kuazima gari SMZ na wao pia hawana inabidi kuazima gari za Maafisa wa Wizarani, vile vile kutoa gari za kukodi na hivyo kufanya watu

kupata asilimia 10 ya kukodi gari na kukaribisha rushwa. Naomba Wizara kuliangalia kwa upeo mzuri ombi hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje, ni Wizara ambayo inaonesha kioo cha nchi katika shughuli za nchi iliyohusika na kwa kuwa Wizara hii ina changamoto nyingi za Mabalozi katika utendaji wao wa kazi, hufanya wafanyakazi kuwa katika hali ngumu pamoja na familia zao na hata huwa ni tatizo katika kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, fedha wanayopangiwa ni ndogo na pili hata hiyo ndogo Hazina huwa hawaitimizi. Ni vyema Hazina kupeleka fedha hizi hasa ilivyokuwa hizi Balozi zetu zipo nje ya nchi na huwa wana majukumu mengi ya kutekeleza, ni aibu kwa Ofisi hizi kuona wanashindwa kulipa pango za ofisi au majengo wanayoishi wafanyakazi kwa sababu mishahara yao hawapati kwa wakati. Majengo nayo mengine huwa ni mabovu na hawana njia ya kuzijenga.

Mheshimiwa Spika, kuna viwanja na majengo ambayo miaka mingi hivi sasa hakujajengwa na majengo hayo hayakukarabatiwa na viwanja hivyo au nyumba hizo tulipewa bure na Serikali za huko, kama Uingereza, Marekani na pia nyumba hizo kuwa ni maficho ya watu wabaya. Namwomba Waziri anapokuja kufanya majumuisho aje na kueleza

viwanja hivi na majengo haya yapo katika hali gani na lini watajenga?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa Urani, ni jambo la faraja kupeleka wanafunzi/wataalam katika mafunzo. Lakini hivi sasa wachimbaji wadogo wamekwishaanza kuchimba na kutokana na kutokuwa na elimu hiyo ya uchimbaji imeanza kuwadhuru. Ingekuwa jambo la busara kwa hivi sasa kutoa elimu kwa hawa wachimbaji wadogo, la sivyo tutaweza kupoteza watu wengi sana hadi hapo mtakapokuwa tayari kwa wataalam kurudi nyumbani kwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, moja katika tatizo la Tanzania kwa vijana wetu ambao ni asilimia 60. Hili ni jambo la faraja kwa wakati wowote ule kuanzia sasa, kutakuwa na ujumbe kutoka Qatar kwa kusaini mkataba ili vijana wetu wapate kazi nchini huko na hasa mlivyokuwa mmeshamaliza mchakato wa makubaliano na mamlaka husika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kubwa sasa ni kwa Mheshimiwa Waziri kutambua namna gani nafasi hizi za vijana kupata kazi zitagawiwa. Kwa upande wa Zanzibar ni nafasi ngapi na Bara ni ngapi na *criteria* gani mtachukua kwa kuwatambua na kuwapa kazi hiyo. Namwomba Waziri atakapokuja kuwasilisha atueleze Bunge hili mgao huo wa vijana wetu kwa nchi zote mbili, kwani mipango na mikakati mmeshaiweka.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Elimu, kuna suala la *change* ya rada ambayo imekabidhiwa katika Wizara ya Elimu yenye jumla ya shilingi bilioni 90

ambayo mpaka sasa haijulikani inakasimiwa vipi kwa kila upande wa nchi mbili hizi Tanganyika na Zanzibar na kwa kutokana na maneno ya hapa na pale inasemekana Zanzibar haitapata mgao huu. Sasa namuuliza Waziri kwa nini wakati suala la rada ni la mawasiliano na mawasiliano ni suala la Muungano? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, ufundishaji wa suala la lugha ya Kiswahili ni muhimu sana na hata katika kutoa mafunzo kwani ikiwa Tanzania hatujakazania lugha yetu, haitokuja juu. Zanzibar kuna Kituo, ni vyema Wizara yako ikashirikiana na Serikali ya Zanzibar kuona jinsi gani mtaweza kupeleka Watanzania kwenda kufundisha katika nchi mbalimbali ili kueneza lugha hii.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni wakati muafaka wa kufungua Balozi ndogo katika nchi za nje, hasa ilivyokuwa tunawapeleka vijana wetu kwenda kusoma katika nchi mbalimbali. Vijana wetu hupata shida hasa wanapokabiliwa na matatizo na wakati huo huo, balozi zipi mbali na wao mfano kijana anaweza kuwa kafa au anaumwa, fedha wanazopelekewa na Bodi ya mikopo hazikufika, huwa katika mashaka hasa kwa watoto wa kike, wanaweza kufanya mambo yasiyostahili na kulitia Taifa katika matatizo na aibu. Hili linaweza kufanyika kwa sababu fedha hiyo inakawia kufika. Mfano, wanafunzi waliopo Algeria inabidi wasafiri kwenda Tunisia au wanafunzi wa China wanahitajika kwenda Beijing na kama unavyoelewa China na ukubwa wake.

Pili Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa Mabalozi kwa nchi yetu bado ni wa kukandamizana, kati ya Mabalozi waliotoka Bara na wale wa Zanzibar, kuna tofauti kubwa. Naomba kuuliza, je, Zanzibar hakuna wasomi? Kwa nini mnaidharau? Namwomba Waziri atakapokuja kuwasilisha atueleze idadi kuu ya Mabalozi pamoja na mgawanyo wao kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Waziri, watumishi wako ni 430, 163 wapo kwenye Balozi zetu za nje, kati ya hawa163 ni wangapi kutoka Bara na wangapi kutoka Zanzibar. Kwa uono wangu wafanyakazi kutoka Bara watakuwa wengi sana, je, kwa nini iwe hivi? Mheshimiwa Waziri haoni kwamba analeta mkandamizo kwa upande mmoja? Ndio hapa inapokuja Wazanzibari kuona kwamba kero za Muungano hazitambuliwi. Waziri naomba utupe picha hii ili kuondoa utata huu na mtajipangaje kuondoa matatizo haya?

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, Tanzania imechukuliwa kama mmiliki wa lugha ya Kiswahili, hii ni nafasi pekee kwa Taifa letu ambapo mikakati thabiti ikiwekwa, tunaweza kujipatia mapato ya kutosha na pia kuendelea kuitangaza nchi yetu, mapato yanaweza kutokana na wataalam wetu wa Kiswahili kuweka mikakati ya kufundisha wageni wanaotembelea nchi yetu. Pia kuitangaza lugha hii kama ambavyo matangazo ya mbuga za wanyama yanavyofanyika. Wizara hii inaweza kushirikiana na Vyuo vya elimu ya juu mfano *UDOM*, *UDSM* na kadhalika katika kulifanyia kazi hili.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Kikanda kama *EAC*, *SADC*, *COMMESA* na kadhalika ni hatua muhimu ya kufikia umoja wa Afrika. Tanzania ni mwanachama wa *EAC* na *SADC* wakati huo huo nchi nyingine kama Kenya na Uganda ni wanachama wa *COMESA*. Nafikiri hapa kuna Mkanganyiko fulani ambapo nchi zilizo katika ukanda mmoja zinakuwa katika Jumuiya tofauti tofauti. Mkanganyiko unaweza kutokea pale ambapo nchi mojawapo inaweza kushindwa kuweka mizania sawa kati ya jumuiya mbili ambayo ni mwanachama. Ni vizuri jambo hili likaangaliwa kwa undani.

Mheshimiwa Spika, tumesikia hivi karibuni na bahati nzuri tumejulishwa na Serikali juu ya Malawi kutaka kuchukua eneo la Ziwa Nyasa. Najua Serikali imejipanga vizuri kulikabili hili, nashauri Serikali na wadau wote kuwa makini na mipaka yetu, si tu eneo tajwa bali na maeneo mengine yote. Tukio hili litupe mafunzo ya kwamba wakati wote tuwe macho kwani huenda kuna njama za kisirisiri za kuihujumu mipaka yetu. Waswahili husema mdharau mwiba, mguu huota tende, naomba tusikae tukajisahau au kudharau tukio lolote hata kama ni dogo kiasi gani, mipaka yetu iwe salama wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuishauri Wizara hii muhimu sana katika nyanja za Kimataifa isaidie katika kuwapata wafanyabiashara na wawekezaji waadilifu. Hii itasaidia kupunguza idadi ya watu wasio na uadilifu kuja kuchuma mali/rasilimali zetu kiulaini, jambo hili linaweza kufanyika kupitia Balozi zetu zilizopo katika nchi husika. Naamini tunaweza

kuinufaisha nchi yetu Kimataifa na Jimbo langu la Kibaha vijijini nalo litakuwa limenufaika.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bernard Membe kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika kusimamia utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali ya nchi juu ya mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa. Nimpongeze pia Mheshimiwa Mahadhi Maalim Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitambue mchango mkubwa sana uliotolewa na unaoendelea kutolewa na Wizara hii ya mambo ya nje katika kuendelea kuifanya nchi yetu kuwa na sauti na heshima kubwa katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Tanzania inaheshimika na kupata sifa kubwa katika masuala ya diplomasia si tu barani Afrika ila ulimwenguni kwa ujumla. Hii yote ni kutokana pia na uongozi mzuri na mahiri wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ambaye binafsi anaheshimika sana katika anga za Kimataifa na hivyo ameweza kuteuliwa kushiriki katika Tume, nafasi kadhaa za Kimataifa kama Kamisheni ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Denmark mwaka 2008, *Commission of Information and Accountability for Women's and Children's Health*.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika pia na hali ya Tanzania na uongozi wa Afrika, jitihada kubwa sana

zilizofanywa na Tanzania (Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Membe) katika kuhakikisha kuwa mwanamama Nkosazana Dlamini-Zuma anachaguliwa na Wakuu wa nchi na Serikali na Umoja wa Afrika kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Afrika. Ushindi wa mama Zuma katika kuongoza chombo hiki muhimu barani Afrika si tu kwamba ni ushindi kwa nchi za SADC bali ni ushindi kwa wanawake wote wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Mheshimiwa Spika, hivyo, nitoe rai kwa Wizara kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa kinara wa kuunga mkono wagombea wanawake wenyewe uwezo watakaogombea/kusimama kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika vyombo vya Kimataifa wanaopendekezwa na nchi mbalimbali za Afrika. Heshima ya Mheshimiwa Rais katika kuchochaea usawa wa jinsia na haki za wanawake Duniani ni kubwa sana hivyo tumsaidie aendelee kuheshimika.

Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi wa Wakuu Idara/Mabalozi wanawake; nipongeze jitihada kubwa zilizofanywa na Waziri wa Mambo ya Nje katika kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za juu za uongozi katika Wizara yake. Jitihada zake zimewezesha uteuzi wa Mheshimiwa Rais wa Wakurugenzi wapya wanne kati ya tisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hali hii itachochaea kasi ya nchi kufikia lengo la tatu la Millenia juu ya usawa wa jinsia na haki za wanawake. Ni matumaini yangu kuwa wakuu hawa wa Idara/Wakurugenzi wanawake

watakeleza majukumu yao kwa ufanisi na umahiri mkubwa na hivyo kudhihirisha kuwa uteuzi wao ni kutokana na uwezo na sifa zao na si kuwa wamependelewa. Pia ni matumaini yangu kuwa wanamama hawa watapewa ushirikiano mzuri na viongozi/wafanyakazi wa Wizara.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu bwana wa viumbe vyote. Pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuifanya nchi yetu iwe na heshima kubwa Kimataifa. Ni dhahiri kuwa Wizara hii inafanya kazi katika mazingira magumu kidogo kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini wameifanya nchi yetu iwe na hadhi kubwa sana duniani ingawa ni maskini.

Mheshimiwa Spika, tofauti na miaka ya nyuma, ni mara ya kwanza nimeona katika kitabu hiki cha bajeti Wizara hii imechangia mchango wa moja kwa moja katika mpango wa Taifa wa miaka mitano tulioipitisha na ambao nchi yetu inautekeleza. Tumeona namna Wizara hii inavyochangia katika Sekta ya Maji, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Miundombinu na Sekta ya Elimu japo kwa uchache wake. Kwa mafanikio machache waliyoyaonesha kama kusaidia kupatikana kwa mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam kunanipa ushawishi wa kuunga mkono Wizara hii kuangaliwa kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, nami nashawishika kuwa, ikiwa tuna dhamira ya kweli ya kutekeleza mpango wetu wa miaka mitano hatuwezi kukwepa kuwekeza katika

Wizara hii. Nchi yetu ina fursa nyingi za kupanua uchumi wetu ambazo ziko nje ya nchi yetu. Masoko yako nje, mikopo ya masharti nafuu ya uendeshaji wa miundombinu iko nje, teknolojia na mitaji kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda navyo viko nje. Hatuwezi kufika huko nje ila Wizara hii ambayo inashikilia funguo huko nje.

Mheshimiwa Spika, ningefurahi sana na wananchi wangefurahi sana kusikia hapa Bungeni kuwa bidhaa tunazozalisha hapa nchini zimepatiwa masoko, lakini najua nitajibiwa kuwa hilo halikufanyika kutokana na ufinyu wa Bajeti. Kila ninaloligusa Mheshimiwa Waziri ataniambia kuwa nia anayo lakini fedha hana. Sina mashaka na uwezo, dhamira na uthubutu wa Mheshimiwa Waziri, tumeona hapa aliahidi fedha za chenji yetu ya rada itarudi na imerudi yote mchana peupe, sasa watoto wetu wanasoma vitabu bila ya wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, ila kinachonisikitisha ni sisi Wazanzibari kufanywa watoto wa kambo na hatukupewa mgao wa fedha hizi nasi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nadhani hatutendi sawa, tuweke fedha pale tunapoweza kupata fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, naamini Wizara hii inaweza kuwa na mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Lakini pia Wizara hii wakipewa fedha za kutosha kama tunavyotoa kwenye Wizara nyingine tunaweza kudai matunda yake, maana hapa nashindwa hata kumbana Waziri

zaidi ya kumhurumia, kumpongeza na kumtia moyo. Wasichoke wala wasikatishwe tamaa na mazingira ya ukata.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii na niwapongeze Mawaziri na watendaji wote Wizarani. Hata hivyo, naomba Wizara izingatie Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje iliyoko Zanzibar ina hali mbaya, jengo limechakaa na kwa kweli hata pale anapokaa (ofisi) ya Naibu Mkurugenzi haipewi heshima inayostahili. Kimekaa kama kibanda au *kiosk* cha kuuzia chipsi na nyama choma.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara kwa makusudi itafute fedha ama ijenge jengo lingine au ifanyie ukarabati mkubwa Ofisi hiyo badala ya kuimarisha bustani nje, wakati ndani vyoo vinauju, samani ndiyo hazisemeki na vitendea kazi vimechakaa.

Mheshimiwa Spika, katika suala la wafanyakazi Wizara haitoi uwiano halisi wa wafanyakazi katika ajira. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho naomba atueleze ni Wazanzibari wangapi hivi sasa ni Mabalozi? Wizara ina Balozi (ofisi) ngapi hivi sasa duniani na kati ya hizo ni zippi zinazoongozwa na Watanzania na Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la usalama kwa ujumla wake, naipongeza Tanzania ilivyojipanga na inavyojenga heshima yake Kimataifa, lakini inajitayarisha vipi na suala la Kiintelijensia kuhusu ugaidi? Tuko salama kiasi gani na nchi zinazotuzunguka?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuna vijana wa Zanzibar waliokuwa Somalia kwa muda usiopungua miaka 10 na wamerejea nyumbani. Je, hawa mnawaunganisha vipi na walikotoka, wakifanya nini huko. Wamerudi wako wapi? Bila ya kusahau ugaidi unaojipenyeza kwa jina la UAMSHO?

Mheshimiwa Spika, kuna Al-shabab, Somalia wako mwambao wa Kenya, Tanga na Zanzibar na si hilo tu Tanzania tumeshaonja dhiki zao hao, tulilipuliwa Ubalozi wa Marekani hapa, jamii na Watanzania wako waliopoteza mali zao, jamaa zao, vifo na kadhalika. Tumejipangaje?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni tajiri sana kimaliasili kama sikosei ni nchi ya pili barani Afrika ikitanguliwa na Congo, tunaona machafuko yaliyoko Congo na kutokuwa na utulivu, unaosababishwa na utajiri wao wa kuchochewa na nchi za magharibi. Nchi za magharibi sasa zinaelemewa na tatizo la uchumi na ukosefu wa rasilimali, wanajipanga kuja Afrika na yaelekea Tanzania ni moja ya *target* zao. Kama hili halitoshi, hata nchi za Kiarabu hazo tunaziona zinavyoteseka na kuteswa kwa sababu ya utajiri wa mafuta waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, nini tunafanya? Je, hali hii tutaweza kuepuka na Wizara imejipangaje katika uwekezaji wa viwanda nchini badala ya kutegemea utalii na mitumba kuingia kutoka nje. Je, Wizara imejipangaje kuleta teknolojia rahisi kwa kushirikiana na nchi za BRICS kwa kuungana nao ili waje kuwekeza

kikweli badala ya kutegemea nchi za magharibi ambazo uchumi wao sasa unatetereka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba bajeti ya Wizara hii iongezwe ili iepukane na fedha za kutolipwa ada stahiki kwa Taasisi za Kimataifa na hivyo kupoteza heshima na haiba ya Kimataifa.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam kwa kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu ya bajeti ndogo:-

Kwanza, kazi ya kwanza nzuri inayofanywa na Wizara kupita Balozi zake ni kuendelea kushiriki katika kuwatafuta na kuwahamasisha wawekezaji wa kigeni katika sekta mbalimbali za kiuchumi kama miundombinu, sekta ya maji, sekta ya kilimo, sekta ya nishati na madini na kadhalika. Hata hivyo, bado Balozi zetu hazijaimarishwa ipasavyo katika kuwa na wataalam waliobobea katika fani za kiuchumi na biashara kwa ajili ya kufanya majadiliano (*negotiations*) na wataalam au wawekezaji katika nchi waliyopo. Kwa maana nyingine Balozi zetu haziko *wellstaffed* katika utekekezaji wa sera ya *Economic Diplomacy*.

Pili, bado tuna ujumbe mkubwa au msafara mkubwa wa wataalam kutoka nchini kwenda kwenye *negotiations* huko ulaya wakati tuna Balozi zetu zinazotakiwa kufanya kazi hiyo ya *negotiations*. Hii ni gharama kubwa kwa Serikali. Misafara hii sharti ipunguzwe kwa kuimarisha Balozi zetu kitaaluma.

Tatu, jambo lingine zuri ambalo limefanywa na Wizara ni kuanzisha Idara ya *Diaspora*, siyo vibaya kujifunza kutoka kwa wenzetu wa Rwanda ambapo kila mwaka au miaka miwili Wanyarwanda ambao wako katika *Diaspora* wanakuja Kigali kwenye mkutano na Raisi kuzungumzia jinsi wanavyoweza kushiriki katika uwekezaji ndani ya nchi. Sina hakika kama Balozi zote na hasa za Ulaya na Marekani zinakuwa na vikao na Watanzania wanaoishi huko kuwaeleza kuhusu fursa za kiuchumi katika nchi yetu na pia kuzungumzia umuhimu wa *Remittance* za fedha zao.

Nne, pia siyo vibaya kwa Balozi kuwahamasisha Watanzania wenyewe taaluma adimu kurudi nyumbani kufanya kazi Tanzania au kurudi kama washauri.

tano, nimetembelea Ubalozi wetu wa Ufaransa mara mbili na wakati wote sikufurahia kuona Ubalozi wetu unaendelea kupanga katika jengo la Uganda. Ni muhimu kuwa Serikali yetu kupata jengo letu wenyewe kwa ajili ya Ofisi zetu za Ubalozi. Ni aibu sana sisi kuendelea kupanga katika Ofisi za Uganda.

Sita, jengo la Ubalozi wetu wa Msumbiji, nafahamu kwamba, kwa muda mrefu Wizara hii imekuwa na bajeti finyu, lakini ni aibu kubwa kwa Tanzania kuona jengo kubwa la Ubalozi wetu wa Msumbiji ambalo tulipewa bure na Hayati Rais Samora Machel linaendelea kuwa katika hali ya uchakavu mkubwa na kwa miaka mingi. Kwa nini jengo hili halikarabatiwi na

kupigwa rangi? Miaka sita iliyopita nilitembelea Ubalozi huu nikasikitika sana kuona hali mbaya ya jengo hili na mpaka sasa jengo hili halijafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, hali ya watumishi katika Balozi zetu ni mbaya sana kutokana na bajeti finyu na Wizara hii kutopewa kipaumbele. Balozi zote nilizozitembelea niliwaona watumishi wakiwa katika hali duni, *miserable*. Balozi zetu zinatoa picha mbaya kwa wenzetu. Serikali haina budi kubadilisha *attitude* yake kwa Balozi zetu.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri Bernard Membe pamoja na Naibu wake Mahadhi Juma Maalim kwa kazi kubwa ya kuendeleza Wizara hii. Pia napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu J. Haule pamoja na timu yake ya Wizara hii. Kwa namna ya pekee, nawapongeza Balozi S. Mushi pamoja na Balozi Kairuki kufuatia uteuzi wao wa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa hizo. Binafsi nawaamini sana na ndugu yetu Balozi Mushi, sisi huku TAMISEMI tunaku-*miss* sana kwa msaada wako wa haraka.

Mheshimiwa Spika, nina hoja kuu tatu. Hivi juzi tu tumeshuhudia Watanzania 26 wakipelekwa Mahakamani nchini Zambia kwa kuishi kinyume cha sheria nchini humo. Sisi Tanzania hususan Rukwa mipaka yetu ni *almost* upo wazi, hakuna ulinzi maalum na watu wengi wanavuka na kuingia kuishi Tanzania, wanapata fursa zote na wengine kuwa ndio chanzo cha uchochezi wa kisiasa hasa katika maeneo ya mwambao. Iko haja ya kuweka kituo cha uhamiaji

maeneo hayo na kuwa na njia rasmi ya kuingia watu ikiwa ni pamoja na kufanya *operation* maalum ya kuwaondoa wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, suala la mpaka Ziwa Nyasa baina ya Malawi na Tanzania, ni vema jambo hilo lishughulikiwe mapema na kwa umuhimu wake wa kipekee. Tumelizungumzia sana suala hili hapo awali na sasa tunazidi kurudia, watu wameshaingia hofu, kila siku tunapata simu juu ya hofu hiyo. Ni vema lipewe uzito wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Balozi zetu, hivi karibuni Julai, 2012 tulihudhuria kikao cha *SADC PF* huko Msumbiji, tukiwa na Mama Anna Abdallah, hali ya nyumba za Balozi zetu ni mbaya, Balozi anaishi nyumba ya kupanga, kwani nyumba yake inahitaji matengenezo makubwa hata *fence* yake tu si salama kabisa. Nilimtania Balozi Shamim Nyanduga kuwa amekimbia nchi, kwa nini ameshindwa kukaa kwenye nyumba yake, hali kadhalika ofisi imo katika nyumba ya kupanga.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sisi sio maskini, kule Msumbiji tuna jengo kubwa lenye ghorofa takribani nane na kiwanja katika maeneo makuu ya mji, tena tulipewa zawadi, lakini hata matengenezo tu ni ya shida. Pia tuliongea na Mkandarasi ambaye amepewa kazi ya kukarabati jengo hilo la ghorofa sita ameshindwa kuendelea na kazi kutokana na kukosa malipo hali kadhalika atatuchaji gharama. Msumbiji kupanga nyumba ni ghali sana. *Flats* hizo zikikarabatiwa, tunaamini Ubalozi wa Msumbiji

unaweza kabisa kujiendesha wenyewe bila tatizo. Ni vema kazi hiyo iliyoanza ipewe msukumo na ikamilike.

Mheshimiwa Spika, Waziri nakushauri utembelee Ubalozi huo, Msumbiji sio mbali lakini ni kwa rafiki zetu muhimu, wametuheshimu, ni mionganini mwa Balozi endelevu, basi heshima tuliyopewa tusiitupe, tulipewa nyumba tuzitunze.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru pia Balozi Nyanduga kwa jinsi alivyotupokea na kutusaidia tukiwa Msumbiji.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii muhimu sana, kwa kazi nzuri wanazozifanya wakishirikiana na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kutoa maoni yangu machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kutoka kwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nchi za nje kuwa hawapati ushirikiano wa kutosha kutoka kwenye ofisi za Balozi zetu zilizopo kwenye hizo nchi wanazosoma na hivyo kusababisha baadhi yao kupata matatizo ama kujiingiza kwenye mambo tofauti na matarajio ya wazazi wao. Je, Wizara ina mkakati gani wa makusudi kushughulikia tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, japokuwa tunafahamu kuwa Balozi zetu zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa

fedha, bado nafasi ya Mabalozi kuitangaza nchi yetu haijatumika kama baadhi ya Mataifa mengine yanavyofanya. Kwa mfano, Mabalozi kuitangaza nchi yetu kwenye sekta ya utalii. Sekta ya utalii ni muhimu sana na inaweza kuiingizia nchi yetu mapato mengi kuliko ilivyo sasa na tulitegemea Mabalozi waliopo kwenye Mataifa ama nchi mbalimbali wangetumika vizuri zaidi katika kuitangaza nchi yetu hasa kwa kutumia vivutio vyetu vya kitalii kama Mlima Kilimanjaro, mbuga zetu za wanyama kama Serengeti, Ngorongoro na kadhalika lakini Serikali bado inaendelea kupunguza bajeti ya Wizara hii kila mwaka. Je, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuboresha Balozi zetu kwa kutenga bajeti ndogo kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikosa fedha za kigeni kutokana na watendaji wasio waaminifu kutotoa takwimu ya mapato yaliyo sahihi. Ninamuomba Waziri anieleze ni hatua gani zitachukuliwa kwa Balozi wa Heshima (*Honary Consul*) anayeishi mji wa *Nice* ambaye amekataa kuchukua mashine ya *Visa Sticker* ambapo mashine hiyo ipo Paris na anaendelea na utaratibu usiokubalika wa kugonga mhuri.

Mheshimiwa Spika, jengo la Ubalozi wa New Zealand nchini Ufaransa linauzwa na kwa sababu sisi ofisi yetu ya Ubalozi tunakodi, kwa hiyo kabla ya mwezi wa tisa mwaka huu, Serikali ya New Zealand ndio mwisho wa kustahamili na watalipiga mnada. Nashauri

Serikali inunue majengo haya ili kuokoa fedha nyingi kwenda kwenye kodi.

Mheshimiwa Spika, tatizo kama hili limejitokeza jijini Milano Italia kutoa *Visa* kwa kugonga mihuri kinyume na utaratibu. Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa mhusika anayekosesha mapato Serikali?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi zimekuwa zikichukuwa mishahara ya watumishi wa Balozi zetu pale Serikali inapochelewesha malipo ya pango mbalimbali na kuathirika sana kimaisha. Nashauri Serikali kupeleka fedha kwa wakati ili kunusuru fedha za watumishi wa Balozi zetu kutokatwa pesa zao kwani mabenki ya nchi hizohizo zina utaratibu unawalazimisha kukata fedha hizo.

Mheshimiwa spika, baadhi ya majengo ya Balozi zetu yamechakaa na hayafanyiwi ukarabati na yanatia aibu nje ya nchi kiasi cha kuleta kero kwa majirani walio karibu na jirani hao. Hivyo ninaishauri Serikali kuyakarabati majengo hayo na kununua mengine kwa ajili ya kukodisha ili kiwe chanzo cha kujipatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Ujerumani wana uhusiano mzuri pamoja na Jimbo la Ujerumani linaloitwa *Lower Saxon* ambapo watengenezaji wa Meli ya MV. Liemba wanatoka katika Jimbo hilo, na wamekubali kukarabati MV. Liemba iliyoko katika Ziwa Tanganyika lakini Serikali ya Tanzania bado ina kigugumizi juu ya kukubali ombi hili. Ninaishauri Serikali

kubali ombi la Ujerumanî kuanza kukarabati MV. Liemba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii na mimi kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, umuhimu mkubwa wa Wizara hii uko katika kudumisha mahusiano yetu na nchi za nje, pia kuitangaza nchi yetu katika sekta muhimu za kiuchumi hasa katika sekta ya utalii ambalo ni eneo muhimu katika kukuza maendeleo yetu na pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nadhani Balozi zetu bado hazijatumika ipasavyo katika kutangaza utalii wa nchi yetu hasa ukizingatia kwamba biashara ni kutangazwa. Kwa mtazamo wangu, endapo Balozi zetu zitatumika ipasavyo kuitangaza nchi yetu, hususan katika nchi za America na Ulaya nadhani tutafanikiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano mdogo tu nchi kama China kutegemea Balozi wetu aliyepo Beijing atangaze utalii wa Tanzania katika nchi kubwa kama China, si kitu rahisi. Pamoja na ugumu wa bajeti yetu lakini hapa ipo haja ya kuangalia katika maeneo mengine kama vile Guanzhou, GuangDang, Shangahai, Shelizen na kadhalika tukaweka maafisa wa vituo maalum kuongeza kasi ya kulitangaza Taifa yetu katika sekta hii muhimu ya kukuza utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la uraia wa nchi mbili. Kwa kweli muda mrefu Taifa letu limekuwa na mpango wa utekelezaji wa uraia wa nchi mbili, lakini utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua.

Napenda kuishauri Serikali ipige hatua mbele katika utekelezaji wa jambo hili kwani sio jambo geni hapa duniani na wala sisi Tanzania hatutokuwa nchi ya kwanza na tunategemea kunufaika zaidi hasa kwa wale Watanzania wengi wenye uwezo ambao kukana uraia wa nchi hizo hawawezi, lakini pia wanatamani kutambuliwa kama raia katika nchi yao ya asili ya Tanzania, waje kuwekeza. Linalowezekana leo tuisubiri kesho.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yetu ya Kamati ya Nishati na Madini tarehe 11 Julai, 2012 Thailand na China kuhusu umeme vijiji unavyoendelezwa, tuliarifiwa Ubalozini Beijing kuwa na changamoto kadhaa ambazo naomba majibu yake:-

- (i) Ukosefu wa Wachumi (au Mchumi) Ubalozini inaathiri Tanzania kukosa fursa nyingi za uwekezaji mikopo zaidi na misaada tunayoweza kuipata kutoka kwa rafiki zetu wa kudumu wa Jamhuri ya watu wa China (PRC) hasa ukilinganisha na Kenya ambao sasa wanajengewa reli *standard gauge*, bandari ya Mombasa

Gati 17 na 18 na pia wanaweza kupewa msaada/mikopo/uwekezaji kwa bandari ya Lamu, reli ya Lamu - Sudan Kusini kupitia Ethiopia mpaka Sudan Kusini na mpaka Uganda. Hii itaathiri uchumi wetu kama hatuchangamkii fursa zitolewazo na Serikali (makampuni ya China na taasisi zake za kifedha na uchumi).

Mawaziri wa Uchukuzi na Fedha hawakuhudhuria Mkutano wa Ushirikiano wa Afrika na China Julai 18 -20, 2012, sijui nani aliratibu mialiko hiyo, ilikuwa muhimu wawepo pamoja na Mheshimiwa Membe kwani ule mkutano ndiyo mwanzo wa miaka mitatu ya bajeti ya Serikali ya China kukopesha na kufadhili miradi ya miundo mbinu, afya, kilimo na kadhalika.

(ii) Mikopo ya China Tanzania inatoa ajira nyingi kwa Wachina kuliko Watanzania hata vibarua. Utaratibu uwekwe ili asilimia 50/50 ziwe vibarua wa China na Watanzania. Tatizo la ajira China lipo pia Tanzania kwa vijana wataalam. Yawezekana uchache wa ajira kwa vijana wetu kunasababisha baadhi wajilingize kwenye biashara ya madawa ya kulevyo. Hivyo basi vijana na akina mama waliloko katika orodha ya kunyongwa na vifungo vya maisha China katika magereza mbalimbali, Wizara ijadiliane na Serikali ya China ili vifungo vifanyike Tanzania na waliohukumiwa kunyongwa hukumu ibadilike kuwa vifungo vya maisha hapa Tanzania au China kwani uwiano wa ajira hauko sawa.

(iii) Majengo ya Ubalozi wa China hali ni mbaya, machakavu, yanavuja, yakarabatiwe au mapya yajengwe.

(iv) Wizara hii na ya Uchukuzi zijitahidi mkopo wa *Exim Bank* ya China, iikopeshe Serikali kupitia *TPA* ili gati 13 na 14 zijengwe, lango lipanuliwe na kina kiongezwe na vifaa vya bandari ili pamoja na reli za kati na *TAZARA* pato liongezeke kwa kubeba mizingo ya DRC, Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi tuipite bandari ya Mombasa.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nchi yoyote duniani ili kujenga uchumi wake ni muhimu sana kuwa na ushirikiano wa Mataifa mengine. Tanzania ni nchi ambayo ina mipaka yake ambayo inaheshimika Kimataifa kwa hiyo ni muhimu kwa Tanzania kuwa na ushirikano na Mataifa mengine ili kuboresha uchumi na mahusiano mazuri na Mataifa mengine kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi na kuimarisha mahusiano mazuri kwa kubadilisha utaalam na utamaduni wa nchi nyingine. Pia ushirikiano wa Kimataifa ni muhimu sana katika kuimarisha usalama na ulinzi wa nchi kwa kutambua utamaduni wa nchi bila kubuguziwa na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto nyingi katika kuinua uchumi wa nchi, ni muhimu kwa Mabalozi wetu kuwa makini sana katika suala la kutafuta masoko

ya bidhaa ambazo zinazalishwa Tanzania ili kupata soko la nje.

- (ii) Kuwa makini sana katika suala la ulinzi wa Watanzania hasa wanaoishi nchi za nje.
- (iii) Kuiga mambo mazuri kutoka nje kama vile matumizi ya teknolojia kutoka nje ili kuimarisha mbinu za uzalishaji mali ndani ya nchi yetu.
- (iv) Kuwatafutia vijana nafasi za masomo na ajira nje.
- (v) Kutumia vizuri rasilimali za nchi ya Tanzania huko nje za nchi.
- (vi) Kuhamasisha wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo muhimu kwa ushauri wangu ili kuimarisha mahusiano ya Kimataifa, kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshniwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu umuhimu wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi yaani walioko kwenye *Diaspora*.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walioko nje ya nchi hutoa mchango mkubwa kwa kutuma fedha kwa ndugu na jamaa zao nchini. Kwa kuzingatia umuhimu wa Watanzania wenzetu, ni bora sasa Serikali itoe

uamuzi kuhusu suala la uraia wa nchi mbili yaani "*Dual Citizenship*".

Mheshimiwa Spika, endapo nchi yetu itawapa Watanzania haki ya kuwa na uraia wa nchi mbili, hakika Watanzania wengi watarudi kuwekeza nchini maana watakuwa na uhakika wa usalama wa mali zao.

Mheshimiwa Spika, Rwanda imejengwa na wananchi wake walioko nchi za nje, kwa nini sisi tusitumie wananchi wetu walioko nje kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu Serikali itatoa ufumbuzi wa jambo hili muhimu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kidiplomasia, naomba kutoa maoni katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya ofisi za Ubalozi kwamba fedha haziendi kwa wakati. Naomba Serikali isimamie vyema suala hili ili kulinda heshima kwa ofisi zetu za balozi na heshima ya nchi yetu.
- (ii) Naomba kuishauri Serikali kutumia vyema ofisi za Balozi kuwa kama kituo cha uchumi ili

zitumike katika kukuza uwekezaji na Utalii kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu maafisa au wafanyakazi waliopo katika ofisi za Mabalozi zetu nje ya nchi. Hali za wafanyakazi hawa ni mbaya sana kwa kuwa mishahara yao inachelewa sana na pia huwa wanalipwa kwa *rate* ambazo haziendani na wakati husika hivyo kupelekea kulipwa kwa *rate* ndogo. Wengi wa wafanyakazi hawa wanaishi kwa mikopo na wale wafanyakazi walioajiriwa *locally* wanalipwa fedha ndogo sana. Mfano Ubalozi wa Uingereza wafanyakazi wa pale sijui ni kwa jinsi gani wanamudu maisha kwa mshahara ule ukizingatia *standard* ya maisha inatofautiana kati ya nchi na nchi. Usafiri peke yake mshahara mzima unaweza kuishia hapo. Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuwaongeza na pia kuhakikisha mishahara inapelekwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pili, nyumba za Ubalozi zinazomilikiwa na Serikali. Kuna baadhi ya nyumba zipo kwenye hali mbaya sana lakini zipo kwenye *prime area* kama kule Uingereza, kwa nini nyumba hizo hazitengenezwi? Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza au kujenga nyumba hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zitachangia kuboresha maslahi ya wafanyakazi hata kuliongezea Taifa pato la fedha za kigeni?

Mheshimiwa Spika, tatu, mapigano Syria. Hapa Tanzania inaonekana kutoa *support* sana kwa nchi ya Syria sababu hapo Dar es Salaam tumekuwa tukiona maonyesho mengi ya kibashara kutoka nchi ya Syria. Pamekuwepo na mapigano, mauaji ya kina mama na watoto na raia wasiokuwa na hatia. Mauaji haya ni ya kulaaniwa, yanavunja haki za binadamu. Ni nini msimamo wa Tanzania kuhusiana na mauaji yanayoendelea Syria?

Mheshimiwa Spika, nne, urejeshwaji wa paundi 29.5 milioni kutoka Uingereza. Ni jambo zuri kurejeshwa kwa fedha hizi lakini bado Serikali haielezi waliosababisha mpaka fedha hizi kurejeshwa wamechukuliwa hatua gani? Ni haki kwa Watanzania kuelezwu ni hatua gani zinazochukuliwa. Fedha hizi hazikuondoka zenyewe, kuna wahusika waliofanya ujisadi huu, lazima wafilisiwe na sheria kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, tano, jengo la Ubalozi Zambia. Jengo hili ni zuri, ni kubwa na kitega uchumi kizuri lakini kwa sasa lilikuwa linavuja na hotuba ya bajeti mwaka 2012, Waziri alilieleza Bunge lako Tukufu ipo kwenye harakati za kulikarabati. Je, mpaka sasa hivi michakato imefikia wapi? Je, jengo hili limeshaanza kukodishwa kwa ajili ya biashara?

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, napenda kupata maelezo kuhusu hali mbaya ya fedha iliyopo katika Balozi za Tanzania nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Balozi nyingi zina madeni makubwa sana, hakika inatia aibu sana. Balozi zinashindwa kulipa ankra za umeme, maji na huduma nyinginezo muhimu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona mishahara imekuwa inachelewa ambapo inafanya watumishi wa Balozi hizi wafanye kazi katika mazingira magumu sana kwani suala la kupatiwa fedha Balozi hizi inakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kuhusu utolewaji wa nafasi za ajira kuwa ni kwa watu wa aina fulani tu. Naomba muwape fursa za ajira vijana wetu bila kubagua wakiwemo watoto wa wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa majumuisho, Waziri aniambie idadi ya vijana waliopata kazi katika Balozi zetu zilizo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na hata Watendaji wengine wa Wizara hii kwa kufanya kazi kwao kwa umakini. Kwa hakika ni dhahiri kuwa uongozi wao makini bado unazidi kutangaza nchi yetu katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, binafsi nitajikita kwa kuuliza maswali ambayo yakijibiwa

yatasaidia kuondoa shaka kwa Watanzania juu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania imefungua Balozi ngapi katika nchi za nje zinazoiwakilisha nchi ya Tanzania hadi sasa? Nchi hizo ni zippi? Kwa nini kwa baadhi ya nchi hatuna Balozi?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Watanzania ambao ni wafanyabiashara mara kwa mara wamekuwa wakifanya biashara kati ya Tanzania na nchi ya Thailand. Hata hivyo, wafanyabiashara hao wamekuwa wakipata adha kubwa kutokana na kukosekana kwa Balozi au ofisi yetu ya Ubalozi katika nchi ya Thailand?

Mheshimiwa Spika, ni vigezo vipi vinavyofuatwa na nchi wakati inapotaka kufungua Ubalozi katika nchi nyingine? Ni sababu zippi zilizoleteleza Tanzania isifungue Ubalozi katika nchi hiyo ya Thailand? Kwa nini sasa Serikali haioni kuwa ni muda muafaka wa kufungua ofisi ya Ubalozi katika nchi ya Thailand?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafanyabiashara toka Tanzania wamekuwa wakitapeliwa nchini Thailand kwa kunyanyaswa na hata kuibiwa fedha. Je, Serikali inalifahamu hilo? Kama inalifahamu, imechukua hatua gani? Je, Serikali haioni kuwa ikifungua ofisi za Ubalozi nchini Thailand, itawaondolea adha Watanzania wenzetu wanaofanyabiashara huko Thailand?

Mheshimiwa Spika, Sera yetu ya nchi za nje enzi ya ujamaa na kujitegemea, ilikuwa ni ya kutofungamana na upande wowote. Sera hii kwa hakika ililijengea Taifa letu heshima katika Mataifa mbalimbali. Je, baada ya mfumo wa Kikomunisti kuvunjika duniani, hadi sasa kuna umuhimu wowote wa kufuata sera hii? Je, sasa nchi yetu inafuata sera ipi? Wizara inafanya juhudini gani za kuitangaza lugha ya Kiswahili Kimataifa?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi kama vile China, Mtanzania akiwa na Hati ya Kusafiria ya Kidiplomasia anaingia bila Viza. Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa nchi zote duniani zinawaruhusu watu wa nchi yetu ya Tanzania wenye Hati za Kusafiria za Kidiplomasia wanaingia katika nchi hizo bila viza?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuna utitiri wa Watanzania hasa wale wa imani ya Kikristo wamekuwa wakienda Israel mara kwa mara kwa lengo la kuhiji. Serikali ina mpango gani wa kufungua ofisi ya Ubalozi katika nchi ya Israel? Je, ni kwa nini tuendelee kutumia Balozi za Kenya zilizopo katika nchi mbalimbali duniani, kwani sisi Tanzania si nchi kamili yenye uhuru kamili?

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mataifa ni taasisi nyeti katika dunia ambayo huunganisha nchi mbalimbali duniani. Kwa nini Afrika haina uwakilishi wa kudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa? Kwa nini Afrika haina kura ya *VETO* katika Umoja wa Mataifa? Je, kwa nini Tanzania haipeleki pendekezo la kuondoa kura ya *VETO* katika Umoja wa Mataifa kwani imepitwa na wakati? Kwa nini Umoja wa

Mataifa unatumia nguvu kutatua matatizo yanayozikumba nchi maskini badala ya diplomasia?

Mheshimiwa Spika, migogoro ya Kimataifa ni tatizo kubwa la Kihistoria. Hali hii ilikwisha pelekea kukatokea vita ya kwanza na ya pili ya dunia. Je, Umoja wa Mataifa umejandaa vipi kukabiliana na migogoro ya mara kwa mara inayoikumba dunia?

Mheshimiwa Spika, Tanzania imesaidia sana nchi nyingi za Afrika kujikomboa na kupata Uhuru. Ilitumia rasilimali nyingi sana ili kufanikisha zoezi la ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Ni lini Tanzania itadai rasilimali kutoka nchi hizo hasa Afrika Kusini, Mozambique, Angola na Zimbabwe? Ni lini Tanzania itapeleka *invoice* ya madai kwa nchi ya Uganda kwa kuikomboa toka kwenye makucha ya Nduli Iddi Amin Dada?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza sinabudi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa maandishi lakini pia nimpongeza Waziri kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kiungo muhimu sana cha nchi yetu na nchi za nje. Hata hivyo, Wizara hii ni Wizara ya muungano na kwa maana hiyo kazi zake zinapaswa zizingatie zaidi muungano wetu. Lakini hakuna ufanisi mzuri baina ya Tanganyika na Zanzibar kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni misaada kutoka nje. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, asilimia kubwa sana ya mikopo na matumizi yamelenga zaidi zile Wizara zisizokuwa za muungano na hivyo kazi kubwa ya Wizara hii inazitumikia zile Wizara zisizokuwa za muungano zaidi. Kwa mfano, misaada ya barabara imekuwa mikubwa, misaada ya kilimo imekuwa mikubwa, misaada ya miundombinu pia imekuwa mikubwa mno, ukiangalia yale mambo ya muungano hayakupewa kipaumbele hata kidogo. Kwa maana hiyo, ni dhahiri Zanzibar ina nafasi ndogo sana kwa kuwakilishwa na hivyo kushindwa kujikwamua kwa yale mambo yasiokuwa ya muungano.

Mheshimiwa Spika, pili, ajira katika Wizara hii. Ukiangalia hotuba ya Waziri amesema kuwa watumishi wote ni 430 na kuainisha wapi wanafanyakazi, lakini ameshindwa kuonyesha ni Wazanzibar wangapi wamekuwa watumishi katika Wizara yake lakini inaonyesha kwamba Wanzanzibar ni wachache sana. Nimuombe Waziri atueleze kuna Wazanzibar wangapi (watumishi) katika Wizara yake?

Mheshimiwa Spika, tatu, mgawanyo wa madaraka. Waziri katika hotuba yake ameshindwa kutuelezea ni Mabalozi wangapi kutoka Zanzibar wako ndani ya Wizara yake? Waziri hakufanya hivyo kwa lengo la makusudi akijua kwamba Zanzibar haikuwakilishwa Kibalozi kama ilivyo Tanzania Bara. Namwombe Waziri atueleze ni Mabalozi wangapi kutoka Zanzibar wako ndani ya Wizara yake?

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu *O/C*, hadi sasa hatujapata jibu lolote kuhusu Tanzania kujiunga na *O/C*. Kwa hiyo, Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kwa nini Tanzania imekaa kimya kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona Serikali inashindwa kuleta Muswada wa Sheria ya *Dual Citizenship* huku tukijua ni jinsi gani nchi zilizoridhia *Dual Citizenship* wanavyofaidi kimapato mfano Nigeria na Kenya. Tatizo ni nini? Ni kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi na suala hili muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu? Ni lini sasa Muswada huu utaletwa hapa Bungeni ili Watanzania wanaoishi nje ya nchi waweze kutoa michango yao kihalali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukandamizaji wa waziwazi dhidi ya wanawake wanaoolewa na *foreigners*. Wakati wanawake (*foreigners*) wanapoolewa na Watanzania wanapata uraia haraka sana lakini Watanzania wanawake wanapoolewa na wageni inakuwa ngumu sana kupata uraia. Huu utaratibu ni mbovu na ni wa kudhalilisha wanawake wa Kitanzania. Ni vipi mwanamke wa Kitanzania asipate uhuru wa kuolewa anapotaka? Kwa kuwa kuolewa nje kunamfanya *partner* wake asiwe na uhuru kamili wa kuishi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni kumekuwa na taarifa kuwa kuna baadhi ya Watanzania wenye mabilioni ya fedha katika mabenki hususan Switzerland

zilizohusu sakata la rada. Waziri alisema anawajua wahusika, ninamwomba sana Waziri Membe sasa atuambie majina ya watu hao ili tuendelee kuwa na imani naye.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kiungo kati ya nchi yetu na nchi nyingine duniani. Ni jambo la kushangaza kuona Wizara hii ikipatiwa bajeti ndogo sana na hata ile inayopitishwa bado kwa mwaka jana wamepata 44% tu. Hii ni hatari sana kwani unapokuwa nje ya nchi huna mtegemezi kama hapa, hivyo ni vyema bajeti ya Wizara hii itolewe kama ilivyopitishwa na Bunge ili kuondoa aibu ughaibuni.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona Balozi zetu zikijikita zaidi katika masuala ya kisiasa wakati kuna masuala mengi hususan ya kiuchumi. Kwa mfano ni kwa vipi Balozi zetu katika nchi kama China, USA, Japan wanatafuta masoko ya malighafi na mazao yetu? Kwa nini imekuwa Tanzania kuwa *importers* wa vitu vya hovyo kama viberiti, vidoli na kadhalika wakati mazao yote kama pamba, kahawa na kadhalika hukosa soko? Ni vyema basi Balozi zetu zihusike zaidi na uchumi kuliko siasa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Balozi zetu hukohuko nchi za nje ni vipi wanaitangaza nchi yetu, hasa katika utalii, kuutangaza mlima Kilimanjaro ili kuepuka jirani zetu Kenya, kuepuka kauli yao ya kusema ukitaka kufika mlima Kilimanjaro pitia Kenya.

Kuna umuhimu kabisa Balozi zetu kuongezewa bajeti ili waweze kutangaza nchi yetu pamoja na vivutio vyake vyote, kama mbuga za wanyama, mlima Kilimanjaro, mambo ya kale mfano, Bagamoyo, Kilwa, Kondoa na kwingineko, kukuza jina la Tanzania na lisikike kote duniani.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana nchi yetu kupitia Balozi zetu kufikiria kupeleka maafisa balozi kwenye nchi kubwa kama China, Marekani, Ulaya na nyinginezo kubwa kama hizi ili kuwafikia watu wengi zaidi wa nchi hizo ili kuleta ufanisi katika sekta hiyo ya utalii. Endapo wazo hili litafanikiwa, tunategemea kupata ongezeko la watalii na ile dhana ya utalii kwa maendeleo itakamilika.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikia mara kwa mara kuwa na uraia wa nchi mbili na kwamba mchakato unaendelea. Napenda wakati Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, anifahamishe mpango huu umefikia hatua gani na lini utatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa nje katika Nchi za Mashariki, kuna baadhi ya Watanzania waliomba hili la uraia wa nchi mbili. Naye pia aliahidi kulishughulikia. Hivyo, ni muhimu sana kulishughulikia, ni vizuri sasa kulimaliza suala hili la uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kama Watanzania kuitangaza nchi yetu na kuipenda. Pia kuthamini lugha yetu ya Kiswahili na kufanya jitihada iongelewe nchi nyingi zaidi na ikiwezekana duniani, Kiswahili ni hazina yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wote wa Wizara ndani na nje ya nchi kwa kuwezesha hotuba ya bajeti ya mfumo mpya wa kuonyesha majukumu yake kusaidia Wizara na sekta nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, pongezi kwa Dkt. Asha-Rose Migiro kwa kazi nzuri aliyofanya nje ya nchi yetu, imetujengea heshima kubwa na kuongeza uwezo mkubwa wa utendaji wa Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Taifa letu lazima litambue hilo na kuwaenzi wote wanaotujengea heshima nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, usaidizi kwa Wizara ya Nishati na Madini. Sekta ya umeme ikiboreka itawezesha kuongeza wigo wa wawekezaji wa viwanda nchini. Mradi wa umeme na *Stiglers Gorge* wa MW 2100 ndio mradi bora wa mtazamo wa muda mrefu wenyewe uhakika wa kuondosha tatizo la umeme Tanzania kwa muda mrefu. Kitabu cha hotuba hakionyeshi jitihada za Wizara kusaidia msaada wa fedha za utekelezaji wa mradi huo ila maelezo ya Waziri katika maelezo yake amelitaja.

Naomba jitihada ziendelezwe ili kuwezesha mradi huo kutekelezwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mikataba ilyiopo katika sekta ya madini ina kasoro nyingi zinazotoa mwanya kwa wawekezaji kunufaika zaidi kuliko Tanzania yenye rasilimali ya madini. Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa isaidie kushawishi wawekezaji waliopo Tanzania na pia katika nchi nyingine duniani kukubali kurekebisha maeneo ya mikataba yenye utata ili kuiboresha na kuwezesha Tanzania kunufaika na rasilimali ya madini ya nchi yetu. Wizara ijenge uwezo wa kupata nakala au mambo muhimu ya makubaliano ya mikataba kati ya wawekezaji katika sekta ya madini Tanzania kwa uwiano na mikataba ya aina hiyo kati ya wawekezaji waliopo nchini ikilinganishwa na mikataba ya aina hiyo kwa nchi nyingine kama vile Ghana, Boswana, Afrika Kusini na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, tatu, wawekezaji viwanda vya usindikaji wa matunda. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kiwete aliahidi kuisaidia Wilaya ya Muheza kupata mwekezaji wa kujenga kiwanda cha usindikaji tangu mwaka 2005 slijaona mwelekeo wa utekelezaji wa ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, nilitembelea nchi ya Italy, Jimbo la Cecily na kukuta mashamba makubwa sana ya machungwa. Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iwasiliane na Ubalozi wetu na Ubalozi wa Italy nchini ili kujenga hoja ya kuona uwezekano wa nchi hiyo kutathmini uwezekano wa

kujenga kiwanda cha usindikaji wa matunda katika Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, mji wa Katrinham nchi Sweden una uhusiano wa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Yapo makubaliano ya ushirikiano wa kuboresha sekta ya umeme na misaada mingine kati ya Tanzania na Sweden. Balozi wa Tanzania nchini Sweden alifika Mkoani Tanga na katika Halmashauri ya Wilaya Muheza mwaka huu 2012 ili kuona hali na uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuweza kushiriki vizuri katika makubaliano na wenzao wa Sweden.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hiyo kwa sekta ya umeme, nashauri pia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iboreshe hamasa hiyo ya ushirikiano na kushawishi uwezo wa wawekezaji kutoka Nchi ya Sweden katika ujenzi wa kiwanda cha usindikaji wa matunda kwa Wilaya rafiki ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:
Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kuweza kufanya kazi zao kwa kujiamini na kushirikiana pamoja katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika Serikali yetu, naiomba Serikali iangalie kwa makini sana maana Wizara hii ina umuhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ofisi iliyopo Zanzibar ni mbovu na haina magari. Naiomba Wizara hii ichukue hatua za makusudi kutatua tatizo hili maana wafanyakazi wa Wizara hii kwa Zanzibar imekuwa ni kero. Hii ni Wizara ya muungano, naomba Zanzibar iangaliwe maana ofisi yao hairidhishi kabisa. Serikali inapanga fungu la fedha, hizo fedha zinatumika kwa matumizi gani ikiwa ofisi zao haziridhishi hata kidogo?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii iangalie kwa makini sana katika mipaka yetu ya nchi kwa sababu nchi yetu imezungukwa na nchi jirani nyingi, kwa hiyo Wizara naiomba iwe makini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii ifanye mabadiliko katika ofisi zao maana Mabalozi wengi wanatoka Tanganyika kuliko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira, naiomba sana Wizara ya Mambo ya Nje itoe ajira sawa katika ofisi za Ubalozi pamoja na ofisi zilizopo ndani. Uwiano wa ajira Zanzibar na Bara uzingatiwe kwa sababu hii ni Wizara ya muugano.

Mheshimiwa Spika, maana ya kuwekwa Naibu Waziri kutoka Zanzibar tumuone anafanya kazi hizo kwa kumsaidia Waziri. Inaonesha ofisi ya Zanzibar haina uhai hata kidogo, angekuwa mtu tungesema yupo /CU.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na Wizara hii, lakini Mabalozi wanaotoka Zanzibar ni kidogo. Waziri namwomba atakapokuja hapa atuambie Mabalozi wapo wangapi? Naomba ufanuzi wa kina Zanzibar wapo wangapi na Bara wapo wangapi? Pia Waziri napenda kujua mgao huu unazingatia nini?

Mheshimiwa Spika, vijana wa Zanzibar wanalamika juu ya suala la ajira zinavyotolewa maana hawasikii matangazo redioni wala magazetini. Sijui nafasi hizo wanaajiriwa watoto wa wakubwa ndio maana hawasikii matangazo? Naiomba Wizara hii ichukue hatua za makusudi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri na kuwasilishwa na Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri mwenye dhamana kwa ufasaha wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba bajeti imeandaliwa vizuri lakini bado haitakuwa na tija sana kama taasisi zote ambazo ziko chini yake hazitaboreshwa kwani ni ndogo sana. Hivyo ninaiomba Serikali kuangalia namna ya kuongeza

fedha kwenye bajeti hii ili iweze kusaidia taasisi zake hususani ofisi za Balozi za nje ikiwemo Balozi ya China ambayo inakabiliwa na upungufu wa watumishi akiwemo Mchumi na kadhalika. Vilevile ukarabati wa majengo yake na bajeti yao ni ndogo sana. Nasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji kwenye sekta mbalimbali nchini. Ni ukweli usiofichika kuwa pamoja na juhudzi za Serikali za kuinua uchumi kuitia sekta mbalimbali lakini bado nchi yetu inakabiliwa na uhada wa fedha. Hivyo ninamuomba Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuongeza juhudzi za kutafuta wawekezaji wenyewe sifa ili tuweze kupata wawekezaji wa kuwekeza kwenye viwanda, madini, umeme, barabara na kadhalika ili uwekezaji uwe na tija ili kuinua pato la nchi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa wafadhili wa wanachuo/ wanafunzi nje ya nchi. Bado kuna tatizo la wanafunzi/wanachuo wanaopata nafasi za masomo nje ya nchi kukosa wafadhili nje ya nchi. Ninaiomba Serikali kufuatilia kwa karibu nafasi za masomo nje ya nchi kisha kutoa taarifa Serikalini sambamba na kuwatafutia wanafunzi au wanachuo wanaopata nafasi za masomo nje ya nchi wafadhili kuitia Balozi mbalimbali ili nchi yetu iweze kuongeza wanataaluma watakaosaidia kuendeleza nchi yetu kiuchumi. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Membe, Waziri mwenye dhamana au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi kukabiliwa na kesi za madawa ya kulevyia nje ya nchi. Kuna

taarifa za kuaminika kuwa Watanzania wengi wanajihusisha na uuzaji wa madawa ya kulevyo nje ya nchi wako magereza mbalimbali mfano nchi ya China karibu Watanzania 100 walikamatwa na madawa ya kulevyo. Hii ni aibu kwa Taifa letu. Hivyo ni vema kuweka sheria kali pamoja na kuwasaka Watanzania wanaokaa nchi mbalimbali bila shughuli maalum kurudishwa nchini ili kuondokana na aibu hii yaani Balozi zetu kuwa na mtandao wa kupeana habari haraka kwa utekelezaji. Ninaomba maelezo ya Mheshimiwa Membe, Waziri mwenye dhamana mkakati wake kupunguza tatizo la Watanzania wanaojihusisha na kuuza madawa ya kulevyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia nikitegemea kuwa Waziri na Naibu Waziri watachukua maoni yangu na kutoa ufanuzi. Mungu awape nguvu, afya na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, nampa hongera Waziri kwa kuwasilisha hoja vizuri na pia nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Wizara imefikia wapi kuhusu lile suala la uraia wa nchi mbili? Je, wamelitazama sana kama lina *elements* za uzalendo ndani yake kwamba watakuwepo watu wenye nchi nyingine mbali na hii ya kwetu?

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa nyuma sana kwenye kutumia fursa za masoko ya nje ambayo Afrika inapewe chini ya mikataba mbalimbali ya Kimataifa kama ile ya *Everything But Arms (EBA)*, *AGOA* na hata soko la nchi za *SADC* na *AEC*, je, wameweka mikakati gani ya kuhakikisha fursa hizi tunazitumia ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, Bunge la Afrika hallna *full legislative powers*. Wizara ina mikakati gani ikishirikiana na nchi nyingine kuhakikisha tunaelekea huko?

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge la Afrika Mashariki hazijulikani sana kwa wananchi. Je, Wizara haioni kwamba kama tungebadilisha utaratibu wa kuwapata wawakilishi wa nchi husika kwenye Bunge hili na kurudisha *mandate* ya kuwachagua kutoka kwa wananchi, tungeweza wananchi kuelewa zaidi shughuli za Bunge hili na kuongeza ushiriki wa wananchi?

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikisaini mikataba isiyo na faida sana kwa Taifa, hali ambayo inapelekea kuvunwa kwa rasilimali yetu bila sisi kufaidika sana. Je, hivi tuna kitengo cha *kuwa-assess* wawekezaji kwa njia za kiintelejinsia ya kiuchumi na kibiashara kabla ya kusaini nao mikataba ili kujua malengo yao yaliyojificha kabla hatujaingia kwenye mikataba mikubwa kama ya madini, nishati (umeme, gesi na mafuta?)

Mheshimiwa Spika, pia je tunavyoingia kwenye ushirikiano wa kimasoko ama hata huu mwelekeo wetu wa kuelekea *EAC federation*, tunazijua agenda za siri

za wenzetu? Je, sisi tuna *competitive intelligence* ya kutosha kujua namna bora ya ku-*infiltrate* kwenye ndoa hizi huku tukijua "what is in it for us?"

Mheshimiwa Spika, kwa nini tatizo la mipaka ya nchi yetu bado linaendelea kuwa *issue* leo hii zaidi ya miaka 70 baada ya *Heligoland Treaty*? Je, hawaoni kama hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ya Afya inategemea kwa kiasi kikubwa misaada na michango ya wabia wa maendeleo mfano kwenye maendeleo na pia kwenye miradi msonge (*TB, AIDS, Malaria*).

Kwa bahati mbaya, wadau hawa hawatekelezi ahadi zao za kutoa mchango wao kama wanavyo-*pledge*. Hali hii imepelekea kukwama kwa mambo mengi, je, Wizara inaliongeleaje suala hili? Mfano *last year*, bajeti ya maendeleo haikutekelezwa ipasavyo kwa kuwa *donors* walileta 36.6% tu ya fedha zote walizo-*pledge*, je, Serikali inajipangaje kwenye hili? Pia viyi wakiamua kuacha kutoa mchango huo – mfano *Global Fund* hawakutupa Tanzania fedha mwaka uliopita, tunajipangaje hapo?

Mheshimiwa Spika, hongera kwa kufanikisha kutuletea fedha za *Rader*. Tunaomba zitumike vizuri kama Waziri anavyosema kila siku.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, uraia wa nchi mbili au zaidi. Kumekuwa na mjadala mkubwa katika nchi yetu kwa Watanzania kuwa na uraia wa nchi mbili. Kwa maoni yangu na kwa faida ya Watanzania wote, uraia wa nchi mbili bado hauonyeshi faida kwa Watanzania hasa wazawa na hivyo hauna tija wala faida badala yake itakuwa ni vurugu kwa nchi yetu.

Kwa uzoefu tulionao, Watanzania wenyе asili ya kiasia ndio wanaoongoza kuwa na uraia wa zaidi ya nchi moja na watu hawa (Wahindi) zaidi ya kunufaika kwa kufanya biashara hapa nchini wamekuwa hawafanyi juhudи za kujenga majengo ya kudumu hasa kwa nyumba zao za kuishi na badala yake wanamiliki nyumba za *NHC* kwa kuogopa kuwa na makazi ya kudumu na endapo lolote litatokea kama kuchafuka au kutoweka kwa amani nchini wao wanakuwa wa kwanza kukimbia nchi na hawana cha kupoteza.

Pia tumeshuhudia hata wakati wa uchaguzi mkuu, Waasia hufunga biashara zao na kuondoka nchini kwenda Canada, Uingereza, Marekeni na kadhalika. Hii maana yake ni kwamba uraia wa nchi mbili haukuzi uzalendo bali mtu anakuwa amegawa nafsi yake pale ambapo ni pazuri tu na pakiharibika hatakuwa na ujasiri wa kutengeneza bali kukimbia, hivyo kama nchi suala la uraia wa nchi mbili lisifanywe haraka bali lisubiri.

Mheshimiwa Spika, pili, rasilimali watu ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Kuna Watanzania wengi sana ambao wanaishi nje ya nchi kwa

kuwekeza huko na Serikali haifanyi jitihada zozote za kuwaandalia mazingira mazuri ya kurudi nchini na kuwekeza hapa. Je, Wizara inafahamu ni Watanzania wangapi walio nje ya nchi ambao wamewekeza huko? Mpaka sasa ina mkakati gani wa makusudi wa kuwarudisha nchini na kujenga nchi yetu pamoja?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna wengine waliokimbia nchi kwa sababu mbalimbali na wengine kuwekewa vikwazo vyta kurudi nchini hasa wakati ule wa vita baridi na mfumo wa chama kimoja, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwarudisha Watanzania hawa nchini pamoja na familia zao ili kufanya kazi nchini? Katika hawa, wapo wengine ambao ni *very potential* ni vema wakarudi nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu, Hati za Kusafiria za Kibalozi. Wabunge pamoja na wale wenye sifa hupewa *Diplomatic Passport* kulingana na nyazifa zao. Hati hizi zinabeba dhamana kubwa na heshima kubwa kwa wanaokuwa nazo. Cha kushangaza Wabunge tunapokwenda nje ya nchi, hati hizi hazipewi kipaumbele chochote na badala yake tunabaki kutangatanga bila kupewa huduma yoyote inayohusiana na hati hizo na hapo ni kwa safari za kikazi sio binafsi.

Ni kwa nini Balozi zetu hazitoi maelekezo maalum kwa wahusika ili Wabunge na wengine wenye hati hizi wachukuliwe na kuangaliwa kwa umuhimu wao? Ni kwa nini wageni wengine toka nje ya nchi wenye hati hizi wanapokuja nchini hupewa *special attention* lakini kwa Watanzania inakuwa tofauti? Je, ni kwa sababu

ya utegemezi wetu kwa wahisani? Ni unyonje au uzembe? Au *Diplomatic Passport* za Tanzania zina tofauti ya hadhi na za nchi zingine? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, nne, mahusiano na nchi za nje kiuchumi. Pamoja na Tanzania kuwa ni nchi yenye mahusiano mazuri na nchi zingine lakini ifike mahali iwe na msimamo thabiti wa kutokuyumbishwa katika maamuzi yake hasa kwenye masharti ya kupewa misaada ya kiuchumi na kijamii kama tulivyoonyesha msimamo wa kukataa ushoga. Ni vizuri tukabaki na msimamo huohuo na pia kuendelea kukataa masharti ya misaada yanayotudhalilisha.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa Tanzania ikaangalia umuhimu wa kuwa na Ubalozi Cuba maana ni nchi ambayo imeonesha kuwa na msaada mkubwa sana kwa nchi yetu hasa kwa masuala ya elimu na kijeshi.

Mheshimiwa Spika, pia ni vema Tanzania ikafikiria kuwa na Ubalozi Israel kwani ni Mji Mtakatifu kwa waumini wa madhehebu ya Kikristo na mara nyingi waumini hawa huenda kuhiji kama njia ya kupata utakaso. Pamoja na kwamba nchi yetu haina dini lakini watu wake wana dini ambazo huwasaidia kuishi kwa upendo. Israel ndiyo nchi ambayo iliyokuwa mwanzilishi wa JTK nchini na faida zake tumezunga katika kujenga uzalendo kwa vijana wa enzi za JKT na hivyo nchi yetu kuona umuhimu wa kurudisha JKT tena.

Mheshimiwa Spika, tano, vijana wanaotoroshwa kwenda nje kwa shughuli mbalimbali. Tumesikia katika vyombo vyaa habari kwamba kuna vijana toka Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma na Dodoma ambao huuzwa na wafanyabiashara wa Tanzania wakishirikiana na wale wa Kenya katika machimbo ya madini huko Ethiopia. Je, Wizara inatoa tamko gani kwa biashara hii haramu? Tumesikia kwamba vijana hawa wanaishi kwa mateso makubwa na hawapewi chakula bali hushindia maji na mikate. Je, Wizara ina habari na hawa wananchi wake? Naomba tamko la Serikali na ni hatua gani kali zinachukuliwa kwa wafanyabiashara hawa wasio na utu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu hususani katika maeneo matatu.

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara muhimu sana kwani inahusiana na ushirikiano wa nchi zingine na nchi yetu, kitu ambacho kwa maoni yangu ni kiungo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, *issue* ya kwanza ambayo nitapenda kuzungumzia ni juu ya utambuzi wa Jumuiya ya Watanzania waishio Ugaibuni (*Diaspora*).

Namshauri Waziri, katika hotuba yake ametuambia kuwa Wizara tayari imeshaunda idara ambayo itakuwa inashughulika na Watanzania waishio nje ya nchi. Lakini uzoefu kutoka nchi zingine

unaonyesha kuwa zile nchi zenyenye wananchi nje ya nchi wenye ujuzi mkubwa na wasomi kwenye taaluma mbalimbali wanapata manufaa makubwa sana ikilinganishwa na zile nchi zenyenye wananchi nje lakini asilimia kubwa ya hao wanakuwa na ujuzi mdogo wa elimu ambao siyo wa kutosha. Hii ni kwa sababu kama hawana elimu ya kutosha basi wanaishia kufanya kazi za mitulinga, kama kubeba maboksi, kufanya kazi kwenye kambi za wazee na vichaa. Tukitaka *diaspora* hii iwe ya manufaa na tija kwa Taifa letu, hatuna budi kijiandaa na kujijenga vyema.

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wasomi wengi sana hapa nchini ambao hawana ajira. Tukitumia Idara hii, tunaweza kuwasaidia vijana hawa kupata ajira nje ya nchi na Mashirika ya Kimataifa. Kwa mfano kuna fursa za ajira kwenye nchi ya Sudan Kusini ambalo ni Taifa jipya ambalo linaitaji wataalam kwenye sekta mbalimbali katika ujenzi wa Taifa lile ambalo halina wataalam wa kutosha, hivyo ingefaa kutumia fursa hii kupeleka wataalam wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi za wenzetu kama Kenya, Nigeria, Rwanda wametumia mbinu hii na inawasaidia sana katika kuchangia uchumi wa nchi zao. Mfano *Diaspora* ya Kenya inachangia shilingi za Kikanya bilioni 700 kwa mwaka ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 12.6 au bilioni 12,600. Hili linaweza kufikiwa kwa kuratibu na kufuatilia kwa kuhakikisha Watanzania walio nje wanajiendeleza na kupata ujuzi wa kuwawezesha kupata kazi zenyenye ujira nzuri. Ili tuweze kufanikisha haya yote niliyosema, ni vyema sasa Wizara iwe na *database* yenye CVS za

Watanzania wasomi na wenyе sifa katika taaluma mbalimbali ambapo sasa tutatumia *CVS* hizo katika kupata wataalam wa kufanyakazi kwenye taasisi mbalimbali na hata Mashirika ya Umma.

Vilevile zinaweza kutumika hata kupata fursa za ajira nje ya nchi mara zinapojitokeza. Mara Wizara ionapo nafasi za kazi basi inakuwa ina-*review* kwenye *database* na kupata mtu ambaye anafaa kwenye kazi husika. Tumeona nchi kama Senegal na Phillipines wanatumia sana mbinu hii na imewaletea mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika hoja hii, napenda kutoa rai kwa Wizara ipanue wigo wa kuwafikia Watanzania waishio nje ya nchi duniani kote, kwani kuna Watanzania kwenye nchi kama za Oman, Botswana, Canada na kwingineko ambapo wengi wao hufanya kazi zenyе ujira mkubwa ikilinganishwa na sehemu kama Marekani na Ulaya ambapo ndipo tuna-*concentrate* kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kujua ni kwa jinsi gani Wizara imejipanga kuhakikisha Watanzania waishio nje ya nchi wanashiriki katika mambo ya kijamii na kisiasa mfano katika suala zima la sensa ya Taifa inayotarajia kuanza tarehe 26/8/2012, kushiriki kwao katika mchakato mzima wa kupata Katiba mpya, mfano sasa wakati Tume ikikusanya maoni na mwisho ni kwa jinsi gani wanashirikishwa katika chaguzi za hapa nchini hususani Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Napenda kupata ufanuzi juu ya haya na ikizingatiwa wenzenetu hawa wamepata *exposure* ambayo

inawasaidia kuwa na upeo pamoja na uzoefu wa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie juu ya ujenzi wa Balozi zetu hasa nyumba za kuishi mabalozi wetu. Kwa sasa Mabalozi wengi wanaishi kwenye nyumba za kupanga ambazo ni ghali sana na hazina huduma kama maji ambapo inabidi zinunuliwe nje na bili inakuwa kubwa, pia inakuwa *too contested* na hazina hadhi za Kibalozi. Pia *replacement* za magari kwenye Balozi zetu mfano Balozi ya Rwanda gari tangu mwaka 2003 halijabadiilishwa hadi leo. Vilevile ucheleweshwaji wa fedha za matumizi ama za kuendesha Balozi hizi, inabidi ziwe zinapelekwa mapema. Mwisho ni malipo kidogo kwa watumishi ambayo inasababishwa na malipo kuwa ni kwa fedha ya Kitanzania ambayo ina-*fractuate* hivyo kushuka thamani.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono bajeti ya Serikali kwa asilimia mia kwa mia. Napenda nimpongeze Waziri na Naibu Waziri, pia nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara, watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuimarisha mahusiano mema kati yetu na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, kila penye mazuri hapakosi mabaya ambayo naiomba Serikali yangu ipokee kama

changamoto. Nitazungumzia mambo yafuatayo, ajira za Watanzania katika nchi za nje, wanafunzi wanaosoma nje na fursa zilizopo na visa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ajira za Watanzania waliopo nchi za nje ni chache sana na kama zipo ni kazi ndogondogo tu na hasa za nyumbani (usafi). Malipo yao ni madogo sana hata kama wanaelimu kubwa. Lakini kumekuwa na nafasi za kazi za Ualimu nchini Gabon. Gabon imeanza kufundisha kwa lugha ya Kiswahili lakini hatuoni juhudhi za Serikali kupitia taasisi yetu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupeleka Walimu. Naomba sasa Serikali yangu ifanye kila njia kuhakikisha fursa inapotokea tunaipata kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunapeleka wanafunzi wengi nje kwa ufadhili na wengine wa kujilipia. Wanafunzi hawa wanapata elimu bora ambayo wakiileta nyumbani itatusaidia kubadilika. Lakini sioni kama wanatambulika na kusaidika na pale tunapohitaji wataalam tuwatumie. Fursa za masomo zinatolewa katika nchi kama vile China lakini Serikali haipeleki wanafunzi, hatujui tatizo ni nini? Kama Serikali inashindwa kutokana na gharama si bora ingefanya utaratibu wa kuwasaidia Watanzania wenyewe moyo wa kufundisha wanafunzi nje kwa kuchangia gharama kuliko kuacha fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, visa imekuwa ni tatizo pale Mtanzania anapotokea kusafiri kwenda nje ya nchi na haswa Bara la Ulaya. Tunatambua matatizo

yanaweza kutokea lakini kuna matatizo sana ya kukosa visa kwa wakati na ukapata baada ya muda mrefu. Naomba Serikali yangu iangalie changamoto hizo na izifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme naunga mkono hoja hii, napenda yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka wa Tanzania na Malawi - Ziwa Nyasa. Mgogoro huu umekuwa na historia ndefu tangu enzi za *Heligoland* na sasa limeibuka upya kutokana na rasilimali ya gesi inayofanyiwa utafiti na Serikali ya Malawi hadi kuingilia upande wa Tanzania. Kigugumizi cha ucheleweshaji huu kinatoka wapi? Serikali tunahitaji itoe tamko la kina na lenye tija na ina mikakati gani katika suala hili, *peaceful negotiations? Shuttle diplomacy?*

Mheshimiwa Spika, sera yetu ya sasa mojawapo kuu ni Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi lakini ajabu *this is not effective*, kwa nini? *Commercial attaché* wetu kwenye Balozi zetu wanafanya nini? Tunahitaji wataalam wabunifu na wenyе sifa Watanzania ambao ni wengi tu ndio wakafanye shughuli hizo kuliko kung'ang'ania watumishi ambao hawako *creative and pro-active*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni *sovereign state* lakini ajabu Balozi nyingi ziko *based* Nairobi, EA na sio

Tanzania hali inayopelekea ukiritimba kwa Watanzania wanaotaka kusafiri kwenda kwenye nchi zao. Mfano, tuna Ubalozi wa Canada na Uingereza hapa nchini, lakini viza hadi uende Nairobi, ni kwa nini? Viza *fee* ya Uingereza ni Sh.230,000/= wakati sisi tunatoza Sh.50,000/= tu na nchi ambayo bado inaendelea lakini yenye vivutio vingi kwa nini? Kwa nini isifanye *lobbying*?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Balozi zetu nchi za nje zimechakaa sana na mishahara ya watumishi kutolipwa *timely*?

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maelezo ya kina na yenye tija juu ya suala la APRM na deni la \$800,000 kwa miaka nane, hii ni aibu kwa Taifa na *embarrassment* ambayo inafanya nchi isiwe na sauti wala ushawishi wowote katika vyombo vya Kimataifa. Madeni yote katika vyombo vya Kimataifa yalipwe kuendeleza diplomasia nzuri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waishio nje (*Diaspora*) wanashirikishwaje katika kuleta maendeleo nchini kama kulipa kodi, pesa zizunguke nchini kwetu, upigaji kura na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Tanzania hadi leo inashindwa kuwa na Ubalozi angalau mdogo pale Tel Aviv, Israel, nchi/Taifa kubwa na lenye teknolojia ya hali ya juu na mbona tuna balozi Palestina, Libya na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja yafanyiwe kazi niliyo-*raise* na nipate majibu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka wa Tanzania na Malawi – Ziwa Nyasa. Suala la utata wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi ni la siku nyingi sana, nachelea kusema kama hatua za dharura hazitachukuliwa yaani mazungumzo ya dhati kati ya nchi hizi mbili kunaweza kutokea vita kati ya nchi hizi mbili. Matamko yanayofanywa na viongozi wa Malawi siyo afya sana kuhusu mpaka halisi wa nchi mbili hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia haliingii akilini kwa viongozi wa Malawi kutamka kwamba maji yote ya Ziwa Nyasa na kama wao wanavyoita Ziwa Malawi ni ya kwao. Narudia kushauri kwamba Serikali yetu ihakikishe inafanya mazungumzo na Serikali ya Malawi ili kufikia muafaka kuhusu mpaka. Aidha, wananchi wetu hasa wa Mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Iringa wafahamishwe maendeleo ya mazungumzo hayo ili waendelee na shughuli zao kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu nje ya nchi. Balozi zetu nje ya nchi hazipewi pesa za kutosha. Hali hii inazifanya Balozi hizo zishindwe kufanya kazi vizuri. Nashauri pesa zaidi ziongezwe kwa ofisi zetu nje ya nchi. naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Bernard K. Membe, Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2012/2013 aliyoisoma kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pili naipongeza Wizara kwa hatua kubwa tuliyopiga katika kuendeleza lugha ya Kiswahili Kimataifa. Taarifa za kwamba kituo cha kufundishia lugha ya Kiswahili cha Kamisheni ya Umoja wa Afrika kilichopo Addis Ababa kinakabiliwa na uhaba wa Walimu na fedha za kuendeshea kituo hicho, ni za kuhuzunisha kwani tunawajibu kama Taifa na kitovu cha Kiswahili kuhakikisha kuwa Walimu wapo na fedha ya kutosha inapatikana. Hili si suala la mjadala, tutafute hao Walimu na hizo fedha tuanze sisi kuonyesha njia wenzetu watatuunga mkono baadaye.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara vilevile kwa wazo la kuanzisha kituo cha Utamaduni cha Kitanzania jijini Addis Ababa chenye lengo la kukuza Kiswahili kwa jamii ya wanadiplomasia na watumishi wa *AU*, jijini Addis Ababa. Naiomba Wizara ihakikishe kituo hiki muhimu kinaanzishwa rasmi na fedha inatafutwa mara moja ili wazo hili lisibakie kwenye karatasi.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuunga mkono hoja.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na

watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kuiweka nchi yetu katika ramani ya dunia. Pamoja na pongezi hizo, naomba kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, amani na utulivu. Nchi yetu inasifika duniani kwa amani iliyojijengea kutokana na busara ya viongozi waasisi wa nchi hii. Lakini hili suala la udini limeanza kujitokeza na hivyo kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu. Je, Serikali inalichukuliaje suala hilo?

Mheshimiwa Spika, pili, Diplomasia ya Kiuchumi. Nchi yetu inahitaji maendeleo ya kiuchumi zaidi kwa sasa kuliko maendeleo ya kisiasa. Hivyo Mabalozi wetu nchi za nje wanatakiwa walione hili ni kipaumbele cha kwanza. Suala la msingi hapa ni kwa kiasi gani Mabalozi wetu wana uwezo wa kutekeleza hili?

Mheshimiwa Spika, tatu, nafasi za ajira. Ni muhimu ajira za watendaji katika taasisi mbalimbali za Kimataifa kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ziwe na uwiano. Naomba Serikali ieleze kwa sasa uwiano huo uko vipi. Wakati huohuo Serikali inatutaka tuchangamkie ajira zilizoko nchini Qatar, hili ni jambo zuri lakini suala hili limekuwa likifanyika kwa muda mferu kimyakimya. Je, Serikali itaweka utaratibu gani ili nafasi za kazi kutokea nchi mbali ziwe wazi kwa kila mwenye sifa na uwezo aweze kupata?

Mheshimiwa Spika, nne, mradi wa kuongeza eneo la bahari nje ya Ukanda wa Kiuchumi (*EEZ*). Mradi huu uliletta sintofahamu kwa upande wa Tanzania Zanzibar

kwamba jambo hili lilitanywa bila ya ushiriki wa Zanzibar na kwamba lengo ni kuchukua ardhi ya Zanzibar. Kwa kuwa jambo hili lilitandiliwa katika Baraza la Wawakilishi kuitia hoja iliyolewa na Mheshimiwa Jussa, naomba Serikali ilitolee ufanuzi jambo hili ili Watanzania waelewe ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tano, suala la mipaka kati ya Tanzania na nchi nyingine. Lazima tukiri kuwa nchi haikufanya juhudini za mapema kuona kuwa mipaka yetu iko salama kwenye maziwa, mito, bahari na nchi kavu pia. Jambo hili linafanya pia watu kutoka nchi jirani waingie Tanzania wapendavyo na mara nyingine kudai kuwa ni sehemu yao. Tatizo la mpaka wa Ziwa Nyasa liangaliwe kwa hekima kubwa ili nchi isiingie vitani.

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kabla sijasahau, nianze kwa kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Kwanza kabisa, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri na Watumishi wa Wizara hii kwa bajeti nzuri walijotuletea mwaka huu. Lakini pia niwapongeze kwa kazi nzuri wanazozifanya hapa Makao Makuu na huko nje kwenye Balozi mbalimbali

pamoja na hali ngumu ambayo inawakabili katika Balozi hizo.

Pili, niseme mchango wangu utajikita kwenye jambo ambalo nilishawahidi kulizungumza hapa mwaka 2011 tarehe 5 Julai, majira kama haya wakati nikihitimisha bajeti ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora, suala la rada. Hili limezungumzwa leo pia na limechangiwa na wachangiaji wengi tu. Waheshimiwa Wabunge wamelichangia jambo hili.

Nilipolizungumza wakati ule, nilidhani nimezungumza nikalimaliza, maana niliwataja watuhumiwa wa rada, niliwataja Waingereza watatu wa *BAE* na nikaeleza waziwazi kwamba, uchunguzi uliofanywa na *Serious Fraud Office* hapa Tanzania ambao walishirikiana na TAKUKURU walisema wazi kabisa kwamba hawaoni ushahidi wowote unaoweza kumuunganisha mtu yejote hapa Tanzania na tuhuma za rushwa. Sasa kule Uingereza wakatazama pia wakakubaliana nje ya Mahakama, lakini baadaye wakaingia Mahakamani wakakubaliana vipengele 10. Katika vipengele vyote hivyo 10 rushwa haikuwemo.

Mheshimiwa Spika, sasa labda niseme vichache, nikupeni taarifa kwanini na sisi hapa tunashindwa kufanya lolote kuhusu jambo hili. Maana kosa la rushwa lina mtoaji na mpokeaji. Katika hili, tungesema labda waliotoa rushwa ni Waingereza, lakini Waingereza wanasema kwao hakuna.

Syo hivyo tu, wakaweka na mkataba kabisa, Serikali ile ikakubali mkataba na ukaenda Mahakamani

ukasajiliwa kama mkataba. Katika mkataba ule, walisema vitu vifuatavyo, nitavisoma vitatu, vinne ambavyo naviona ni muhimu. Kipengele cha sita katika mkataba wao kinasema hivi: "*The Serious Fraud Office (SFO) shall not prosecute any person in relation to conduct other than conduct connected with Czech Republic or Hungary.*"

Kwa hiyo, kwa Tanzania na Saudi Arabia sisi tunasema hawawezi, *other than Czech na Hungary*. Kule wanaweza, lakini Tanzania na nchi nzingine hawawezi.

Kipengele cha saba walikubaliana: "*The SFO shall forthwith (yaani mara moja) terminate all investigations into the BAE systems group.*" Walikubaliana.

Wakakubaliana tena: "*There shall be no further investigation or prosecution of any member of the BAE systems group for the conduct preceding of the 5th of February, 2010 (yaani kabla ya kipindi kile ambacho vitendo hivi vilifanyika).*

Mheshimiwa Spika, la muhimu zaidi ambalo na sisi linatuwia gumu, wanasema: "*No member of the BAE systems group shall be named as or alleged to be (yaani hata ile kumtaja tu) as an inducted co conspirator or in any other capacity in any prosecution of the FSO may bring against any other person.*"

Mheshimiwa Spika, sasa nasema katika hali kama hii tukichukua hapa tukamkamata mtu yejote tukaenda naye Mahakamani, mashahidi

tunaotegemea sisi wanetoka upande ule wa *BAE*, *SFO*, maana huku hakuna mashahidi, lakini kule wameshajifunga wakasema hakuna, kule hata kumtaja hairuhusiwi, wacha kumshitaki au kumwita na Serikali hii iliyoingia mkataba na hawa, hata mkiwaambia tunataka kumwita fulani huko, mleteni hapa watakataa, hawataweza kufanya hivyo kwa sababu waliingia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, nililisema hili mwaka 2011 tarehe 5 mwezi wa Saba hapa ndani ya Bunge lako, nikadhani jambo hilo limekwisha, lakini inaonekana bado linajirudia. Wananchi hawajalielewa vizuri. Jamani hakuna kesi ya rushwa dhidi ya mtu ye yote hapa Tanzania kuhusu sakata la rada? Hakuna! Nikaomba hapa, mara ya mwisho nilisema kama kuna mtu ye yote ndani ya Bunge au nje ya Bunge hili mwenye ushahidi wowote *independent* aulete, sisi tutam-*prosecute* huyo ambaye wanaleta ushahidi dhidi yake. Maneno maneno Mahakamani hakuna. Mahakamani ni ushahidi.

Nikaambiwa kuna kitabu kimeandikwa, hiki hapa na mimi nimekisoma sana. Nimekisoma kitabu hiki na kwa wale wallotajwa kwenye kitabu hiki ningekuwa ndiyo *counselor* wao ningewashauri kum-*prosecute* huyu Bwana. Huyu bwana misingi ya kitabu chake ni magazeti. Anasema fulani fulani, mwizi ana-*quote This Day*; fulani fulani, mwizi ana-*quote The Guardian*. Yaani wewe ni mwandishi *serious* unakwenda ku-*quote* magazeti ndiyo unasema hawa ndiyo watu wanaothibitisha kwamba kuna rushwa! (*Makofi*)

Kwa hiyo, nasema kitabu hiki kipo kweli, lakini siyo kitabu, siyo lolote! Kama kuna mtu aliyetajwa humu ambaye anadhani kweli anahitaji ushauri wangu wa kisheria ningemwambia tuwachukue (tuwapeleke) Mahakamani walioandika kitabu hiki na nina hakika tutashinda kwa sababu hakina msingi, hakijafanyiwa utafiti. Hakuna kitu ambacho huyu bwana anakijua kuhusu sakata hili *other than* alisoma gazeti fulani na anayasema magazeti aliyoyasoma. Anasema nilisoma hapa, waliandika hivi, kwa hiyo, ni hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema, hakuna mtu mwenye ushahidi. Lakini bado nasema kwamba natoa *challenge*, tena tunataka tulifikishe jambo hili mwisho. Kama yuko mtu Tanzania ama nje ya Tanzania mwenye ushahidi madhubuti (*independent*) kwamba kuna mtu Mtanzania ye yote amehusika na jambo hili atuletee. Sisi kama Serikali tungependa kuji-*clear* tumpaleke huyo mtu Mahakamani na ushahidi madhubuti.

Nimeongea na *DPP* leo, nikamwuliza una *anything new* nataka kwenda kuongea? Akasema sina! Nikamwuliza Hoseah, una *anything new* kwenye uchunguzi wenu? Akasema na wala uchunguzi hatufanyi kwa sababu hakuna kitu.

Kwa hiyo, *please* naomba jambo hili tufike mwisho, hakuna rushwa katika sakata la rada ambalo linawahu su Watanzania. Nami nasema kama mtu anao anaowajua atwambie, lakini asitwambie maneno, asitulee vitabu hivi, atulee ushahidi *concrete* kwamba huyu mtu aliingia kwenye rushwa

tuna *tape*, tuna picha tulimwona, tulikuwa naye, asituletee mambo ya kwamba nilisoma gazeti, hatutakwenda Mahakamani kwa misingi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka tulifikishe hili jambo mwisho. Nilisema nitasimama nichangie maneno haya. Niliyasema, mtu akitaka kurejea *Hansard* ya tarehe 5 mwezi wa Saba, mwaka 2011, niliyasema vizuri na leo nimeyasema tena.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa hayo, naomba kuchangia hoja hii kwa kuiunga mkono sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Ameipa sifa sana nchi yetu huko nje na anaendelea kufanya hivyo. Namtakia kila la heri ndugu yangu aendelee vizuri. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Tutakupa dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyoendelea kuionesha kwangu kwa kunteua tena kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii.

Pia nichukue tena fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Mohammed Gharib Bilali kwa kuendelea kulijengea heshima Taifa letu kote duniani kwa namna wanavyoliongoza vyema Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru kipekee Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa msaada wake mkubwa na wa dhati kwangu kwa kunionongoza na kunielekeza vyema ili kufanya kazi zangu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake mahiri ndani na nje ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kukupongeza sana wewe mwenyewe pamoja na Naibu wako kwa namna mnavyoliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Pongezi hizi pia ziwaendee Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Nawaombea kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wananchi wenzangu na wapiga kura wangu wa Jimbo la Muyuni kwa imani waliyonayo kwangu na ushirikiano mkubwa wanaonipa Mbunge wao katika kutekeleza majukumu yangu. Nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao katika kuliletea Jimbo letu maendeleo. Kwa pamoja, tutaendelea kuliinua kimaendeleo Jimbo letu la Muyuni.

Mheshimiwa Spika, vilevile shukrani za dhati ziende kwa Watendaji wa Wizara hususan Katibu Mkuu - Ndugu John Haule, Naibu Katibu Mkuu - Balozi Rajab Gamaha, Wakurugenzi, Mabalozi, Wasaidizi wangu pamoja na wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mwisho, napenda kuishukuru sana familia yangu kwa uvumulivu wao kwangu na namna wanavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa wananchi wote wa Jimbo langu la Muyuni, Wazanzibari pamoja na Watanzania kwa ujumla kutokana na msiba uliosababishwa na kuzama kwa meli ya MV. Skagit. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira waliopoteza ndugu zao, awape uzima wa haraka waliojeruhiwa na awalaze Peponi waliopoteza maisha kwenye mkasa huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni dhahiri kwamba michango yao itatusaidia sana katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi na utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ambalo wachangiaji wengi wameligusia ni jinsi Wizara yetu inavyotekeleza au inavyostahili kutekeleza diplomasia ya uchumi. Wengi wamezungumzia na kupongeza shughuli ambazo Wizara yangu imekuwa ikizifanya, lakini pia wamebainisha baadhi ya maeneo ambayo wanahisi yakifanyiwa kazi yatasaidia zaidi, ikiwa ni pamoja na kuzidi kuvipigia debe au kuvinadi vivutio vilivyopo nchini, kuwahamasisha wawekezaji waweze kuja nchini kuwekeza lakini pia na kutafuta masoko kwa bidhaa zetu huko nje.

Waheshimiwa Wabunge, mbalimbali wametambua pia kazi kubwa inayofanywa na Mabalozi na Watendaji katika Balozi zetu huko nje katika kufanikisha diplomasia ya uchumi. Baadhi ya Waheshimiwa ambao wamegusia maeneo hayo ya diplomasia ya uchumi ni pamoja na Mheshimiwa Seleman S. Jafo, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Eng. Athumanu R. Mfutakamba, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis,

Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse na Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage. (*Makof*)

Waheshimiwa wote hawa wamefafanua mambo mbalimbali ambayo wanataka au wanashauri yafanyiwe kazi. Mojawapo ya mchango uliotolewa na Wabunge kadhaa wamesema tuongeze umakini wa watumishi wetu katika Balozi hizo na wengine wameeleza kwamba, kuna ufinyu wa wafanyakazi katika Balozi mbalimbali na wataalam katika diplomasia hii ya uchumi. Tumeyachukua mawazo hayo.

Pia kuna waliofafanua kwamba kuna tatizo kubwa la kuweza kutekeleza diplomasia ya uchumi ambalo ni kukosa nyenzo na raslimali, jambo ambalo tunalikubali na tatizo hili la ukosefu wa raslimali litakuja kutolewa ufanuzi mzuri zaidi na Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kujibu hoja.

Sehemu ya pili ambayo iligusiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ilikuwa ni juu ya umuhimu wa kuwathamini na kuwatumia Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*diaspora*) na pia suala la uraia wa nchi mbili. Baadhi ya Waheshimiwa waliozungumzia suala hili ni pamoja na Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Beatrice M. Shelukindo, Mheshimiwa

Martha M. Mlata na Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu. Hawa nao wote wamegusia umuhimu wa kutambua michango ya Watanzania walioko nje na pia kuwahamasisha waweze kuleta utaalam nyumbani na pia kuja kuwekeza nyumbani.

Mheshimiwa Spika, labda mchango ambao ulikuwa wa kipekee kwenye eneo hili ni wa Mheshimiwa Esther N. Matiko ambaye alisema kwamba, kuna umuhimu wa kuwa na Watanzania wanaoishi nje ambao ni wataalam na sio wabeba makasha (*boxes*) kwa lugha yake. Hatua hii ni kweli na tunachukua juhudni mbalimbali hasa katika kitengo chetu cha *diaspora* za kuweza kutafuta fursa za kitaalam nje na kuweza kuziweka wazi au kuzitangaza hapa nchini ili Watanzania wenye sifa waweze kuchukua nafasi hizo na tuweze kuwa na wataalam ambao wako huko nje na watasaidia kutumia utaalam wao lakini pia kuongeza utaalam na kuuleta hapa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, pia michango ya Waheshimiwa Wabunge kadhaa ilielezea kuwepo kwa malalamiko ya wanafunzi wa Tanzania kukosa ushirikiano kutoka Balozi zetu na wengine pia walizungumzia umuhimu wa Wizara yetu kuendelea kutafuta fursa za ufadhili wa masomo kwa Watanzania huko nchi za nje. Waheshimiwa waliozungumzia hili ni pamoja na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Rebecca Mngodo na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa Balozi zetu zimekuwa zikijitahidi kuwa karibu na Watanzania wote wanaoishi nje, lakini jitihada hizo lazima zionekane kwa pande mbili. Ni lazima na Watanzania wenyewe watambue na kuthamini Balozi zetu pale ambapo zipo. Milango ya Balozi zetu iko wazi kwa Watanzania na kwa hiyo, lazima Mabalozi wetu wapate ushirikiano kutoka kwa Watanzania wote wanaoishi huko nje wakiwemo wanafunzi. Sidhani kama kuna ukweli kwamba, Mabalozi wetu wamekuwa wakiwabagua wanafunzi walioko nje. Isipokuwa kuna mchango wa Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli ambaye alitaka Balozi zetu labda ziweze kuwasaidia wanafunzi wanapokuwa na shida za kifedha.

Mheshimiwa Spika, hilo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wameelezea hali ya kifedha hata kwa zile shughuli muhimu siyo nzuri. Hivyo siyo rahisi kuweza kuwa na fedha sasa za kuwashudumia kwa kuwapatia Watanzania wanapokuwa nje, isipokuwa hali inapojitokeza na tukawa na matatizo makubwa, licha ya matatizo yetu ya kifedha, tumeweza kutafuta raslimali za kuwasaidia Watanzania walioko nje ya nchi kama vile yalivyotokea matatizo Libya na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, kuna mchango pia ambao ulizungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kuhusiana na tatizo la mpaka baina ya Tanzania na Malawi. Waheshimiwa Wabunge walizungumzia kuhusu umuhimu wa tatizo hili kutafutiwa usuluhishi mapema iwezekanavyo. Wengine walipongeza hatua ya Mheshimiwa Waziri kutoa ufanuzi na kutoa kauli ya

Wizara leo hii katika Bunge hili. Wengi wamezungumzia umuhimu wa kuendelea kuwa na diplomasia, lakini bado suluhisho hilo lipatikane haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alizungumza wakati anasoma hotuba yake, bado tunaipa na tungependa tuipe diplomasia nafasi wakati huo huo tukijali na kuthamini Watanzania walioko katika maeneo hayo na tukionesha nia yetu ya kuendelea kuwatetea Watanzania na kulinda mipaka yetu. Tutaendelea na diplomasia na kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna uwezekano majadiliano yasipofikia suluhisho, tukahitaji kutatua tatizo hili kwa njia ya kisheria kwa aidha kutumia msuluhishi au Mahakama kama wenzetu watashindwa kutuelewa. Kwa hiyo, bado diplomasia tunaipa nafasi katika hili lakini tukiwa na nia thabiti ya kulimaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wachache kidogo wakiwemo Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Abuu H. Jumaa na Mheshimiwa Felix F. Mkosamali ambao walipongeza hatua ya Wizara kukuza Kiswahili na kuanzisha mafunzo Mjini Addis Ababa. Wakaomba hatua hizo zichukuliwe kwingineko na pia kuwe na raslimali za kutosha kuweza kukikuza Kiswahili na kukifundisha huko nchi za nje. Hili tunalichukua.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limezunguzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi la hali mbaya ya kifedha katika Wizara ambalo kama

nilivyoeleza hapo awali, Mheshimiwa Waziri atakuja kulitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.
(Makofi)

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Waziri, atapewa dakika zake 40. Mheshimiwa Mtoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Edward Lowassa - Mwenyekiti kwa hotuba nzuri ambayo imeonyesha matatizo ya Wizara na kupendekeza namna ya kuyatatua baada ya ziara zao nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuipongeza Kambi ya Upinzani kwa hotuba yao iliyowasilishwa hapa Bungeni na Waziri mwenzangu kivuli, Mheshimiwa Ezekia Wenje - Mbunge wa Jimbo la Nyamagana. Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi na kwa kuzungumza. Michango yenu kwa hakika ni uchambuzi mkubwa ambayo kwa kiasi kikubwa imewezesha na itawezesha Wizara yangu kujua maeneo yanayohitaji kufanya kazi maeneo ya kipaumbele ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala huu wa Wizara yangu ambao Bunge lako Tukufu linatarajia kuuhibitisha leo ulichangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 79.

Kati ya hao, 13 wamechangia kwa kuzungumza na 66 wamechangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niwataje wachangiaji wote kwa majina. Waliochangia kwa kuzungumza ni hao wafuatao: Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa John S. Magalle, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe na Mheshimiwa Mahadhi J. Maalim - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuandika ni hawa Wafuatao: Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Athumani R. Mfutakamba, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Selemani S. Jafo, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Tauhida C. G. Nyimbo, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa DKT. Hamisi A. Kigwangalla, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Magadalena H. Sakaya, Mheshimiwa Margareth S. Sitta, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa Zaynabu M. Vullu. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Abuu H. Jumaa, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Rukia K. Ahmed, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa January Y. Makamba, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Saleh A. Pamba, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa, Charles J. P. Mwijage, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu,

Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Mwigulu N. Madelu, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Maryam S. Msabaha, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Said M. Mtanda, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla na Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa. Kama kuna niliowaacha, wanilettee majina, nitawatambua rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kusema kwamba matatizo yote yanayoikabili Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataita msingi wake mkubwa ni ufinyu wa bajeti. Kwa kweli nashukuru sana kwa jambo hili, kwa mara ya kwanza katika historia ya Bunge kuja kuchangiwa na Wabunge wote asilimia 80 ya Wabunge wote ukijumuisha kwa ujumla wake wamezungumzia suala la ufinyu bajeti.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 fedha zote tulizopata Shilingi bilioni 76 zile zilikuwa sawa na asilimia 44 ya mahitaji ya Wizara ya Mambo ya Nje. Jiulize unapata asilimia 44 kati ya 100 unakosa asilimia 56, unategemea nini? Kwa hiyo, tumekuwa *victims* kwa kupata bajeti ya asilimia 44 na leo ninaomba Shilingi bilioni 98.

Waheshimiwa Wabunge, Shilingi bilioni 98 mtakazonipa leo ni sawa na asilimia 42 ya mahitaji yote ya Wizara ya Mambo ya Nje. Utadhani kuna shetani mahali ambaye lengo lake ni kuhujumu siyo tu Wizara, lakini kwa kweli utendaji kazi mzuri wa wenzetu walioko nje. Inanitia huruma kama Waziri wa Mambo ya Nje kupokea asilimia 42.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie kwamba sasa mahitaji ya kweli ya Wizara ya Mambo ya Nje, kwa upande wa *Other Charges* tukitaka kulipia watoto wetu shule, tukitaka kulipia pango zetu za nyumba katika kipindi hiki cha mwaka 2012/2013, tukitaka kukarabati majengo mliyoyasema, tukitaka kuwanusuru baadhi ya Mabalizi wasiangukiwe na zile gari mlizozisema, tunahitaji nyongeza ya Shilingi bilioni 75, kama mnataka nifike mwakani hapa kwa uzima na kwa kutamba kwamba nimeweza kufanya kitu. Vinginevyo tutategemea muujiza na hiyo ni *Other Charges*. Nitahitaji Shilingi bilioni 61 za maendeleo kwa nyongeza ya hizi ambazo tumezipata leo, kama tunataka kuiweka Wizara yetu katika hali nzuri ya kuheshimika duniani.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninarudia kwamba, asilimia 42 kama ningempata mtu mwenye muujiza wa kuiendesha Wizara kwa kiwango hicho, kesho ningeweza kujiuzulu achukue nafasi. Haiwezekani kwa mazingira ya kibinadamu ku-*operate* kwa asilimia 42. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze kwamba, mwaka 2011 tulipokuwa tunalilia hili suala tulipata *support* ya Kamati ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nilipata *support* ya *Cabinet* na Mheshimiwa Rais, alitamka na kuitaka Wizara yetu ya Fedha kwamba jamani kwa kesi ya Wizara ya Mambo ya Nje, hatuna ujanja wa kupunguza fedha zozote kwa sababu yote hayo ni *contractural obligations*, nilipata *support* zote. Tukaishia kupata asilimia 44. Nashukuru na niliwaambia Mabalozi muwe wa wazi na wa kweli kwa Wajumbe wote na kila Mbunge bila kujali anatoka Chama gani, waambieni ukweli. Kutokana na ukweli huo, labda tutasaidiwa. Nazungumza kwa uchungu, hatuwezi kuendesha Balozi zetu za nje kwa asilimia 42. Tutakuzaje Diplomasia ya uchumi? Diplomasia ya uchumi haiwezi kuja kwa asilimia 42.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa niseme tena kwamba ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwamba mmeliona na mimi naomba msaada wenu katika Kamati zetu msichoke kutusemea ili tuweze kupata nyongeza tunahitaji kuipata.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme tena kwamba sisi Wizara tunafanya nini baada ya kuona matatizo haya? Naomba niseme kwamba ubunifu na mambo ambayo tunabuni kufanya Wizara ili mtusaidie. La kwanza, tumeamua kupata vitega uchumi nje, na wengi mmezungumzia masuala ya Ubalozi wa Washington ambao tumenunua jengo mwaka 2008/2009 na tuna jengo pale 21, 38 L street Washington na jengo lile limechakaa, linahitaji Dola milioni moja na nusu ili kukarabati ili tuweze

kulipangisha na ili tupate fedha. Lakini tunalo tatizo. Tatizo tulilonalo Washington ni la mfumo wa fedha. Kama dada yangu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo alivyolizungumza na tatizo lenyewe ni rahisi kulielewa. Tuna *choice* mbili.

Choice ya kwanza ni kukubali Kampuni moja ya Marekani ifanye Mkataba na Ubalozi wetu ili walikarabati jengo lile kwa Dola milioni moja na nusu, lakini baadaye wajilipe wenyewe kwanza. Tukimaliza deni lao, ndipo sisi tuanze kufaidika. Hiyo ni *first choice*.

Choice ya pili tuliyonayo ni Wizara ya Fedha na mfumo wetu wa fedha hapa nchini waturuhusu Wizara ya Mambo ya Nje kutumia majengo tuliyonayo Washington kuombea mkopo pale pale Washington kwa sababu ni majengo yenye thamani. Jengo letu tunalokaa sasa, lina thamani ya Dola milioni nane.

Naweza kwenda benki kesho nikipata vibali na kurekebisha mfumo wa fedha zetu. Namshukuru sana Mheshimiwa John Cheyo ameliona hili na ameona umuhimu, na ninamshukuru pia CAG Utouh ameona umuhimu wa kufanya marekebiso ya kimahesabu na ya kifedha katika Serikali ili kuiruhusu Wizara yangu yenye majengo mengi duniani ili majengo yale tuyatumie ku-*mortgage* kupata fedha ili tuweze kujenga majengo na kuyakarabati ili tuwapangishe watu tutokane na fedheha hii tunayoipata humu ndani ya kuomba omba na tunaishia kupata asilimia 42. Niunge mkono kwa hilo tu. Tatizo siyo Wizara ya Mambo ya Nje, tatizo ni msimamo na mfumo wa fedha tulionao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wataruhusu leo kunipa *exception* kama tulivyoitoa kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama kwamba Wizara ya Mambo ya Nje, tuiruhusu kuchukua mikopo nje. Tukiruhusu kupata mikopo kutokana na nyumba walizonazo, mkinipa kibali hicho na mfumo huu ukabadilika, mwakani tutakuja hapa tukitamba kwamba tunazo fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, naomba niseme kwamba hali ya Balozi imekuwa mbaya kutoka huko, ni Wizara yangu sikumbuki Wizara nyingine. Lakini Wizara yangu ilikuwa Wizara pekee ambayo haikuwa inapata *Development Budget* mpaka mwaka 2007 hatukuwa tunapata sisi bajeti ya maendeleo.

Kwa hiyo, tulikuwa tunanunua majengo, tunashindwa kuyakarabati. Siwezi kuyakarabati kwa kutumia mishahara ya wafanyakazi. Mwaka 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 ndipo tulipopata *development budget* mliidhinisha Shilingi bilioni 41.5 mwaka 2008/2009 nikaishia kupata Shilingi bilioni 24. Mliidhinisha Shilingi bilioni 44.5 mwaka 2010/2011 nikaishia kupata Shilingi billioni 26. Mliidhinisha billioni 44.5 mwaka 2011/2012 kufika sasa zikapunguza mpaka nikapata Shilingi bilioni 26. Tena, mwaka huu napata Shilingi bilioni 16, nitanunuaje jengo la Paris kuondoa fedheha ya Ubalozi wetu kupangishwa kwenye Ubalozi wa Uganda?

Mheshimiwa Spika, nitapata wapi fedha za kukarabati majengo yote kama *development budget*

mnayoidhinisha hapa nikienda kule napata robo? Kwa hiyo, tunachokisema hapa ni nini? Tunachokisema hapa ni kwamba sisi *Foreign Affairs* tumeanza miaka minne tu kupata *development budget*. *It will take time!* Itachukua muda kutuwezesha kutatua matatizo mengi yaliyopo kwenye Balozi zetu na ndiyo maana nimependekeza kwamba tatizo kubwa hili limekuja baada ya kufuta *Visa*.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wa *critical* wanasema, hapana. Ni utaratibu mzuri, lakini nataka niwaambie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge utaratibu wa kuondoa *Visa* wa kuwaambia watalii na wageni wote wanaokuja Tanzania kuja kuchukulia *Visa* nchini una hasara mbili. Moja yangu na moja ya usalama. Ya kwangu ni kwamba, tunakosa maduhuli ya kuendesha Balozi zetu ambazo sasa watu wanashindwa kujilipa mishahara.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa usalama wa Taifa ni kwamba Uwanja wa Kimataifa wa Dar es Salaam hauwezi kuwa chujio la kumchunja nani *criminal*, nani mzuri pale *as long as wame-line* kwenye mstari ule, *as long as wame-line* ku-exist ni vigumu kupata vyombo vyote vya kufanya kazi na kuweza kuwarejesha wengine wasiofaa nje kule. Balozi zetu ni chujio linaloweza kujua nani aingie nchini na nani asiingie nchini. Silazimishi kama mnadhani ni utaratibu mzuri kuchukulia *Visa* hapa hapa Dar es Salaam, *fine*. Lakini sisi inatukosesha fedha, lakini *it is a risk at masuala* ya usalama wa Taifa. Hayo ndiyo maelezo ya bajeti katika *Economic Diplomacy*.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Shibuda na wengine wengi wamelizungumzia suala la *Economic Diplomacy*. Leo kwa mara ya kwanza nimeyatoa maeneo nane tuliyoyatekeleza pamoja na ufinyu wa bajeti yetu. Lakini naomba nikubali kwamba moja ya matatizo tuliyonayo nchini ni *Inter-ministerial linkage*, *De-economical Diplomacy* haifanywi na *Foreign Ministry* peke yake lazima Wizara zote za Kiuchumi, Kilimo, Viwanda na Biashara, Utalii na Wizara zote ambazo zinahusika na uchumi ni lazima zihangaikie kuleta watu wake sasa. Tuna majengo mazuri, kuleta watu wake kwenye Balozi zetu na kusaidia kukuza na kudumisha *Economic Diplomacy*. Sisi ni *Coordinators*, lakini tunahitaji *input* kutoka kwa Dar es Salaam *Chambers of Commerce* kutoka kwa Tanzania *Investment Centre* na tunawaandikia Wizara zote za kiuchumi, sisi ndiyo tuna *form a hub pale*, ndiyo tunafika. Kwa hiyo, masuala ya Pamba, masuala ya Kilimo, masuala ya madini na kila kitu ni *Inter-ministerial*.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama nimewaelewa vizuri, kinachohitajika sasa hapa ni *coodination* ya Wizara zote ku-*coodinate* na Wizara ya Mambo ya Nje ili tuweze kuwapatia nyenzo Mabalozi ili ku-*promote* hiyo, kitu kinaitwa *Economic Diplomacy, is not a one Ministry responsibility*. Sisi ni *Coordinators* tu.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Wizara nyingine tusaidiane ili kwa pamoja Wizara zote zituletee *opportunities* zote ambazo wageni kule nje watapenda kuzipata, watuletee mambo yote ambayo wanataka tuya-*promote* kule ili tuweze kuyasaidia.

Mheshimiwa Spika, sasa zipo hoja ambazo ningeweza kuzipitia kwa haraka haraka tu za Waheshimiwa Wabunge, na nyingine tutazijibu kwa utaratibu mwingine wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja hapa ya Mheshimiwa Ezekia Wenje katika ukurasa wake wa nne na wa tano ametoa pale mazungumzo yaliyofanyika na gazeti la *the Guardian* na kwamba katika mazungumzo yale Tanzania imelaumiwa kweli.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda kwenye *Google* kujaribu ku-*google* ndiyo nilipo-*google* Jamii Forum nimekuta kila kitu kipo pale. Nimekwenda *deep* zaidi nikagundua kwamba kilichofanyika kumbe Richard Bruceweek na Linda Croucher hawa walikuwa *wana-react* kwa Mkutano ambao Mheshimiwa Rais alikwenda Davos. Sasa kwenye ule Mkutano, *the Guardian* iliandika *topics* nzuri sana wakieleza kila Mheshimiwa Rais alichokisema, *then zikafika reaction* katika zile. Sasa Bruceweek pamoja na Linda wakazitoa na *zika-reflected* kwenye Jamii Forum. Nina hakika kama siyo yeye aliyempa taarifa hizi amezichukua pale aka-*access* kwa Linda Croucher na aka-*access* kwa Bruceweek, inakuwa ngumu sana. Kila uki-*google* pale unapata Jamii Forum. *So, ni reaction* za watu hao nisiowajua na ole wao ningewajua au ningewatambua!

Mheshimiwa Spika, hawa ndio walioweka maneno yale ya kupambapamba na kutusemasema na mimi siwezi kuchukulia kama ni *authority* ya Uingereza au *out the guardian*. Someni *the guardian*, imetoa

presentation nzuri sana. Kwa hiyo, nilitaka niseme hivi, picha iliyotokea hapa ni kana kwamba *the guardian* imezungumza vile. *The guardian* imetoa *topic* nzuri sana. Lakini Jamii *Forum* ilichoniudhi kwa kuwatumia watu hawa wawili mmoja anaitwa Linda Croucher na Bruceweek na Waziri mwenzangu ukayachukua ukayaleta hapa kwangu, nasema tena nitajibu kwa njia ile ile kama akina Bruce na Linda Croucher walivyoyafanya. Wamemsingizia Rais wangu, alifanya kazi moja nzuri sana Davols alipokwenda katika *economic forum*.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine hili la Mheshimiwa Mnyaa. Mheshimiwa Mnyaa ameniletea jambo *very serious* ambalo ningeweza kulisema. Wewe ni mwenzangu na wewe ni ndugu yangu, malalamiko ya Maafisa wanne walioretwa Makao Makuu yangu kutoka Zanzibar na ambao hawakuweza kuwa *promoted* au kupata nafasi nzuri katika sehemu ile. Suala hili nimelichukua, nimelipeleka kwenye Menejimenti, Menejimenti ikaniambia ilianza kulishughulikia suala hili, nimeagiza Menejimenti kwa kipindi kifupi sana tufanye marekebisho kwa hawa watu. Lakini nimegundua kwamba sio hawa peke yao, hata wenzetu wengine wa Bara wanaoingia Wizarani kutoka kwenye Mashirika na sehemu nyingine kuna ule mfumo wenyewe wa kuwa-*integrate* hawa na kujaribu kuwapa vyeo wakati mmoja, wanapofika pale inakuwa matatizo.

Kwa hiyo, nimejumuisha Wazanzibar na wale wote ambao hawajapata *promotion* zao na ambao hawajapata stahili zao kwa haraka sana, Wizara ya

Mambo ya Nje, ikishirikiana na Utumishi walimalize tatizo hili. Mheshimiwa Mnyaa ulinipa barua nikasema umenikamata pabaya. Naomba uniletee shilingi yangu usiikamate ili tuweze kushughulikia suala hili. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia lipo suala la *Honorary Consular's* wengine huko duniani kuandika *visa* bila ya kutumia *stickers* ambazo huwezi uka-forge. Wanatumia tu kwa mkono na wanaandika kwa mkono. Nimetoa onyo na kwanza kitakachotokea ni mambo mawili. Moja, tumeiomba Wizara ya Fedha ambayo huu ndiyo mradi wake wa kutengeneza fedha nje ya nchi na mashine zile wanazinunua wao wanazipandisha wao na wanaziendesha wao na wanazi-service wao.

Nazungumza na kaka yangu Mheshimiwa Mgimwa ili kwanza Balozi zetu zote zipatiwe *visa stickers* na pili, mtaona utaratibu utakaobadilisha, tutapeleka *consulate generous* Watanzania kwenye vituo vyote vile ambavyo tunadhani kuna fedha tunazopoteza ili hao wengine wakae pbeni. Fedha zile zitasaidia Serikali yetu kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, liko suala la Morocco nimelizungumza asubuhi, naomba nitoe ufanuzi kidogo tu pale. Tumesema sisi Tanzania hatuna tatizo la kuwa na *dual relationship* na watu wanaopambana wenyewe kwa wenyewe. Israel tuna Ubalozi. Ubalozi wetu wa *Egypt* ana-service Israel. Palestine wana Ubalozi wao Dar es Salaam. Watu hao wawili ni wapinzani wa jadi na sisi tunapokwenda kwenye Umoja wa Mataifa wakati wote tunaunga mkono

jitihada zote za Palestine. Lakini tuna *diplomatic relations* na nchi zote hizi. Israel tuna *diplomatic relations* na Palestine tuna *diplomatic relations*.

Nilipokwenda Morocco kupeleka barua ya Mheshimiwa Rais ujumbe ulikuwa huo kwamba tuko tayari sisi Watanzania kuwa na *diplomatic relations* na Morocco lakini wakati huo huo tuna *long historical diplomatic relations* na *Saharawi Arab Democratic Republic*, yaani watu wa Sahara Magharibi, na tumesema hatutaki masharti, wote tutawatambua, lakini mmoja asiseme tumkatae mwenzake.

Kwa hiyo, tunataka tuwe na uhusiano wa Kidiplomasia, mahusiano kwenye nyanja za elimu, mahusiano katika masuala ya *communications*, mahusiano katika masuala ya biashara na nia yetu ni kuwawezesha Watanzania wale wanaotaka biashara waweze ku-access kokote katika Bara la Afrika bila ya kujisikia kwamba Serikali yao inawabanabana wasiende kwenye maeneo fulani eti tu kwa sababu tu uhusiano na mtu mmoja na sio mtu wa pili.

Nilitaka niliweke hili *clear* kwamba tuko njia moja ili kuhakikisha kwamba hatufungwi mkono na mtu yejote. Sisi ni rafiki wa kila mtu, lakini *liberation struggle* yetu ambayo ilianza mwaka 1963 bado iko pale pale.

Mheshimiwa Spika, liko suala ngoja niseme, siyo aibu kupangisha nyumba Paris. Sisi tunapangisha kwenye Ubalozi wa Uganda pale Paris. Ni kweli na tunatafuta nyumba pale Paris. Lakini *inversely*

Waganda wanapangisha nyumba yetu Sudan na Malawi. Lakini siyo kitu cha kujivunia.

Nilikuwa nasema tu ni jambo la kawaida kwa mwenzako wa Afrika Mashariki anapokuwa na nyumba mahali, unaweza ukaipangisha wewe halafu mali isiende mbali na tunagawana wenyewe.

Sasa lingine ambalo limesemwa hapa kwamba Wizara ya Mambo ya Nje ichague watu wazuri kwenye stesheni zake. Mimi nalikubali hilo, nimeagiza Wizara yangu kwamba ni vizuri tukawa na watu kwanza wenye *specialization* hasa katika masuala ya uchumi, mahesabu, na wataalamu kabisa kwenye utalii; pili, hata *immigration*. Sasa tuwe na watu *professionals* kwenye *embassies* zetu kwa sababu hatuwezi kukidhi kuwa na watu wengi, lazima tuwe na watu wachache, lakini wenye utaalamu wa kuweza kuendesha na kuongoza Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, nina dakika ngapi?

SPIKA: Wewe endelea tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Mbunge ametuletea mchango wake hapa anasema Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, wale Mabalozi wawe wanashiriki katika kuweka mikataba mbalimbali na sisi tumekubali. Tumesema kwamba Mabalozi kila watakapopata fursa na tunaomba kwamba Wizara mbalimbali zinapopeleka ujumbe wake kwa ajili ya mkataba au

kufanya jambo lolote duniani, washirikishe Balozi zetu. Mnaposhirikisha Balozi zetu, Mabalozi wetu wanapata fursa ya kuweza kuchangia kwa maana ya kuweka mikataba tutakayoagiza na kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, iko hoja moja imetueleza kwamba kuna matatizo ya utapeli unaofanywa na baadhi ya watu huko nje kwa Watanzania wetu. Ningependa kulikubali hilo, na pia niseme kwamba Wizara inaomba, kabla hujaingia mkenge, kabla hujafanya jambo lolote na watu wa huko nje, chonde chonde wasiliana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ili tu-cross *check* na huyo mtu ambaye umekubaliana naye kufanya jambo lolote la biashara au lolote lile ili tujiridhishe kama kilichosemwa ndicho na kama huyu mtu ni *genuine* kweli au ni tapeli ili likuwezeshe wewe kuendeleza hizo biashara zako. Usipofanya hivyo, kuna hatari ya kutapeliwa na kuna hatari ya kujisikia kabisa kwamba sisi hatujakusaidia ilhali hukutuhusisha toka mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge mwingine amelielezea suala la kwamba Balozi zetu hasa kwenye viwanja ambavyo tulivipata Nairobi, London, Derwood hatukuvijenga. Ningependa tena kurudi palepale kwamba hili ni kwa sababu ya *development budget*. Bajeti ya Maendeleo tulikuwa hatupewi na tunavyopewa tunapata nusu. Pindi mtakapotupa *Development Budget* ambayo itakuwa kubwa nina hakika kabisa haya mambo tutakuwa tunayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa na hasa linalohusu Balozi zetu za Afrika ni suala zima la Maafisa wetu kukaa kwa muda mrefu. Watu wamesema kwamba Maafisa wanakaa kwa muda mrefu na hawatoki. Tunarudi palepale kwamba Maafisa wetu wa nje tungependa warudi kwa wakati baada ya kutekeleza vipindi vyao vya miaka minne minne, lakini mara nyingi baada ya kushindwa kupata fedha kwa ajili ya kurudisha Mabalozi pamoja na Maafisa wa Mabalozi, tunashindwa kufanya hivyo. Lakini pindi tutakapopata fedha za kurudisha Mabalozi wetu, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutajitahidi kufanya hivyo bila kuchelewa kuwarudisha watu wetu pale.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la magari ambalo yanazimika njiani na watu kueleza kwamba Mabalozi wetu China na sehemu nyingine walikuwa na utata mkubwa. Naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba suala la magari ni kweli tulikuwa hatujapata magari kwa muda mrefu, tunategemea katika kipindi hiki kununua magari 15 kuyapeleka kwenye matatizo yale sugu. Lakini wakati mwingine habari hizi za magari kuzimika njiani na likaleta soga za ajabu, ni habari ambazo hata mimi nilipokuwa kwenye Ubalozi, habari hii ilikuwepo. Ni ajabu inajirudia hata miaka 12 baadaye.

Kwa hiyo, inawezekana ni ka-joke fulani ka kuelezea tu jinsi tulivyokuwa na matatizo ya magari kwenye Balozi zetu. Kwa sababu hata mimi nilipokuwa Ubalaozini habari hii ilikuwepo ya kuzimikiwa gari halafu

baadaye unapitwa na wenzako, la kwako linakuwa na sauti kubwa kama treni, halafu baadaye linakwenda pale. Ni kitu kinatokea kila mwaka, lakini *at the end* ni *message* inayosema kwamba hatuna magari na sisi tunasikiliza suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza hapa ni kwamba katika Balozi zetu katika zile *Embassies* ambazo tupo kwenye Balozi 32 wenzetu wengine wametuambia tuzifunge Balozi nyingine halafu tubaki na chache. Ni wazo zuri, lakini kuna *political implications* kwamba unapofunga Ubalozi wa nchi jirani au ubalozi ambao mlikuwa na *historical links*, sababu za kihistoria, halafu unapofunga tu leo ghafla ili kufungua Ubalozi mwingine au kukaa kimya kidiplomasia inakuwa shida kidogo. Ni afadhali kupunguza idadi ya Watendaji kuliko kufungafunga tu Balozi hizi kwa sababu zozote zile. Lakini kama nilivyosema mwanzoni, dawa hapa kwa kweli ni suala la fedha.

Mheshimiwa mwingine ametueleza hapa kwamba tuchangamkie *opportunities* za China na anasema hii misaada ya kuombaomba kutoka nje, kwa nini tusijitegemee sisi wenyewe? Jibu lake ni *very simple*. Ni kwamba, nchi zote duniani zinakopa, hata yale Mataifa makubwa yanakopa. Kikubwa hapa katika kukopa, unakopa ili ufanye nini? Kama unakopa kwa ajili ya kuwa mtaji wa maendeleo ili baadaye uondoe hiyo *vicious circle* ya kuombaomba, *then* mkopo wako ni wa faida kubwa. Lakini pia ziko nchi ambazo zinatoa mikopo ya mitego mitego na Wizara ya Fedha iko pale kujaribu kuhakikisha tu kwamba mitego mitego ya aina

hiyo haitokei mara nyingi. Kwa hiyo, mara nyingi tunapochukua mikopo kutoka nje, siyo jambo la aibu. Tunapoomba wakati mwingine misaada kutoka nje siyo jambo la aibu sana.

Mheshimiwa Spika, kikubwa pale unatumiaje hizo fedha unazozipata kutoka nje ili baadaye uweze kujitegemea? Sasa mtu mmoja akaniambia tungeweza kujitegemea bila kuomba mkopo wowote kutoka nje? Nikamwuliza swali: Je, kwa mfano uchimbaji wa gesi Mtwara na *offshore* ile *rig* ya kuchimba gesi pale unatakiwa ulipie dola milioni moja na nusu kila siku ili kuchimba, na ile gesi ipo kilomita sita chini ya ardhi na una visima vinne. Maana yake *rig* peke yake kwa mwaka mmoja uzidishe *1.5 million per day* mara 365 mtaji ule unaupata wapi kama unasema tuna kila rasilimali tujitegemee wenyewe?

Mheshimiwa Spika, siyo vibaya kuwa na mkopo au kuwa na msaada wa mkopo kwa ajili ya mtaji wako ili baadaye usimame mwenyewe. Mimi nasema, kwa hilo hatuna sababu sana ya kuliogopa. Pale tunapokuwa na nia ya kukopa kutoka nje au kupata msaada wa kutoka nje wa kukuwezesha kupata mkopo wa kuweza kujitegemea wewe mwenyewe hilo siyo jambo la aibu. Lakini kukopa kwa ajili ya kula tu au kwa ajili ya chakula tu au misaada *handouts*, hili na mimi naunga mkono kwamba Wizara ya Mambo ya Nje haifanyi vile, na kila tunapofanya vile tunajirudi kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mmoja ameniuliza hapa suala la safari za viongozi, kwamba safari za

viongozi nje lazima mllichukulie hatua. Ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tatizo hili Mheshimiwa Rais aliniagiza miaka miwili iliyopita. Aliniagiza mwaka mmoja uliopita, tumeshatoa mapendekezo yetu ya kupunguza idadi ya watu wanaokwenda ama kwenye misafara mikubwa au kwenye safari zao wao wenyewe ili kuipunguza kukidhi na mahitaji ya bajeti ambayo tunapewa hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, nimepata swalii hapa, na nani ameuliza swalii hili? Ni Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Khalifa na nimeulizwa habari ya rada. Sasa mwenzangu Waziri wa Katiba na Sheria amesimama kwa muda wa dakika 10 amejibu na mmemshangilia, mmeridhika na yale majibu? Nami nasema nisingependa tena kurudia majibu ya mwenzangu wa Katiba na Sheria aliyojibu. Lakini Mheshimiwa Wenje tutaonana kesho.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo...

SPIKA: Muda unakwenda hivyo, kengele ya kwanza bado lakini inagonga sasa hivi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Sawasawa namaliza. Bado sijaishiwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimeulizwa swalii na Wabunge sita ya maandishi ikinieleza kwamba lazima nitoe maelezo ya meli za Zanzibar. Ningependa kutoa taarifa tu kwamba meli zilizodaiwa zilikuwa zinapepea bendera ya Iran, tuliomba marafiki zetu na marafiki

zetu wametujibu na kwa mujibu wa uchunguzi wao wamethibitisha, Serikali ya Zanzibar hivi ninavyozungumza inaifanyia kazi taarifa ambayo imefika rasmi kutoka kwa marafiki wa nje waliofanya utafiti meli zile 25 za mizigo na 11 za mafuta.

Nimezungumza na viongozi wote wanaohusika wa juu katika Taifa na wameniambia nitoe taarifa hii, kwamba mara zoezi la kulinganisha meli zote zilizotajwa na orodha ya meli zilizokuwa *registered* na ZMA zoezi hili la kulinganisha litakapothibitika na kumalizika, dakika yoyote kuanzia sasa uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar utakuwa ni kuzifutia meli zote zilizohusika na kupeperusha bendera ya Tanzania kutoka Iran.

La pili, Kampuni iliyopo Dubai ya Filtex kwa mujibu wa maagizo niliyopewa leo iliyoshughulikia *registration* hiyo baada ya zoezi hili kukamilika leo, Kampuni ile itavunjwa. Rais wa Zanzibar anategemea kuunda Kampuni tena maalum na Tume ya Kuchunguza fedha zilizokuwa zinapatikana katika shughuli hizi zilikuwa zinakwenda wapi na kama kulikuwa na mjanja alikuwa anazichukua fedha zile.

Kwa hiyo, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hili sasa linafanyiwa kazi na si ajabu baada ya kumaliza na shughuli hizi mtakuwa mmezipata rasmi. Ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua za haraka ambazo wanazichukua kuhakikisha kwamba sisi Tanzania pamoja na Zanzibar haturubuniwi, na mtu yejote yule huko katika anga za

Kimataifa na kwamba wakati wote sisi ni Wajumbe wa kuaminika katika anga za Kimataifa na tunayotekeleza *resolutions* na mikataba mbalimbali ya Umoja wa Mataifa. Nataka nitoe hilo kwamba tunaishukuru Serikali ya Zanzibar kwa kulimaliza suala hili vizuri na wanafanya vizuri sana na mimi kwa niaba ya wenzangu wote Bara tunatoa pongezi hizo.

Mheshimiwa Spika, mengine nitayajibu yatakapokuwa yanajitokeza, lakini ningependa kumalizia kwa kusema nashukuru sana. Nimejibu hoja mbalimbali nyingine zinazobaki, nitazijibu wakati muafaka utakapofika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Kimataifa**

Kif. 1001 *Admin and HR Management* Shs 5,796,623,000/=

MWENYEKITI: Naomba muwe *very brief* jamani.
Tunaanza na Mheshimiwa Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa sera ya mambo ya nchi za nje ni kuwa na Balozi nchi mbalimbali kwa sababu mbalimbali, mimi napenda kuuliza kwamba: kwanini Tanzania mpaka leo hatuna Ubalozi kamili na nchi ya Israel, ukizingatia kwamba Watanzania wengi wanakwenda huko kwa masuala ya kiimani na kibiashara na kama vile wanavyokwenda Jeddah na wanapata huduma nzuri kamili ya Kibalozi: Kwanini Tanzania tusiwe na Ubalozi Israel?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunao Ubalozi kamili nchini Israel. Labda anachokifikiria, hatuna Balozi mkazi kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri. Balozi wetu wa Tanzania nchi Israel ye ye yupo nchini Misri. Lakini matatizo ambayo yamejitokeza kabla, ndiyo yanatuzaia kufungua Ubalozi. Uwezo wa kifedha hauturuhusu kufungua Balozi kila nchi ambayo ni rafiki kwetu. Lakini suala hilo tunalizingatia.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani tulihoji: Kwanini mpaka sasa Serikali kupitia Wizara hii imelimbikiza madeni ya *APRM* mpaka kufika Dola laki nane? Ni lini hili deni linakwenda kulipwa ili kuliepushia Taifa letu aibu ya kudaiwa kila mara?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Waziri mwenzangu kivuli kwamba utaratibu wa kulipia fedha kwa ajili ya ada kwenye *International Organization* zetu zote ikiwemo *APRM* ni utaratibu unaojikita kwenye Wizara yetu ya Fedha. Wizara yangu inachofanya ni kujumuisha madeni yote kutoka kwenye *APRM*, *SADC*, Afrika Mashariki, *AU* kote kule ambako sisi tunashiriki Wizara ya Fedha ndiyo inatoa fedha zile.

Wizara ya Fedha wanatoa kwa mgao, kwa hiyo, ushiriki wetu kwenye *International Organization*. Sasa hivi bado madeni yetu tunayalipa vizuri. Afrika Mashariki wameshalipwa tayari, *AU* tumeshalipa tumebakwa na kidogo, kwenye upande wa *SADC* tumelipa kwa asilimia 75. Sasa kwa upande wa *APRM* sababu ya kuchelewa kulipa milioni 800 hazijatuvunja heshima bado kwa sababu katika takwimu za nchi 29 ambazo ni Wajumbe wa *APRM* kuna wenzetu wana madeni zaidi ya dola milioni mbili, sisi bado. Lakini tumeshaliandikia na tunategemea kwamba Wizara ya Fedha itaturudishia fedha hizi.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIBU JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ahadi zake ni uungwana mzuri sana alioufanya. Jambo dogo tu nataka ufanuzi. Nilipochangia Wizara ya Uchukuzi kulikuwa na suala mtambuka na siku ile ulikuwepo, na leo pia nimechangia hilo suala kwa maandishi.

Nilitaka kujua, huu ubaguzi unaoetendeka katika nchi za *SADC* kwa hizi ndege ambazo zinaruka zikilala na zikiondoka Tanzania lazima ipulizwe ile *insectside* ambayo ina madhara kidogo ukivuta harufu yake. Lakini nchi nyingine za *SADC* kwanini isipulizwe ndege inapolala na kuondoka? Sasa haya matatizo kwanini yametokea? Kama ni Malaria, kwanini wasipulize kabla abiria hawajaingia mule ndani ya ndege.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kwa mujibu wa Sheria za Afya za Afrika ya Kusini tangu zile zilizokuwepo wakati wa ubaguzi, yaani *apartheid* Tanzania na Mozambique, zilijulikana kama nchi ambazo zina Malaria ya kuua. Kwa hiyo, kila ndege iliyokuwa inatoka kule kuja huku hadi sasa lazima ipulizwe ile *flight insect side*. Lakini pia kwa *Seychelles* na wenyewe wanapuliza vilevile.

Kwa hiyo, ni jambo ambalo lilikuwepo na sisi hatukuweza kuliingilia sana. Lakini hizo ni Sheria za Afya. Kuna nchi nyingine ambazo kama wewe una *yellow fever* watakukataza kuingia kwenye ile nchi na bahati nzuri dawa ile haidhuru sana wanapopulizia, na maana yao siyo ubaguzi, maana yao ni kuzuia mbu wasiingie kwenye ndege. Sasa wazo la kupuliza kabla abiria hawajaingia, tatizo liliopo ni kwamba unapoingia mwingine na begi lako ambalo halifungwa kuna mbu sita mle. Unapoingia kwenye ndege inakuwa matatizo pale pale.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa sera ya kutumia *financial system* kama vile *mortgage* ili kuweza kutengeneza baadhi ya nyumba zetu ambazo zipo katika hali mbaya kabisa. Lakini kitu kinachonishangaza, bila kuwa na kasma ya maendeleo, bado uliweza kutumia Shilingi bilioni 60 kununua majengo mawili kule *Washington* pamoja na *New York*. Lakini mpaka leo huna utaratibu wa kuzipata hizo pesa ambazo ume-*invest*. Labda utueleze basi hizo pesa zitapatikana kwa njia ipi?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Cheyo na lazima nikubali amenipa paper nzuri sana. Tunachokusudia ni kwamba katika Bajeti ya sasa ambayo tuna *development budget ya 16.6 billion*. Tunakusudia kuondoa Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kukarabati jengo la 2139, R Street Washington ili liwe *converted* katika hosteli inayolingana na *condominium* ili tuweze kuwakodisha wanafunzi hasa wa *George Town University* ili tuweze kupata pesa za kuweza kuendeshea kule. Lakini pia kwenye jengo lile jipya tulilolinunua lilikuwa na nyufa zake.

Tunategemea kutumia bajeti finyu ya *development budget* kiasi cha dola laki nne sawa na karibu Shilingi milioni 600 au 700 ili kuweza kukarabati nyufa zilizokuwa zimepatikana katika jengo lile. Kwa sababu tunazo ghorofa nne za kuweza kupangisha.

Kwa hiyo, tunachojikita ni kwamba mkinipa hela leo tutanyofoa wastani wa Shilingi bilioni mbili kutoka

kwenye *development budget* ili tuanze kazi ya kujenga uchumi na kuondoa fedheha ambayo sasa hivi inatugharimu.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia kuhusu mauaji yanayoendelea nchini Syria, akina mama na watoto wengi wanauawa. Hapa Tanzania tumeona pale Dar es Salaam kuna maonyesho ya Syria ya kibiashara, inaonyesha kama nchi yetu inawa-*support*. Nataka kujua msimamo wa Tanzania kuhusu mauaji yanayoendelea nchini Syria.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Syria duniani linatusumbua wengi sana. Jana kulikuwa na kupiga kura kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa na nchi 133 zili-*vote for resolution* inayotaka hatua zichukuliwe za kimataifa za kuzuia mauaji yale. Lakini pia kama mnavyojua, Urusi na China wame-*veto*. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba mauaji yanayoendelea nchini Syria na Syria ikiwa mionganoni mwa marafiki zetu.

Sisi Tanzania hatuyaungi mkono. Lakini kwa sababu ya wakubwa wameingia tena Syria kama walivyofanya Libya, Marekani, nchi za Ulaya zinataka kuchukua hatua wakati Urusi pamoja na China wanataka kuizua hatua ile Syria. Sisi wadogo katika anga za kimataifa tumeamua ku-*abstain* lakini kuwaomba wakubwa walimalize tatizo hili kwa haraka kwa maana ya kuendeleza juhudii alizoziacha Mheshimiwa Koffi Annan ambaye amejiuzulu siku

chache zilizopita. Bado tunaamini kwamba Baraza la Umoja wa Mataifa na Umoja wa Mataifa wanaweza kulimaliza tatizo hili na sisi Tanzania tunawaombea wafanikiwe badala ya kuingia kwenye mgogoro ambao tuliouna Libya kipindi kilichopita.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi, nilihoji kuhusu *Visa*. Miaka ya nyuma *visa* za Uingereza tulikuwa tunapata katika Ubalozi wa Uingereza ambao uko Dar es Salaam. Lakini katika miaka ya hivi karibuni, utaratibu huo umebadilika, *Visa* ya Uingereza ni mpaka ipelekwe Nairobi na inachukua zaidi hata ya wiki mbili. Wao wanapokuja raia wa Uingereza wanapata *Visa on arrival* hapa. Sisi Nairobi kwanini? Naomba utaratibu wa zamani urudishwe, tupate hapa hapa katika Ubalozi wa Dar es Salaam ama na sisi raia wa Tanzania tupate *on arrival* huko Uingereza. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la *visa* liko katika uwezo wa nchi husika. Lile ambalo amelizungumzia kuhusu sisi kuweza kuamua tunatoa viyi visa yetu kwa Uingereza, ndiyo ambayo lipo katika madaraka yetu. Lakini wao wana haki ya kupanga hivyo, ingawa Wizara imechukua hatua ya kuwaeleza na kuwaomba waondoe usumbufu huo kwa Watanzania.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea sana suala la *shuttle diplomacy*.

Nilitaka kujua tu nini sera ya Serikali kwa upande wa *shuttle diplomacy* ukichukulia kwamba kuna mgogoro umedumu kwa muda mrefu katika Ziwa Nyasa na Mheshimiwa Waziri ametuelezea hapa historia pamoja na suala la Heligoland. Naomba maelezo.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza *shuttle diplomacy* karibuni sana. *Diplomacy* ya *shuttle* ni diplomasia ambayo inawataka wale wanaotaka kutafuta amani kwa njia ya kidiplomasia wawe wanakwenda, wanarudi, wanaita, wanawaona, wanaruka wanakwenda kutekeleza na kurudi. Kwa hiyo, *shuttle diplomacy* ndiyo tumeanza tarehe 27 na 28. *Shuttle diplomacy* ya pili itakuja tarehe 20 Mzuzu, halafu mwisho wa mwezi wa nane tutakuwa na *shuttling* tena kati ya Mawaziri wawili sisi katika kuhakikisha tunalimaliza suala hili *diplomatically*.

Pia tunategemea kuwa na *shuttle diplomacy* kati yetu na *DRC Congo* kwa sababu, kama mlivyosikia asubuhi, kuna *M23* na kuna mapigano yanayoendelea kule na kwa hiyo, kwa kuwa sisi ni watu wa *SADC* na tunachukua Uwenyekiti wa *SADC* in *Security Tracker* itakuwa na *shuttle* katika nchi hizo ili kujaribu kuleta amani kwa wale wanaohusika.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kuongeza ajira katika nchi, Serikali huwa zinajenga miradi ya miundombinu. Serikali ya China imetoa mikopo pamoja na misaada mingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Sera yetu ni ipi kwa maeneo ambayo China inatupa

mikopo na kuleta wafanyakazi wengi kuliko ajira ambazo wanapata wananchi wetu hapa Tanzania na kwingine Afrika kwa mikopo kutoka China?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kunakuwa na mikopo na mimi ndiyo kwa niaba ya Afrika niliweka saini ya Shilingi bilioni 20 wiki mbili zilizopita, mikopo kwenye Bara la Afrika na sera yetu ni hii, kwamba ni vizuri Serikali ikabuni miradi ambayo ni *labour intensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo ukichukua mkopo kutoka China itakuwa na vijana wengi sana watakaoajiriwa katika *labour*, kwa mfano *textiles*. Nazungumzia Ubungo kwa mfano, hiyo ndiyo moja ya kushughulikia. Kwa sababu *textile industries* na Wachina wako bora. Kwa hili wanaweza kabisa kufufua Ubungo *Textile Mill* na mkaajiri watu zaidi ya 3,500 kwa *shift* kwa siku hiyo, ndiyo miradi ya kuichangamkia. Siyo tu miradi kwa kuwa kuna mkopo kutoka China mlete kila mradi. Ni lazima kwanza kujipima ni mradi gani unaoutaka kutoka China au kokote kule ambaa *utah-employ labour*. Hiyo ni sera moja ambayo tutaweka uzito. (*Makofii*)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nirudi katika suala hili la Syria.

MWENYEKITI: Kanuni zinakataza, huwezi kurudia mara mbili suala lile lile.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Sawa. Labda niulize katika *angle* tofauti. Mara nyingi nchi zinapoingia katika vita ya wenyewe kwa wenyewe wale ambao wanapigana na Serikali iliyoko madarakani kwa Kiingereza wanaitwa *rebels* na Serikali inayopigana na hawa *rebels* ambao ni waasi wanaitwa *regime government* kwa maana ya Serikali ya kidhalimu. Nini msimamo wa nchi yetu katika tafsiri hizi? Kwa sababu *rebels* ambao ni waasi wanapopigana na Serikali iliyopo Madarakani ambayo Mataifa makubwa yanaita *Regime Government*, Serikali yetu msimamo wake ni upi katika tafsiri hizo?

MWENYEKITI: *Rebels* na *regime*, basi ndiyo tofauti? Naomba ujibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *term* kubwa inayotumika ni *regime change*, kwa maana ya Serikali iliyopo Madarakani wale wanaoleta fujo nchini wameichoka na wanataka kuiondoa na wale *rebels* baadaye wakishashika nchi ndiyo wanapata heshima. Lakini hizi ndiyo *terminologies* za wakati huu. Kuna kitu kinaitwa *Arab Spring* ambayo wakubwa na watu ambao hawaridhiki na utawala uliokaa muda mrefu wanataka kuuiondoa na kuwaleta watu wengine mle ndani, lakini itajitatua yenyewe kwa sababu nchi nyingi sana zinachukua demokrasia ya uchaguzi haya masuala ya arab *spring* yatapitwa na wakati.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge hapa amegawiwa ramani na ninaamini kwamba ni Wizara ya Mambo ya Nje imegawa ramani

hiyo ambayo mipaka minene na mizito inaonesha ramani hii *in favor* ya Malawi, haioneshi ile ambayo Watanzania tunataka. Lakini naamini kabisa na ninaomba nitumie neno hili kwamba *we are not going to give an inch of our country to Malawi*, na tutahakikisha kwamba tunailinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mambo ya Nje hapa amezungumza kwa masikitiko makubwa namna ambavyo Wizara ya Fedha haiipi fedha Wizara ya Mambo ya Nje. Katika mazingira kama haya tuliyonayo, *Chief Ambassador* wa nchi analalamika, tutaweza kweli *ku-negotiate* vizuri na kuhakikisha tunalinda mipaka ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha atoe *commitment* hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba fedha zote ambazo zimetengwa na zitapitishwa na bajeti leo, asilimia mia moja zitakwenda Wizara ya Mambo ya Nje ili kuhakikisha kwamba Wizara isiwe na msongo wa mawazo itakapokuwa inatetea kulinda mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba umpe fursa Waziri wa Fedha na mimi ni *Shadow Minister* wa Fedha kwamba asimame atoe *commitment hundred percent* kwenda Wizara ya Mambo ya Nje kulinda mipaka ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kanuni inakataa, tunaendelea.

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninazungumzia mradi wa *Exclusive Economic Zone*, (EEZ) mradi wa kuongeza eneo la bahari nje ya mipaka ya kiuchumi ambayo Mheshimiwa Waziri amezungumza katika kitabu chake ukurasa wa 34, mradi huu umeleta malalamiko makubwa sana kule Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi, nafikiri ulikuwa unafuatilia hilo. Nataka kujua: Je, ni nini msingi wa malalamiko yao? Tanzania kama nchi, ina msimamo gani kuhusu malalamiko hayo?

MWENYEKITI: Naomba jibu kwa kifupi, muda umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya Zanzibar kwenye mradi wa kuongeza eneo la ukanda wa bahari ilikuwa kwamba Uongozi wa Zanzibar haukushirikishwa. Huo ndiyo ulikuwa msingi. Lakini maelezo hayo yana walakini kwa sababu hata hivi sasa ambapo kuna timu, iko New York kutetea, upo pia Uongozi wa upande wa Zanzibar.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGWALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine, imekuwa ikipata fursa ya kuwa kwenye mikataba mbalimbali ya kimataifa ya ushirikiano wa kibishara, mfano ni Mkataba wa *Everything but Arms, African Growth and*

Opportunities Act, (AGOA) NEPAD na sasa hivi kuna SADC, na East African Community. Wasiwasi wangu ni kwamba Tanzania tumejipanga kiasi gani kwa kutumia intelijensia yetu ya kibiashara kuhakikisha tunatumia fursa ambazo zinaletwa na mikataba hii ya kimataifa? Badala ya sisi kuwa soko na sisi tuwe na mikakati yetu ya kuingia kwenye hizo nchi nyingine na kutumia fursa ambazo zinaletwa na mikataba hiyo ambayo nimeitaja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Waziri kwa kifupi sana tuna dakika tano tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru mwenzangu. Ni kweli kabisa kwamba tumeingia kwenye mikataba mingi, lakini kwa funzo tunalolipata kwa *Economic Partnership Agreement (EPA)* ni kwamba tunajifunza mengi kwamba kama tunakwenda kwenye mikataba ya aina hii, tusipokwenda kama Jumuiya, kwa mfano Afrika Mashariki, au tusipokwenda kama SADC, au tusipokwenda kama Bara la Afrika, tukaacha nchi moja moja kuingia kwenye mikataba ambayo ina mitego kama *Economic Partnership Agreement, then* tunakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkakati wa kwanza uliopo katika ukanda wa Afrika Mashariki, *SADC* ni kwamba tunapokwenda kwenye

makubaliano na majailiano ya mikataba ambayo ni *commercial*, ni lazima twende *as a group*. Ile inaturuhusu kuwa na *intelligence* ya kutosha ya kuchambua *authenticity* na mitego ambayo tunategewa na watu wa aina hii.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka 2004 katika Kikao cha Bunge la Afrika kikiwemo ndani yake, Umoja wa Afrika pamoja na UNESCO walitoa kauli pamoja na kauli nyingine kwamba nchi ambayo wanataka mali zao zirejeshwe nchini, wanaweza kurejeshewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna mali nyingi nchi za nje, tuna mafuvu ya binadamu, tuna vitu vya samani viliviyotoka Olduvai, kuna mjusi aliyetoka Lindi Dinasaur. UNESCO walikuwa tayari katika harakati za kurejesha mali hizo pamoja na uhifadhi wake.

Je, Serikali ya Tanzania inatoa kauli gani kuhusu suala hili hasa mjusi wa Tanzania? (*Makofi/kicheko*)

MWENYEKITI: Hata kabla hujasimama, nilijua tu ni *Dinasaur*. Mheshimiwa Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanamwona anauliza mara nyingi suala la Mjusi, ni kwa sababu anatoka kwenye Jimbo na sehemu aliyozaliwa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya sisi kumpatia taarifa ya awali kuhusu uwekezano wa kuungwa mkono na AU,

UNESCO na kurudisha mjusi ambaye ana upana wa mita 22 na urefu wa mita 14 kwenda juu na mtoto wake ambaye ana mita nne kwa nne aliyepo Berlin, anatoka Lindi Vijijini anakotoka Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Mheshimiwa Rais ametuomba tuunde *Committee*, ikiwezekana na Bunge, ili iende Addis Abba ambayo wana uzoefu wa hivi karibuni wa kurudisha mali ambazo zilikuwa Italy minara ile. Wale waliunda Kamati, na baada ya miaka miwili wameweza kurejesha ile mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inabidi iundwe Kamati iende ikajifunze ni mbinu zipi walizozitumia, mikakati waliyoitumia ya kuweza kurudisha mali ile ili tujaribu bahati yetu?

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hata nikijitahidi, vipi siwezi kuwaliza wote. Afadhalii nifanye *administration* ili kusudi nifanye kazi iliyo bora zaidi. Kwa hiyo, naingia Kanuni ya 104 (2) *guillotine*.

Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 539,841,000/=
Kif. 1003 - <i>Foreign Affairs Office</i> Zanzibar...	Shs. 392,254,000/=
Kif. 1004 - <i>Policy and Planning</i>	Shs. 552,224,000/=
Kif. 1005 - <i>International Cooperation</i>	Shs. 2,487,483,000/=
Kif. 1006 - <i>Europe and America</i>	Shs. 358,055,000/=
Kif. 1007 - <i>Asia and Australia...</i>	Shs. 372,913,000/=
Kif. 1008 - <i>Africa</i>	Shs. 5,619,645,000/=
Kif. 1009 - <i>Regional Cooperation</i>	Shs. 4,976,580,000/=

Kif. 1010 - <i>Protocol</i>	Shs. 15,161,069,000/=
Kif. 1011 - <i>Legal Services</i> ...	Shs. 1,748,855,000/=
Kif. 1012 - <i>Government Comm. Unit</i>	Shs. 161,226,000/=
Kif. 1013 - <i>Middle East Division</i>	Shs. 355,701,000/=
Kif. 1014 - <i>Internal Audit Unit</i> ...	Shs. 211,612,000/=
Kif. 1015 - <i>Procurement Unit</i> ...	Shs. 192,762,000/=
Kif. 1016 - <i>Info. and Comm.</i> <i>Technology</i>	Shs. 101,847,000/=
Kif. 1017 - <i>Diaspora Engag. &</i> <i>Opportunity</i>	Shs. 168,700,000/=
Kif. 2001 - <i>Embsdy of TZ - Addis</i> <i>Ababa</i>	Shs. 1,136,253,000/=
Kif. 2002 - <i>Embassy of Tanzania -</i> <i>Berlin</i>	Shs. 2,056,338,000/=
Kif. 2003 - <i>Embassy of Tanzania -</i> <i>Cairo</i>	Shs. 569,696,000/=
Kif. 2004 - <i>Embassy of Tanzania -</i> <i>Kinshasa</i>	Shs. 1,089,208,000/=
Kif. 2005 - <i>Embassy of Tanzania -</i> <i>Abuja</i>	Shs. 766,750,000/=
Kif. 2006 - <i>High Commission of TZ -</i> <i>London</i>	Shs. 2,342,461,000/=
Kif. 2007 - <i>High Commission of TZ -</i> <i>Lusaka</i>	Shs. 641,909,000/=
Kif. 2008 - <i>High Commission of TZ -</i> <i>Maputo</i>	Shs. 753,513,000/=
Kif. 2009 - <i>Embassy of Tanzania -</i> <i>Moscow</i>	Shs. 1,064,978,000/=
Kif. 2010 - <i>High Commission of TZ - New</i> <i>Delhi</i>	Shs. 884,116,000/=
Kif. 2011 - <i>Perm. Mission to the UN- New</i> <i>York</i>	Shs. 1,669,877,000/=

Kif. 2012 - *High Commission of TZ - Ottawa*... Shs. 1,233,851,000/=

Kif. 2013 - *Embassy of Tanzania - Paris* ... Shs. 1,436,736,000/=

Kif. 2014 - *Embassy of Tanzania - Beijing* ... Shs. 1,112,608,000/=

Kif. 2015 - *Embassy of Tanzania - Rome* ... Shs. 1,713,609,000/=

Kif. 2016 - *Embassy of Tanzania - Stockholm*... Shs. 1,533,442,000/=

Kif. 2017 - *Embassy of Tanzania - Tokyo* ... Shs. 1,908,264,000/=

Kif. 2018 - *Embassy of Tanzania - Washington*... Shs. 2,023,973,000/=

Kif. 2019 - *Embassy of Tanzania - Brussels*... Shs. 1,520,025,000/=

Kif. 2020 - Perm. Mission to The UN-Geneva... Shs. 2,506,358,000/=

Kif. 2021 - *High Commission of TZ - Kampala* ... Shs. 997,930,000/=

Kif. 2022 - *High Commission of TZ - Harare*... Shs. 542,203,000/=

Kif. 2023 - *High Commission of TZ - Nairobi* ... Shs. 2,033,328,000/=

Kif. 2024 - *Embassy of Tanzania - Riyadh* ... Shs. 1,160,810,000/=

Kif. 2025 - *High Commission of TZ - Pretoria*... Shs. 1,334,471,000/=

Kif. 2026 - *Embassy of Tanzania - Kigali* ... Shs. 578,674,000/=

Kif. 2027 - *Embassy of Tanzania - Abu Dhabi*... Shs. 1,898,355,000/=

Kif. 2028 - *Embassy of Tanzania – Bujumbura*... Shs. 739,988,000/=
Kif. 2029 - *Embassy of Tanzania – Muscat*... Shs.1,675,231,000/=
Kif. 2030 - *High Commission of TZ- Lilongwe*... Shs. 636,565,000/=
Kif. 2031 - *Embassy of Tanzania – Brasilia*... Shs.1,748,966,000/=
Kif. 2032 - *High Comm. of TZ – Kuala Lumpur*... Shs. 1,178,627,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif. 1004 - *Policy and Planning* Shs.16,653,204,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)
(*Bunge lilitrudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa mafungu na

kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi kwa niaba yenu kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wake na watalaaam wake wote waliofanya kazi hii kuiwezesha Wizara hii ifanikiwe. Lakini natoa wito kwa Mheshimiwa Waziri, wewe upo ndani ya Serikali usiwe unalalamika. Kama kuna hoja, iweke kwa utaratibu unaohusika iende kwa hatua zinazohusika, sisi tutawasikilizeni ninyi. Kwa hiyo, hatupendi hii habari ya kulalamika, sijui kufanya nini, sijui sheria gani, na nini. Kwani mlileta tukakataa? Kwa hiyo, mfanye hayo na itapitia kwenye Kamati zetu vizuri sana na kama inaungwa mkono italetwa hapa ili tufanye maamuzi. Fanyeni mageuzi ya Kidiplomasia kwa kutumia Bunge lenu kufanya mabadiliko. (*Makofi*)

Tumekwenda kwenye Balozi za Tanzania mimi mwenyewe nimeona, zimekaa katika hali mbaya sana na ndiyo maana Wabunge wanaosafiri popote nje ya nchi kama kuna Ubalozi nimewaagiza wakague na Balozi hizo, popote wanapokwenda. Waliokagua kitabu chao kipo hapa, hali ni mbaya, inatia aibu. Kuna wengine wamemwandikia barua Waziri, hivi Balozi umefunga? Maana *OC* mwaka mzima hawakupata. Kwa hiyo, tunataka mtumie *innovation* ili kusudi kufanya mambo ambayo yana heshima kwetu wote.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nitamwita Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

HOJA BINAFSI

**Hoja ya Mheshimiwa Selemani S. Jafo Kuhusu
Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii
Kwa Ajili ya Kuweka Fao la Kujitoa (*Withdrawal Benefit*)**

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Naomba kwa idhini yako na Bunge lako Tukufu, naomba kutoa maelezo yangu binafsi ya kuitaka Serikali iwasilishe Bungeni, marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa ajili ya kuweka fao la kujitoa (*Withdraw Benefit*) chini ya Kanuni 50 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maelezo yangu binafsi hapa Bungeni, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na pia napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Kamati yako ya Uongozi kwa kunipa Baraka ya kuandaa na kuwasilisha maelezo yangu hapa Bungeni kwa maslahi ya Watanzania. Napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah kwa kuratibu vyema mchakato wa kuwasilisha maelezo yangu binafsi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati - Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Bunge siku ambayo alitoa Mwongozo wenye hekima wa kuwezesha Bunge hili Tukufu mpaka Kamati ya Uongozi ikaweza kukaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Lolesia Bukwimba pamoja na Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kuniunga mkono katika msafara mzito wa kukutana na Watanzania ili waweze kutoa maoni yao. Napenda kuwashukuru Watanzania wenzangu wote kwa kuniunga mkono na kunipa moyo wa ushirikiano wa juu katika kuhakikisha kwamba maelezo yangu haya binafsi nayafikisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wafanyakazi wa Umma, Taasisi zisizo za Kiserikali, Wafanyakazi wa Makampuni ya Madini, Makampuni ya Ujenzi na barabara, majengo, hoteli, Benki, Chama cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu pamoja na Wafanyakazi wote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wa Geita, Mara na Shinyanga kwa kuweka mazingira mazuri ya kiusalama katika mchakato mzima nilipokuwa nakusanya maoni ya wadau.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru sana familia yangu na mama yangu mzazi na wananchi wenzangu wa Kisarawe kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika mchakato huu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufanyika kuitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Na. 5 ya mwaka 2002 (*The Social Security Law Amendments Act, Na. 5, 2012*) kulikuwepo na utaratibu wa wanachama wa mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini kufaidika na fao la kujitoa (*Withdraw Benefit*).

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo uliwezesha watumishi walioacha au kuachishwa kazi kabla ya kutimiza umri wa miaka 55 kulipwa mafao yao ya uzeeni na hivyo kupata kianzio cha kuendeshea maisha yao baada ya kuacha kazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo uliwezesha hata watumishi ambao walikuwa bado wapo kazini kutumia kiasi kidogo cha mafao yao ya uzeeni kwa ajili ya kuwezesha kujijengea nyumba na pia kupata mahitaji au kianzio cha kufanya shughuli nyingine za kipato.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo uliwekwa na kutekelezwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kuzingatia hali halisi ya mishahara midogo na pia kipato kidogo cha Watumishi walio wengi hapa nchini. Katika marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilitegemewa kwamba utaratibu huo ungewekewa msingi wa kisheria baada ya kuonekana ulikuwa umekubalika na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na pia kuonekana kuwa ulikuwa na manufaa makubwa sana kwa wafanyakazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, Sheria ya Marekebisho ya Hifadhi ya Jamii, imeweke vifungu vya sheria vinavyohusu mtumishi kutumia kiasi cha mafao yao ya uzeeni kulipa mikopo ya nyumba, yaani *home mortgage* kwa ajili ya kuwawezesha watumishi nchini kuwa na nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, katika hali halisi, nyumba za kuishi siyo hitaji pekee linalohitajika na watumishi wote, bali kila mtumishi anahitaji lake binafsi katika maisha yake. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu pia wa kuweka kifungu cha sheria kinachoruhusu mtumishi asiyehitaji nyumba ya kuishi kutumia kiasi cha mafao yake ya uzeeni kwa ajili ya kulipa gharama za shughuli yoyote nyingine kwa ajili ya kujewekea mazingira mazuri baada ya kustaifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutozingatia ukweli huo, Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Na. 5 ya mwaka 2012, haikuweka kifungu chochote cha sheria kwa ajili ya kuweka msingi wa kisheria wa kuwawezesha kuwepo kwa malipo ya fao la

kujitoa (*Withdraw Benefit*) kwa ajili kuwawezesha watumishi ambao wanahitaji kutumia kiasi cha mafao yao ya izeeni kugharamia shughuli nyingine muhimu zinazogusa ustawi wa masiha yao na nje ya maisha ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa kifungu cha sheria cha kuwezesha kuwepo kwa fao la kujitoa, kutaleta athari kubwa kwa watumishi ambao kwa sababu moja au nyingine wataacha au kuachishwa kazi kabla ya kufikisha umri wa kustaafuli na hivyo, kuhitaji fedha za kuendesha maisha yao baada ya kuacha kazi na pia kwa watumishi ambao wanahitaji kutumia kiasi cha mafao yao ya izeeni kwa ajili ya kugharamia mambo mengine nje ya nyumba ya kuishi ili kujiwekea mazingira mazuri ya kuishi kwa ajili ya kujiandaa kwa maisha ya kustaafuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hilo limekuwa tete sana ndani ya nchi yetu kiasi kwamba hushusha uzalishaji katika sekta mbalimbali hapa nchini hususan Sekta ya Madini. Hali hiyo imedhihirika wazi kwa wafanyakazi wa migodi ya madini kuitisha migomo na kupanga kufanya maandamano makubwa kama ilivyojionesha katika azimio lao kwa mujibu wa barua yenye Kumb. Na. TAMICO/Geita/2012/001 iliyoandikwa na Tanzania *Mines energy Construction and Alliance Workers Union TAMICO* kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Geita. Aidha, wafanyakazi hao waliendesha kura ya maoni ya kupinga marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Jamii Na. 5 ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto nyingi zilizojitokeza, naomba niende moja kwa moja katika suala zima la Azimio.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto kubwa, wafanyakazi hapa nchini, wengine wakiwa wanaishi maisha ya kuunga unga na kazi zisizokuwa za uhakika, kwa hiyo, kuna kila sababu na umuhimu wa Serikali kufanya yafuatayo:-

Moja, katika Mkutano ujao wa Tisa wa Bunge, Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Jamii, kwa ajili ya kuweka vifungu vya sheria vinavyohusu fao la kujitoa katika Sheria za Mifuko hiyo kwa wafanyakazi wanaoacha au kuachishwa kazi kabla ya kufikisha umri wa miaka 55 au 60.

Pili, pamoja na kifungu hicho cha sheria kinachoruhusu watumishi kutumia kiasi cha mafao yao ya izeeni kulipia mikopo ya nyumba (*Home Mortgage*), Muswada huo wa sheria pia uweke vifungu vya sheria vinavyohusu watumishi kutumia kiasi cha mafao yao ya izeeni kwa ajili ya kulipia gharama au shughuli nyingine yoyote ya kuiwekea mazingira mazuri kwa ajili ya kuiandaa na maisha ya kustaifu. (*Makofii*)

Tatu, katika Muswada huo wa Sheria, Serikali iondoe vifungu katika sheria hiyo vinavyoweka masharti ya kumtaka Mtumishi kuwasilisha maombi kwa Rais, kupitia utaratibu wenyewe urasimu mkubwa wa kupata msamaha kwa fao la kujitoa. (*Makofii*)

Nne, Serikali iagize Makampuni ya Madini hususan mgodi wa Bulyankhulu kutomsimamisha mfanyakazi yeote aliyeoji kwa kina juu ya mafao yao baada ya kupatwa na mshituko wa taarifa ya kutoruhusiwa kuchukua mafao yao baada ya kuacha kazi au kuachishwa kazi.

Tano, wakati tunasubiri kuletwa kwa Muswada huo kwa hati ya dharura katika Bunge la Tisa Ijalo, Serikali itoe waraka maalum wa maelekezo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuendelea kuwalipa mafao Watumishi walioacha kazi au kuachishwa kazi kabla ya kufikisha umri wa kustaifu.

Sita, katika Muswada huo, Serikali iangalie upya Kanuni inayotumika katika kukokotoa mafao ya watumishi waliostaifu ili kutozua balaa lingine kwa siku za usoni.

Saba; vile vile Serikali iangalie utaratibu wa Watumishi wote wanaolipa kodi kuitia mishahara yao wapewe *TIN Number* ili itambulike kama ni walipa kodi halali ndani ya nchi yetu kuliko ilivyo hivi sasa.

Nane, aidha, Serikali isipowasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama nilivyoombwa, nitawasilisha Muswada binafsi ndani ya Bunge hili, ili Wabunge wote tuweze kuleta marekebisho hayo muhimu niliyoyapendekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maelezo yangu binafsi. Ahsante sana. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Toa hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Maelezo binafsi huwa hayana kutoa hoja, lakini sasa nawahoji.

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kesho Waziri wa Kazi atapitia hotuba yake, tunaamini atatoa *reaction* lakini kama tunavyosema ni vizuri.

Tulikaa kwenye Kamati ya Uongozi kupitia ombi aliloleta Mheshimiwa Jafo siku ile, tukajadili kwa kirefu kwamba sheria irudi halafu tuanze tena kuangalia lakini kwa *certificate of urgency* kwa sababu muda hakuna Muswada sasa hivi.

Kwa hiyo, itabidi Bunge la Tisa ije katika mfumo wa dharura, lakini wanao muda wa kutosha kuanzia sasa mpaka wakati huo kuweza kuangalia ile sheria upya. Tukifanya hivyo maana yake na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii itahusika, ikibidi hata *public hearing* tena itahusika. Kwa hiyo, naomba tuweze kutumia nafasi hiyo.

Wanaofikiria kwamba Serikali iangalie Muswada huo upya wameshinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo lingine dogo. Mnakumbuka baada ya kuchaguliwa Mheshimiwa Masele kuwa Naibu Waziri, nafasi ya Ubunge wa Afrika ilibakia wazi. Kwa hiyo, nimeombwa na *Returning Officer* niwatangazie kwamba taarifa ya uchaguzi mdogo wa Bunge la Afrika imebandikwa kwenye ubao wa matangazo *ground floor* jengo la Utawala.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaoomba kugombea nafasi hiyo, wakachukue fomu za kugombea katika Ofisi ya Katibu wa Bunge na kuzirejesha kabla ya saa kumi jioni siku ya Ijumaa, tarehe 10 Agosti, 2012.

Waheshimiwa Wabunge tumechukua muda mfupi, lakini naomba niwashukuru sana kwa kazi ya siku ya leo. Naomba niwatakie jioni njema. Halafu bado Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga, kwa niaba ya Waislamu anasema kesho tarehe 7 Agosti, 2011 jioni saa 12.30 anawakaribisheni kwenye kufuturu hapa katika ukumbi wa *basement*. Wabunge wote wanaalikwa waliofunga na wasiofunga na Wafanyakazi wa Bunge waliofunga katika futari maalum kesho saa 12.30 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tunawashukuru sana. Maana yake mara ya mwisho tulikaribishwa na tena tunakaribishwa. Kwa hiyo na

ninyi tena mwende wote mkiwa mmeva a mahsus. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 12.05 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 7 Agosti, 2012 Saa Tatu Asubuhi)